CHURCH OF THE NAZARENE
AFRICA

# MASOMO

## YA SHULE YA JUMAPILI

### KWA WATU WAZIMA

Nakala ya 22

# MASOMO

## YA SHULE YA JUMAPILI

## Kwa Watu Wazima

Nakala ya 22

Hati Miliki © 2020 Shirika la Uchapishaji la la

Afrika Nazareti

Hati Zote Zimehifadhiwa.

ISBN 978-0-7977-1538-7

Chapa ya Kwanza 2020

This book was originally published in English with the title:
*The Path – Volume 10*

Mesoamerica Region Discipleship Ministries

www.SDMIresources.mesoamericaregion.org

Copyright © 2017

All rights reserved.

This edition is published by Africa Nazarene Publications Copyright © 2020

All rights reserved.

Printed by
Africa Nazarene Publications

**MPANGO WA JIMBO LA AFRIKA WA MWAKA WA**

**MASOMO YA BIBLIA KWA WATU WAZIMA**

**Nakala ya 22 Nambari 21**


**Mawazo ya Kuwafundisha Watu Wazima** 5
**Jinsi ya Kutayarisha Somo** 5
**Jinsi ya Kuwasilisha Somo la Shule ya Jumapili** 6
**Vidokezo Muhimu vya Kuwafundisha Watu Wazima** 6
**Jinsi ya Kuomba na Wale Wanaotafuta Uso wa Mungu** 7
**Mwongozo wa walimu wa kuwasilisha somo kupitia njia ya Kusimulia** 7


**ROBO YA KWANZA: BARUA MBILI MUHIMU: WAGALATIA NA WAEFESO**


Injili Huleta Uhuru 9
Kuishi Tu Kwa Imani Katika Yesu 12
Uhuru wa Baraka Katika Yesu! 15
Kuongozwa na Roho Mtakatifu 18
Kuwatendea Wengine Mema 21
Waliochaguliwa Kubarikiwa 24
Utajiri wa Kweli wa Muumini 27
Kukua Katika Maarifa ya Mungu 30
Kuokolewa Kwa Imani Ili Kutenda Mema 33
Upendo wa Mungu Ulio Bora 36
Kanisa: Timu ya Mungu 39
Kuukomboa Muda 42
Kila Mmoja 45


**ROBO YA PILI: MAISHA YA MAADILI YA KIKRISTO**


Mienendo Yetu Mikononi Mwa Mungu 48
Silaha Dhidi ya Vikosi Vya Shetani 51
Yesu, Mwokozi Wetu 54
Nafsi ya Mkristo 57
Kutawala Hisia Zetu 60
Usisumbuke, Amini! 63
Yale Biblia Inatueleza Juu ya Dhiki 66
Mungu Huwasamehe Wale Wanaosamehe 69
Tosheka! 72
Tulilinde Hekalu! 75
Mungu Anayeponya 78
Tumaini Letu Kuu 81
Kuishi na Magonjwa 84

**ROBO YA TATU: CHANGAMOTO NA ZAWADI: MAMBO YA WALAWI**


Jinsi ya Kuheshimu Uwepo wa Mungu 87
Ahadi ya Mungu kwa Daudi 90
Mungu ni Mwaminifu, Hata Kama Sisi Hatuwi Waaminifu 93
Mradi Muhimu zaidi wa Mfalme Daudi 96
Maandilizi na Mgao wa Raslimali ya Wanadamu 99
Matayarisho ya Kujenga Hekalu 102
Ombi Muhimu 105
Nyumba Inayostahili Mungu 108
Mfalme Aliye na Hekima ya Kipekee 111
Kuchagua Timu Inayofaa 114
Imani Inajaribiwa 117
Badiliko Muhimu Kila Wakati 120
Fanya Yaliyo Mema 123


**ROHO YA NNE: MAISHA NA MAONO YA DANIELII**


Imani na Kujitolea 126
Kumtii Mungu Kuliko Kuwatii Wanadamu Wafalme 129
Ndoto ya Nebukadneza 132
Thamani ya Uaminifu 135
Kiburi Hutangulia Kuanguka 138
Maandishi Kwenye Ukuta 141
Ujasiri Katikati ya Majaribu 144
Falme na Ufalme wa Mungu 147
Maono ya Danielii juu ya Kondoo na Mbuzi 150
Maombi, Raslimali Yetu Kuu 153
Kumtafuta Bwana wakati wa Mapambano 156
Danielii na Unabii wa mwisho 159
Danielii na Tumaini Letu la Baadaye 162

**KUWAFUNZA WATU WAZIMA**

Kuna sifa mbili muhimu za kuwa mwalimu wa Shule ya Jumapili: Ni lazima upende Mungu na uwapende watu. Jambo muhimu unalohitaji kufanya ni kuwasaidia wale walio darasani mwako waone upendo wa Mungu. Unaweza kufanya hivi kwa kuonyesha mfano wa uhusiano wa maisha yako binafsi na Yesu mbele yao na kuwafundisha kuwa na uhusiano wa binafsi na Mungu.

Fuata maagizo yaliyopeanwa juu ya *Jinsi ya Kutayarisha Somo la Shule ya Jumapili.* Kisha fuata miongozo ya *Jinsi ya Kuwakilisha Somo la Shule ya Jumapili:*

## JINSI YA KUTAYARISHA SOMO

### Mwanzo wa Mwaka:

Mwanzoni mwa mwaka wa kufundisha, chukua kama masaa mawili kuweka vitu vyote ambavyo kwa kawaida ungetumia katika shule ya Jumapili kwenye pakiti moja au sanduku. Hii itapunguza wakati kwa kila wiki ambao unaweza vinginevyo, kutumia kutafuta vitu tofauti, kwani utajua viko wapi.

Weka rekodi ya anwani, siku za kuzaliwa, na maelezo ya mawasiliano ya wanafunzi wote darasani mwako.

Kwa ufupi pitia kitabu chote cha masomo ili kupata wazo la sisitizo mbali mbali za mwezi. Hii itakupa muhtasari na hali ya mwelekeo. Utafahamu ni masomo ngapi yaliyomo kwa kila kichwa na kukosa kwenda mbele ya mafundisho.

### Masaa mawili ya Kila Wiki

**Dakika 30** — **Pitia somo ili ulifahamu.** Jumapili mchana, wiki nzima kabla ya kufundisha somo, chukua muda wa kujifahamisha na somo. Muombe Mungu akupe hekima na ufahamu wa njia bora ya kuwasilisha vifaa kwenye darasa lako.

**Dakika 10** — **Weka rekodi ya fikira na mawazo yako ya wiki.** Weka kijitabu kidogo au karatasi ya Shule ya Jumapili pamoja nawe. Wazo linapokujia, liandike kwenye karatasi ili ulikumbuke baadaye.

**Dakika 20** — **Soma kifungu cha Biblia mara 3 au 4 wakati wa wiki.** Ruhusu Neno la Mungu likubadilishe unapolifikiria na kulisoma. Kusoma huku kutaruhusu ukweli unaotaka kufunza darasa lako kubalidisha maisha *yako* kwanza.

**Dakika 50** — **Leta somo lako pamoja.** Kusanya kila kitu unachohitaji kutoka kwa pakiti lako la rasilimali. Pitia maandishi yako na upange somo katika mtindo unaokupendeza na ambao utaweza kuufuata na kuuelewa vyema.

**Dakika 10** — **Ukaguzi wa dakika ya mwisho.** Hili ni jambo la mwisho kufanya kabla ya kwenda darasani Jumapili asubuhi. Hakikisha kwamba unayo Biblia, somo lako na vifaa vingine unavyohitaji. Rejelea maandishi yako au nakala katika mwelekeo wako wa uongozi mara ya mwisho. Mwishowe, chukua dakika moja au mbili kulikabithi somo hili kwa Bwana na umuombe akutumie. Labda tayari umeomba hili mara kadhaa wakati wa ibada zako, lakini tambua utegemezi wako kwake mara nyingine.

## JINSI YA KUWASILISHA SOMO LA SHULE YA JUMAPILI

Kusoma kunastahili kuwa katika viwango vyote: kihisia, kiroho, kijamii, na kiakili. Elimu ya Kikristo inakusudia kutoa majadiliano yaliyo na Ukweli wa injili katika hali ya kubadilisha maisha ya wanafunzi. Haitoshi kujua na kuelewa dhana ya kiakili, ukweli unapaswa kuadhiri kila hali ya maisha ya mtu, kutoka kwa vile wanafikiria juu ya kichwa cha somo hadi vile wanavyoitikia na kuwatendea watu wengine.

Muda wa somo lako unapaswa kupangwa kwa uangalifu na mpangilio ili kuweka katika matendo matayarisho na mawazo yako. Tungependa kupendekeza muhtasari wa msingi ufuatao kwa wakati wako wa darasa la shule ya Jumapili. Nyakati zilizopewa zinategemea darasa la saa. Nambari zilizo kwenye mabano ni dakika 45 za darasa.

1. Wasili angalau dakika kumi kabla ya darasa ili kutayarisha sehemu ya mafunzo yako na kupanga vifaa vyovyote vya masomo ambayo waweza kuhitaji.
2. Fanya sehemu ya ***UTANGULIZI*** wakati wa **dakika 15 (10).** Ruhusu muda wa kufikiria na kuangazia ; usitarajie majibu ya mara moja kwa kila swali au zoezi. Kuwa huru kufanya mabadiliko ili zoezi liwe la muhimu zaidi kwa maisha ya wanafunzi.
3. **Dakika 15 (10)** zinazofuata zitumike kwa sehemu ya ***YALIYOMO***. Kumbuka KUTOWAHUBIRIA au KUWASOMEA. Wasilisha somo kama hadithi katika maneno yako mwenyewe.
4. **Dakika 15 (10)** ziangazie ***MASWALI YA MAZUNGUMZO.*** Sisitiza umuhimu wa kuruhusu ukweli wa kupenya katika maisha na tabia za kila mmoja katika maisha yao ya kila siku.
5. Wakati wa **dakika 5** za mwisho, funga kwa maombi na usafishe sehemu ya darasa.

Rejelea mafanikio ya somo mara unavyoweza. Tumia mchache ukitengeneza maandishi mafupi ya kile kilikamilika na kile hakikukamilika kwa marejeleo ya baadaye. Kumbuka kufundisha Shule ya Jumapili ni juu ya kujenga uhusiano na Mungu, Wakristo wenzetu na watu wengine.

**Sababu ya Ushirika**

## VIDOKEZO MUHIMU VYA KUWAFUNDISHA WATU WAZIMA

Marafiki ndio sababu kuu ambayo watu wengi huchagua kanisa. Kutoka asilimia 75 hadi asilimia 90 ya watu wanaokuwa washirika wa kanisa tayari wanao marafiki ndani ya umati. Ingawa umuhimu wa mafundisho mazuri katika ukuaji wa kundi la Ushirika wa Biblia, uhusiano mzuri ni muhimu zaidi! Ushirika *si* jambo tunafanya tu ili kuwa na wakati mzuri Ushirika wa Kikristo ni tendo la huduma kwa sababu unasaidia watu kuwa na hisia ya kuwa.

Kuwa kiongozi mkamilifu wa kundi la Ushirika wa Biblia wa Watu Wazima (darasa la Shule ya Jumapili) unapaswa kuifanya kuwa kipaumbele kukuza na kutumia ujuzi wa uongozi wa wengine darasani: * *Wahusishe:* Huwezi kuifanya peke yako! Kuhusika kwa washirika wa kikundi kunaweza kufanya kujitoa kuwe kwa ndani zaidi na kuendeleza ujuzi wa uongozi wao; * *Wathibitishe:* Onyesha shukrani zako kwa maafisa na viongozi, na upeana majibu mazuri; * *Watie nguvu:* Usiwape kichwa tu, waruhusu kufanya kazi; * *Watambue:* Usiache kazi iliyofanywa bila kuonekana iachwe nyuma. Sema 'asante' wakati wote.

### Misingi ya Muundo wa Kiroho

Hatua tatu za mabadiliko ya kiroho:

- *Kuamini:* Imani katika Kristo haiwezi kutenganishwa na Neno. Kutangaza kwa Habari Njema kunahitaji matokeo (tazama Warumi 10:17).
- *Kufaa:* Tunahitaji kila mmoja! Tunahitaji mfano na msaada unaotoka kwa jamii. Ni muhimu kujua kwamba tunafaa.
- *Kuwa:* Mungu hajamalizana na sisi. Sisi sote tuko katika hatua. Tunapomtumikia na kufuata imani yetu, tuko katika sehemu ambayo anaweza kufanya kazi kwetu.

Lengo la kila sehemu ya darasa ni kuitika kwa utiifu kwa ukweli wa Neno la Mungu. Kushiriki tu ujumbe hakuwezi kuridhisha kusudi letu. Haitoshi kwa ukweli kujadiliwa na kuchunguzwa au hata kukubaliwa. Tunayo nafasi ya kushughulika na ukweli ulio muhimu sana ambao wanataka jibu. Ile inayoanza kama zoezi la sababu inapaswa kuisha na zoezi la imani. Lengo letu ni ukweli wa Neno kuingia ndani kabisa kama imani na kuwa ndani kama kitendo.

Kusudi la kundi la darasa lako ni kubalidilisha maisha. Kama kiongozi, utakuwa na furaha ya kuona hifadhi yako kwa wengine ikizaa mabadaliko makubwa katika maisha yao . . . wakati mwingine. Lakini pia utapata uchungu wa kuwatumikia wengine ambao wanaonekana kutobadilika. Je, utaitikaje kwa wale wanaoonekana kutobadilika? Endelea kuwa mwalimu mwaminifu na rafiki wa kweli. Endelea kutafuta nafasi ya kuwa karibu nao. Endelea kumtumainia Mungu kufanya mambo yake mazuri katika maisha ya wale unaotumikia!

**Mstari wa Kumbukumbu**

Kuweka Neno la Mungu kwa akili ni ulinzi bora zaidi tunao juu ya majaribu. Mzaburi alielewa wazo hili, karne zilizopita aliposema: ‘Nimeliweka neno lako moyoni mwangu, nisije nikakukosea’ (Zaburi 119:11). Ni k weli kwa watu wa Mungu wa kila umri. Litie moyo darasa lako kukariri *Mstari wa Kumbukumbu* kila wakati.

**Kufikia Zaidi ya Sisi Wenyewe**

Utumishi kwa wengine si jambo la kuongoezewa kwa yale tunayoyafanya. Ni kielelezo cha jinsi tulivyo. Paulo anatueleza *tutumikiane kwa upendo* (Wagalatia 5:13). Kundi lako ni uwanja mzuri wa kuhusika katika utumishi wa Kikristo. Hakika, vikundi vinavyoibuka mara nyingi vitapeana nafafsi fulani ya kuhusika kwa maana katika huduma. Zile sehemu za zoezi mara nyingi ni chanzo cha uhai katika kundi.

## JINSI YA KUOMBA NA WALE WANAOTAFUTA USO WA MUNGU

(Tafadhali badili kama inahitajika)

Jitayarishe kuomba na wale wanaotaka kuomba darasa linapoendelea na somo katika imani. Fanya mipango ya mchungaji na/au waumini wengine waliokomaa wakusaidie hasa wakati majibu mengi yanatarajiwa.

a. Tambua umuhimu wa muda huo, ipatie umakini kamili na uwe mwangalifu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu
b. Piga magoti, kaa au simama karibu na mtu ambaye unakusudia kumsaidia.
c. Kwa kimya omba mwongozo wa Mungu na, bila kukatiza maombi yake, waombee pia. Yeye ndiye anayepaswa kuomba - wewe uko tu kusaidia kama Roho Mtakatifu anavyoongoza.
d. Sikiliza sala ya mtafuta ili kubaini ikiwa wanahitaji msaada.
e. Wakati mtafuta amemaliza kuomba, tafuta ikiwa ana uhakika kwamba maombi yake yalijibiwa. Si lazima ujue ombi ni juu ya nini labda iwe anataka kuzungumza juu yake.
f. Kama mwenye anatafuta maombi ataendelea kuomba bila kufika mwisho, au bila kuwa wazi:
   i. Muulize kwa uangalifu ikiwa unaweza kusaidia. Mara ruhusa ikipewa,
   ii. Tafuta ni kwa nini alikuja kuomba.
   iii. Muongoze kwa ufupi na Maandiko husika.
   iv. Pamoja ombeni kwa hitaji maalum na mtumaini Mungu na ombi.
   v. Wakati mmemaliza kuomba, tafuta ikiwa ana uhakika kwamba maombi yake yalijibiwa. Kama sivyo, wahimize kwa muda mfupi waendelee kumwamini Mungu na kutembea katika nuru kama vile Mungu anamwongoza. Mkumbushe kwamba ni kwa imani tu kwa Mungu wanaweza kupata ushindi na, mara tu kazi imekamilika, Roho Mtakatifu atashuhudia pamoja na roho zao. Kunaweza kuwa hakuna udhihirisho wa mwili lakini uhakikisho wa Roho Mtakatifu utakuwapo kila wakati.

g. Kumbuka kumpa mchungaji majina ya wale wote wanaotafuta maombi na matokeo ya maombi yao.

## MWONGOZO WA WALIMU WA KUWASILISHA SOMO KUPITIA NJIA YA KUSIMULIA

**Muhtasari:** Yesu alichagua kuwahudumia watu wa wakati wake katika njia ya kuungana nao kimatendo, kwa kumbukumbu na kuwahusisha. Alieleza hadithi na kuuliza maswali Vyombo hivi maalum bado vinatumika kwa hali ya juu hata sasa. Ili kuwafaidi wengi kutoka kwa kuwafikia kwa njia simulizi ni kukubali majukumu mawili ya kuwa mwelezaji wa hadithi na msaidizi. Jifahamishe na hadithi, kisha shiriki hadithi katika

njia ya kushurutisha na ili mwafaka na kuwaruhusu wahusika kushiriki mawazo yao wanapojibu maswali.

**Hatua:** Shiriki lengo la somo lako la siku na kichwa cha somo kwanza. Fungua mazungumzo kwa kushiriki mithali ya nyumbani. Acha kila mtu aangazie na kushiriki kile wanafikiria mithali inamaanisha. Kisha waulize wasikilize hadithi yako na kuishikiri kwa shauku na ufasaha. Onyesha picha na uulize watu waone katika michoro inayowakumbusha hadithi. Hatua inayofuata uliza maswali ya ku pendekeza kwa utaratibu. Waweke watu waangazie yaliyomo ya hadithi na wala sio maoni yao. Baada ya mazungumzo, shiriki mstari wa somo ambao ni mstari wa kumbukumbu ukiurudia mara nyingi. Mwishowe shiriki himizo na uulize jinsi linavyohusika na mithali ya nyumbani ambayo ulianza nayo. Rudia himizo la hadithi mara kadha ili kuwasaidiwa watu kukumbuka hadithi na somo linalofundisha.

**Mapendekezo ya Mafanikio:**

1. Kwa wanafunzi wa kusimulia, ni lazima ukweli utolewe katika njia ambayo inafahamika katika mawasiliano yao na kila mmoja. Ruhusu muda wa majadiliano.
2. Hakuna majibu ya makosa kama utauliza swali vilivyo. Mruhusu kila mmoja kuhusuka.
3. Wakati wa mazungumzo rudia sehemu za hadithi ili kuwasaidiwa watu kuelewa somo kutoka kwa hadithi. Lengo lako ni *kuwaruhusu kutambua ukweli,* si kuwaeleza majibu.
4. Vumbua hekima ya nyumbani kupitia kujadili mithali. Picha hizi zinazoonekana zilizoundwa na mithali hizi zitawasaidia watu kukumbuka na zitawaunganisha na maandiko.
5. Usikawie kwa swali moja kwa muda mrefu. Lengo lako ni kuuliza maswali ya kufuatilia yatakayowasaidia watu kugundua ukweli na kujua jinsi kutumia katika maisha yao.
6. Usiruhusu mtu mmoja au wawili kujibu maswali yote. Wachague watu wengine ili usikie kutoka kwa kila mmoja. Watu watajifunza vizuri wakati wanahusika vikamilifu.
7. Himizo la hadithi ni muhimu kwa watu kukumbuka ukweli. Tumia marudio kuweka mkazo yale wamejifunza.
8. Mukhtadha wako utaamua matumizi ya masomo haya. Kama ni kwa muundo wa vijijini watie moyo wanafunzi kutumia masomo haya katika mukhtadha huo. Kama ni ya muundo wa mjini matumizi yatuakuwa tofauti. Mwito wa kutenda mara nyiingi ndio lengo la kujifunza.

**Mwezeshaji Mzuri:** Lengo lako si kufahamika na hadithi bali pia ni kuongoza ujuzi wa mafundisho. Ni lazima ujue yaliyomo, kuwa tayari kuendeleza mazungumzo, na unda njia za kumbukumbu na ubunifu za kugundua ukweli. Picha zilizopeanwa ni za kusaidia kuona sehemu muhimu za somo. Fanya iwe nafasi ya kusikiliza vizuri majibu ambayo watu wanatoa na kuthibitisha majibu na kuhusika kwao. Watu wanapenda hadithi nzuri kwa hivyo watarudi tena na tena kama wewe ni msimulizi na mwezeshaji mzuri.

**Sasa . . . Nenda ukasimulie Hadithi.**

| Somo la 01 | INJILI HULETA UHURU |
|---|---|
| | **Maandiko:** Wagalatia 1 na 2 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza na kutumia injili na mafanikio yake kwa maisha yetu kama waumini. | "Lakini, hata kama mmoja wetu au malaika kutoka mbinguni, atawahubirieni injili tofauti na ile tuliyowahubirieni sisi, basi huyo na alaaniwe! **Wagalatia 1:8** |

## UTANGULIZI

Katikati ya karne ya kwanza Baada ya Kristo, Wagalatia ulikuwa mkoa wa Rumi uliokua katikati mwa jimbo la Asia Minor, sehemu ya ile sasa inajuliakana kama Uturuki. Katika waraka kwa Wagalatia, Paulo anazungumzia makanisa ya Wagalatia bila kutaja jina la mji wowote. Paulo alitetea uhalisi wa injili aliyokuwa amehubiria Wagalatia, akisisitiza kwamba alikuwa amepokea misheni yake kutoka kwa Mungu kupitia Yesu Kristo, na wala si kwa wanadamu.

Kama vile ilivyokuwa na siku za mtume Paulo, injili imechanganywa na kupotoshwa katika histori yote ya kanisa na watu walioitumia kwa matamanio ya kigani kwa injili. Somo hili ni muhimu kwa sababu litatusaidia kugundua injili ya kweli na faida zake; na, kama mtu yeyote anajaribu kubadilisha ujumbe, "basi na alaaniwe." (Wagalatia 1:8)

### I. Injili Inapokelewa na Ufunuo (Wagalatia 1:6-17)

#### A. Injili Ni Ufunuo

Tunapata injili kupitia kukutana na Mungu, ikifunuliwa kupitia Mwanawe Yesu Kristo. Yeye ni "Mungu pamoja nasi." Kukutana ambapo mtume Paulo alikuwa nao na Bwana Yesu kulibadilisha maisha yake; alibadilika kutoka kwa kuwa mtesi wa kanisa hadi mhubiri wa injili (Matendo ya Mitume 9:1-19, Wagalatia 1:15-16). Tangia wakati huo, alienenda kulingana na ufunuo, kama vile alivyosema katika Wagalatia 2:2. Tunaweza haya na tukio la Waisraeli jangwani; walisonga wakati wingu lilisonga; na wakatulia wakati wingu lilisimama; hivyo ndivyo Waisraeli walitambua uwepo wa (Kutoka 13:17-22). Katika hali ya Paulo, kilichokuwa cha maana kilikuwa kukutana kwake na Kristo.

#### B. Injili si Jambo ambalo Tunajifunza Tu

Haitoshi kujifunza tu injili. Kama ingelikuwa hivyo, ni watu wa elimu wachache tu ndio wangekuwa Wakristo. Kumbukuka Nikodemo akimtembelea Yesu (Yohana 3). Nikodemo alikuwa mshirika wa Mafarisayo, mwalimu wa dini, mtu mwaminifu ambaye alivutiwa na sifa na mafundisho ya Yesu.

Hivyo, wakati Mafarisayo walimtafuta Yesu usiku, Bwana alimwambia wazi kwamba alihitaji kuzaliwa mara ya mbili (Yohana 3:3). Nikodemo, kama mwanaelimu na mwalimu wa Wayahudi, bila shaka, alijua kwamba sheria ilikuwa Neno la Mungu. Hata hivyo, Bwana alieleza kwamba hii haikutosha wala ilikuwa hakikisho kurithi ufalme wa Mungu. Njia pekee ambayo angekuwa mwanafunzi kamili, kubadilishwa kwa kukutana na Mungu, ndilo alihitaji ili kuzaliwa mara ya pili (Yohana 3:5).

### II. Injili Hulete Uhuru na Wala Si Utumwa (Wagalatia 2:1-5)

#### A. Uhuru wa Nguvu ya Kulazimisha Ya Dhambi

Katika sehemu ya kwanza, uhuru ambao Kristo anatupatia ni uhuru kutoka kwa minyororo ya dhambi (Yohana 8:34,Warumi 6:5- 23), na pia, kutoka kwa udanganyifu wa bure ambao watu wanaweza kupata maisha na uhuru chini ya mpango wao. Injili ina nguvu ya kutuweka huru kutoka kwa dhambi na matokeo ambayo dhambi huleta pamoja nayo kupitia kifo cha Yesu. (1 Yohana 1:7). Uhuru huu huanza na kuendeleza hatua ya kuwekwa huru kabisa kiakili, kimwili, kijamii, na kiroho. Mpango wa ufalme wa Mungu uliotabiriwa katika Isaya 61:1-3, ulithibitishwa na Bwana katika Luka 4:18-21.

Haya yote yanadhihirisha uhuru kamili ambao Yesu Kristo analeta kwa mwanadamu.

## B. Uhuru ni Tendo la Kujitolea

Wagalatia 2:3 says: *"Lakini, hata mwenzangu tito, ambaye ni Mgiriki, hakulazimika kutahiriwa."* Mungu, kupitia kupitia ujumbe wa injili, anatutaka tuchague uhuru, hatulazimishi kuwa huru. Watu wako huru kufanya chaguo. Uhuru wa kujitolea unamaanisha kujitoa kwa Anayetuweka huru. Kama Wakristo, tunajitoa kwa hiari kwa kanuni na thamani Ufalme wa Mungu. Kumbuka kwamba wokovu ni kwa neema ya Mungu (Waefeso 2:8 Yohana 6:44). Ujumbe wa Injili ya Mungu ni ya kila mtu (Waefeso 2:8). Neema ni zawadi bure kutoka kwa Mungu.

## III. Injili Huleta Haki Kwa Imani (Wagalatia 2:15-17)

A. Haki Haipatikani Kwa Kazi Za Sheria. Katika agano la kale, kulikuwa na sheria ya jumla ya watu, na pia, sheria fulani za wahalifu, kama walitaka kuhusishwa kwa hatia. Hata hivyo, sheria hizo zilianguka kwa sababu hali ya uwanadamu iliyoathirika haingeweza kukutana na mahitaji. Kwa hivyo, agano mpya lilikuwa muhimu ambapo hakuna mtu angeweza kufanywa haki kwa kazi za mwanadamu. Moja ya Zaburi: *"Usinitie hukumuni mimi mtumishi wako maana hakuna yeyote aliye mwadilifu mbele yako."* (Zaburi 143:2).

### B. Injili Huleta Haki Kwa Imani

Tunafanywa haki na Mungu wakati anatusamehe. Kupitia upendo wa Kristo, Mungu anasamehe dhambi zetu, lawama zinafutwa, adhabu yetu inatolewa, na tunakuwaliwa na Mungu kama watu wa haki. Shukrani kwa damu ya Kristo, kuna nafasi ya kuondolewa na kufutwa kwa dhambi zetu. Kuptia Adamu, dhambi iliingia duniani, na kuptia Yesu Kristo, haki iliingia duniani (cf. Warumi 5, 6) *"Mlikombolewa kutoka kwa utumwa wa dhambi, mkawa watumwa wa uadilifu.""* (Warumi 6:18)

## IV. Injili Ni Maisha Mapya ya Kristo (Wagalatia 2:20)

### A. "… Siishi Tena …"(v. 20)

Paulo alidhihirisha kuwekwa wakfu kamili kwa Bwana. Hii inaonyesha kufa kwa mtu binafsi, kwa sababu Mungu anatukamilisha tunapojiachilia chini ya mapenzi yake. Kuwekwa wakfu inamaanisha kutoa yote inatuhusu kwa Mungu. Nguvu za dhambi katika maisha yetu zimevunjwa kwa sababu tumekufa kwa dhambi na Kristo. Kufa kwa mtu binafsi na Kristo ndio njia ya pekee ambayo wale waliofungwa kwa sheria wanaweza kupata uhuru. Kinachokufa ni ule utu wa zamani ambao ni usiofanya kazi na kuchanganywa kabisa na dhambi.

### B. ". . . Kristo Anaishi Ndani Yangu . . . "

Usalama gani huu mkuu! Dhihirisho hili linaonyesha kwamba Kristo ni mmiliki wa maisha yetu. Kwa maneno mengine, Yeye si kama mpangaji anayeishi kwa nymba, ambaye wakati wowote anaweza kuondolewa, badala yake, anakuja kuwa mmiliki kamili wa nyumba, kwa sababu tayari aliinunua kwa gharama. Kunazo sheria zingine ambazo zinaeleza sehemu muhimu ambayo Yesu anapaswa kuchukua katika maisha yetu na maisha ya kanisa kama vile rubani, mkuu, jiwe kuu la pembeni, na kichwa cha mwili. Kuwekwa wakfu kwa Kristo huleta thamani kamili maishani mwetu.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ufunuo ni nini?
- Je, waweza kusema, kama Mtume Paulo, yafuatayo: "... Siishi tena…"? Kwa nini?
- Kwa vile umepokea injili, je, umewekwa huru kutoka kwa?


## HITIMISHO

Injili, ambayo ilitangazwa na mtume Paulo, ni ufunuo wa uungu na una maelezo yake ya kutosha katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Ni yeye tu kwa dhabihu yake msalabani, anaweza kutupa uhuru kutoka kwa dhambi katika njia zake nyingi. Katika Kristo, tunatangazwa kuwa haki. Katika Kriso, tumetangazwa kuwa waelekevu mbele ya Mungu. Tusidanganywe na muundo mpya wa karne ya sasa!

## Somo la 1:

### INJILI HULETA UHURU

**Lengo la Somo:** Kujifunza kutumia injili na faida zake katika maisha yetu kama waumini.
**Methali**: Hakuna haja ya kubeba mzigo wa mtu juu ya kichwa ndani ya gari.
**Kifungu cha Kusoma:** Wagalatia 1 na 2
**Mstari wa Kumbukumbu:** Lakini, hata kama mmoja wetu au malaika kutoka mbinguni, atawahubirieni injili tofauti na ile tuliyowahubirieni sisi, basi huyo na alaaniwe! Wagalatia 1:8
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini inakupa kipaumbele katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, tunasikia nini juu ya uhuru au utumwa katika kifungu hiki?
Swali la 3. Je, wewe au mtu mwingine unayemjua, mmeweza kupata tukio kama hilo katika hadithi ya leo?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini juu ya kuishi maisha yaliyojazwa na Roho na ni kwa nini jambo hilo ni muhimu?
Swali la 5. Je, ni ukweli gani katika hadithi ambao utashiriki na mtu mwingine wiki hii?
**Himizo la Hadithi:** Injili ya Kristo yatosha kutuweka huru.



| Somo la **02** | **KUISHI TU KWA IMANI KATIKA YESU** |
|---|---|
| | **Maandiko:** Wagalatia 3 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba Roho wa Mungu anapokelewa kwa imani na wala si kwa matendo ya sheria. | "Ni dhahiri kwamba sheria haiwezi kumfanya mtu kuwa mwadilifu; maana Maandiko yanasema: "mwadilifu kwa imani ataishi." the righteous will live by faith." **Wagalatia 3:11** |

## UTANGULIZI

Katika mistari ya kwanza ya Wagalatia 3, tunaona kwamba mtume Paulo alighadhabishwa na kanisa la Wagalatia; aliwaita Wakristo wapumbavu. Pengine, ndugu na dada hawa walielewa maana ya kusulubiwa kwa Yesu Kristo na walikuwa wanashuhuduia baraka za Roho Mtakatifu katika maisha yao. Hata hivyo, kile walichokuwa wakifanya kiliwashusha mitume moyo. Wakristo wa Wagalatia walikuwa wanaruhusu washawishiwe na watu wa Yuda waliokuwa wakiwafanya Wakristo wa mataifa kufuata matendo yao ya 'kimwili' (tamaduni na matendo ya sheria)

Ni kupitia kwa imani ndani ya Mungu kwamba kila baraka inapokelewa, tangu wakati wa Abrahamu hadi wakwati wetu. Baraka zetu haziji kupitia kufuata sheria tu, balika kwa imani katika dhabihu ya ukombozi wa Yesu Kristo. Paulo aliwaambia Wagalatia, akikosoa mukhtadha wao uliochanganywa wa maisha mapya katika Kristo. Roho Mtakatifu anapokelewa kwa Imani (Wagalatia 3:1-5)

### A. Kutegemea Kusikostahili Kwa Matendo ya Sheria

Paulo alizungumza kwa nguvu dhidi ya imani dhaifu ya Walatatia kupitia kutegemea kwao kwa kila wakati kwa matendo ya sheria. Walikuwa wameanguka katika upumbavu wa kuruhusu wenyewe kushawishiwa na matendo ya kidini (kuhalalishwa) ambayo pengine yangeimarisha maisha yao ya kiroho. Wagalatia walikuwa wakishawishiwa na tamaduni za Kiyahudi, pengine zilizochanganya na vipengele vya wapagani, na tamaduni hizi zilikuwa zinaadhiri ushuhuda wao.

Tamaa ya Wagalatia ya kufuata matendo ya kidini ambayo hayakuhitajika na injili, kwa mfano, tarehe maalum au kuangazia matukio ya kihistoria (Wagalatia 4:9-10), ilibadilisha mawazo yao kutoka kwa roho ya kutegemea na kujitoa kwa Kristo.

### B. Kutegemea Muhimu kwa Roho Mtakatifu

Dhambi huwatengatisha watu na Mungu. Mwenye dhambi, kupitia toba yake mbele ya Mungu, anakubali dhabihu ya damu ya Yesu Kristo kama malipo pekee ya dhambi. Mungu humthibitisha mwenye dhambi aliyetubu, bila kujali kama atafuata sheria (matendo ya sheria au tamaduni za Kiyahudi). Kufanywa haki kunapokelewa kwa imani katika hali hiyo ya kipekee na kazi za ukombozi wa kimiujiza za Bwana Wetu Yesu Kristo.

Hii inakamilishwa na nguvu za miujiza za Roho Mtakatifu (Warumi 5:17,8:11).

Kanisa la Bwana linatia moyo mkutano waishi kulingana na kazi za Roho na wali si sheria. Ni lazima tutiwe motisha na imani na muungano na Mungu, ambaye ametupokea kama watoto wake. Paulo alikuwa na msimamo imara katika kukabiliana na tatizo hili, akiwakumbusha, bila kufuata sheria fulani, nguvu za Mungu za uadilifu katika kubadilishwa kwao.

### I. Agano la Imani Na Abrahamu Linathibitishwa Katika Kristo (Wagalatia 3:6-18)

A. Abrahamu Alifikia Baraka Kupitia Imani

Agano la Kale pia linatoa ushahidi kwa ukweli kwamba Abrahamu alifanywa haki kwa imani yake, wala si kwa matendo. Thibitisho hili lilitokea wakati wa mkutano wake na Mungu na utiifu wa mwito wake, akitii kila kitu ambacho Mungu alikuwa amemwambia afanye. Mwanzo 12:7 inasema: *"Ndipo Mwenyezi-Mungu akamtokea Abramu akamwambia, 'Wazawa wako nitawapa nchi hii.' Basi, Abramu akajenga madhabahu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu aliyemtokea."* Abramu, ambaye baadaye Mungu alimbadiisha jina na kumwita Abrahamu,

aliacha nchi yake na kwenda katika nchi ambayo Mungu alikuwa ameahidi kumwonyesha, *"... ingawa hakujua alikokuwa anakwenda"* (Waebrania 11:8). Baada ya Abrahamu kufika katika nchi, Mungu alitangaza kwamba atakipatia kizazi cha Abrahamu nchi hiyo.

Mwanzo 15:6 inasema: *"Abramu akamwamini Mwenyezi-Mungu, naye Mwenyezi-Mungu akamkubali Abramu kuwa mwadilifu."* Paulo alitumia wa Abrahamu katika Waraka yake wake wa Wagalatia. Abrahamu hakupokea heshima ya kazi yake bali heshima ya imani yake.

**B. Tumebarikiwa Kupitia Imani**

Katika kuangazia mpango wa Mungu kwa Abrahamu na kizazi chake, bila shaka sifa yake ya uadilifu, na wala si kazi zake, ingehusisha misingi ya utiifu na kuthibitishwa kwa kila wakati kwa baraka zake nyingi za Mwenyezi Mungu kwa wanadamu, kupitia Roho Mtakatifu. Kwa hivyo, baraka za Mungu na ahadi za watoto bado ni halali. Misheni yetu kama kanisa ni kupata baraka hizo za ukombozi na vipaji kwa wale wote wanajiunga na makusudi ya uungu kwa imani katika Yesu Kristo.

Hata leo, sisi ni ndugu na dada wa Abrahamu kwa sababu sisi pia tunakiri imani. Tumebarikiwa kwa kupokea neema ambayo inatuelekeza kuamini na kupokea haki. Kuishi kwa imani inamaanisha kwamba ukombozi wa Kristo na kazi za uadilifu zanafanya kazi kwa kila mmoja wetu kwa ajili ya wokovu wetu, na kutuweka huru kutoka kwa kila nira, iwe ni sheria za halali, imani za uongo, tamaduni na upagani. Yesu ni utimizo wa kila baraka ambayo Bwana kuupatia ulimwengu kuptiia Abrahamu, ndugu yetu.

## II. Sheria Huja Kabla Ya Ahadi (Wagalatia 3:19-29)

### A. Kusudi La Sheria

Urithi wetu kama waumini unasimama kwa misingi ya ahadi, na tutaupokea kwa imani, kama tu vile Abrahamu alivyopokea. Urithi huu hauji tu kutoka kwa kufuata sheria. Katika Agano la Kale kulingana na sheria, mwanadamu alichukuliwa kuwa amelaaniwa kwa kufia mtini, bali Yule aliyekufa kwa ajili yetu msalabani alileta baraka kuu. Katika Kristo Yesu, tumebarikiwa na kuwa huru kutoka kwa kila nira ya kuhalalishwa au ya kitamaduni ambayo agano ya Agano la kale ilikuwa imeweka juu ya watu.

Paulo alitoa maelezo wazi na ufahamu Wagalatia 3:2, 5 na Warumi 3:20-26 jukumu la sheria. Paulo alisema kwamba kwa kufuata tu sheria peke yake hakuwezi kutupatia haki ya kiroho, Mungu Baba, na Yesu Kristo wanataka kila mwumini, anayeongozwa na Roho Mtakatifu, kutimiza sheria ya upendo wa Mungu kwa wengine. "*Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatimiza sheria ya Kristo.*" (Wagalatia 6:2).

**B. Faida za Kuwa Warithi Na Kristo** Tunayo faida ya furaha ya kuwa huru katika Kristo, sheria mpya katika Kristo haiwakilishi tena nira nzito. Anatuelekeza kwa upendo kuptia Roho Mtakatifu tuziweke amri kwa matendo kama matokeo ya uadilifu wa maisha yetu. Kristo ametubatiza kwa Roho Wake, tumevishwa utakatifu wake, na kuwezeshwa kutimizia makusudi ya ukombozi ambao Mungu ametuitia. Mungu ametuita. Umuhimu wa urithi wa baraka hautufautishi na rangi zingine, tamaduni, n.k. bali unatuunganisha na kututia nguvu katika muungano na wengine, bila ubaguzi.

**C.** Hali ya 'Agano Mpya' inatuweka kwa umoja wa imani ya kweli katika Kristo, kama warithi wa neema yake ya uhuru. Tunapaswa kuwa wazi kwamba Roho wa Mungu ndani mwetu alitufunika na rehema yake wakati tuliamini katika Yesu kristo na kukubali kazi yake ya kipekee nay a ajabu ambayo ilituweka huru kutoka kwa utumwa wa kimwili. Hivyo, tuwe na usawa wa injili ya kweli, tukifuata imani yake iliyo hai na kuishi kulingana na imani ambayo inatuunganisha na waumini wa kweli.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, una hakikisho kwamba umefanywa mwadilifu na Mungu? (Wagalatia 3:6-7)
- Je, una hakikisho kwamba tayari umekombolewa kutoka kwa laana ya sheria (kwa kutoitimiza) Maoni (Wagalatia 3:10-14).

## HITIMISHO

Kwa sasa, tamaduni zetu, hata kama zinaweza kuonenaka kuwa za sheria na za kusaidia, zinaweza kudhoofisha imani yetu katika Roho, na kutuzuia kufikia hadi kuu za thamani za Bwana wetu Yesu Kristo.

## Somo la 2:

### KUISHI TU KWA IMANI KATIKA YESU

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba Roho wa Mungu hupokelewa kwa imani na wala si kwa vitendo vya sheria.

**Methali:** Jua litawaangazia wanaosimama, kabla halijawaangazia wanaopiga magoti chini yake.

**Kifungu cha Kusoma:** Wagalatia 3

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Ni dhahiri kwamba sheria haiwezi kumfanya mtu kuwa mwadilifu, maana mwadilifu ataishi kwa imani." Wagalatia 3:11

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini inakupa kipaumbele katika hadithi hii?


Swali la 2. Je, tunasikia nini juu ya uhuru au utumwa katika kifungu hiki?

Swali la 3. Je, wewe au mtu mwingine unayemjua, mmeweza kupata tukio kama hilo katika hadithi ya leo?

Swali la 4. Je, tunajifunza nini juu ya kuishi maisha yaliyojazwa na Roho na ni kwa nini jambo hilo ni muhimu?

Swali la 5. Je, ni ukweli gani katika hadithi ambao utashiriki na mtu mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Tamaduni zinatuweka kwa mtego; imani katika Kristo hutuweka huru!



| Somo la 03 | UHURU WA BARAKA KATIKA KRISTO! |
|---|---|
| | **Maandiko:** Wagalatia 4-5:13 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujua na kuonyesha shukrani yetu kwa uhuru ambao tumepokea kama watoto Wake; kuelewa kwamba hakuna jambo linalokuja kupitia nguvu zetu pekee, bali tumewekwa huru na Yesu Kristo. | "Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa." **Wagalatia 5:1** |

## UTANGULIZI

Mara nyingi kama wanadamu, tunaonekana kusahau ni nani aliyetuleta katika hali hii ambayo tuko ndani. Katika somo hili, tutajifunza maana ya kweli ya uhuru ndani ya Kristo, tukiangazia masuala yanayotuzuia kufurahia uhuru huu.

Mtume Paulo aliwatembelea Wagalatia kwenye safari yake ya kwanza ya umishenari, akianzisha makanisa huko kama vile alivyokuwa amefanya katika sehemu zingine. Kwa bahati mbaya, miaka baadaye, alifahamu kwamba Wayuda walikuwa wamechanganya kanisa ambalo alikuwa ameanzisha. Wakristo walikuwa wanadanganywa kwa kiwango ambacho watu wengine waliacha Ukristo wa Kweli kwa kukubali tamaduni na mila za Kiyahudi. Paulo alitambua kwamba kulikuwa na mizozo mikali katika makanisa haya, ambayo yalileta machungu na wasiwasi.

### I. Tumekombolewa na Kristo na Kupokelewa Kama Wana (Wagalatia 4:1-7)

A. Watumwa Chini Ya Vipengele Vya Ulimwengu Mtume Paulo alitumia mifano kama uhuru ambao mtoto hupokea anapofika umri wa utu uzima, na ishara ya utumwa.

Tulipokuwa watoto, tuliishi chini ya sheria zilizoanzishwa na familia zetu. Tulipofika watu wazima, hatukushurutishwa tena kufuata sheria zilizowekwa juu yetu tulipokuwa watoto. Wagalatia 4:1 inasema: *"Lakini nasema ya kuwa mrithi watoe ambao awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote."* Hivyo, mtoto hana tofauti na mtumwa katika kutegemea sheria zilizoanzishwa nyumbani, hata wakati mtoto anamiliki kila kitu nyumbani.

Kama watu, sisi ni watumwa wa sheria za ulimwengu huu, kama watoto walio chini ya sheria zilizoanzishwa, au kama watumwa chini ya sheria za bwana wao. Ni baba tu au bwana anaweza kusema ni muda gani wameshurutishwa kufuata sheria, na ni bwana peke au baba anayeweza kusema wakati wanaweza kujisimamia au kuwa huru.

B. Kutimia kwa Wakati

Wagalatia 4:4 inasema: *"Lakini wakati ule maalum ulipotimia, Mungu alimtuma Mwanawe aliyezaliwa na mwanamke, akaishi chini ya sheria…"*

Wakati muda ulikuwa ulitimia, yule ambaye angetuongoza kutoka kwa utoto hadi ukomavu, kutoka kwa utumwa hadi uhuru, alikuja kwa ulimwengu wetu. Uhuru huu mzuri ulikuja wakati Bwana aliamua wakati umefika, kwa sababu hali zilikuwa sawa.

Bwana hutuongoza kutoka kwa utumwa hadi uhuru. Lakini, hatupati uhuru huu kwa faida zetu. Kristo pekee ndiye anayeweza kutupa huu uhuru tunapomtambua kama mwana wa Mungu na kuyatoa maisha yetu kwake. Baba hutuwela huru na kutupokea kama watoto wake.

### II. Tuko Huru Kutoka kwa Tamaduni za Wanadamu (Wagalatia 4:8-11)

A. Vishawishi Vya Tamaduni

Kuna watu wengi ambao wanashawishiwa na tamaduni. Hata hivyo, Kristo anapoingia katika

maisha yetu, anatufanya kuwa viumbe vipya (2 Wakoritho 5:17), nah hii inamaanisha mabadiliko katika njia yote ya maisha. Leto tunapambana na vishawishi vya Kikristo, ambapo wengi waliomjua Kristo hawajawacha nyuma upagani wa kitambo na tamaduni za ibada ya sanamu. Wengi wanamwimbia Mungu Jumapili, bali Jumatatu, wanamchezea 'Baali', na kuendelea kana kwamba hawakumfahamu Mungu. Katika Wagalatia 4:8, tunasoma: *"Zamani hamkumjua Mungu na hivyo mliitumia miungu isiyo miungu ya kweli."*

Kwa kupokea uhuru wa Kristo katika maisha yetu, tuku huru katika njia ya uadilifu. Hiyo ni kusema hatuko huru kutoka kwa vitu vingine tu, bali ni uhuru kamili. Kwa hivyo, tunapaswa kutambua kwamba Kristo hashiriki nafasi yake maishani mwetu na mtu mwingine, hasa si na mtu aliyetuweka katika utumwa kwa muda mrefu. Ni lazima tukumbuke kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana pekee, na ni lazima tumtambue hivyo.

## III. Sisi ni Watoto Wa Ahadi (Wagalatia 5:1-13)

### A. Ishara Katika Uhuru

Katika Wagalatia 5:1, tunasoma yafuatayo: *"Kristo alitupa uhuru, akatakat tubaki huru. Basi, simameni imara wala msikubali tend kuwa chini ya nira ya utumwa."* Kristo aliweka huru na anatutarajia tuwe chini yake na wala si kwa imani za ulimwengu. Hataki tuishi chini ya nira ya utumwa. Anataka tuishi kama watoto wa kweli wa Mungu, tulio huru kupitia damu ya Yesu Kristo.

Uhuru hauji kwa sababu ya kuwa kwa umati, au kutokana na kufanya mambo mawili au matatu kanisani. Uhuru hauji kwa sababu ya yale tunafanya au kutoka kwa faida tunazoweza kuwa nazo, bali huru huja kupita kwa kazi ya Yesu Kristo.

Uhuru uko kwa misingi ya uaminifu. Tuko huru, kwa sababu Yesu Kristo alikuwa mwaminifu kwa makusudi ya Mungu. Kusimama imara katika uhuru wa Kristo kunahitaji uaminifu uliopita kiasi.

### B. Chachu Kidogo Huchachusha Donge Lote la Unga

Wagalatia 5:9 inatueleza: *"Chachu kidogo tu huchachusha donge lote la unga."* 'Chachu' katika maneno haya haiwakilishia uovu, bali mafundisho ya uongo juu ya kutahiriwa na 'donge' huwakilisha makanisa. Tafsiri ya Ujumbe wa Wagalatia inaiweka vizuri: *"Mwenendo wenu ulikuw mzuri! Nani, basi aliyewazuia kuuzingatia ukweli? Aliyesababisha hali hiyo si Mungu ambaye mawaiteni. Na tafadhaili msiiache hii kuwa muhimu. Inachukua chachu ya muda mfupi, mnajua, kuingia ndani ya mikate. Kwa undani, Bwana amekupa ujasiri ambao huataondoka. Lakini yule anayekuchagua, awe nani, atakutana na hakimu ya uungut"* (mistari ya. 8-10).

Tuwe waangalifu tusiache mlango ufunguke kidogo kwa mafundisho machafu kuingia! Wakati mwingine, tunaharibu kazi ya Kristo kwa kujipa uhuru wa kufikiria au kuamini kwamba dhambi inaweza kwenda pamoja na utakatifu ambao tumeitwa kuishi. Mara tu tumeitwa kuwa huru na Kristo, Anatubadilisha ili tuishi katika utakatifu. Katika maisha ya utakatifu, hakuna nafasi ya uovu

## MASWALI YA ZIADA

- Je, tulikuwa watumwa wa nani kabla tukutane na Kristo?
- Je, tumewekwa huru kweli kutoka kwa tamaduni za uwanadamu?
- Je, tunapaswa kuwa na nia gani kuhusiana na huru ambao Kristo alitupatia?

## HITIMISHO

Kristo alilipa gharama kubwa kwa ajili ya uhuru wetu, na ni yeye peke yake anayeweza kutupa huo uhuru kupitia imani. Haijalishi sisi ni nani; hakuna njia ya kupata huru kwa faida zetu. Tunamhitaji Kristo ili kuwa huru kabisa.

**Somo la** 3:

## UHURU WA BARAKA NDANI YA KRISTO!

**Lengo la Somo:** Kuonyesha shukrani zetu kwa Mungu kwa uhuru ambao tumepokea, na kujua kwamba Kristo ametuweka huru, sasa sisi ni wana wa Mungu.

**Methali:** "Mtu anayechukua uhuru wa mtu mwingine ni mfungwa wa chuki"

**Kifungu cha Kusoma:** Wagalatia 4 - 5:13

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru. Basi simameni imara wala msikubali tena kuwa chini ya nira ya utumwa. (Wagalatia 5:1)


**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini inakupa kipaumbele katika hadithi hii?

Swali la 2. Je, tunasikia nini juu ya uhuru au utumwa katika kifungu hiki? Swali la 3. Je, wewe au mtu mwingine unayemjua, mmeweza kupata tukio kama hilo katika hadithi ya leo?

Swali la 4. Je, tunajifunza nini juu ya kuishi maisha yaliyojazwa na Roho na ni kwa nini jambo hilo ni muhimu?

Swali la 5. Je, ni ukweli gani katika hadithi ambao utashiriki na mtu mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Uhuru wa kweli hupatikana katika utumwa wa Kristo.



| Somo la 04 | KUONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU |
|---|---|
| | **Maandiko:** Wagalatia 5:16-26 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujitia motisha kuona kile inachomaanisha kuishi tukiongozwa na Roho Mtakatifu | "Basi, nasema hivi: mwenendo wenu na uongozwe na Roho, nanyi hamtafuata tena tamaa za dunia." **Wagalatia 5:16** |

## UTANGULIZI

Kila mtu anayekuwa Mkristo anaanza kuona mapambano ndani mwao: tamaa zinaanza kuibuka kutoka kwa moyo ambao haujapeanwa kwa Kristo kamili, na kiu kisichotosha cha kuridhisha mwili, mapambano juu ya kile kinachotolea mioyoni mwetu kwa tendo la Roho Mtakatifu. Wakati Mungu anatufanya upya, tunapambanano na mambo ya ndani ambayo yanaisha wakati tu tunajitoa kwa Mungu na Roho wa Mungu anatujaza. Hii inadhihirishwa kupitia kwa onyesho la tunda la Roho maishani mwetu.

Roho Mtakatifu hutuongoza na kutujaza, lakini tunapaswa kuchagua kumruhusu afanye hivyo. Kwa sababu watu wengine hawajafanya chaguo lao, tunaweza kuona kanisa waumini wa kitambo ambao wanahangaika na maisha yao ya Kikristo na mara kwa mara wanaanguka dhambini tena na tena. Moja ya sababu ni kwamba hajayatoa maisha yao kabisa kwa Kristo, hivyo wanachanganya kazi za Roho Mtakatifu.

### A. Je, Ni Nini Kinapaswa Kusulubiwa? (mistari ya 19-21)

Kanisa la Bwana linapaswa kuwa na watu wanaoenenda kwa Roho na wametubu na kusamehewa mambo yote maishani mwao yasiyompendeza Mungu (kazi au tamaa za mwili). Tunapaswa kufa kwa njia za zamani za maisha. Roho Mtakatifu, kupitia kwa ujumbe wa Biblia, anatufundisha jinsi ya kuishi katika ufalme wa Mungu.

Paulo alisema kwamba wale wanaoendelea kutenda dhambi hawataridhi ufalme wa Mungu (Wagalatia 5:21). Haitoshi kwenda kanisa, kuwa mshiriki wa msimamo mzuri, kutoa zaka, kubatizwa, kuwa kiongozi, n.k. Haya yote ni muhimu, lakini ni lazima tusulubishe mwili, kwa sababu kutenda matendo ya mwili, kwa sababu yatatuzuia kurithi ufalme wa Mungu. Mungu anataka watu waongozwe na Roho Wake na kuishi kwa wingi wa maisha ambao anatupatia. Watu wanaoasi mapenzi yake, wasiomweka Mungu kwanza, watalipia matokeo yake.

### B. Sulubisha Mwili.

**Hapa kuna baadhi ya mapendekezo ya vitu ambavyo tunaweza kufanya ili kupata ushindi:**

1. Tafuata kuwa na ujuzi wa kweli na Roho Mtakatifu.
2. Ishi kila siku katika ukamilifu ambao anatoa.
3. Mpe Mungu tamaa za ubinafsi kwakati wa maombi ya binafsi.
4. Epuka sehemu, watu, na hali ambazo zinaweza kukujaribu kuanguka au kurudi nyuma.

Watu kanisani mwetu wanahitaji kumjua Mungu binafsi na kuwa na ujuzi naye ambao unaadhiri maisha yao. Hii ndio njia peke yake hatua ya mabadiliko katika mfano wa Kristo yanaweza kutendeka.

### I. Je, ni hatua gani zinazoweza kutendeka kulubisha mwili. Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22-26)

Dhihirisho la tuna la Roho katika maisha ya mtu ni onyesho linaloonekana la uwepo wa Mungu katika maisha ya mwumini. Katika makanisa mengi leo, watu hutafuta ujuzi wa kiasili, ibada iliyo hai, kunena kwa lugha, ujuzi wa urofiki, na mengine mengo. Hata hivyo, matukio hayabadilishi moyo wa mwanadamu, na watu wengi wanaendelea kuishi bila kubadilishwa. Lengo kuu ni kwa Kristo kuishi ndani mwetu. Paulo alisema: *"Bali tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu upole na kiasi. Hakuna sheria inayoweza kupinga mambo hayo"* (mistari ya 22-23).

Wakati tumepata ukamilifu wa Roho Mtakatifu,

tunadhihirisha tunda lililotajwa katika Wagalatia 5:22-23 maishani mwetu.

**1. Upendo:** Upendo unaoonyeshwa katika neno hili ni upendo wa '*agape'*. Neno hili la Kigiriki linatumiwa sana katika Agano Jipya na linamaanisha yafuatayo: upendo wa ulimwengu usio na vipimo ambao unapita na kudumu licha ya mazingira. Upendo wa agape utatafuta mema kila wakati. Kwa upendo wa agape, hatupendi tu *'kwa sababu ya'*, bali *'licha ya.'* Mungu anawataka waumini wapende kwa upendo wa agape. Tukiwa tumejazwa na Roho Mtakatifu, maisha yetu yataonnyesha upendo upendo kwa Mungu na wale walio karibu nasi. Acha upendo uwe ndio unaotofautisha maisha yetu kama waumini! (1 Wakorintho 13:1-2)

**2. Furaha:** Neno la Kigiriki linamaanisha furaha ile inakuja kutoka kwa kile muumini anapata kiroho (Warumi 14:17). Furaha ya kweli inapatikana kwa Mungu, na haipatikani kwa mazingira ya maisha. Muumini anaweza kuwa na wakati mgumu, na bado awe na furaha. Furaha hii inahusiana nautimilifu wa kusudi la Mungu katika maisha yetu. Wakati hayo yanatendeka, Roho Mtakatifu anatufanya tuwe na furaha. Mfano wazi ni Yesu: *"Kwa ajili ya furaha iliyokuwa inamngojea, yeye alivumilia kifo msalabani"* (Waebrania 12:2b).

**3. Amani:** Mara nyingi katika Agano Jipya neno la Kigiriki '*eirene'* linaambatana na neno la Kihebrania '*shalom'* na halimaanishi huru tu kutoka kwa matatizo, bali kila kinachofanya maisha kuwa mazuri. Amani ni utulvu wa moyo unaoibuka kwa kuwa na imani ya kwamba kila kitu ki mikononi mwa Mungu.

**4. Uvumilivu:** Una maana ya kusubiri wakati wa Mungu katika kila sehemu ya maisha yetu. Roho Mtakatifu hutuongoza kuwa watulivu, na kumruhusu Mungu afanye kazi. Tukiwa watulivu, tutajua wakati wa kwenda mbele na wakati wa kusubiri.

**5. Wema:** Wale wanaoongozwa na Roho mara nyingi wana sifa ya wema na upole. Wanawatendea wengine kwa upendo, upole.

**6. Fadhili:** Ni fadhila inayotumika; utayari wa kutenda mema kila wakati, kuwa wengine. Mtu mwema huweka masilahi ya kibinafsi pembeni na anamjali jirani yake. Mfano wa Msamaria mwema unaonyesha wema vizuri sana (Luka 10:25-37). Hapo tunaona Msamaria mwema akijitahidi kumtendea mema mtu bila kuhesabu kama alistahili au hapana. Ni nia ya kutoa inayoendelea.

**7. Uaminifu:** Hali ya kuaminika.

**8. Upole:** Umeunganishwa sana na unyenyekevu, upole ni neema ya roho. Si udhaifu, lakini badala yake ni nguvu inayodhibitiwa. Yesu alitupa mfano mkubwa wa upole au utu wema (Mathayo 11:29). Watu wapole hawana vita na ni wanyenyekevu. Waumini wa vita bado hawajajazwa na Roho. Upole unajaribiwa katika njia tunayotenda kwa ukosoaji. Jibu la kukasirika, au wazo kwamba tunajua mengi kuliko wengine, tutaanguka mtihani. Wakati 'tunda' hili la Roho liko mioyoni mwetu, haijalishi watu wametutendea nini, tutatafuta msamaha na wema wa watu wengine.

**9. Kiasi:** Ni nguvu ambayo Roho wa Mungu ametupatia ili kuthibiti tamaa zetu dhambi na kusema "hapana" kwa mwili wetu. Inatumiwa katika nidhamu ya mwana riadha (1 Wakorintho 9:25) na katika uwanja wa ngono ambao ni tabia ya Kikristo (1 Wakorintho 7:9). Kiasi hutupatia nguvu ya kusema "ndio" kwa Roho na kuangazia mavuno mazuri, yaliyojaa ya tunda la kiroho!

## MASWALI YA ZIADA

- Orodhesha matunda ya Roho.
- Je, matunda ya Roho yanadhihirikaje katika maisha yako.
- Chukua muda kiasi wa kufanya uchambuzi wa binafsi katika hali hii.

## HITIMISHO

Tukisema sisi ni watoto wa Mungu bali tunapambana kila wakati na tamaa za dhambi zinazoelekeza kwa kujikwaa na kurudi nyuma kwa sababu tunataka kuridhisha mwili, ni lazima tutafute kwa haraka kusuluhisha hesabu na Mungu na kumpa utu wetu wote kwa dhati na kabisa. Kwa Mungu, hakuna jambo lisilowezekana! (Luka 1:37). Mkristo aliyejitoa atazaa mavuno ya tuna linalofanana na Kristo katika maisha yao.

**Somo la** 4

## KUONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU

**Lengo la Somo:** Kujifunza jinsi ya kuishi kwa kufuata Roho na tunda la Roho Mtakatifu.

**Methali:** Wale hupanga bile msaada wa Roho lazima wapange tena.

**Kifungu cha Kusoma**: Wagalatia 5:16-26

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Lakini matokeo ya kuongozwa na Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi. Hakuna sheria inayoweza kupinga mambo hayo". Wagalatia 5:22-23


**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini inakupa kipaumbele katika hadithi hii?

Swali la 2. Je, tunasikia nini juu ya uhuru au utumwa katika kifungu hiki? Swali la 3. Je, wewe au mtu mwingine unayemjua, mmeweza kupata tukio kama hilo katika hadithi ya leo?

Swali la 4. Je, tunajifunza nini juu ya kuishi maisha yaliyojazwa na Roho na ni kwa nini jambo hilo ni muhimu?

Swali la 5. Je, ni ukweli gani katika hadithi ambao utashiriki na mtu mwingine wiki hii?

Himizo la Hadithi: Mwenendo wenu na uongozwe na Roho, nanyi hamtafuata tena tama za kidunia.



| Somo la 05 | KUWATENDEA WENGINE WEMA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Wagalatia 6:1-10 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba injili ya Kristo inamaaninisha kuwatendea wengine wema; na kwamba maisha ya ukweli katika Roho hutenda wema kwa upendo. | "Basi, tusichoke kutenda mema, maana tusipolegea tutavuna mavuno kwa wakati wake." **Wagalatia 6:9.** |

## UTANGULIZI

Je, inamaanisha nini kumrejesha mtu aliyeanguka kwenye dhambi au magumu? Je, makanisa yetu hakika yako? Je, ni nini hufanyika tunapogundua kwamba ndugu au dada ana hatia? Je, tunawakosoa au hata kuwafukuza kutoka kwa mkutano? Au tunawarejesha kwa roho ya upendo na upole.

### I. Hali ya Kweli ya Kiroho Hurejesha (Wagalatia 6:1-2)

Mtume Paulo aliwatia chamamoto Wakristo wa Wagalatia kwa suala hili. Je, urejesho inamaanisha nini? Neno 'urejesho' linamaanisha kurudisha kitu katika hali yake ya mwanzo. Uchambuzi wa maana hii unatuelekeza kujiuliza: Je, ni katika makanisa mangapi ambapo suala hili ni la kweli? Inaonekana, makanisa ya Wagalatia walihitaji kukumbushwa kwamba tendo hili ni la kufuatana na roho wa kweli wa Kikristo.

Hata hivyo, injili ya kweli, injili ya neema, haikuwa hivyo. Wakati Roho Mtakatifu anatawala kanisani, hakupaswi kuwa na hali ya kulaumu wale walioanguka, bali badala yake kuwarejesha. Kwa hivyo, wakati mshirika wa kanisa anapatikana akitenda dhambi, wasihukumiwe na kulaumiwa, bali warejeshwe kupitia kupitia hatua sawa ya kuwaelekeza kwa uhusiano mpya uliokamilika na Mungu.

**A. "… Wale Mnaoenenda Katika Roho …" (mstari wa 1b)** Paulo anasema inapaswa kufanywa kwa 'upole' (mstari wa 1c) akimaanisha kulinda, uvumilivu na upendo ambao mrejeshaji anapaswa kuweka katika huduma hii. Hatua hii ya urejesho inahitaji kufanywa kwa upendo, kuweka kando fikira za ukuu ambazo zinaweza kusababisha kukatishwa tamaa au kutakuwa na starehe. Paulo anawaonya wale wanaotafuta kuwarejesha wengine: "Bali fanyei hivyo kwa upole, mkiwa na tahadhari msije nanyi wenyewe mkajaribiwa" (mstari wa 1d). Hakuna mahali pa ubora wa kiroho. Hatuko bora kuliko wengine, na Mungu hajatufanya tuwe waamuzi wao; sisi ni ndugu tu na dada ambao hawajaokolewa kwa kuitii sheria vikamilifu, bali kwa imani katika Kristo.

**B. "Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatimiza" (mstari wa 2a)**

Katika safari hii ya Kikristo, hatuwezi kukana kwamba tunahitaji msaada wa kila mmoja. Tukimwona Mkristo mwenzetu ana makosa, tunapaswa kumrejesha. Wakituona na kosa lolote, tutahitajika pia kurejeshwa kwa upendo. Kwa hivyo, mara nyingi tunahitaji kila mmoja. Hii haimaanishi ya kwamba tutaendelea kutenda dhambi. Hata hivyo, tunapopitia katika matatizo, tunapojaribiwa, tunapaswa kujua kwamba ndugu na dada zetu watatutsaidia; na tukianguka, tutarejeshwa, kama tu tunavyowatendea wengine.

### II. Hali ya Kweli ya Kiroho ni ya Unyenyekevu na ya Kupendeza (Wagalatia 6:3-6)

**A. Tambua Kwamba Bila Kristo, Sisi ni Kitu Bure (mstari wa 3)**

Sisi Wakristo, bila Kristo, ni kitu bure. Kwa hivyo, hatuna haki ya kumlaumu yule anayehitaji na kujuta kwa yale aliyotenda. Badala ya kuwalaumu, tunapaswa kufanya kiinyume na kuwasaidia kuingia katika hatua ya urejesho. Kama tu vile tunavyomhitaji Yesu, ndugu au

dada yetu pia wanamhitaji. Kama tunafikiria tunaweza kushinda kwa nguvu zetu, tunajidanganya sisi wenyewe. Tunaweza tu kushinda dhambi katika nguvu za Roho wa Mungu. Hakuna mtu aliye huru kutokana na kujaribiwa. Kwa haya yote, hatustahili kujidanganya … Sisi sote tunamhitaji Yesu!

**B. "Mwenye kufundishwa neno la Mungu na amshirikishe mwalimu wake riziki zake." (mstari wa 6)**

Tunaweza kuuliza, mstari huu una nini na sisi? Ni muhimu kufikiria mukhtadha wa shukrani.

Mafundisho haya juu ya shukrani yanaweza kutumika katika hali zifuatazo:

1. Kutoka kwa wema wetu kanisani kwa baraka za watumishi wa Bwana wanaofanya kazi kwa kuwahifadhi na kuwarejesha 'kondoo' walioodoka kutoka kwa nyumba ya Bwana.
2. Kushiriki na wengine na kusaidiana kama vile Mungu alivyotuendeleza, na tunaposaidiana kwa raslimali, tunasaidia pia kwa hali ya kiroho.

Kwa hivyo, katika hali ya ukweli wa kiroho wa injili, tunahitaji kushukuru na kushirili mali yetu pia. Hatufai kusahau haya!

**III. Hali ya Kweli ya kiroho Hutenda Wema (Wagalatia 6:7-10)**

A. **"Alichopanda mtu ndicho atakachovuna" (mistari ya 7-8)**

Kifungu hiki kinasimama kama onyo. Ni kweli kwamba hatuokolewi kwa kazi, hata hivyo, ni kweli pia kwamba imani ya kweli itadhihirishwa katika matendo yetu (Yakobo 2:18). Hatuwezi kumdanganya Mungu. Tunachopanda, tutakivuna kwa wakati wake.

**I. Aina Mbili za Kuvuna (mstari wa 8)**

**A. Kupanda katika Ulimwengu kwaweza kuhusisha:**

1.) Kutoshiriki mali zetu, lakini tunajifikiria sisi wenyewe, kuwa wabinafsi (mstari wa 6).

2.) Kukosa kumrejesha ndugu au dada wanapoanguka. Kuamua kukosa kuwasaidia au kuonyesha haja katika kurejeshwa kwao, kuwa watu wa kuhukumu badala ya kuwaongoza katika hatua ya urejesho, kuwageuka, tukiwaacha peke yao.

3.) Kuendelea kutenda dhambi na kukosa kuachana na maovu katika maisha yetu ya binafsi.

**B. Kinyumbe chake, kupanda kwa Roho inamaanisha:**

1.) Kushiriki kwa upendo kile umepokea kutoka kwa Bwana.

2.) Kuachana na maisha ya dhambi na kuishi uketenda yale yanayompendeza Mungu. (Wagalatia 5:22-23).

**II. Aina Mbili Za Mavuno (mstari wa 8)**

- Ukipanda katika mwili, utavuna mabaya. *"Apandaye katika tamaa za kidunia, atavuna humo uharibifu"* (Wagalatia 6:8). Uharibifu huo unamaanisha uharibifu wa mtu mwenyewe, kupoteza kwa wokovu wa binafsi, na mwishowe, kupoteza kwa uzima wa milele.
- Ukivuna katika Roho, utavuna uzima wa milelel! Asante hii ya mavuno ni msingi wa mawazo mazuri ya haki kwa imani, tunachovuna huamuliwa na hali hii. Kwa sababu hii, ni muhimu kusisitiza: *"apandaye Roho, atavuna kutoka kwa Roho uzima wa milele."* (mstari wa 8)

## MASWALI YA ZIADA

- Je, utamweleza Mkristo wa kiroho?
- Kwa maneno yako mwenyewe, eleza maana ya "unyenyekevu."
- Je, kupanda na kuvuna inamaanisha nini katika kifungu hiki cha kibiblia?

## HITIMISHO

Injili ya kweli ya Kristo ni injili ya Roho anayewajaza waumini ili waishi katika upendo mkamilifu. Waumini wanaokaa katika upendo wa Mungu mkamilifu hutenda wema: Kurejesha kwa upole wale walioanguka; kushiriki vile walivyo navyo na wale ambao ni walimu wao na wale wote walio na uwezo wa kufanya hivyo; na kuishi maisha ya utakatifu, yaliyotengwa na dhambi.

**Somo la** 5:

**KUWATENDEA WENGINE MEMA**

**Lengo la Somo**: Kuelewa kwamba injili ya Kristo inamaanisha kuwatendea wengine mema.

**Methali:** Hata kama chakula ni kidogo kiasi gani, tutakishiriki pamoja haijalishi ni nzige moja. Unachotoa, ndicho unakipata mara kumi.

**Kifungu cha Kusoma:** Wagalatia 6:1-10

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Basi tusichoke kutenda mema; maana tusipolegea tunavuna mavuno kwa wakati wake! " Wagalatia 6:9

**Maswali ya Kuuliza:** Swali la 1. Je, ni nini inakupatia kipaumbele katika hadithi hii?


Swali la 2. Je, tunasikia nini juu ya uhuru au utumwa katika kifungu hiki?

Swali la 3. Je, wewe au mtu mwingine unayemjua, mmeweza kupata tukio kama hilo katika hadithi ya leo?

Swali la 4. Je, tunajifunza nini juu ya kuishi maisha yaliyojazwa na Roho na ni kwa nini jambo hilo ni muhimu?

Swali la 5. Je, ni ukweli gani katika hadithi ambao utashiriki na mtu mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Muumini aishiye katika upendo wa Mungu mkamilifu hutenda mema.



| Somo la 06 | WALIOCHAGULIWA KUBARIKIWA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Waefeso 1:3-6 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujua kuhusu na kufurahia baraka za Mungu kwetu kama waumini | "Kabla ya kuumbwa ulimwengu, Mungu alituteua tuwe wake katika kuungana na Kristo ili watakatifu na waelekevu mbele yake." **Waefeso 1:4** |

## UTANGULIZI

Kutembea katika njia ya injili ya Kristo, tunafahamu Mungu ni nani pole pole, na yale aliyo nayo kwa wana na binti wake. Katika somo hili, tutaona kwamba wanadamu wote wamechaguliwa kubarikiwa. Mungu ni kama baba na mama wa upendo ambao huwatengea watoto wao wote urithi fulani, na sheria maalum kwamba ni watoto wao.

### I. Baraka za Mungu (Waefeso 1:3)

Kumbuka kwamba mtumpe Paulo alikuwa Myahudi, Myahudi aliyedai uaminifu kwa Neno la Mungu. Hata hivyo, baada ya kubadilishwa kwake na kuwa Myahudi Mkristo kuanzia wakati huo, kusudi lake lilikuwa kumtukuza Baba wa mbinguni, ambaye katika rehema zake alimchagua kuwa chombo cha baraka kwa Watu wa Mataifa (Matendo ya Mitume 9:15), wakiwemo Waefeso.

A. Je, Wanadamu Wanaweza Kumbariki Mungu?

Kwanza, tutachunguza mstari wa 3: *"Atukuzwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, maana ametubariki kwa kutujalia zawadi zote za kiroho mbinguni."* Papo hapo baada ya kuwasalimia Waefeso, Paulo aliomba maombi ya shukrani na baraka kwa Baba: *"Atukuzwe Mungu na Baba …"* Hebu tutazame ombi hili.

1. Ni kawaida kusoma maelezo ya kitabu cha Zaburi cha aina hii. Zaburi 34:1 inasema: *"Nitamtukuza Mwenyezi-Mungu nyakati zote sitaacha kamwe kuzitamka sifa zake"* (tazama Zaburi 41:13; 96:2;103:1-2).

2. Tunaweza kumbariki Mungu ka kumsifu na kumpa utukufu. Kwa maneno mengine, tunambariki Mungu wakati tunamwabudu. Yale Paulo alitufundisha ni kwamba kazi ya kwanza ya kila Mkristo ni kumwabudu Mungu. Tunahitaji kumpa nafasi ya kwanza katika maisha yetu, tukitambua kwamba bila yeye, hatuna chochote.

B. Baba Wa Bwana Wetu Yesu Kristo

1. Biblia inathibitisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu: "na Roho Mtakatifu akamshukia akiwa na umbo kama la njiwa. Na sauti ikatoka mbinguni: "Wewe ndiwe Mwanangu mpendwa; nimependezwa nawe." (Luka 3:22); Yesu ni sehemu ya Utatu na ni lazima tumwabudu yeye pia (1 Yohana 5:20). Lazima tusisitize juu ya uungu wa Yesu Kristo kwa vile watu wengi wanaokosa kusoma Biblia kwa uangalifu hujipata wanathibitisha maoni kinyume na uungu Wake, au wanakana kuwepo kwa Baba na Mwana kama watu wawili tofauti. Mungu ni Mungu mmoja katika watu watatu.

2. Kwa Wakristo, Kristo ni kiini cha kila kitu tunachofanya. Hii ndio sababu, katika kumsifu Mungu, tunafanya hivyo kwa Utatu wote, haijalishi tunamweleza Baba ana kwa ana, mwana, au Roho Mtakatifu kando, au kwa watu watatu pamoja. Sauti iinuke pakubwa katika kumbariki Mungu wetu mwema kila wakati.

### II. Kuchaguliwa Kuwa Watakatifu Na Waelekevu (Waefeso 1:4)

Mstari wa 4 unasema: *"Kabla ya kuumbwa ulimwengu, Mungu alituteua tuwe wake katika kuungana na Kristo ili watakatifu na waelekevu mbele yake."* Baada ya kumsifu Mungu, Paulo alisema kwamba watoto wa Mungu wamechaguliwa na Kristo, kabla ya msingi wa dunia, waishi maisha matakatifu.

A. Mungu Atawataka Watu Waokoke

Mpango wa Mungu ulivunjwa na uasi wa Adamu na Hawa ulisababisha kifo (Warumi 6:23). Bali mpango wa Mungu wa kwanza haukubadilika. Aliendelea kutafuta njia ambayo mwanadamu hangeendelea kulaumiwa kabisa, bali kuokolewa, ikiwa ni pamoja na kila mtu (2 Petro 3:9). Na tufanye uamuzi wa kumtii na wala si kumkana. Mpango wa

Mungu wa ukombozi hatimaye uliwadia kupitia Yesu Kristo (Luka 3:23-38).

A. Wokovu Ni Kupitia kwa Yesu Kristo

1. Yesu ndiye njia ya pekee (Yohana 14:6). Kabla Kristo, kulikuwa na sheria ya Mungu, kwa wazo kwamba yeyote atakayeitii atakubaliwa na Mungu (Kumbukumbu la Torati 28:23). Lakini ukweli ni kwamba hakuna mtu angeweza kutii sheria ya barua. Kwa hivyo, kazi ya dhabihu ya Kristo ilikuwa muhimu ili tukombolewe na kuwa watoto wa Mungu. (Yohana 3:16).

2. Kipaji cha Mungu cha ukombozi kupitia Mwanawe kilikuwa cha wanadamu WOTE. Hakibagui mtu yeyote (Yohana 3:15-17). Hakuna rangi, tamaduni, au kikundi cha wanadamu, hakuna mwenye dhambi anayetengwa katika kufaidika kwa mpango wa Mungu wa ukombozi. Hakika, umeukubali. Tunamshukuru Mungu kwa baraka zake za ajabu katika Yesu Kristo!

### III. Tumenuiwa na Kupokelewa Kwa Upendo Ili Kumsifu. (Waefeso 1:5-6)

Kifungu cha mwisho tunachoenda kusoma kinasema: *"Mungu alikuwa ameazimia tangu zamani kutuleta kwake kama watoto wake kwa njia ya Yesu Kristo. Ndivyo alivyopenda na kunuia. Basi, tumsifu Mungu kwa sababu ya neema yake tukufu ambayo ametujalia katika Mwanawe mpenzi"* (mistari ya 5-6). Watu wengi husema 'Sisi sote ni wana wa Mungu' lakini hii si kweli. Sisi sote ni viumbe vya Mungu, hiyo ni kweli (Yohana 1:3). Hali ya kuwa wana na mabinti wa Mungu ni kufuata njia ambayo Mungu mwenyewe amepeana kwa ajili ya wokovu: Imani katika Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu (Yohana 1:12).

#### A. "Katika Upendo Alitunuia Sisi..."

1. Katika mukhtadha wa jumla wa kibiblia, Mungu, awanuia wanadamu wote kwa ajili ya mbinguni. Lakini kunuiwa huku ni kwa sheria. Inalingana na kama tunataka kujitoa kwa Mungu na kukubali NJIA PEKEE ya kwenda kwake kupitia Yesu Kristo (Yohana 14:6).

2. Kunuiwa kwa Mungu ni juu ya upendo (Yohana 3:16). Kama hatuna upendo wa Mungu, Kristo hangekuja. Isingelikuwa ni kwa upendo wake, dhabihu yake msalabani pale Kalvary, au kufufuka kwake, hili halingetendeka. Kwa hivyo, isingelikuwa ni kwa upendo wa Mungu, ulimwengu huu haungekuwa na tumamaini. (2 Petro 3:9).

#### B. Tulinuiwa Kuwa Wana Wa Mungu

1. Paulo alitumia kielezo cha 'kupokelewa'. Tunafahamu kwamba familia inaweza kumpokea mtoto aliyezaliwa katika familia ingine. Kwa sababu hii, mchakato wa mahakama uafuatwa. Mara tu mahitaji yote ya kisheria yametimizwa, hakimu anatangaza hayo tangu wakati huo, mtoto ni mtoto wao wa kupokelewa. Kwa hivyo, kwa sisi kufanywa watoto wa Mungu, Kristo alitimiza mahitaji yote ya kisheria. Kwa hivyo tunahitaji kusema: "Ndio, Bwana. Nakubali kwamba umenipokea mimi kama mwanao".

2. Yule anayepokelewa kama mtoto wa Mungu hupokea faida zote ambazo Yesu Kristo anazo. Paulo alisema, sisi warithi pamoja na Kristo (Warumi 8:15-17) Kwanza, tumeokolewa kutoka kwa dhambi, lawama na kifo cha milele. Pili, Mungu ametupokea sisi kama watoto wake na haki zote za Mwanawe, Yesu Kristo. Tatu, anafungua mlango wa maisha mapya mahali ambapo sisi "ni watu tulioteuliwa, makuhani wa mfalme, taifa takatifu…" (1 Petro 2:9).

#### C. Watoto wa Mungu Husmifu Muumba na Mwokozi Wao

Kila mtoto anapendwa na wazazi wake waliomzaa na anawapenda pia. Wanawazungumzia wazazi wao vizuri, na wazazi wao wanajivunia watoto wao. Sisi ambao tumepokelewa kama watoto wa Mungu kupitia upendo mkubwa tunapaswa kumsifu, kumwinua na kumtukuza Baba yetu wa upendo ambaye ametupokea kama watoto wake, kupitia Yesu Kristo.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, tunawezaje kumbariki Mungu?
- Je, unashiriki ujumbe wa wokovu na wengine?


## HITIMISHO

Kama wana na mabinti wa Mungu, tunayo nafasi ya kuwa tumechaguliwa kwa baraka za sasa na za milele za Kristo. Kwa hivyo, kama watoto wa Mungu, tunapaswa kumwabudu Muumbaji wetu kila wakati na kumtumikia katika ulimwengu huu na baadaye tumtumikie milele.

**<u>Somo la</u>** <u>6:</u>

# WALIOCHAGULIWA KUBARIKIWA

**Lengo la Somo:** Kujua na kufurahia baraka za Mungu sisi waumini
**Methali:** Amuabuduye mfalme hufanyika kuwa mfalme.
**Kifungu cha Kusoma:** Waefeso 1:3-6
**Mstari wa kumbukumbu:** "Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika upendo." Waefeso 1:4
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini unakipa kipaumbele katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, hadithi hii inatuelezaje kuhusu maisha mapya katika Kristo?
Swali la 3. Je, Katika hadithi hii, inafaa tuachane na nini, na kuna faida gani kama tutaishi maisha mapya katika Kristo?
Swali la 4. Je, kuna jambo lingine lolote umejifunza katika hadithi hii?
Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli katika hii hadithi na mwingine wiki hii?
**Himizo la Hadithi**: Kuna faida ya kuchaguliwa kwa baraka ambazo zipo na za milele katika Kristo.



| Somo la 07 | UTAJIRI WA KWELI WA MUUMINI |
|---|---|
| | **Maandiko:** Waefeso 1:7-13 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba vipimo vya neema ya Mungu ziko, katika mtu wa Yesu Kristo. | "Nanyi pia watu wa mataifa mengine, mliusikia ujumbe wa kweli yaani Habari Njema iliyowaletea wokovu, mkimwamini Kristo; naye Mungu, ili kuonesha kuwa nyinyi ni wake, akawapiga mhuri kwa kuwapeni yule Roho Mtakatifu alietuahidia…" **Waefeso 1:13**. |

## UTANGULIZI

Wokovu ndicho kiini muhimu katika Biblia nzima. Karibu na mafundisho yaya, hali yetu kama wanadamu tunaotii inaelezwa, ambayo ilisababisha kifo katika vipimo vyote. Biblia pia inatuonyesha baraka za Mungu wa upendo na mwenye rehema ambaye ametukomboa katika jitihada yake ya kurejesha hali ya mwanzo ambayo tuliumbiwa. Wokovu wetu kisha unakuwa kiini muhimu cha ujumbe tunaokiri kama Kanisa la Yesu Kristo. Kanisa linahitaji kuwa wazi juu ya vipengele na hatua zilizo sehemu ya wokovu ambao Mungu anawapwa wanadamu.

Katika darasa hili, tutasoma Waefeso 1:7-13, ambapo mtume Paulo alitaja baadhi ya faida Yesu Kristo anatuletea kupitia dhabihu yake kwa kuyatoa maisha yake msalabani kama gharama ya ukombozi wetu.

**I. Je, Ukombozi Una Maana Gani? (Waefeso 1:7-8)** Neno "ukombozi" linasisitiza matokeo ya tendo la kuwekwa huru ambalo Bwana wetu Yesu alifanya. Ukombozi wetu ni ujuzi wa kweli, uliotolewa kwa ajili yetu kupitia kumwagwa kwa damu yake takatifu. Pia, neno ukombozi, kama kupokelewa, ni neno la kisheria na linamaanisha kipengele cha nje cha wokovu wetu. Yesu alitimiza mahitaji yaliyohitajika ya kutuweka huru.

Katika Agano Jipya, ukombozi unamaanisha kuondolewa kwa dhambi na kuwekwa huru kutoka utumwani. Katika Mambo ya Walawi 25:47-52, tunasoma jinsi mtumwa angekombolewa na kupata uhuru wake. Wana wa Israeli waliwekwa huru na kukombolewa kutoka kwa utumwa wa Misri kwa matendo makuu ya Mungu. Katika ukombozi, mtu anawekwa huru kutoka kwa hali ambayo hawangeweza kujiweka huru wenyewe, au kutoka kwa deni ambayo hawangeweza kulipa peke yao.

A. Ukombozi Hutaka Kumwagwa kwa Damu

Tumekombolewa kwa tendo la uhuru la Yesu Kristo aliyemwaga damu yake msalabani. Inamaanisha yale Yesu alitenda, na matokeo ya matendo yake. Katika karne ya kwanza, akimaanisha damu ya Yesu ilikuwa njia muhimu ya kuzungumza juu ya kifo chake. Kifo chake kinaonyesha ukweli mbili za ajabu: Ukombozi na msamaha.

Ukombozi ulikuwa gharama iliyolipwa ili kupata uhuru kutoka kwa utumwa (Mambo ya Walawi 25:47-54). Kupitia kifo chake, Yesu alilipa gharama ya kutuweka huru kutoka kwa utumwa wa dhambi. Gharama hii ilikuwa damu yake. Katika Agano Jipya, damu ni ishara ya kibiblia inayowakilisha kifo cha Yesu msalabani.

B. Ukombozi Uhitaji Msamahani

Msamaha ulihakikishiwa katika Agano la Kale kwa misingi ya damu ya wanyama (Mambo ya Walawi 17:11). Sasa, tunapokea msamaha kwa misingi ya kumwagwa kwa damu ya Yesu kwa sababu alikufa kwa ajili yetu na ilikuwa dhabihu kamilifu nay a kweli. Yaani, katika Yesu, waumini wote wana ukombozi kupitia kifo chake msalabani. Ukombozi ni wetu kupitia kifo cha Kristo. Katika Waefeso 1:7, maelezo ya *"msamaha wa dhambi"* yanakaribiana na wazo la ukombozi wetu, lakini, ni mukhtadha unaofanana.

C. Ukombozi Unahitaji Neema

Neema ni kibali cha hiari na upendo iliyotolewa na Mungu kwa wote. Hatuwezi kuipata, hatuistahili, na hakuna jitihada ya maadili au dini inayoweza kuipata. Wokovu huja tu kwa rehema na upendo wa Mungu. Bila neema ya uungu, hakuna mtu anayeweza kuokolewa. Ili kuipokea, ni lazima tutambue kwamba hatuwezi kujiokoa wenyewe, bali ni Mungu peke yake anayeweza kufanya hivyo, na kuna njia moja tu, kupitia imani katika Kristo (Waefeso 2:8-9).

**II. Tunayo Maarifa ya Kiroho (Waefeso 1:8-10)**

Neema hii ya uungu *"…aliyotukirimia sisi. Kwa hekima na ujuzi wake wote"* (mstari wa 8). Paulo alijaribu kuwasilisha maana mwafaka ambayo kwayo Mungu ametupatia hekima na ujuzi ulio hai wa sisi kuishi maisha ya haki kulingana na kusudi lake. Hivyo, maelezo 'kukirimiwa' inaonyesha kupindukia. Matokeo ya utendaji kazi wa neema yake ya kimungu hutusaidia kuelewa njia zake na kuelewa mapenzi yake kwa maisha yetu pia, kama kufungua mawazo yetu kujua kitu juu ya makusudi yake kwa ulimwengu huu. Paulo alidokeza kwamba chanzo cha hekima na uelewa huu sio wa kibinadamu bali ni wa kiungu.

**III. Tunao Urithi (Waefeso 1:11)**

Tayari tumejifunza kwamba katika Kristo, tumepata ukombozi wa ajabu, na kwamba katika Yeye, Mungu amefunua mpango wake wa wokovu kwa mwanadamu. Kupitia dhabihu ya Kristo, tunapokea baraka zifuatazo:

A. Urithi Kama Watoto Waliopokelewa (mstari wa 5)

Wazo hili linapatikana tu katika Agano Jipya, na linamaanisha kwamba tumechaguliwa kama urithi au sehemu yake, na limetokana na dhana iliyowasilishwa katika Agano la Kale (Kumbukumbu la Torati 9:29; 32:9-10; Zaburi 16:6) kuhusu makabila ya Isrfaeli yaliyochaguliwa na Mungu kuwa watu Wake.

Kama watoto waliopokelewa, tunarithi kila kitu ambacho Baba anacho juu yetu. Urithi huu unatuletea baraka nyingi na uliwezeshwa kupitia Kristo. Chanzo na matendo yake ni vya Mungu peke yake.

B. Urithi Wetu ni Kwa sababu Tulichaguliwa (mstari wa 11)

Urithi huu (sehemu) umefafanuliwa na kuamuliwa mbeleni, na tumechaguliwa kama wapokezi wake. Mipaka na sheria zake imeamuliwa katika eneo la mbinguni kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Wale wanaoitika watafurahia urithi huu, na tayari wamechagulia na Mungu, ingawa sasa ni kwa muda tu hadi mpango wa uungu umetambuliwa kabisa wakati Kristo atakuja katika utimilivu wake wa hakika wa wakati huo. Maelezo "Katika yeye" katika mwanzo wa mstari wa 11 yanaeleza yale yaliyo katika mstari wote. Si kwamba Mungu amechagua watu fulani kiholela kwa wokovu, bali kwamba Kristo ndiye aliyechaguliwa, na wale wanaompokea kama Mwokozi wao wanamtii na kumtumikia, na pia wamechaguliwa na Mungu katika Yeye. Paulo anatukabili na ukweli wa urithi ambao hatuwezi kufikiria itakuwaje itakapofunuliwa kwa ukamilifu, lakini pia alitutia moyo kufurahia kutoka sasa faida ambazo zinajumuishwa katika uwepo wa Roho Mtakatifu ndani yetu, kama warithi wa Baba yetu wa mbinguni.

Hatimaye kama watu wa Mungu, ni lazima tutangaze habari njema kwa wote. Kanisa liliamriwa kutangaza ujumbe wa ukombozi huu kwa neema ya Mungu kwa kila mtu.

## MASWALI YA ZIADA

- Fafanua ukombozi.
- Fafanua Neema
- Taja baraka mbili ambazo ni sehemu ya urithi wetu kama watoto wa Mungu, na kile unachoona katika maisha haya.

## HITIMISHO

Ingawa ni vigumu kupima ukubwa na kina cha wokovu ambao Mungu alitupatia katika Kristo, tunapaswa kuwa na shukrani kwa yale yote Bwana alifanya kwa kutuokoa kutoka kwa utumwa ambao ulituweka katika dhambo. Kwa upande mwingine, tunapaswa kufurahia wokovu huu ambao ulitupatia uhuru kutoka kwa kile kilitufunga na kutafuta kutenda mema na kuwapenda wengine kwa upendo huo ambao Mungu alitupenda, anatupenda sasa na atatupenda kila wakati.

**Somo la** 7:

## UTAJIRI WA KWELI WA MUUMINI


**Lengo la Somo:** Kuelewa ya Kwamba Biblia inasema tuheshimu uwepo wa Mungu
**Methali:** Utajiri wa kawaida unaweza kuibiwa, utajiri halisi hauwezi.

**Kifungu cha kusoma:** Waefeso 1:7-13

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Nanyi pia watu wa mataifa mengine mliousikia ujumbe wa kweli yaani habari njema iliyowaletea wokovu mkamwamini Kristo, naye Mungu ili kuonyesha kuwa nyinyi ni wake akawapiga mhuri kwa kuwapeni yule Roho Mtakatifu alivyotuahidia." Waefeso 1:13.

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, unapatia nini kipaumbele katika hadithi hii?
Swali la 2. Je hadithi hii inatuelezaje kuhusu maisha mapya katika Kristo?
Swali la 3. Je, katika hadithi hii, inafaa tuachane na nini, na kuna faida gani kama tataishi maisha mapya katika Kristo?
Swali la 4. Je, kuna jambo lingine lo lote umejifunza katika hadith hii? Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli katika hii hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Yeyote anayeamini utajiri wake ataanguka, amini Kristo badala yake.



| Somo la 08 | KUKUA KATIKA MAARIFA YA MUNGU |
|---|---|
| | **Maandiko:** Waefeso 1:17-23 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kukua katika maarifa ya Mungu | “Ili Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba mtukufu, awajalieni Roho wake atakayewapa hekima na kuwafunulieni Mungu mpate kujua.” **Waefeso 1:17** |

## UTANGULIZI

Moja ya sababu Mtume Paulo aliandika waraka huu ilikuwa ni kueleza kuzudi la Mungu la milele, dhana kuu ya kuelewa katika barua hii. Huu ni ukweli sio tu kwa waumini wa mji wa Efeso, lakini pia kwa jamii yote ya Kikristo ya wakati wake, kwa kuwa walikuwa katika hatua ya malezi. Katika muda huu, misingi ya imani ya Kikristo ilikuwa inasimamishwa. Katika siku zetu, changamoto ambazo waumini wanapitia pia zinahitaji kwamba tuweke imani yetu juu ya misingi iliyo imara ambayo itatusaidia kuimarisha imani yetu ili tukue katika imani zaidi na zaidi.

Baada ya kupokea habari za kanisa katika Efeso, mtume alihamasishwa kuomba. Maombi ambayo, kando na kuwa orodha ya maombi ya kuridhisha baadhi ya mahitaji ya mwili ya Waefeso, aliangazia katika kuuliza kile alifikiria muhimu kwa kuzuia Waefeso kutoka kwa kusudi la Mungu kwa maisha yao. Kwa kuongezea, aliuliza kwamba Bwana atawawezesha kumjua kwa undani zaidi. Katika maombi, alisisitiza kile kilikuwa muhimu, cha milele, na ambayo ingeunganisha misingi ya imani yao, ikiwapa nguvu ya kuishi kulingana na injili kikamilifu.

### I. Mwito wa Kipekee (Waefeso 1:17-19)

Katika mistari hii, Paulo alianza kueleza sababu za maombi yake kwa waumini, kwanza akimweleza Mungu kama Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo na Baba wa utukufu. Mtume alitambua kwamba ni Yesu Kristo anayeonyesha njia ya kwenda kwa Baba, aliyemtukuza, na kuwapa wanadamu nafasi ya kuweza kupatanishwa naye na kufurahia maisha mapya yaliyojaa imani na tumaini ndani ya Mwokozi wetu. Kwa hivyo, umuhimu wa kuwa na roho ya hekima na ufunuo. Katika kifungu hiki, tunaweza kuelewa kupitia ‘roho ya hekima na ufunuo” (mstari wa 17) uwezo wa kutambua kile kilichofunuliwa kwetu, kwa kuelewa mwelekeo na maana ya kile Mungu anataka sisi tujue. Watu wengi wanafahamu juu ya Mungu, na wengine hata wanasema wanamwamini, lakini matendo yao yako mbali na kuangazia madai haya. Wanajua uwepo wake na kukubali kwamba yeye ni wa kweli, lakini hawamjui kwa sababu hawajamuona katika maisha yake. Kwa hivyo, ujuzi wao ni wa nadharia tu au wa kitaaluma.

Kwa wanafunzi wa Kristo, kumjua Mungu inamaanisha kumtambua kama chanzo cha maisha na kweli, kupitia ufunuo wake kupitia Kristo, na kutambua kwamba yeye huangazia akili zetu kwa nguvu ya Roho wake Mtakatifu, akitusaidia kuelewa kweli za ndani za uzima. Kwa Wayahudi, ilikuwa kawaida kuuliza roho wa hekima na na ufunuo. Kwa hivyo, Paulo hakuwaombea tu wapokee ujumbe maalum, lakini kwamba wawe tayari walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu wajifunze kutambua na kumjua Mungu zaidi kwa ndani kama vile alifunuliwa ndani ya Kristo. Vipawa vya Roho Mtakatifu, kama vile hekima, wepesi na ufunuo, vilikuwa vipawa vya kawaida ambavyo Wayahudi wangetarajia.

Tumaini la mwito wa Mungu huturuhusu kukabiliana na machungu ya maisha. Utajiri wa utukufu wake hutuwezesha kufurahia hata wakati hali ni mbaya. Tunaweza kushinda kushushwa moyo wakati tunakumbuka nguvu za Mungu zikidhihirishwa katika ufufuo wa Kristo, Bwana na Mwokozi wetu.

### II. Nguvu Isiyo na Mfano (Waefeso 1:20-21)

Katika mistari hii, Paulo alionyesha jinsi nguvu ya Mungu inavyopatanishwa kupitia Kristo kwa Wakristo. Mada kuu ya sehemu hii ya kifungu ni onyesho la Mungu katika Kristo kupitia ufufuo na kuinuliwa kwake. Kuhusu ufufuo wake, ingawa tunatambua kwamba kifo cha Kristo ni dhihirisho kuu la upendo wa Mungu, tunajua pia kwamba ufufuo ni dhihirisho kuu la nguvu zake. Katika Waefeso 3:20, Paulo alipeana maelezo zaidi kuhusu dhana hii akitangaza kwamba nguvu iliyomfufua Yesu ni nguvu inayotenda kazi kwetu; hivyo umuhimu wa ufufuo kwa ujuzi wa Mungu na nguvu zake.

### III. Kanisa la Ushindi (Waefeso 1:22-23)

Kama tu vile Zaburi 110:1 ni mwaliko kutoka kwa Mungu hadi kwa Bwana ili kukaa mkono wake wa kulia hadi atakapowaweka adui zake chini ya miguu yake, Waefeso 1:22-23 inathibisithsa kwamba Mungu tayari ameweka mambo yote chini ya Yesu. Zaburi 8:6 inamwakilisha Adamu kama taji ya uumbaji, na kutawala viumbe kwa kudhibitisha yafuatayo: "Ulimpa madaraka juu ya kazi zako zote; uliviweka viumbe vyote chini ya mamlaka yake." Sasa, Yesu Kristo, Adamu wa pili, amevunja nguvu za kuanguka, na kwa Kazi yake ya Ukombozi, amekuwa Mtawala kama kichwa cha uumbaji mpya. Ili kuelewa kwa undani nguvu za matendo ya kanisa, mtume alitumia taswira mbili, moja ya mwili na ingine ya wingi.

Paulo aliwasilisha kanisa kama mwili ambao ni wa Yesu na umeunganishwa na yeye. Kwa hivyo, Kristo anasimamia kanisa katika mambo yote. Kristo ni kichwa, kwa maana ya kuwa msingi wa uwepo wa kanisa, chanzo chake cha maisha na mtawala (Waefeso 5:24). Kanisa pia ni lengo la kifo cha upatanisho cha Kristo. Kama vile Baba alimtoa Mwanawe kwa ajili ya ulimwengu (Yohana 3:16), Kristo alijitoa kwa ajili ya kanisa (Waefeso 5:25-26).

Kama mwili wa Kristo, kipengele kilicho hai au uinjilisti wa kanisa ni lazima vitiliwe mkazo. Chini ya ishara hii, tunazingatia umoja, ukuaji na aina mbali mbali za huduma ya kanisa. Umoja wa knaisa ni umoja wa Roho.

Dhana hii inapaswa kutusaidia kufanya utofauti katika kujitoa kwetu kwa Kikristo kama sehemu ya jamii ya imani ambayo tunahudumia. Sisi ni mwili wa Kristo, sio tu wakati tunakutana katika ibada ya kuabudu, bali pia katika kila sehemu ya maisha yetu, kama vile nyumbani kwetu, katika uhusiano wetu na watu wa familia na majirani, jamii yetu, n.k. Hata kama mara nyingi mambo hayatendeki kama vile tulivyotarajia, bado tunaendelea kuwa mwili wa Krist, ushindi wa kanisa ambao, utiifu kwake anayeisimamia, akihubiri na nguvu kupitia ushahidi na huduma.

Mstari wa 23 unasema kwamba Yesu ni: "…ukamilifu wa yule anayejaza vitu vyote katika kila njia." Dhana ya kujaza ni pamoja na jukumu la kuleta vitu vyote pamoja na maelewano katika Kristo, ambaye ni kichwa. Paulo aliomba kwamba waumini waelewe kwamba nguvu inayotenda kazi kanisani pia itazaa ulimwengu mpya wenye usawa na umoja chini ya Kristo. Kwa hivyo, umoja kati ya Kristo na kanisa ni kionjo cha mwisho huo.

Kama kanisa, tunayo nafasi ya kipekee ya kuishi kwa ukamilifu, na katika kila jambo tunalofanya, tuwe kanisa la ushindi ambalo Kristo ni kichwa. Kama matarajio ya yale yanayokuja, leo jamii zetu za imani zinaweza kuhisi upendo, msamaha na rehema, na hii, si kwa waumini pekee, bali pia katika jamii ambayo tuko ndani, kuangazia hata maeneno yenye giza kabisa ambapo dhambi imefunika mapenzi ya watu. Ni lazima waumini ambao, siku kwa siku, waishi pamoja na hali ya giza, waking'aa na imani yao na matendo mema, wakiruhusu ulimwengu kumjua Kristo kupitia kwao. Wakati Yesu alizuru vijiji na miji, watu waliathiriwa na nguvu zake. Leo, kanisa letu ni lazima litembee kwa ushindi na injili ambayo inabadilisha maisha, katika nguvu zilizomfufua Kristo.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni nini dhihirisho kwamba nguvu za Mungu zinatenda kazi kwetu?
- Je, inamaanisha nini kumjua Mungu kwa undani?
- Je, inamaanisha nini kwamba kanisa ni mwili wa Kristo?

## HITIMISHO

Leo, tunaweza kukua katika maarifa ya Mungu! Ili kufanya hivi, tunapaswa kufahamu yule aliyetuita, kuelewa na kujua mwito, na kujua sisi ni nani na ni wapi tunaenda.
Pili, tunapaswa kuweka kwa mawazo kwamba nguvu ile ile iliyomuinua Kristo kutoka kwa wafu sasa inatenda kazi kwetu.
Na mwishowe, fahamu kwamba kama mwili wa Kristo, tunaleta nuru kwa ulimwengu huu kila mahali tunaenda kupitia ushahidi na utumishi wetu.

**Somo la** 8:

# KUKUA KATIKA MAARIFA YA MUNGU

**Lengo la somo:** Kukua katika maarifa ya Mungu.

**Methali:** Maarifa bila hekima ni kama maji kwa mchanga.

**Kifungu cha kusoma:** Waefeso 1:17-23

**Mstari wa kumbukumbu:** "Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima nay a ufunuo katika kumjua yeye" **Waefeso 1:17**

**Maswali ya Kujadili:**

Swali la 1. Je, unapatia nini kipaumbele katika hadithi hii?

Swali la 2. Je, hadithi hii inatuelezaje kuhusu maisha mapya katika Kristo?

Swali la 3. Je, Katika hadithi hii, inafaa tuachane na nini, na kuna faida gani kama tutaishi maisha mapya katika Kristo?

Swali la 4. Je, kuna jambo lingine lo lote umejifunza katika hadithi hii?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli katika hii hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Maarifa bila matendo haifaidi yeyote



| Somo la 09 | KUOKOLEWA KWA IMANI ILI KUTENDA MEMA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Waefeso 2:1-10 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuchukua mtazamo mzuri juu ya mafundisho ya wokovu katika Kristo, jinsi ya kuhifadhi, na umuhimu wa kutenda mema. | "Sisi ni viumbe vyake Mungu, na kwa kuungana na Kristo Yesu, alituumba kwa ajili ya kuishi maisha ya matendo mema aliyotutayarishia tuyatende." **Waefeso 2:10** |

## UTANGULIZI

*"Wokovu si mpango wa dakika ya mwisho, ni dhihirisho la mapema la upendo wa Mungu"* (Cleverdon, Frederick T., Encyclopedia of Moral and Religious Quotations, pg. 391).

Ni moyo tu ambao umehisi upendo wa Mungu ambao unaweza kushukuru upendo mkuu wa Mungu uliodhihirishwa kamili (Waefeso 2:4) kutuokoa kutoka kwa lawama ya hatari na ya milele. Wacha tuangalie kwa jicho la bidii na moyo wa kushukuru juu ya kifungu hiki cha thamani Waefeso 2:1-10.

### I. Wokovu Kutoka kwa Maisha ya Dhambi (Waefeso 2:1-3)

Wakati mtu anaokolewa kutoka kwa kijito kinachokimblia na mtu anayempenda, haiepukiki kwamba mtu aliyeokolewa anasifu na kushukuru muokoaji wake na kila wakati atamkumbuka. Wale ambao tumeokolewa kutoka kwa hali ya kifo cha kiroho na lawama ya dhambi zetu hatuna maneno ya kutosha ya kusifu, kupenda, na zaidi, shukrani kwa Mungu ambaye ametuokoa. Tumshukuru Mungu kila wakati kwa upendo wake Mkuu kwetu ambapo ametuokoa kutoka kwa kifo cha kiroho na cha milele.

A. "Ninyi Mlikuwa Mmekufa Kwa Sababu Ya Makosa Na Dhambi Zenu" (mstari wa 1)

Mtume Paulo aliwakumbusha Waefeso kwamba maisha yao katika Kristo yalikuwa matokeo ya kitendo kikubwa sana. Kabla hawajamjua Kristo, (pamoja na kila mtu aliye bila Kristo leo), walikuwa wamekufa kiroho. Kifo, katika mawazo ya kibiblia, inamaanisha utengano. Maandiko yanazungumzia aina tatu ya kifo:

1. Kifo cha mwili, ambacho ni kutenganishwa kwa mali na kiroho au roho ya mtu. Sisi sote tutapitia kifo hiki;
2. Kifo cha kiroho, ambapo ni kutenganishwa kwa mtu kutoka kwa Mungu kwa sababu hawajayatoa maisha yao kwake. Kila mtu aliye bila Kristo yuko katika kundi hili, bali wanaweza kuchagua maisha na mwishowe,
3. Kuna kifo cha milele, ambacho ni utengano wa milele wa Mungu au hali ya wale wanaokataa wokovu wa milele tunaopewa na Kristo; na hakuna njia ingine.

B. "Wakati Ule Mliishi Kufuatana Na Mtindo Mbaya wa Ulimwengu Huu, Mkawa Mnamtii Mtawala wa Pepo Wenye Nguvu wa Anga," (mstari wa 2)

Katika ulimwengu wa kiroho, kuna falme mbili peke yake: ufalme wa Mungu na ufalme wa Shetani. Kwa hivyo, sisi ni wa ufalme wa Mungu au wa ufalme wa Shetani. Watu wanaofikiria kwamba wako huru katika kila njia kwa sababu hawako chini ya mchungaji, ya kanisa au dhehebu, au hata kwa Mungu, wanaonyesha tu kwamba ni watiifu kwa mfalme wa nguvu ya anga, na giza.

1. Waliishi katika tamaa za mwili wao, kwa tamaa ambazo zilitawala mapenzi yao. Waliishi katika mapenzi ya mwili, kwa maneno mengine, hawako tayari kujitoa kwa mapenzi ya Mungu.
2. Walifanya walichotaka, na mawazo yao yaliendelea kuwa upande wa uovu, kinyume na mapenzi matakatifu ya Mungu; na walikuwa watoto wa hasira, kama wengine.

### II. Wokovu wa Mbinguni Kupitia Upendo wa Mungu (Waefeso 2:4-7)

Ingawa wengi wanakataa, wanadamu wana tamaa maalum ya

mbinguni. Hata hivyo, wanaieleza kwa njia ya kiburi au kupuuza. Mungu, anayejua tamaa ya ndani ya wanadamu, ameturidhisha kwa tamaa hiyo kupitia Mwanawe, Yesu Kristo. Na matoleo hayo ni ya kila mtu.

A. "Mungu ni Mwenye Huruma Nyingi" (mstari wa 4)

Upendo wa Mungu hauna kipimo. Wanadamu, kwa bidii nyingi, wanajaribu kupima ukubwa wa ulimwengu, lakini haijalishi tunajaribu kiasi gani, hatuwezi kupima upendo wa Mungu. Kwa sababu ya upendo huu, anaonyesha rehema kwa wote, bila ubaguzi (Yohana 3:16). Kila siku inayopita ulimwenguni, tunapoona habari, tunasikia uhalifu kwa watoto, mama, baba, n.k. Ukatili mwingine ni mbaya sana, uhalifu wa kinyama ambao kibinadamu hauna msamaha, lakini upendo wa Mungu unafikia bila kueleweka kwa wote pamoja na wale wauaji wote, wanajisi, wezi, wanyonyaji, n.k. Upendo wa Mungu ni wa utajiri.

B. "Alitufanya Hai Pamoja Na Kristo" (mistari ya 5-6)

Hapa taarifa iliyotolewa katika mstari wa 1 imesisitizwa. Mungu alitupa uzima licha ya kuwa tumekufa katika dhambi. Uzima huo umepewa kwetu kupitia Yesu Kristo, na kama tu vile Kristo aliinuliwa kutoka kwa wafu, sisi tunaomwamini pia tumefufuliwa kutoka kwa mauti ya kiroho, na siku moja tutaketi sehemu za mbinguni pamoja na Yesu Kristo. Hii inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba kwa kuwa tumemwamini Kristo na kuwa na maisha mapya katika Yeye, tunaelekea kwenye ukumbi wa nchi ya mbinguni. Hii ni nzuri! Tunafurahia uhusiano maalum na Mungu, tunaishi katika uwepo wake, tunahakikishiwa uwepo wake, tunajua kwamba Kristo ni mwenzi wetu mwaminifu na thabiti, na Roho Mtakatifu anatuongoza kila siku katika kila jambo.

### III. Wokovu kwa Imani Bali Kwa Matendo Mema (Waefeso 2:8-10)

A. Kuokolewa kwa Neema, Kupitia Imani (mstari wa 8)

Binadamu wameokoloewa kwa kipawa cha Mungu cha neema katika Kristo Yesu. Kama vile Yohana 3:16 inasema: *"Kwa maani jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili yeyote amwaminiye asipotee bali apokee uzima wa milele."* Hiyo ni neema, kupokea kila kitu bure, lakini tunapaswa kufahamu kwamba neema hii ilimgharimu Yesu maisha yake Msalabani!

Tumeokolewa 'kwa imani'. Hatujaokolewa kwa sababu tulilipa kitu kwa ajili ya wokovu wetu. Hata hivyo, Mungu anatarajia kwamba tufanye jambo ili kupokea huo wokovu: kwamba tuweke imani yetu katika Kristo. Imani ni kuamini, kutumaini. Kama mtu haamini na kuweka imani yao katika Kristo, zawadi ya Mungu haina athari. Ni kama vile mtu anapogonjeka, na familia inamleta daktari anayeeleza tembe zitakazotumiwa, bali mgonjwa anakataa daktari na kukataa kutumia tembe, haitakuwa na athari. Hivi ndivyo ilivyo na wokovu wetu.

B. "Wala Halitokani na Matendo Yenu Wenyewe, Asije Mtu Akajivunia Kitu" (mstari wa 9)

Tunajiuliza: "na je, wale wanaosema kwamba ni lazima tufanya kazi ili kujiokoa? Lakini mistari hii iko wazi. Ukweli ni kwamba wengi hawajitoi kwa Neno la Mungu, bali himizo la imani za viongozi wao. Paulo alisema wazi kwamba wokovu ni bure na si kwa sababu ya chochote ambacho tumefanya. Hatuwezi kupata wokovu kwa matendo yetu mema. Kama ingekuwa hivyo, watu wangeishi wakijivuna kwa matendo yao yakiwa yanastahili wokovu. Au wangekuwa na haja ya kujua kama wanachofanya kinatosha kupata wokovu. Wokovu ambao Kristo anapeana si kwa kazi, bali kwa kutegemea sifa za kafara za Kristo msalabani, na kwa upendo wa kina wa Mungu ambaye anatupatia wokovu kupitia Mwanawe Mpendwa.

## MASWALI YA ZIADA

- Eleza maana ya maelezo "kufa kwa uasi na dhambi".
- Je, unatarajia Mungu akuonyeshe nini katika maisha ya baadaye?
- Je, ni kwa nini Mungu haruhusu wokovu wa vitendo?

## HITIMISHO

Kwa sababu ya upendo wake mkuu, Mungu alitupatia uzima katika Kristo Yesu kwa neema, kupitia imani. Kwa kutupatia uzima, Ametuhamisha kwa mwelekeo mpya, kwa ufalme wa Mungu. Na katika Ufalme huo, lazima tuishi tukifanya kazi ambazo Mungu ametuandalia sisi kumheshimu Yeye na kushuhudia kwa nguvu kazi Yake ndani mwetu na kwa wanadamu wote.

**Somo la** 9:

## KUOKOLEWA KWA IMANI ILI KUTENDA MEMA

**Lengo la somo:** Kuelewa wokovu ndani ya Kristo, uvumilivu na kutenda mema.


**Methali:** Tendo nzuri ni kitu cha mtu kurejesha

**Kifungu cha Kusoma:** Waefeso 2:1-10

**Mstari wa kumbukumbu:** "Sisi ni viumbe vyake Mungu. Na kwa kuungana na Kristo Yesu alituumba kwa ajili ya kuishi maisha ya matendo mema aliyotutayarisha tuyatende." Waefeso 2:10

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, unapatia nini kipaumbele katika hadithi hii?
Swali la 2. Je hadithi hii inatuelezaje kuhusu maisha mapya katika Kristo?
Swali la 3. Je, katika hadithi hii, inafaa tuachane na nini, na kuna faida gani kama tataishi maisha mapya katika Kristo?
Swali la 4. Je, kuna jambo lingine lo lote umejifunza katika hadithi hii? Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli katika hii hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Mungu aliniumba nifanye mapenzi yake, na nitafanya!



| Somo la 10 | UPENDO WA MUNGU ULIO BORA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Waefeso 3:14-19 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa maombi ya Mtume Paulo na kuifanya kuwa sehemu ya maisha yetu | "… mpate kujua upendo wa Kristo upitao elimu yote, mjazwe kabisa utimilifu wote wa Mungu.." **Waefeso 3:19** |

## UTANGULIZI

Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

- Je, upendo ni nini?
- Je, tutajuaje kwamba mtu anatupenda?
- Je, tutawapendaje wengine?

Katika barua hii, mtume Paulo anamwelezea Mungu maombi mbili kwa Waefeso. Katika ombi la kwanza (Waefeso 1:16- 23), anaomba kwamba waelewe kwa undani ukuu wa Mungu, na katika ombi la pili (Waefeso 3:14-19) ombi lilikuwa kwao kupokea nguvu ambazo zingewaelekeza kwa ujuzi wa ndani wa Mungu, na kwa sababu hiyo, waweze kuona kwa ukamilifu nafasi za kiroho ambazo Mungu anazo kwa ajili yao. Mtazamo wa somo hili utakuwa kwa ombi la mbili.

### I. Kujaliwa Nguvu ya Kuwa Imara ndani yenu (Waefeso 3:16)

#### A. Je, Mtu wa Ndani ni Nani?

Mada ya mtu wa ndani inamaanisha vipengele vinavyojumlisha asili ya mwanadamu. Ili kuweleza asili ya mwanadamu, tunaweza kutofautisha kipengele cha kiroho na cha kimwili. Inatosha kujua kwamba mgawo unawakilisha mwanadamu na vipengele viwili tofauti: kimwili (mwili) na isiyo ya maana (kiroho).

Hata hivyo, kwa ajili ya somo hili, inatosha kujua kwamba tumeumbwa kwa asili mbili: ya kimwili, inayowasiliana na ulimwengu wa mali, na isiyo ya maana, inayotupatia uzima, inaweza kuwasiliana na Mungu na mahali utu wetu upo. Vipengele hivi vya uhai wetu vemeunganishwa na hufanya kazi kama kitengo kimoja. Kwa hivyo, sisi ni watu kamili lakini tuna vipimo tofauti.

#### B. Nguvu Ndani ya Mtu

Katika ombi hili, mtume Paulo anamuomba Mungu kama chanzo cha utajiri wa kiroho na ambaye kusudi lake ni kutia nguvu, kupitia Roho Wake Mtakatifu, viumbe ambavyo ni chombo cha ulinzi wake. Hapa, kipengele 'utajiri' ni neno la Pauline linalotumika kuelezea neema, kibali tusichokistahili kinachotoka kwa Mungu. John Wesley anaeleza kipengele 'utajiri katika utukufu wake' kama ifuatavyo: "Utimilifu mkubwa wa hikima yake tukufu, nguvu na rehema."

#### C. Kazi ya Pili ya Neema

Katika ombi hili, inaonekana Paulo alikuwa anaomba kazi ya pili ya neema ili moyo wa muumini usafishwe na kutiwa nguvu kabisa. Ni katika mzozo huu, wakati mapambano ya ndani ya moyo yamegawanyika kati ya uaminifu wake kwa Baba na ulimwengu huu ulioanguka unakoma, na mtu wa ndani anaanza kufurahia ndani ya Mungu. *"Ndani kabisa katika moyo wangu naifurahia sheria ya Mungu."* (Warumi 7:22)

Uzoefu huu au shida zinaathiri jumla ya mtu katika kiroho, kiakili, kihisia na mambo ya maadili. Kutiwa nguvu huku ndio kunaturuhusu kujisogeza mbele kwa siku zijazo na ujasiri. Kunatuwezesha kuishi maisha ya ushindi, yaani, maisha ambayo tunaweza kushidna minyoror na woga ambao unatufunga na kutulemaza, na hivyo kutuweka huru kabisa: *"Mwana akiwapeni uhuru mtakuwa huru kweli."* (Yohana 8:36)

## I. “Naye Kristo Akae Mioyoni Mwenu…” (Waefeso 3:17)

### A. Uzoefu Wa Kristo Na Roho Mtakatifu

Katika somo hili, tunahitaji kusisitiza kwamba Kristo na Roho Mtakatifu wanafanya kazi kwa wakati mmoja katika maisha ya muumini. Kutiwa nguvu kwa Roho Mtakatifu na kukaa kwa Kristo ndani ya muumini si uzoefu ulio kando. Tunapokuwa na uzoefu wa uwepo wa Roho Mtakatifu. Pia tunapata kuwa na uzoefu wa uwepo wa Kristo. Yaani, mahali Roho wa Mungu yuko, Kristo yuko pia (Mathayo 28:20, Yohana 14:15-20, 2 Wakorintho 13:14).

### B. Maisha Yaliyokita Mzizi Na Msingi katika Upendo

Maisha yaliyokita mzizi na msingi katika upendo ni yale yaliyobarikiwa na kutiwa nguvu kila siku kupitia uhusiano na Kristo. Matoke yanayoonekana ni maisha ya kiroho thabiti na yanayokua kila wakati. Kwa kuzingatia hili, Paulo anatuhimiza tusiwe kama mtu mwenye akili mbili wa Yakobo 1:8. Nabii Yeremia anatueleza: *“Abarikiwe mtu anayemtegemea Mwenyezi-Mungu, mtu ambaye Mwenyezi-Mungu ndiye tegemeo lake. Huyo ni kama mti uliopandwa kando ya maji, upendezao mizizi yake karibu na chemchemi. Hauogopi wakati wa joto ufikapo, majani yake hubaki mabichi. Hauhangaiki katika mwaka wa kame, na hautaacha kuza matunda.”* (Yeremia 17:7-8)

## II. Kufahamu Upendo wa Kristo (Waefeso 3:18-19)

### A. Vipimo Vya Upendo wa Kristo

HIsia ya kuona inatuwezesha kutambua vipimo vinne, upana, urefu, kina na urefu wa vitu na mandhari katika maumbile. Katika mistari hii, mtume Paulo anatumia vipimo hivi kueleza ukubwa wa mandhari nzuri ambayo imewasilishwa mbele yetu tunapotafakari juu ya njia zan Mungu.

Paulo anatualika kuelewa kwamba tafakari hiyo juu ya njia za Mungu haifanyiki kwa kujitenda lakini ni uzoefu unaopandwa katika ushirika na watakatifu wote, wale wanaodai tumaini moja katika Kristo. Kwa hivyo, kujaribu kuishi maisha ya upweke ya kirho ni ngeni kwa uzoefu wa Kikristo. Ikiamua, inapaswa kuwa haijakamilika.

### B. Utimilifu wa Mungu

Kadiri uwezo wetu wa kupokea unakua, Mungu hutujaza tena na tena. Wazo la utimilifu lina maana kwamba tunaweka mawazo yetu, hisia na hiari yetu kwa Mungu katika Kristo. Wesley alitafsiri kwamba maneno *“utimilifu wote wa Mungu”* (mstari wa 19) kumaanisha: “Kwa upendo wake wote, nuru Yake, hekima yake, utakatifu wake, nguvu zake na utukufu wake”

Utimilifu huu haumanishi kwamba tutakuwa na uwezo wa kuwa kama Mungu, au kuwa mungu. Au haumaanishi kwamba tuko bora kuliko wale ambao hawajamjua Mungu. Bali, unatukumbusha kwamba ubinadamu kila wakati unatafuta upendo katika njia ambazo ni za muda tu, na inatuwekwa jukumu kutangaza ujumbe wa upatanisho na tumaini katika Kristo.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, mtu wa ndani ni nani?
- Je, ni mahitaji gani yanayohitajika katika moyo wa mtu ili Kristo akae ndani mwao?
- Je, tunaweza kukuaje katika upendo wa Mungu.

## HITIMISHO


Kama tunataka kukua katika ukomavu wa kiroho, tunahitaji kuwa na ufahamu wa upendo mkamilifu wa Kristo juu yetu. Tukifanya hivi, tutakuwa na uwezo, yaaani, tutapata kile tunachoweza kupata katika Kristo.

**Somo la** 10:

## UPENDO WA MUNGU ULIO BORA

**Lengo la somo:** Kuelewa kuwa maombi ni muhimu na yatupasa kuyafanya sehemu ya maisha yetu
**Methali:** Nyumba anayoishi umpendaye si mbali
**Kifungu cha Kusoma:** Waefeso 3:14-20
**Mstari wa Kumbukumbu:** Upendo wa Kristo ni Zaidi ya mtu yeyoye kuufahamu. Lakini ninaomba kwamba mkaweze kuufahamu upendo huo. Kisha mkajazwe na utimilifu wa Mungu Waefeso 3:19
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, unapatia nini kipaumbele katika hadithi hii?
Swali la 2. Je hadithi hii inatuelezaje kuhusu maisha mapya katika Kristo?
Swali la 3. Je, Katika hadithi hii, inafaa tuachane na nini, na kuna faida gani kama tutaishi maisha mapya katika Kristo?
Swali la 4. Je, kuna jambo lingine lo lote umejifunza katika hadith hii? Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli katika hii hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Upendo wa Kristo ukitiririka ndani yangu waweza kufanya jambo lolote



| Somo la 11 | KANISA: TIMU YA MUNGU |
| --- | --- |
| | **Maandiko:** Waefeso 4:1-16 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
| --- | --- |
| Kuelewa matokeo ya maisha mapya katika Bwana, na hisia na vitendo vya kuwa mali ya kanisa kama mwili wa Kristo. | "Kila mmoja wetu amepewa neema kadiri ya kipimo alichojaliwa na Kristo." **Waefeso 4:7** |

## UTANGULIZI

Kwa miaka kadhaa, nilikuwa wa timu ya mpira wa kuzunguzhwa. Nakumbuka kwamba waliponikubali kwenye timu, waliniambia kwaba timu hii ilikuwa ya juu sana ambayo ilihusika kila mara katika mashindano ya ubingwa. Kiwango hicho kiliniweka kwa washirika wake katika kujitoa kuwa na cheo cha juu walichokuwa wamepaga miaka nyingi.

Ninapofikiria juu ya kanisa, napenda kuilinganisha kwa timu, kwa sababu sifa nyingi za timu zinafanana na sifa zinazotofautisha kanisa. Maana kuu ya kulinganisha kanisa na timu ni kupendekeza mambo mawili muhimu: (1) Uundaji wetu wa kibinafsi katika uzoefu wa imani na mwili wa Kristo, na (2) Jinsi mafunzo yetu yanavyoshirikiana na mwili wote katika kupta malengo ya timu.

### I. Malezi ya Kibinafsi (Waefeso 4:1-3)

Katika Waefeso 4, mtume alitupatia mfululizo wa sifa ambazo tunapaswa kuziona, zikiambatana na kile alitaja "maisha yanayostahili wito mlioitiwa" (mstari wa 1). Paulo alisisitiza sifa ambazo zinafaa kuthihirishwa kwetu sisi sote ambao tumeitika kwa imani mwito wa Mungu katika Yesu Kristo, kwa sababu ambayo, tuko sasa sehemu ya mwili, ambao, ni kanisa.

#### A. Unyenyekevu

Unyenyekevu, kulingana na kamusi ya mtandao "ni sifa ya kuwa mnyenyekevu na njia ya kuweka mahitaji ya mtu mwingine mbele yako, na kuwafikiria wengine mbele yako. Pia inamaanisha kutojifikiria mwenyewe, na inaweza kumaanisha kukubali kwamba hauko imara kila wakati." Mtu mnyenyekevu ni yule anayetoa kwa hiari sifa yake ili kuhimiza uhusiano mwema na wengine. Mtu huyu mnyenyekevu huunganisha tabia yake kwa mpango wa huduma, kikosi na upendo. Kama tu vile Yesu alifanya! Mtu mnyenyekevu hutoa vilivyo bora zaidi ili amani itawale jirani yake.

#### B. Upole

Katika kitabu hicyo niliandika juu ya tunda la Roho, upole unaelezewa kama nguvu inayodhibitiwa: upole ni tabia ya mtu mpole, na unajidhihirisha katika kushughulika na wengine. Hata hivyo, leo tutajifunza mtazamo mpya katika ufafanuzi wa neno hili: "Upole ni nguvu, kwa sababu ni sehemu ya tunda la Roho Mtakatifu mwenye ushujaa. Lakini ni nguvu ambayo lazima tuimarishe katika roho yetu. Ni nguvu ambayo inapaswa kuwa sehemu ya utu wetu wote, ili utu wetu wote umtiishwe na kudhibitiwa na nguvu hiyo" (Dr. Elvin Heredia PhD, 2015)

#### C. Uvumilivu

Kama upole, uvumilivu ni sehemu ya tunda la Roho. Uvumilivu ni sehemu ya tabia ya kila muumini kwa sababu imani hutegemea uvumilivu. Uvumilivu ni mazoezi ya vitendo thabiti na isiyoyumba. Mtu mvumilivu anajua kusubiri. Kwa sababu hii, imani ndani ya Mungu inatufanya tusubiri jibu lake kwa uvumilivu. Katika kitabu changu, natoa ufafanuzi ufuatao wa vitendo wa uvumilivu: Karibu kwa bahati mbaya niligundua ukweli huu. Tukiweka pamoja neno 'amani' na 'sayansi' tutapata uhusiano wa kuvutia kati ya maneno haya mawili.

### II. Kujumuishwa kwa Mwili wa Kristo (Waefeso 4:4-16)

Wazo kuu la mtume Paulo katika Waefeso 4 lilikuwa kusisitiza umuhimu wa kukua kwa afya katika uzoefu wa imani kwa sababu afya na ukomavu wa kila muumini ungeonekana katika ukuaji wa kiafya wa kanisa. Yaani, kanisa lingeonyesha ulimwengu ufanisi wa injili katika kiwango ambacho kila muumini na/au washirika wa kanisa wangeweza kuingiza nguvu inayofaa ya injili katika tabia zao. Jambo

hili kwa upande mwingine, linatuongoza kuzingatia ukweli wa tatu juu ya sisi ni nani kama Wakristo, na jinsi unaturuhusu kuwa seheme ya jamii ya Wakristo, sehemu ya kanisa na sehemu ya timu ya Mungu.

A. Ufafanuzi wa Tabia (Waefeso 4:7-10)

Paulo alisisitiza kwamba *"kila mmoja wenu amepewa neema kadiri ya kipimo alichojaliwa na Kristo.* (mstari wa 7), akimaanisha kwamba sote tumejazwa na vipengele vya tabia sawa nay a Yesu ili tufanane naye katika tabia na mwenendo. Yesu mwenyewe alituambia *"jifungeni nira yangu, mkajifunze kwangu, maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo…"* (Mathayo 11:29) Paulo alirudi kwa ufafanuzi wa tabia ya Kristo kanisani kusisitiza umuhimu ambao tabia hii inayo katika kiwango cha utendaji. Kwa maneno mengine, kwa kiwango ambacho tabia yetu binafsi inaelezwa kama ile ya Yesu, ndivyo tabia ya kanisa la Kristo ulimwenguni itaelezewa. Kanisa la Kristo, basi, linapaswa kufanana na Kristo wa kanisa.

B. Kujitolea kwa Timu (Waefeso 4:11-13)

Kumbuka kumbukumbu ya awali, tunaweza kufanya matumizi ya matendo kwa nia ya mtume: Ni lazima pia tujitolee kwa timu ya Mungu. Ni lazima pia tuwe wakamilifu katika mienendo yetu. Ni lazima tujitahidi kwa utakaso kamili. Sababu ya hii imeelezewa katika kifungu cha kibiblia cha masomo. Kila mshirika wa timu ya Mungu anajitoa kwa ukuaji mkamilifu, kwa sababu katika njia hii mwili wote wa Kristo pia utakua kwa usawa. Kila mmoja wetu amejitolea kuwa sehmeu ya mwili na ni lazima awakilishe ukuaji bora.

Kama vile tunavyoona katika mstari wa 11, kila mmoja wetu ana kushiriki dhahiri katika utendaji wa mwili. Kwa upande mwingine, kila sehemu ya mwili hufanya kazi kwa faida ya mwili kwa ujumla. Kama vile mstari wa 12 unasema, utenda kazi wa kila mmoja wa washirika wa timu hukuza "ujenzi wa mwili wa Kristo." Yaani, tulibarikiwa sote kutimiza kazi fulani ambayo kila mshirika wa mwili anayo, na kwa sababu hiyo, tutafikia lengo la *"alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo"* (mstari wa 12).

Tatu, tutaona matokeo ya utu wa Kikristo katika uhusiano wetu na Mungu. Kama Baba wa upendo, anataka tufurahie upendo wake na uwepo wake katika ushirikiano unaoendelea. Kwa kuishi maisha katika Roho, tutaendeleza tunda lake maishani mwetu. Uwepo wa Mungu katika maisha yetu utaleta furaha isiyoelezeka, amani inayopita ufahamu wote, na maisha tele kama vile Yesu alivyotuahidi (Yohana 10:10b). Uzoefu huu unaweza kutusaidia kumkaribia Mungu na kutamani kubali katika umoja naye.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, unafikiri tunaweza kubadilisha utu wetu? Je, unaweza kushiriki mabadiliko ambayo kibinafsi umeyaona?
- Je, unaweza kushiriki baadhi ya mawazo mengine juu ya matokeo ya jinisi ya kuendeleza utu wa Kikristo leo?

## HITIMISHO

Kila tunda la Roho ni sifa muhimu na kipengele cha kipekee cha utu hakika wa Kikristo. Tunahitaji kujichunguza wenyewe. Je, tunadhihirisha vipi fadhila hizi? Kuruhusu Roho kufinyanga tabia zetu kutaleta matokeo ya faida sana katika maisha yetu ya binafsi, familia na kijamii. Tunaweza kutumaini kwamba Mungu, Baba yetu wa mbinguni, anataka tuwe na afya, wenye furaha, na tuwe karibu naye, na nguvu zake, haya yanaweza kupatikana maishani mwetu.

## Somo la **17:**

### NAFSI AU TABIA YA MKRISTO

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba Mungu anaweza kufanya upya nafsi au tabia zetu.


**Methali:** Upendo, kama mvua, hauchagui mahali pa kuangukia. Au nyasi ya kuangukia.

**Kifungu cha kusoma:** Warumi: 12:1-21

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Msijione kuwa ni kitu zaidi kuliko mnavyopaswa kuwa, Fikira zenu na ziwe na kiasi kadri ya kipimo cha amani Mungu alivyogawia kila mmoja" Warumi 12:3b

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?
Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?
Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?
Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi**: Kwa uwezo wa Mungu tunaweza kuwa wenye afya, na furaha na kuwa kama Yeye!



| Somo la 18 | KUTAWALA HISIA ZETU |
|---|---|
| | **Maandiko:** Marko 14:32-42 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza kukumbuka kwamba Mungu hataki tutawaliwe na hisia zetu. | "Mwekeeni matatizo yenu yote, maana yeye anawatunzeni." 1 Petro 5:7 |

## UTANGULIZI

Sisi wanadamu na roho, nafsi na mwili (1 Wathesalonike 5:23). Kwa hawa kufanya kazi kwa usawa na kila mmoja, tunahitaji kuwa na amani na Mungu, Muumba wetu, na sisi wenyewe, na wengine.
Katika utamaduni wa baada ya kisasa wa karne ya 21, kuna watu wengi wanaoteseka kwa ukosefu wa amani, na ukosefu huu wa amani ndani ya moyo wa mwanadamu husababisha matokeo ya kuudhi. Vile vile, ukosefu huu unamaanisha mafadhaiko, usumbufu, na magonjwa ya kihemko na kiroho. Kutokuwa na wasiwasi hii ni kwa sababu ya ukosefu wa maelewano katika roho zetu ambayo hutendeka wakati hatuna amani. Yote haya yanaishia kuathiri akili zetu, mioyo na roho, na mwishowe, yote haya huathiri miili yetu.

### I. Kushiriki Hali Yetu ya Akili na Marafiki Zetu (Marko 14:32-34)

Hisia zetu ni dhihirisho la hisia linaloonyeshwa katika tabia za nje/za ndani, ambayo huathiri mitazamo yetu. Udhihirisho huu wa hisia unaweza kuwa na sumu au kukosa sumu; mara nyingi unatoka kwa mawazo yetu, na unaweza kuonekana baada kwa njia zingine.

Hisia zetu tofauti ni sehemu ya kuwa mwanadamu. Tunasoma jinsi Yesu, kwa kujua kwamba wakati wake mbaya ulikuwa unawadia, alienda mahali Gethsemane kuomba pamoja na wanafunzi wake watatu wa karibu: Petro, Yakobo na Yohana (mstari wa 32-33). Hapa, Yesu aliwaambia wanafunzi wake: *"'Nina huzuni kubwa moyoni hata karibu kufa,' aliwaambia. 'Kaeni hapa na kukesha.'"* (mstari wa 34) Tuliona kwamba katika ya hisia za huzuni, Yesu aliamua kushiriki hisia zaka na wanafunzi wake wa karibu. Kwa sababu ya yale alikuwa anapitia, aliwaomba msaada wao wa hisia katika maombi. Hii inatufundisha kwamba katikati ya nyakati zetu ngumu, tunaweza kushiriki na jamii au marafiki wetu wa karibu jinsi tunavyohisi. Tunaweza kutafuta msaada wa hisia zao na msaada wa maombi. Wagalatia 6:2 inasema: *"Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatitimiza sheria ya Kristo."*

### II. Kumlilia Mungu Katikati ya Hali Ngumu (Marko 14:35-36)

Katika kifungu zawa na Marko, Mathayo aliandika kwamba Bwana Yesu alishikiri na Baba yake wa mbinguni katika njia ya binafsi mateso yake kupitia maombi mazito: *"Baba yangu, kama inawezekana kikombe hiki kinipite. Bali si kama nitakavyo mimi, ila utakavyo wewe."* (Mathayo 26:39b) Bwana alishiki na Baba yake wa mbinguni hisia zake zote, na akamtumainia Mungu, akionyesha kutegemea kwake kwa Baba. Ili kuelewa kilio cha moyo wa mtu katikati ya hali ngumu, tunahitaji kujua hali yao ya akili na jinsi wanaweza kusaidiwa kuwa washindi. Ni lazima tujifunze kufanya makosa katika hali hii. Acha tutazame baadhi ya wahusika wa Biblia kueleza haya.

#### A. Hasira ya Musa Kwa Sababu ya Kung'unika Kwa Watu (Hesabu 20:1-13)

Katika hadithi hii, watu walimwuliza Musa kwa nini alikuwa amewaleta jangwani kuwaua na kiu. Kwa kukabilira na hili, Mungu alimwamuru Musa anene juu ya jiwe ili wapate maji; lakini kwa wakati wa kukataa tamaa na hasira, Musa aligonga mwamba kwa fimbo yake (Hesabu 20:10-12) badala ya kulizungumzia kama vile Mungu alivyokuwa amemwamuru. Mlipuko huo wa kuchanganyikiwa na hasira vilimgharimu Musa pakubwa. Kwa sababu hiyo, Mungu alimwambia: *"basi kwa sababu hiyo hamtaiingiza jamii hii katika ile nchi niliyowapa.""* (Hesabu 20:12)!

#### B. Udhaifu wa Eliya (1 Wafalme 19:1-4)

- Alishushwa moyo hadi alitaka kufa, kama tu vile wengine wetu uhisi tunapokabiliwa na matukion

fulani yanayotufanyikia (mstari wa 4).

- Mlipuko huo wa kuchanganyikiwa. Hii inaweza kuonekana katika maombi ya moyoni ambayo nabii huyu alielekeza kwa Mungu: *"Imetosha! Siwezi tena. Ee Mwenyezi-Mungu, sasa utoe uhai wangu. Mimi si bora kuliko wazee wangu"* (mstari wa 4). Tunaweza kuelewa vile maombi yetu yanaweza kuwa ya upumbavu wakati hali yetu ya akili imekosa.

### III. Kukabidhi Kila Hali Katika Mikono ya Mungu (Marko 14:39)

Kwa kukabiliana na yale Bwana Yesu alikuwa anapitia na mateso, Aliendelea kulia katika hali hiyo: *"Baba yangu, kama inawezekana kikombe hiki kinipite. Bali si kama nitakavyo mimi, ila utakavyo wewe."* (Mathayo 26:39b) Tunaona, basi, kwamba yale Bwana wetu alikuwa anapitia hayakumwelekeza kuchukua uamuzi mwingine; Aliomba akiendelea kumtumainia Mungu, katikati ya mateso yake.

Nashangaa tunaweza hisi vipi kama tungejua kwamba tulikuwa karibu kufa. Je, hisia zetu zingekuwaje? Lakini muhimu zaidi, tungefanya nini wakati huo? Watu wengi hufanya uamuzi wa haraka wakati huo mzito wanapopitia hali tofauti ya akili, na baadaye, wanajuta juu ya uamuzi huo. Hii mara nyingi huelekeza kwenye hali inayowasababishia mahangaiko zaid, kutokuwa na hakika, nk. Kuliko yale walikuwa nayo mbeleni.

#### A. Kesi ya Asafu (Zaburi 73:1-23)

Mwandishi wa Zaburi Asafu alikuwa mwimbaji wa Daudi. Baada ya miaka 12 ya huduma kwa Mungu, alikuwa na shaka, alipoteza tumaini lake kwa Mungu, na akawa na wivu kwa wasiomcha Mungu. Hata akasema: *"Je, nimetunza bura usafi moyoni, na kujilinda nisitende dhambi."* (mstari wa 13) Mtu huyu alikuwa na hisia ya kunung'unika na manung'uniko yake yalikuwa kwa Aliye Juu. Lakini haya yalibadilika alipoingia patakatifu pa Mungu (madhabahu), na alitambua yatakayowapata waovu mwishowe (mstari wa 17). Tangu wakati huo, Asafu alikiri na kukubali kwamba alikuwa amefanya makosa. Katika hali hiyo, hali fulani ya akili ndani mwetu inaweza kutuelekeza kuwa na shaka kwa upumbavu na kumkana Mungu, kisha tunaingia katika mapigano na yeye. Tuwe waangalifu! Tumuombe Bwana tukimwitisha uvumilivu wakati wote.

#### B. Upole wa Mungu Kwa Eliya (1 Mfalme 19:1-18)

Mungu alimjibu Eliya kwa kumpa yafuatayo:

- Alimpa pumziko (usingizi) (mstari wa 5). Ingawa inaonekana ya kushangaza, pumziko la mwili pia ni baraka kutoka kwa Mungu. Fikiria juu ya hili: Je, ni watu wangapi ambao hawawezi kulala kwa amani au kama kawaida?
- Alimpa chakula cha kutosha (mstari wa 6).
- Alimruhusu azungumzie shida zake. Hii mara nyingi ni njia nzuri sana ya kusaidia wengine katikati ya hisia zao. Hivyo, Eliya alimweleza Mungu shida yake na kufunua huzuni yake (mstari wa 10).
- Mungu alijifunua katika njia zake mbalimbali. Upepo, tetemeko, moto na sauti ndogo tulivu zilikuwa zote sauti za Mungu (mistari ya 11-12).
- Bwana alimpa Eliya kazi zaidi ya kufanya: kuwapaka wengine mafuta, akimwonyesha nabii wake aliyhuzunika kwamba alitaka kuendelea kumtumia. Hivyo, Mungu alibadilisha huzuni ya Eliya kupitia kazi (tendo). Hii ilikuwa tiba kamili (mistari ya 15-16).
- Alimwambia Eliya habari njema, kwamba kulikuwa na waaminifu elfu saba waliobaki Israeli (mstari wa 18). Katika njia hii, hisia ya upweke iliondolewa (Spurgeon, Charles, Notes on Sermons, USA: Editorial Portavoz, 1974, pg. 55).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, kwa nini Bwana Yesu aliwauliza wanafunzi wake Petro, Yakobo na Yohana waende pamoja naye?
- Je, ni nini inaweza kufanyika wakati mtu anaamua kutenda kwa haraka chini ya hali ya akili ambayo wanahisi?
- Je, ni maneno gani maombi ya Bwana yanaonyesha kwamba alishiriki na Baba yake wa mbinguni hali ya uchungu aliyokuwa akipitia?


## HITIMISHO

Katika maisha yetu binafsi, ni mara ngapi tumepitia hali zilizotusababishia machungu, mahangaiko, n.k. Kumbuka, katikati ya wakati huo wote, kujifunza kupumzika na Yesu Kristo (Mathayo 11:28). Hakuna mwana au binti wa Mungu ameachwa katika matatizo ya binadamu. Bwana Yesu mara nyingi anasikiliza hali zetu; anataka tuje kwake.

**Somo la** 18:

## KUTAWALA HISIA ZETU

**Lengo la Somo:** Kukumbuka kwamba, Mungu hatutaki sisi tutawaliwe na hali ya muda tu ya akili au hisia.
**Methali:** Simanzi ya huzuni ni faida ya moyo.
**Kifungu cha Kusoma:** Marko 14:32-42
**Mstari wa Kumbukumbu:** "Akawaambia, "Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa. Kaeni hapa mkeshe." Marko 14:34
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?
Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?
Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?
Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?
**Himizo la Hadithi:** Tusipozitawala hisia zetu, hisia hizo zitatutawala.



| Somo la 19 | USISUMBUKE, BALI AMINI! |
|---|---|
| | **Maandiko:** Luka 12:22-31 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba shaka au wasiwasi ni uovu unaoathiri watu wengi, na kwamba Mungu hataki tuwe na wasiwasi. | "Msiwe na wasiwasi juu ya kitu chochote, ila kwa kila hali, mwombeni Mungu katika sala juu ya mahitaji yenu, kwa shukrani. Nayo amani ya Mungu ipitayo akili zote za watu italinda salama mioyo na akili zenu katika kuungana na Kristo Yesu." **Wafilipi 4:6** |

## UTANGULIZI

Mara nyingi katika maisha, tunakutana na hali tusizotarajia ambapo hatuwezi njia ya kutokea. Wakati wa shida, tunajiuliza maswali juu uamuzi tunaofanya au ni wapi raslimali itatoka ya kukutana hitaji. Katikati ya hali hii yote isiyotarajiwa, ni kawaida kwamba wasiwasi na shaka zinatokea kwetu tunapotazama yale yote tunayoyaona kama mambo ya baadaye tusiyoyajua, na wala si kama ukweli wa sasa. Yesu alijua kwamba wanafunzi wake waliuliza juu ya maisha ya baadaye na vile mahitaji yao yatatimizwa. Katika Luka 12:22-31, tunaona kwamba Bwana alitumia muda wake kuwafahamisha kwamba Mungu alikuwa anakutana na kila hitaji lao, hivyo walihitaji tu kutumaini katika ulinzi wake wa uungu.

## I. Chanzo cha Wasiwasi

Wasiwasi ni:: *"hisia ya kuwa na shaka, woga, au kutokuwa na starehe, kawaida juu ya tukio la karibu au kitu kilicho na matokeo yasiyo na uhakika."* Hiyo ni kusema, wasiwasi ni hali ambayo mtu anakosa starehe kabisa na kuwa na uoga kiasi. Hali kama hiyo ni athari ya kawaida na ya asili, ambayo inaibuka wakati mawazo yetu yaliyoghadhabika yanaamsha tendo hili mioyoni mwetu. Wasiswasi husababisha mabadiliko ya kisaikolojia ndani yetu ambayo inatuandaa kuongeza utendaji na kukaa macho. Hii ni kawaida, hata hivyo, kilicho kawaida ni kuwa na wasiwasi kila wakati kwa sababu tofauti.

### A. Maisha ya Kawaida na Mahangaiko

Hali ya sasa ya maisha na shughuli nyingi na kazi zinaweza kuwa chanzi cha wasiwasi na mafadhaiko kila wakati. Wakati hatuweki vipaupmbele vinavyofaa na kuruhusu hali au watu wengine kufanya maamuzi juu ya wakati wetu na shughuli, tunaweza kuwa na wakati ambapo tunakuwa na kazi nyingi, ambayo hutuweka katika misukosuko ya kila wakati.

### B. Kutoridhika

Moyo wa mwanadamu hauwezi kutosheka; tamaa na utaftaji wa mapnezi vinaweza kututawala. Wakati mtazamo wetu hauko kwa Kristo, na haturuhusu Roho wake Mtakatifu aongoze maisha yetu, tunalazimika kufuata tamaa zetu wenyewe. Utafutaji huu wa kudumu wa kuridhika zaidi huishia kutuchosha na kutuacha bure. Katika mkutano wake na mwanamke Msamaria, Yesu alitambua hitaji la mwanamke huyu na kumsaidia kuona uamuzi wote aliokuwa amefanya katika kujaribu kujiridhisha. Kisha, akajitoa kuridhisha kiu yake na kumpa uzima wa milele (Yohana 4:13-14). Yesu ndiye pekee anayeweza kuridhisha mahitaji yetu yote na kutuepusha kutawaliwa na raha za dunia hii.

### C. Mzozo na Kutokuwa na Uhakika

Kumpoteza mpendwa kwaweza kuacha pengo kubwa sana ambapo inaweza kutufanya tufikirie kwamba hatutawahi kurudi kwa hali ya kawaida. Kwa hivyo, tunaangazia mtazamo wetu juu ya siku za baadaye zisizotarajiwa na jinsi tunaweza kuendelea na maisha kuanzia wakati huo. Kuvunjika kwa familia au uhusiano wa ndoa kunaweza pia kutufanya kuhisi wasiwasi. Baada ya kuweka imani yetu katika uhusiano tunaona jinis mipango yetu inaangahishwa na tunajihisi bila mpangilio. Pia, kupoteza kwa kazi, migogoro kati ya watu au hali nyingine yoyote ambayo inakosesha utulivu huishia kusumbua akili zetu, ikiweka njia kwa

mawazo yasiyoturuhusu kusonga mbele.

## II. Tujifunza Kutoka kwa Ndege na Maua

### A. Usijali kuhusu Maisha ya Kila Siku

Wakati tunafikiria juu ya mahitaji yetu kama chakula na mavazi, tunaweza kuona kwamba yanakuwa muhimu kuhakikisha maisha yetu hapa duniani. Hata hivyo, Yesu aliwasaidia wanafunzi wake kuona vile Mungu hutunza uumbaji wake kwa bidii (Luka 12:24b, 28). Tunapogeuza macho yetu kuelekea mateso ya ulimwengu huu, ni rahisi kusahau kwamba Mungu ndiye anayetawala na kusimamia kila kitu. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu taweka utunzaji wake mzuri juu ya maisha yetu na mahitaji yetu.

### B. Mungu Anakujali

Katika Luka 12:29-30, tunaweza kuona wazi Yesu akionyesha ukweli kwamba hatupaswi kuwa na wasioamini, ambao maisha yao yanazungukia wasiwasi na mahangaiko. Kwa Yesu, wasiwasi katika maisha yetu ni matokeo ya kusahau kwamba tunaye Baba mpendwa anayetulinda na kuyafahamu mahitaji yetu.

Dawa Inayofaa Dhidi ya Wasiwasi

### A. Tunahitaji Kuweka Tumaini Letu Kwa Mungu

Jambo muhimu tunapokutana na wasiwasi ni kuelewa, kuwa waangalifu, na kutambua kwamba shaka au hali ambazo zinaweza kusababisha wasawasi zinachukua kipaumbele cha juu katika maisha yetu kuliko tumaini tulilo nalo kwa Mungu. Tunapokutana na moja ya migororo hii katika maisha yetu, tunaangalia raslimali zetu kwanza na njia (Zaburi 20:7). Tunapoanza kuzitegemea, tunadhoofisha tumaini letu kwa Mungu. Tunapogundua kwamba kile tunachoweza kufanya hakitoshi, kile tutahisi ni wasiwasi. Kuangazia vipaji vya Mungu, na kukumbuka jinsi amekutana na mahitaji yetu hapo awali, ni njia ya kukuza imani yetu. Ili kuweza kupumzika na kupinga mawazo yanayochochea wasiwasi, tunahitami kurejesha tumaini letu kwa Mungu.

### B. Kuyaweka Mawazo Yetu Kwa Mungu

Tatizo la wasiwasi ni kwamba inachochea mawazo yetu na akili. Inaondoa amani yetu na haitufanyi tuone wazi hatua bora tunayoweza kufanya. Isaya alitukumbusha kwamba Mungu anamweka katika amani aliye thabiti kwa Mungu, na anayemtegemea (Isaya 26:3). Tunahitaji kujaza akili zetu na mawazo ya Mungu, tukitambua matendo yake katika kila muda wa maisha yetu, ili tuepuke mashaka yanayochukua nafasi yake na kutusumbua.

### C. Tunahitaji Kushukuru

Paulo alitupatia ushauri mzuri katika barua yake kwa Wafilipi. Hapa alitukumbusha kwamba hatuna sababu ya kuhisi wasiwasi. Wakati huo ambao tunahisi wasiwasi, tunahitaji kuwasilisha haja zetu mbele ya Mungu, tukiomba kwa shukrani (Wafilipi 4:6). Kushukuru ni dana kamili ya wasiwasi yoyote kwa sababu inaweka ukuta wa upinzani kwa wasiwasi na shaka zetu. Inatufanya pia tuone kwamba, hata kama tunakutana na hali ngumu, tunayo raslimali ya thamani kwa Mungu, ambaye tunaweza kumgeukia wakati wote.

### D. Tunahitaji Kuomba

1 Petro 5:7 anatukumbusha kwamba tunaweza kuweka wasiwasi yetu yote kwa Mungu, tukitambua kwamba anatulinda. Mungu anajua kwamba sisi ni wanadamu. Anayafahamu mahitaji yetu na yeye ni Baba wa upendo anayekutana na mahitaji yetu katika kila sehemu ya maisha yetu. Ujasiri wetu katika uhakika wa ulinzi wake ni raslimali ya bora ya kuwa huru kutoka kwa wasiwasi. Ingawa wasiwasi ni hali ya kawaida ya matendo ya mwanadamu ambayo wakati mwingine inatuweka macho na kutusaidia kuzuia hatari na vitisho, tunapaswa kufahamu kwamba mara nyingi tunakuwa na shaka na kukasirika na hali ambazo zinaonyesha ukosefu wa imani na tumaini kwa vipaji vya kwa maisha yetu.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni katika njia gani ambayo kuwa na shughuli nyingi inaweza kusababisha wasiwasi? (Mathayo 13:22)
- Je, tunawezaje kukuza tumaini letu kwa Mungu kwa kuona kujali kwa viumbe vyake? (Luka 12:24-28)
- Je, unafikiri ni kwa nini Paulo anatushauri tuwe na shukrani ili kupunguza wasiwasi? (Wafilipi4:6)

## HITIMISHO

Mungu anatutarajia tuamini kwamba yeye ni Baba anayejali ambaye anajua mahitaji yetu na anataka kukutana na kila hitaji. Tunapokutana na hali ambapo hatuoni jinisi Mungu anaweza kutusaidia, tunahitaji kutafuta msaada wake kwa maombi na shukrani, tukiangazia macho yetu Kwake.

**Somo la 19:**

## USISUMBUKE, BALI AMINI!

**Lengo la somo:** Kuelewa kwamba Mungu hataki tusumbuke.

**Methali:** Masumbuko hayaondoi simanzi ya kesho, Husababisha nguvu za sasa kuwa dhaifu.

**Kifungu cha Kusoma:** Luka 12:22-31

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Basi Yesu alisema na wanafunzi Wake. Akawaambia, "Msisumbukie maisha yenu, mtakula nini. Na msisumbukie miili yenu, mtavaa nini." Luka 12:22


**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?

Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?

Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii? Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Masumbuko huiba; maombi hufunua, hivyo tuombe!



| Somo la 20 | **YALE BIBLIA INATUELEZA JUU YA DHIKI** |
| --- | --- |
| | **Maandiko:** Mathayo 11:25-30 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
| --- | --- |
| Kuelewa kwamba Mungu anawataka watoto wake waishi maisha yaliyo na pumziko kimwili, kiroho na hisia. | "Njoni kwangu nyinyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, name nitawapumzisha." **Mathayo 11:28** |

## UTANGULIZI

Katika historia yote ya mwanadamu, matatizo na misukumo yamekuwa kwetu kama wanadamu. Yanaweza kuwa ya kimwili, kijamii, kiroho na/au kihisia. Katika kifungu chetu cha masomo, Yesu anazungumzia watu wa Kiyahudi, watu walikuwa na mambo mengi. Kama taifa, Wayahudi walikuwa chini ya nira ya Roma. Wakati ni kweli kwamba wangelima shamba lao, walihitajika kulipa ushuru juu yake. Pia, wakati ilikuwa kweli kwamba walikuwa na mahali pa ibada (Hekalu la Yerusalemu), ilikuwa kweli kwamba viongozi wao wa kidini waliwekwa juu yao na utawala uliowadhulumu. Tukiendelea zaidi, ni kweli kwamba walikuwa na uhuru wa kumwamini Mungu, lakini dini yao ilijaa sheria nyingi ambazo hazikuwezekana kutimiza. Kwa haya yote akilini, acha tusome Mathayo 11:25-30 na tuone yale Mungu anayo kwetu tunapomtafuta kwa moyo wote.

### I. Mfadhaiko, Sababu na Matokeo Yake

#### A. Sababu Za Mfadhaiko

Kadiri nyakati zinavyosonga, tumesababisha shida zetu wenyewe. Ubinadamu unazidi kubeba shida. Tunajitahidi sisi wenyewe kwa sababu tunataka kujua zaidi. Hii imesababisha kizazi cha shinikizo za kila aina, ikiwa ni pamoja na za hisia, kwa sababu hatujaweza kupata majibu ya kuwepo kwetu. Kwa nyakati ambazo kuna sayansi zaidi, pia kuna kujiua zaidi, watumizi zaidi wa madawa ya kulevya, ulevi zaidi na mambo yanayofanana. Na haya yote yanatufanya tunashangaa. Kuna majibu mengi, lakni nafikiria moja yake ni tunaishi kufadhaika zaidi na zaidi kwa sababu hatuwezi kupata majibu halisi.

#### B. Mfadhaiko na Matokeo Yake

Mfadhaiko umefafanuliwa kama hisia ambayo kila kitu kinatawanyika, na kinaweza kuchochewa na kutoweza kutatua shida. Ni hisia pia ya kuwa na shaka nyingi juu ya kazi, nyumba, familia, pesa, gari na mfululizo wa mambo. Haya yote yanaweza kusababishwa shinikizo la damu na ugonjwa wa ngozi kutaja tu machache. Lakini inaweza pia kuelekeza kwa matatizo ya kiroho kama vile kukata tamaa na uchungu, ambazo huwasababisha watu wengine kutafuta ushauri wa kila kitu kinachohusika na kiroho na uchawi. Matatizo ya hisia na mvutano wa akili ni nguvu zinazoweza kukosa kuonekana zinazovuta au kumsukuma mtu. Pia mfadhaiko hujionyesha kama hasira, machozi, ulemavu, kukosa kiasi, kupoteza tamaa ya njia, kula, kusababisha makosa, hasira, unyongovu wa misuli, na, wakati mwingine, matukio makubwa sana au ajali.

### II. Majibu ya Yesu kwa Tatizo la Mfadhaiko

#### A. Jamii ya Kidini Wakati wa Yesu

Tatizo la watu wa Kiyahudi wakati wa Yesu lilikuwa kwamba dini ya Kiyahudi haikuwapa suluhiso tofauti kwa machungu yao. Dini yao ilijaa amri na sheria nyingi. Yesu mwenyewe aliwapinga viongozi wa dini, akisema kwamba waliweza kuwawekea watu mizigo ambayo hata hao wenye hawangeweza kubeba (Mathayo 23:4).

#### B. Jamii Leo

Kila kitu ambacho kinaendelea kutuzunguka leo kinaweza kuwa cha kufadhaisha. Kwa mshango, hata dini zimekuwa chanzo cha mfadhaiko. Katika jamii yetu, watu wanatafuta kupata vitu. Vijana wanataka kuwa na kazi nzuri ili waweze kununua gari, nyumba, mavazi, n.k. Wanaamini kwamba hii itawafanya wahisi kuwa na furaha, lakini badala yake vitu haviwaridhishi. Wanandoa wanaamin kwamba watakuwa na furaha wakiwa na vitu vyote vyote wanavyohitaji kwa hatua yao mpya ya maisha. Lakini tunazungumzia tena juu ya mali. Dini, au pesa, au cheo, au vitu tunavyoweza kupata vinatusaidia kuwa na furaha.

C. Kile Yesu Anatupatia

Katika hali hii, Yesu alifanya mwaliko ufuatao: *"Je, umechoka? Umechoshwa? Umebebeshwa mizigo ya dini? Njoni kwangu. Nifuateni na mtarejesha maisha yenu. Nitawaonyesha jinsi ya kupata pumziko la kweli."* (Mathayo 11:28) Pamoja na mwaliko huu wa thamani, tunahitaji kujiuliza maswali mawili muhimu: "Je, tutakujaje kwake?" na "Je, ni aina gani ya pumziko ambao Bwana anapeana?" Kuna watu wengi ambao husikia juu ya Yesu, na wanaalikwa kuamini kwamba anaweza kusamehe dhambi zao na kuwapa maisha mapya. Wengi wao wanasema wanaweza kutatua mambo mengine katika maisha yao, na kisha wakubali mwaliko. Hata hivyo, ukweli ni kwamba kama tungeweza kusuluhisha maisha wenyewe, je, tunamwitaji Yesu kwa nini? Kumbuka kile mwandishi wa Zaburi alisema: *"Mwachie Mwenyezi-Mungu mzigo wao, naye atakutegemeza; kamwe hamwachi mwadilifu ashindwe."* (Zaburi 55:22)

## III. Kufungiwa Nira na Yesu

A. "Jifungeni nira yangu, mkajifunze kwangu…" (Mathayo 11:29a)

Mtu anapokuja kwa Yesu, ni lazima wajifunze kutembea katika sheria mpya: hakuna majivuno tena, na hakuna sheria za ubinafsi tena. Sasa, ni lazima wafuate sheria za Yesu. Inashangaza kwamba anatuambia tujifunge nira yake, yaani, mafundisho yake, na kuanza njia mpya, njia ya unyenyekevu, utiifu, kujifunza tena jinsi ya kutembea maisha mapya. Yesu alituambia: *"...jifunze kutoka kwangu…"* mstari wa 29). Lakini ni wapi na ni jinsi gani mtoto wa Mungu ajifunze kutoka wa Yesu? Yeye mwenyewe alitupatia jibu: *"…tusome Maandiko kwa bidii kwa sababu unafikiri kwamba ndani yake unao uzima wa milele. Haya ni yale yale Maandiko yanayoshuhudia juu yangu mimi."* (Yohana 5:39)

B. "... Mimi Ni Mpole Na Mnyenyekevu Wa Moyo…" (Mathayo 11:29b)

Maelezo ya Yesu mwenyewe yalikuwa tofauti kabisa na vile viongozi wa Kiyahudi walikuwa: wenye kiburi, majivuno, wenye sheria na wenye mamlaka. Yesu ni mpole, kwa maneno mengine, ni mpole na mkarimu, tofauti sana na tabia ya makuhani wa wakati huo! Asili ya Yesu ni ya amani. Ni yeye tu anayeweza kufariji roho zetu. Katika hadithi za nabii Eliya katika 1 Wafalme 19:1-18, tunampata nabii akimtoroka Ahabu na Yezebeli, akiwa amefadhaika na kuhangaika. Mungu alimsaidia alale, na kisha akazungumza naye akiwa ndani ya pango. Mungu alitumia upepo, tetemeko na moto kuwasiliana na Eliya, lakini hakumwona Mungu ndani yake.

C. "... Na Mtapata Pumziko Rohoni mwenu" (Mathayo 11:29c)

Tamaa kubwa ya watu ni kuweza kupata pumziko kutoka kwa mateso makali. Tunahitaji kuwa na amani wenyewe. Katika Wafilipi 4:6, mtume Paulo anatualika kuombea mambo yanayotuhusu, na kuondoa amani yetu. Suluhisho basi ni kwamba tunahitaji kusema zaidi na Mungu. Tukiombea mambo yote yanayotuhusu, tutakuwa na mfadhaiko kiasi. Hapa kuna mapendekezo mawili ya vitendo ya kupata amani ya roho zetu: Kwanza, kuwa na muda zadi wa kuwa na Yesu, muda wako, na kuacha kufuata mambo. Pili, ridhika, yaani, jifunze kuwa na kile Mungu amekupatia.

## MASWALI YA ZIADA

- Katika maneno yako mwenyewe, je, ni nani ambao unafikiria wanaishi kwa mafadhaiko wa mara kwa mara?
- Je, kanisa la wakatu huu linaweza kusababisha mafadhaiko katika jamii? Eleza
- Je, ni uhusiano wa aina gani ambao unaweza kuwa nao na Yesu?

## HITIMISHO

Mungu ana haj asana kwamba watoto wake waishi maisha ya pumziko kimwili, kiroho, na kihisia. Ili kufanya hivi, tunapaswa kuacha kuangalia yale ambayo hatuna au kile kinachosababisha machungu au haja. Badala yake, tushiriki yote na Mungu kwa maombi, na kisha tutapata amani ya kweli ambayo inatoka tu kwa Mungu.

**Somo la** 20:

# YALE BIBLIA INATUELEZA JUU YA DHIKI

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba Mungu anataka watoto wake waishi maisha yaliyotulia.

**Methali:** "Unaweza kujiepusha na yale yanayokufuata; bali huwezi kujiepusha na yaliyo ndani yako."

**Kifungu cha Kusoma:** Mathayo 11:25-30

**Mstari wa Kumbukumbu**: "Njoni kwangu, ninyi nyote msimbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?


Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?

Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?

Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Mungu anajali kwamba watoto Wake waishi maisha yaliyotulia



| Somo la 21 | MUNGU HUWASAMEHE WALE WANAOSAMEHE |
|---|---|
| | **Maandiko:** Mathayo 18:23-35 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza kwamba Mungu anataka tuwasamehe wengine makosa ambayo wametufanyia. | "Je, haikukupasa nawe kumhurumia mtumishi mwenzako kama nilivyokuhurumia?" **Mathayo 18:33** |

## UTANGULIZI

Moja ya mada ambayo Mathayo alishughulika nayo katika injili alizoandika ilikuwa ni mada ya msamaha. Tunasoma kwamba ili kuwa watoto wa Mungu inamaanisha kuishi maisha ya amani (Mathayo 5:9). Tunasoma pia kwamba ikiwa kabla ya kutoa sadaka zetu (kiuchumi au sifa) kwa Bwana, tunakumbuka kwamba tunalo jambo juu ya Mkristo mwenzetu, tunahitaji kusimama, kwenda, na kupatanishwa na mwingine, na kisha tumwabudu Mungu (Mathayo 5:23-24). Inashangaza kwamba sura ya 5 inakamilika na mwito wa dharura wa kuwapenda maadui kama tunataka kuwa watoto wa Baba wetu wa mbinguni (mistari ya 44-45). Inaonekana, ukamilifu wetu katika utakatifu unategemea kuwasamehe wengine (mstari wa 48).

### I. Sifa ya Msamaha wa Mungu (Mathayo 18:23-27)

A. Msamaha wa Mungu Hautafuti Yake Mwenyewe

Mtumishi alimwambia mfalme na bwana: *"... unisubiri..."* (mstari wa 26). Kamusi ya mtandao inafafanua uvumilivu kama: *"uwezo wa kukubali au kuvumilia kucheleweshwa, shida, au kuteseka bila kukasirika au kuchafukiwa."* Mtumishi pia alimwambia Bwana wake: *"...nami nitakulipa deni lote."* (mstari wa 26) Jibu la mtumishi huyu lilionyesha kiburi chake. Hakuomba asamehewe deni lote au sehemu ya deni. Hakuomba malipo ya starehe ya kulipa deni lake. Lakini aliomba jambo lilikuwa ngumu kwake kulipa kwa mshahara wa mtumishi. Dhambi iniatuongoza kuona chaguzi za kupindukia, badala ya kutafuta msamaha wa uungu ambao tunapewa.

B. Msamaha wa Mungu Ni wa Rehema

Tunasoma: *"...bwana wa mtumishi alimwonea huruma."* (mstari wa 27a) Wazo lililoelezewa hapa mara nyingi linapatika katika Biblia (Waamuzi 2:18, Luka 10:33, 15:20, n.k.). Mfalme alimhurumia sana mtumishi wake. Sisi pia tunahitaji kuonyesha rehema wakati tunahitaji kumsamehe mtu. Kama tu vile tunahitaji rehema ya Mungu, hivyo tunapaswa kuionyesha kwa mahusiano na wengine. Tumealikwa katika Biblia kuwa kama Yesu, tukimdhihirisha Yesu maishani mwetu. Kujifunza kusamehe mwingine kutatuunganisha pamoja, na hiyo itatoa ushuhuda kwa ulimwengu (Yohana 17:21).

C. Msamaha wa Mungu Huleta Uhuru

Hatima yetu ilikuwa ikienda kuzimu, gereza la kudumu kwa roho zetu (Luka 16:26), lakini Mungu katika rehema zake alilipa deni letu, kuondoa hatia zetu na kututangaza kuwa wenye haki, hivyo kutuhakikishia uhuru wetu wa milele kama tutabaki katika Kristo. Tuko huru kwa sababu msamaha wa kimungu ulileta haki katika maisha yetu. Mfano huu wa wadaiwa pia unatusaidia kuelewa hilo na sisi wenyewe, hatuwezi kununua uhuru wetu. Majivuno yetu hayawezi kufanya, au makusudi yetu mazuri. Jambo pekee linaloweza kutuweka huru kwa uzima ni msamaha wa kimungu (Yohana 8:36). Mathayo 18:27 inakamilika kwa kusema: *"Akamsamehe lile deni, akamwacha aende zake."*

### II. Maonyesho ya Kutosamehe (Mathayo 18:28-30)

Tuelekee sasa kwa yule mtumishi mwingine aliyekuwa na deni la mtumishi wa kwanza la dinari mia moja, mshahara wa siku mia moja. Wakati huu, itakuwa sawa na misharaha tatu ya chini, deni linaloweza kulipwa. Hii ni tofauti na deni ambalo bwana wake alikuwa amemsamehe, ambalo lilikuwa sawa na mamilioni ya dola. Lakini mtumishi wa kwanza alikataa kumsamehe (mstari wa 28).

A. Ukosefu wa Msamaha Huathiri Wengine

Mtumishi aliyesamehewa hakuwa na msamaha na nia hiyo ya msamaha kama bwana wake alikuwa nao. Kifungu kinasema kwamba mtumishi kwa fujo alimchukua mtumishi mwenzake na akataka kumwua (mstari wa 28). Na hata kama mtumishi huyu alijitupa kwenye miguu yake na kumuomba (mstari wa 29), akitumia maneno ambayo alikuwa ametumia awali kwa mfalme (mstari wa 26), hakutaka kumsamehe. Hapata tunaweza kuelewa kwamba ukosefu wa nia ya msamaha unatusababishia kuwa na fujo kwa wengine, kuwabana wenzetu, kufufua hasira, ghadhabu, maumivu yasiyo ya lazima, matusi, mashtaka n.k.

B. Ukosefu wa Msamaha Hushtaki

Mtumishi alimwambia mwenzake: *"Nilipe deni langu!"* (mstari wa 28). Mara nyingi kama waalifu, tunataka kusamehewa sio tu na Mungu, bali pia na majirani wetu ili tusihisi tena mzigo wa hatia. Lakini wakati hali inabadilika, wakati tuko katika hali ya kuwa ni isis tumekosewa, ni vigumu kiasi gani kusaheme! Tunataka kuendelea kuwalaumu waliotukosea na kutafuta kuwafanya wakumbuke yale wametutendea kwa sababu yale walifanya yalituumiza. Nivigumu kusamehe. Hata hivyo, msamaha wa kweli hauangalii upungufu, makosa na dhambi tulizotendewa.

**III. Matokeo ya Kutosamehe (Mathayo 18:31-35)**

A. Kutosamehe Kutaonekana na Wengine.

Miongoni mwa wahusika wengine waliotajwa katika hadithi hii ni watumwa wengine, ambao wanginie walihuzunika na wengine kukasirika juu ya kile walikuwa wameona: *"Basi watumishi wenzake walipoona jambo hilo walisikitika sana, wakaenda kumpasha habari bwana wao juu ya mambo hayo yaliyotukia"* (mstari wa 31)

Viongozi wa Kiyahudi waliweka sheria vizuri, *"Jicho kwa jicho, jino kwa jino."* (Kutoka 21:24, Mambo ya Walawi 24:20, Kumbukumbu la Torati 19:21). Lakini haikuwa kulipiza kisasi bali ni kwa sababu adhabu ilikuwa kawaida. Mfalme alilazimika kutenda kwa haki katika hali hii. Mtumishi mwovu alikuwa amemwumiza mtumishi mwenzake; alihitaji kuadhibiwa. Punde tu, watu wataanza kutaka haki. Kulitakiwa kuwa na msamaha kati ya watumishi wawili.

B. Ukosefu wa Msamaha Hurudisha Hukumu ya Mungu

Mungu atatukosoa tusiposamehe. Kukosolewa kwa kimungu kulikohitajika kutoka kwa mtumishi ambaye hakutaka kusamehe ni kuhumu ile ile angepata kama hangesamehewa (mstari wa 34). Sasa alilazimika kulipa deni lote. Mfalme hakuwa na haja ya pesa, wala hakumlaumu mtumishi mwovu kwa sababu wengine wote walitaka, bali kwa sababu hakutaka kumsamehe mtumishi mwenzake. Kwa hivyo, mfalme aliwambia: *"'Wewe ni mtumishi mbaya sana,' akasema, 'Uliniomba name nkakusamehe deni lako lote. Je, haikukupasa nawe kumhurumia mtumishi mwenzako kama nilivyokuhurumia?'"* (mistari ya 32-33).

C. Huleta Kutosamehe kwa Mungu

Katika dhana ile ile iliyo katika Mathayo, kuna hitaji kama tunataka msamaha wa Mungu. Ni lazima tukubali Kristo na kupokea nia ya msamaha kutoka kwake. Katika sala la Bwana, tunasoma, *"Na utusamehe.. kama na sisi tunavyosamehe"* (Mathayo 6:12). Haya ni mapenzi ya Mungu. Na kwa kufunga kifungu hiki, Yesu anaongezea: *"Ukiwasamehe wengine wanapokukosea, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe."* (Mathayo 6:14) Yesu anajua mienendo yetu ya kibinadamu: *"Lakini usipowasamehe watu makosa yao, Baba yenu hatawasamehe makosa yenu."* (Mathayo 6:15)

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni sifa gani za msamaha wa Mungu kulingana na Mathayo 18:23-27?
- Je, ni nini inasababisha ukosefu wa msamaha kulingana na kifungu? Eleza.
- Je, unawezaje kumsaidia mtu amsamehe mkosaji wake?

## HITIMISHO

Wakati mwingine ni vigumu kwetu kusamehe, bali upendo wa Mungu mkamilifu unatuwezesha kufanya hivyo. Je, tunawezaje kumsamehe mnajisi, mwizi, mshushaji wa uhusiano, mauaji, deni la kiuchumi, nk? Hatuwezi kufanya hivyo kwa nguvu zetu, bali kwa msaada wa Mungu, tunaweza. Yesu alituachia mfano (1 Petro 2:21- 23). Tunaweza kuwezeshwa kupitia Roho Wake Mtakatifu kusamehe.

**Somo la** 21:

## MUNGU HUWASAMEHE WALE WANAOSAMEHE

**Lengo la Somo:** Kujifunza kuwa kama umemuudhi mtu, omba msamaha: kama umeudhiwa, samehe.

**Methali:** Moyo mchungu unakula mmiliki wake.

**Kifungu cha Kusoma:** Mathayo 18:23-35

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Je, haikukupasa nawe kumhurumia mtumishi mwenzako kama nilivyokuhurumia." Mathayo 18:33

**Maswali ya Kujadili:** Swali 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?


Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?

Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?

Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Upendo wa Mungu mkamilifu utuwezesha kumsamehe yeyote.



| Somo la 22 | TOSHEKA! |
| --- | --- |
| | **Maandiko:** 1 Timotheo 6:3-10 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
| --- | --- |
| Kuelewa kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba wanawe mabinti watosheke na kuishi wakiwa wametosheka na kile walicho nacho. | "Kwa hiyo basi, kama tunacho chakula na mavazi, tunapaswa kuridhika navyo." **1 Timotheo 6:8** |

## UTANGULIZI

Miongo kadhaa baadaye, imekuja kuonekana kwamba imepatikana kuwa utajiri, uhuru na ubinafsi umesababisha mshikano na kuondoka kwa sababu ya upweke mkubwa unaowaelekeza wengi kwa kujiua. Matokeo ya mwisho ya uhuru sio furaha, bali utupu na kuchoka bila kufikiria kabisa. Kwa kukabiliana na ukweli huu, kifungu cha 1 Timotheo 6:3-10 kinatuonyesha njia bora ambayo ni uungu na kutosheka.

### I. Faida Za Uungu Zikiandamana na Kutosheka (1 Timotheo 6:3-6)

A. Kufuata Mfano wa Yesu wa Uungu

Mtume Paulo alisisitiza ucha Mungu au uungu wakati alimsihi mwanafunzi wake Timotheo kufundisha juu ya suala hili. Katika 1 Timotheo 6:3, alionyesha wazi kwamba mafundisho yanapaswa kuwa: *"maneno ya kweli ya Bwana Yesu Kristo na ...ya uchaji mungu."* Wakati Bwana Yesu Kristo alianza huduma yake, Alionyesha hali ya uungu inajumlisha. Siku moja wakati alikuwa katika sinagogi, Bwana alisoma kitabu cha Isaya, alitaja kwamba angeleta habari njema kwa maskini, na uhuru kwa wafungwa, kufunguliwa macho kwa vipofu (Luka 4:18). Matendo haya yanaonyesha matendo ya upendo kwa wengine, yanastahili ucha Mungu. Pia, Yesu alikuwa na huruma kwa umati uliokuwa bila msaada (Mathayo 9:36). Pamoja na vitendo vyake vya huruma yake, udhihirisho wake mkubwa wa upendo wa huruma ulikuwa kujitoa kwa kifo msalabani kwa ajili yetu s (Wafilipi 2:8).

B. Kutosheka

Kamusi ya mtando inafafanua "kutosheka" kama: *"hali ya furaha na kuridhikika."* Katika Kigiriki, neno hili ni *'autarkeia'*, kumaanisha *'kujitosheleza'* na lilitumika na wanafilosofia wa Stoic kumweleza mtu ambaye hasumbuliwi na mazingira ya nje. Ni lazima Wakristo watosheke na kuridhika, bila kuhisi hitaji la kutafuta vingi zaidi ya yale Mungu tayari amewapa. Kristo ndiye chanzo cha kutosheka kwa kweli (2 Wakorintho 3:5; 9:8, Wafilipi 4:11-13:9).

C. Faida za Kutosheka kwa Uungu

Katika 1 Timotheo 6:6, mtume Paulo alisema kwamba kuna faida kubwa wakati ucha mungu unaambatana na kutosheka. Ucha mungu, kama kitendo kingine cha upendo, wakati ni halisi, mara nyingi inamaanisha dhabihu. Hivyo, Bwana Yesu alikuja na kujitoa msalabani Kalvari: *"Yeye, kwa asili alikuwa daima Mungu; lakini hakufikiri kwamba kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kung'ang'ania kwa nguvu. Bali, kwa hiari yake mwenyewe, aliachilia hayo yote, akajitwalia hali ya mtumishi, akawa sawa na wanadamu, akaonekana kama wanadamu."* (Wafilipi 2:6-7) Fikira ya mwanadamu inasema kwamba, je, mkono mtupu wawezaje kutufanya tuwe na furaha? Hata hivyo, Paulo alitukumbusha maneno ya Yesu: *"... Heri zaidi kutoa kuliko kupokea."* (Matendo ya Mitume 20:35)

### II. Dhihirisho la Maisha Yaliyoridhika (1 Timotheo 6:7-8)

A. Tambua Kwamba Hatukuwa na Chochote Tulipozaliwa Na Tutaondoka Bila Kitu

Katika 1 Timotheo 6:7, Mtume Paulo alinukuu moja ya ukweli dhahiri uliombatana na maisha dunia; *"Maana hatukuleta kitu chochote hapa duniani, wala hatutachukua chochote"* Katika tamaduni zingine, watu walikuwa na desturi ya kuwazika wafu na vifaa ambavyo wangevitumia katika 'maisha ya baadaye", hasa kama walikuwa na utajiri. Hata hivyo, kwa hakika, hakuna chombo chochote ambacho

kingetumiwa. Licha ya ukweli huu wote, ni muhimu kufahamu kwamba raslimali za kifedha na bidhaa ni vya manufaa kwa maisha yetu ya binafsi, kwa misheni, na kwa upanuzi wa Ufalme wa Mungu. Mtume Paulo alifanya kazi ili kupata mapato, na kwa sababu hii alisema: *"...Mtu yeyote asiyependa kufanya kazi, asile chakula"* (2 Wathesalonike 3:10).

B. Kufurahia Maisha Rahisi

Moja ya sifa ya dunia tunayoishi ni mazoea ya kununua vitu kbila kukoma. Kinyume na haya, 1 Timotheo 6:8 inatutia moyo kutafuta kuridhika katika mambo madogo ya maisha. Neno la Mungu linatuhimiza kutumia mali yetu kwa hekima: *"Mbona mnatumia fedha yenu kwa ajili ya kitu kisicho chakula, ya nini kutoa jasho len kwa kitu kisichoshibisha?"* (Isaya 55:2). Asili ya mwanadamu iliundwa kutambua vizuri malengo. Katika bustani la Edeni, Mungu alimpa Adamu na Hawa mamlaka ya kusimamia nchi (Mwanzo 1:28); Mungu aliwapa uwezo wa kufanya hivyo. Kwa bahati mbaya, kuanguka kuliharibu mpango wa Mungu. Hivyo sasa, sisi wanadamu ni lazima tufanye kazi ili kukutana na mahitaji yetu. Tamaaa ya kuwa na nyingi na wala zisichukue nafasi yetu ya kumtegemea Mungu, uchaji mungu, na kutosheka. Ni lazima turidhike kwa kuwa na mahitaji, kufanya kazi, na kuwa tayari kushiriki (Waefeso 4:28). Hii ndiyo siri ya kuwa na furaha.

### III. Matokeo ya Kutotosheka (1 Timotheo 6:9-10)

A. Majaribu, Ulafi na Uharibu

1 Timotheo 6:9 inasema kwamba: *"Lakni wale wanaotaka kutajirika haunguka katika majaribu, na kunaswa katika mtego wa tamaa nyingi mbaya za kipumbavu, ambazo huwavuta mpaka kwenye uharibifu na maangamizi."*

Kuondolewa kutoka kwa Mungu huzaa ndani yetu mioyo nyingi iliyo migumu ambapo tunaita vitu vizuri kuwa vibaya na vibaya kuwa vizuri (Waefeso 4:17-19). Kutafuta kwa wema wa mtu ambapo tunaweza kutosheka ni muhimu kwa Mungu, lakini hatuwezi kuupata bila yeye. Kuingia kwa majaribu kunaweza kutuelekeza kwa matokeo mengi ambayo ni hasi, kutoka kwa inayoonekana nzuri hadi mbaya kabisa. Kutafuta kwa kwa wema wa binadamu bila Mungu huleta majaribu ya uasherati haramu, upweke na ulafi – vyote vikilaumiwa na Mungu (Kutoka 20:17).

B. Maangamizo na Uharibu

Katika siku za hivi karibuni, tumeona mtando ukiwasilisha matukio ya ufisadi serikalini na vichwa vikubwa. Kabla ya ripoti, tulikuwa tumewapa heshima wale wanaotekeleza shuhguli za serikali. Hata hivyo, mashtaka, shutuma na hata lawama za idadi kubwa ya maafisa katika ngazo zote, ikiwa ni pamoja na uwanja wa michezo, umesababisha hasira ya raia (Mithali 29:2). Hii imesababisha pia kupoteza kwa watu na familia za o, hata kwa wale waliotaka kuwa na maisha ya he shima; sasa wanaishi kwa kuangaliwa na ishara.

C. Kupoteza Kwa Imani

1 Timotheo 6:10 inasema, *"Kwa maana kupeda sana fedha ni chanzo cha uovu wote."*

Katika kifungu hiki, maneno ya msingi ni "kupenda sana". Kama vile tulivyosema, pesa ni raslimali muhimu. Hata hivyo, kama vile msemo unavyosema: *"Pesa ni mtumwa mzuri; bali Bwana mbaya."* Katika mwaka wa 2008, kulikuwa na changamoto za kifedha ambazo zilitishia kuanguka kwa nchi zote za ulimwengu ulioendelea. Iliwekwa wazi na ile ilitajwa kama *"hofu ya fedha"*. Nakala nyingi zimechapishwa baada ya tukio hilo baya, na kwa zote, ni rahisi kutazama jinsi *"kupenda pesa"* ilikuwa chanzo cha matatizo. Mungu anasema: *"Fedha na dhahabu yote duniani ni mali yangu"* (Hagai 2:8). Wakati imani yetu imewekwa kwa mabati haya, imani yetu inakoma kuwa ya *"Kikristo"* na kuwa ya sanamu. Hiyo ilikuwa uzoefu wa watu wa Israeli jangwani (Kutoka 32).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni nini inapaswa kuwa mafundisho sawa kulingana na mstari wa 3?
- Je, utafafanuaje mtindo rahisi wa maisha leo (I Timotheo 6:8)
- Je, ni hatua gani za vitendo unaweza kuchukua ili kuzuia matokeo ya *"kutoishi katika kutosheka"?* (mistari ya 9-10).

## HITIMISHO

If we'recontentwithwhat wehavenowanddon't worry about things, we can trust the owner of all the silver and gold to help us have what we need to cover our needs, and at the same timeexperience the joy of sharing.

## Somo la 22:

### TOSHEKA!

**Lengo la Somo:** Kuelewa kuwa mapenzi ya Mungu kwa watoto wake ni kuishi kwa kutosheka.

**Methali:** Mtaka yote hukosa Yote

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Timotheo 6:3-10

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Basi kama tunacho chakula na mavazi, tunapaswa kuridhika navyo." 1 Timotheo 6:8

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?


Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?

Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?

Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Kumtumainia Mungu kunatusaidia kutosheka na kushiriki na wenzetu



| Somo la 23 | TULILINDE HEKALU! |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Wakorintho 6:12-20 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza kwamba miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu na tunahitaji kuilinda. | "Je, hamjui kwamba miili yenu ni hekali la Roho Mtakatifu aliye, ambaye mlimpokea kutoka kwa Mungu? Nyinyi basi, si mali yenu wenyewe?" **1 Wakorintho 6:19** |

## UTANGULIZI

Biblia inatufundisha kwamba Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu na kutuwezesha kuabudu Mungu wetu anayeishi na wa kila mahali. Katika Agano la Kale, mahali pa kukaa pa Mungu palikuwa hema ya mkutano. Leo, kila mwumini ni ya ambapo Mungu anaishi kwa njia ya Roho Mtakatifu. Kwa hivyo, ikiwa mwili wetu ni makao ya Mungu, tunapaswa kujali kwamba hakuna sehemu yako iliyochafuliwa. Hii pia inamaanisha kwamba ni lazima tuwe waangalifu kwamba akili zetu (mawazo) ni safi na takatifu, kwa sababu Biblia inasema katika Wafilipi 4:8: *"Hatimaye, ndugu zangu, zingatieni mambo mema na yanayostahili kusifiwa; mambo ya kweli na bora; mambo ya haki, safi, ya kupendeza na ya heshima."*

### I. Je, Tunatumiaje Miili Yetu?

Wanafalsafa wa Plato waliamini kwamba mwili ulikuwa wa mali na ulioharibika, na kwa hivyo ulikuwa mbaya, na hivyo ni roho tu ndiyo ilikuwa ya uzima. Waumini wapya wa Korintho ambao Paulo aliwaandikia walishawishiwa na wazo hili. Wengine hawakuamini katika ufufuo. Paulo alikuwa wazi katika 1 Wakorintho 15 kwamba kutakuwa na ufufuo wa mwili. Paulo pia aliwafundisha katika 1 Wakorintho 6:12 kwamba Mungu ametupa hiari ya buri ya kuchagua vizuri: *"Kwangu mimi kila kitu ni halai. Sawa; lakini si kila kitu kinafaa. Nakubali kwamba kila kitu ni halali kwangu lakini sitaki kutawaliwa na kitu chochote."* (1 Wakorintho 6:12)

Paulo aliwaambia Wakorintho wazi kwamba kama watu waliozaliwa upya na Bwana wetu Yesu Kristo, miili yao ilihusishwa katika mabadiliko yaliyofanywa na Bwana, wakiunda hema yao wenyewe (mahali pa Mungu pa kukaa) ambayo haipaswi kuchafuliwa. Kwa mafundisho haya mawazoni, tunapaswa kubaki huru kabisa kutoka kwa michafuko yoyote inayokuja kuvamia miili yetu, nafsi na roho. *"Hapa Bwawna ni Roho, na pale alipo roho wa Bwana ndipo ulipo uhuru."* (2 Wakorintho 3:17)

### II. Dhambi Ambazo Zinaharibu Uadilifu na Afya ya Mwili

Kama tu vile hema ya mkutano ilikuwa mahali pa Mungu pa kukaa wakati wa Musa (Kutoka 26, 27, 33:7-11), leo mwili wetu ni hekalu na makao ya Bwana, *"Je, hamjui kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, ambaye mlimpokea kutoka kwa Mungu? Nyinyi basi, si mali yenu wenyewe."* (1 Wakorintho 6:19) Tunaweza kusema tumeumbwa na sehemu kadaa: mwili, nafsi na roho (1 Wathesalonike. 5:23). Kwa hivyo, ni jukumu letu kuulinda mwili tuliopewa na Mungu kwa sababu anakaa anakaa ndani yake kama sisi ni wana na binti wa Mungu (Waefeso. 1:13). Je, ni dhambi gani ambayo inaweza kuharibu uadilifu na afya ya mwili?

Dhana ya kihistoria ya jamii ya kanisa la Korintho ilikuwa imejaa uzinzi. Juu ya mlima wa Korintho kulikuwa na hekalu la mungu wa kike Afrodite, ambapo zaidi ya makahaba elfu waliajiriwa kama makuhani wa kike, na ngono ilikuwa sehemu ya ibada ya kuabudu. Mtume Paulo aliwaonya waumini katika 1 Wakorintho 6:13-18 "*Wajiupushe na uzinzi."*

Dhana tunayoishi sasa haiwezi kuwa tofauti na ile ya kanisa la Korintho. Leo katika sehemu nyingi, kuna moteli na danguro ambapo wanawake na wanaume wanatekeleza vitendo vya uzinzi. Hivyo nasi pia tunpaswa kufuata onyo la *"Kujiepusha na uzinzi."*

Kuna pia hila nyingine na ya hatari zaidi inayosubiri watu wa Mungu: ukafiri wa kiroho bila kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu, kutokuwa mwaminifu. Paulo alimwambia Timotheo: *"tukikosa kuwa waaminifu, yeye hubaki mwaminifu daima, maana yeye*

*hawezi kujikana mwenyewe"* (2 Timotheo 2:13a). Tunapokuwa karibu na Mungu, tunafanya yale yanayompendeza: *"Lakini aliyejiunga na Bwana huwa roho moja naye."* (1 Wakorintho. 6:17)

Kwa hivyo, tuwe waangalifu na waelekevu katika kutembea na kushiriki na Bwana. Tunahitaji kumpenda kwa mioyo yetu wote. Tukimekeuga Bwana, uadilifu wetu utaangamziwa, tutakuwa kitu bure (Yohana 15:15).

### III. Njia za Kumtukuza Mungu katika Mwili Wetu

Kama vile tumetaja, tumeundwa na mwili wa vitu tofautu, nafsi na roho *"Mungu mwenyewe anayetupatia amani awatakase nyinyi kabisa kwa kila namna na kuzilinda nafsi zenu-roho, mioyo na miili yenu-mbali na hatia yoyote wakati wakuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye anayewaita nyinyi atafanya hivyo kwani ni mwaminifu!"* (1 Wathesalonike 5:23) Kama tu vile Waisraeli walimwabudu katika hema, tunaweza na tunapaswa kumtukuza Bwana katika miili yetu (1 Wakorintho 6:20). Lakini tunaweza kufanya hivi kwa njia gani? Hapa kuna baadhi ya mapendekezo.

A. Kumtukuza Mungu Katika Mwili Wetu

Tunahitaji kukuza mwili wetu afya, tuwe waangalifu ni nini tunakula kama vile Danieli alivyofanya (Danieli 1:8). Katika tamaduni yetu ya kisasa, kuna vyakula vingi visivyokuwa na afya. Chakula cha taka kinaweza kuwa kitamu, lakini kinaweza kuwa cha uharibifu kwa miili yetu. Chakula bora kulingana na nafaka, samaki na nyuama nyeupe, na matunda na mboga ya kutosha itatoa chanzo muhimu cha protini, vitamini na madini, n.k. ambavyo tunahitaji ili kutuweka na afya na wenye nguvu. Tunahitaji kula kwa wakati unaofaa. Tukila milo yenye usawa kwa mtindo mzuri, tutakuwa tunailinda miili yetu kama mahali Mungu anakaa. Tunajua kwamba kama wana na mabinti wa Mungu, tulinunuliwa kwa gharama (1 Wakorintho 6:20).

Tunapaswa kuangalia kile tunachokunywa. Tunajua kwamba pombe ni hatari na inaweza kusababisha ulevi, lakini pia soda au maji mengine ya matua huharibu miili kwa sababu vinakuwa na sukari nyingi. Tunapaswa kunywa maji zaidi. Kila kitu kinachosababisha ulevi (utegemezi) ni hatari kwa mwili.

B. Kumtukuza Mungu katika "Saikolojia" Au Nafsi

Kuna aina mbili ya kufikiria. Acha tuone ni gani:

- Ø Mawazo yasiyokuwa ya sumu hututia motisha na kuhimiza hiari yetu (moyo) kutenda matendo mazuri. Chanzo cha mawazo mazuri (yasioyokuwa ya sumu) hutegemea Neno la Mungu, ambalo hutusaidia kutambua yaliyo mema na yaliyo maovu (Zaburi 15:1-5, 24:3). Hivyo, tunaweza kushughulikia ile sehemu ya hema ya mtu binafsi kwa kulisha akili zetu kila wakati na Biblia. Katika hali hiyo, tunaweza kumtukuza Mungu kwa mawazo yetu (Luka 6:45a).
- Ø Mawazo ya sumu ndiyo yanachafua fikra zetu na kuvuruga uhusiano wetu na Mungu. Haya yatamwelekeza mtu kukosa kumtukuza Mungu kwa matendo yake. Biblia inasema kwamba fikira zetu zitatuelekeza kwa matendo. Je, ni aina gani ya fikira tunazoruhusu kuwa nazo na ni ushuhuda gani ambao tunatoa?

Kwa kumtukuza Mungu katika roho yetu, sehemu ya tatu ya hema ya mtu binafsi, tunapaswa kutatufa kujazwa na fadhila za tunda la Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22-25). Tunahitaji kukuza talanta ambayo Mungu ametupa, tukiziangazia na kuzitumia kwa ajili ya huduma yake na kwa kujenga kanisa lake.

Ni lazima tuendelee kusoma Biblia kila wakati. Kusoma na kutafakari juu ya Biblia kutatuelekeza kwa njia ya haki na tutamfuata Bwana Yesu. Zaidi, inatupatia nguvu za kuweka mafundisho yake kwa vitendo, na kushiriki na wengine, kwa sababu kuu ya kumtukuza Mungu.

## MASWALI YA ZIADA

- Kulingana na 1 Wakorintho 6:19, je, mwili ni nini?
- Je, ibada ya sanamu ni nini, na inazaa nini ndani ya mtu?
- Orodhesha matendo ambayo unaweza kumtukuza Mungu katika mwili wetu.

## HITIMISHO

Na tumtukuze Mungu kwa miili yetu, kama hekalu za Roho Mtakatifu. Tusiiharibu. Tuachane na kila kitu ambacho kinaweza kuumiza miili ili tuishi maisha ya kumtukuza Mungu wakati wote.

## Somo la 23:

## TULILINDE HEKALU

**Lengo la somo:** Kuelewa ya kuwa miili zetu ni hekalu ya Roho-Mtakatifu na yatupasa kuilinda.

**Methali:** Moyo wenye amani huupa uhai mwili.

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Wakorintho 6:12-20

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mwapaswa kujua kwamba miili yenu ni hekalu ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu yu ndani yenu. Mmepokea Roho-Mtakatifu kutoka kwa Mungu. Nyinyi si mali yenu wenyewe" 1 Wakorintho 6:19

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?
Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?
Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?
Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Mwili ni mtakatifu, uuweke ukiwa Mtakatifu.



| Somo la 24 | MUNGU ANAYEPONYA |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Wakorintho 6:12-20 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuangazia ugonjwa nini nini, na jinsi Mungu anataka kuabiliana nao. | "Yule mtu aitwaye Yesu alifanya tope, akanipaka machoni. Akaniniambia niende Siloamu nikanawe. Hivyo, Nilienda nikanawa, na nikaweza kuona" **Yohana 9:11** |

## UTANGULIZI

Ugonjwa umekuwepo tangu wakati wa kuanguka kwa mwanadamu, na kuna imani na tafsiri nyingi juu vile tunagonjeka. Hapa kuna baadhi ya maswali: Je, Mungu husababishwa ugonjwa? Je, tunagonjeka kwa sababu tumetenda dhambi? Je, Mkristo anapaswa kugonjeka? Je, Mungu mara nyingi huponya? Maswali haya ni ya muhimu kuanza darasa, na tutapata majibu wakati wa darasa.

### I. Ufafanuzi Juu ya Magonjwa (Yohana 9:1-3)

A. Ufafanu wa Kiyahudi

Yesu alikutana na watu wagonjwa ambao alijaribu kusaidia, na wakati huo, pia mawazo ya Kiyahudi juu ya ugonjwa. Kulingana na imani hizi za Kiyahudi, wanafunzi walitaka kujua ni nani aliyekuwa ametenda dhambi, mtu aliye kipofu tangu kuzaliwa au wazazi wake (mstari wa 2). Wayahudi walikuwa wanadajili kwa karne nyingi tatizo la kama mtu arithi ugonjwa au kwa sababu ya dhambi za mtu binafsi. Tunapaswa kujiuliza maswali yafuatayo: Je, ni nini chanzo cha magonjwa? Je, ni kwa nini watu wengine wanazaliwa wakiwa vipofu, viziwi nlk.? Jibu ni kwamba kila kitu kilikuja kwa sababu ya kuingia kwa dhambi ulimwenguni.

B. Ufafuniwa wa Kuharibu

Katika hali hiyo ambayo Wayahudi walikuwa na ufafanuzi wao juu ya magonjwa, makanisa leo pia wanatoa mawazo mengi ya sasa na ufafanuzi juu ya kichwa hiki, kama kukiri kwa imani, na pia ufafanuzi hasa wa waumini. Tunaenda kuchambua baadhi ya ufafanuzi ulioenea na wa kuahribu ambao umepata nafasi katika mikutano ya Kikristo.

1. Ugonjwa Unasababishwa na Ibilisi

Kuna sababu zingine ambapo kupagawa na pepo kunaweza kusababisha ugonjwa na kwamba baada ya kuwekwa huru, mtu anaponywa kabisa. Yesu, katika hali nyingi, alikemea mapepo ambayo yalikuwa ndani ya mwili wa mtu, na kuwaponya maradhi waliyoumia (Mathayo 9:33, 17:18, Luka 8:29-35). Lakini haya yanatendeka tu kwa wale wasio Wakristo ambao hawajakutana na uwepo wa Mungu.

2. Wakristo Hawagonjeki Kamwe

Hakuna mahali katika Maandiko pameeleza kwamba Wakristo hawagonjeki; uzoefu wetu unathibitisha kwamba haya ni ya uongo. Sisi sote tunagonjeka, wengine zaidi na wengine kidogo, lakini ugonjwa mara nyingi hugusa mlango wetu. Biblia inathibitisha kwamba Mungu ana nguvu ya kutuponya (Kutoka 15:26), na kwamba Yuko upande wetu wakati wote (Mathayo 28:20).

3. Watu Wanagonjeka Kwa Sababu ya Ukosefu wa Imani

Tunaweza kuponywa kwa imani kama ni mapenzi ya Mungu. Yeye ndiye anayeponya, na hata kama mtu anazo imani zote za ulimwengu, mapenzi ya Mungu ni ya enzi. Kwa hivyo, mwumini anaweza kuteseka, na si kwa sababu ya ukosefu wa imani. Mungu ni Mungu anayeponya, haijalishi kama uko na imani au la. Hata hivyo, ingawa imani ni muhimu, hata wakati mtu ana shaka hii si kizuizi kwa mapenzi ya Mungu kuponya mtu.

### II. Mapenzi ya Mungu Katikati ya Magonjwa (Yohana 9:4-5)

Jambo la muhimu ambalo kifungu cha kusoma kinanukuu ni kwamba mtu huyu alikuwa kipofu hadi Yesu alipokuja kumponya. Wakati Wayahudi walikuwa wakijadili upofu

wa huyu mtu ulitoka, na kisha akapona, Yohana alisisitiza kwamba Yesu alimaliza hali ya mtu kipofu.

A. Magonjwa Kwa Waumini

1. Yote Ni kwa Utukufu Wa Mungu Kung'aa

Ugonjwa wa mtu kipofu ulionesha kwamba Yesu alikuwa Mungu; alionyesha nuru yake (Yohana 9:5). Ugonjwa unaturuhusu kupata kumjua Mungu kama mponyaji. Njia pekee tutapata kumhisi Mungu anayeponya ni wakati tumekuwa wagonjwa na Mungu ametenda mwujiza. Mara nyingi, ni kupitia miujiza ya uponyaji wa uungu ambapo watu hujithibitishia katika imani na wengine kuja kwa maarifa ya kweli. Lakini kama Mungu hatendi miujiza, utukufu wake pia unajionyesha kwa watoto wake wanaokabiliana na ugonjwa kwa amani, wakijenga ushuhuda wa hadharani wa ukuu wa Mungu.

2. Kila Kitu Hutimiza Kusudi Katika Maisha Yetu

a.) Zinatuthibisha katika imani yetu. Tunamjua Mungu katika uzoefu wetu, tunaona ulinzi na kujali kwake siku baada ya siku. Katikati ya majaribu, Anaonekana zaidi.

b.) Uongofu wa Kristo. Unamruhusu mwumini kuwahubiria wengine walio katika hali kama yao, na kupitisha ujumbe wa tumaini na habari njema ya wokovu. Familia ambayo haimjui Kristo huona mfano wa kufuata, na hospitali na kushauriana na daktari kunakuwa mimbari bora.

c.) Umoja wa Familia. Katika hali nyingi za mgawanyiko wa familia, ugonjwa huleta umoja ambao Mungu hutumia kuunganisha famila.

d.) Miujiza ya uponyaji inaweza kutendeka. Mungu anaweza hata kutumia sayansi ya madawa.

B. Magonjwa Kwa Wasio Waumini

Waumini pia na wasio waumini hugonjeka, ni sehemu ya maisha baada ya Edeni. Moja ya madhumuni ya kimsingi ambayo magonjwa hutimiza ndani ya wasio waumini ni kuwaleta kwa ufahamu wa uwepo wa Mungu na kumkubali katika mioyo yao, ingawa haya hayafaulu mara nyingi.

**III. Njia Za Ajabu za Kuponya (Yohana 9:6-12)**

Ukweli wa Kimaandiko ni kwamba Mungu ndiye anayeponya, na anafanya hivyo kwa mapenzi yake, kuptia yule anayetaka, wakati anataka, na yule anayetaka.

A. Kujua Uponyaji wa Mungu

Jambo ambalo mtu kipofu na wale waliokuwa karibu na Bwana hawakutarajia ni kwamba atatema mate na kutengeneza tope, na kupitia kwa tope hili apake macho ya kipofu, na kumwauru anawe katika kisima cha Siloamu ili apone (Yohana 9:6-7). Haikuwa mate, au tope, au kisima, bali mtu aliyehusika - Yesu! Si matendo ya mwanadamu ambayo mtu hufanya inayotenda miujiza, ni Mungu anayestahili utukufu.

B. Misheni ya Kuombea Uponyaji

Watoto wote wa Mungu, bila kubaguliwa, wana mamlaka ya kuwaombea wagonjwa ili waponywe na yeye. Jukumu hili ni la kanisa lote. Ni kanisa, kama mwili wa Kristo, ambalo linawajibika kutekeleza hitimishola misheni ya Mungu, na sehemu ya kimsingi ni kuombea uponyaji. Kanisa la Mnazareti, katika Kanuni yake ya Imani namba 14, inahimiza washirika wake kuomba maombi ya imani kwa wagonjwa.

## MAZWALI YA ZIADA

- Je, ni fafanuzi gani zilizo na ubaguzi ambazo kanisa la sasa linalo juu ya magonjwa?
- Taja vipengele vya watu wanaoishi na ugonjwa.

## HITIMISHO

Kuna ufafanuzi tofauti ya kwa nini watu hugonjeka. Hata hivyo, tunapaswa kuwa wazi kwamba ugonjwa uliingia kwa mwanadamu baada ya kuanguka kwa Edeni. Habari njema ni kwamba Mungu yuko tayari kuwaponya watu wake kulingana na mapenzi ya matakatifu na kamilifu. Vile anavyofanya inatofautiana. Vile vile, kanisa ni lazima likumbuke kwamba sehemu ya misheni yetu ni kuombea uponyaji wa watu, na kutumaini kwamba Bwana atafanya kulingana na mapenzi yake.

**Somo la 24:**

## MUNGU ANAYEPONYA

**Lengo la Somo:** Kuangazia juu ya maradhi ni nini, na vile Mungu anataka tukabiliane nayo.

**Methali:** Anaye shida ya Tumbo ndio hukimbia kuufungua mlango.

**Kifungu cha Kusoma:** Yohana 9:1-12

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?

Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?


Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?

Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mtu yule aitwaye Yesu alinifanya tope, akanipaka macho akaniambia, niende Siloamu nikanawe. Basi nikaenda nikanawa na nikarudi nikiwa ninaona." Yohana 9:11

**Himizo la Hadithi:** Mungu yuko tayari kutuponya kulingana na mapenzi yake.



| Somo la 25 | TUMAINI LETU KUBWA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Yohana 9:1-12 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza jinsi ya kuweka imani yetu kwa vitendo; na wakati tunakutana na kifo, tutumaini katika nguvu za ahadi ya Bwana Yesu Kristo. | "Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi ufufuo na uhai. Anayeniamini mimi hata kama anakufa, ataishi.'" **Yohana 11:25** |

## UTANGULIZI

Swali muhimu sana katika dini yoyote ni lile linalohusu kifo. Kuna maswali yanayohusu maisha; lakini jambo kubwa ni kifo. Kristo anatupatia faida nyingi sasa, lakini faida kubwa zaidi ni uzima wa milele. Kwa hivyo ni muhimu kuuliza swali lifuatalo: Je, wafu watafufuka tena? Maisha ni mafupi. Mtu yeyote ambaye amempoteza mpendwa anajua kwamba tumaini la ufufuo ni la msingi. Tusipokuwa na tumaini hili tunapokabiliwa na kifo, hakika tutasumbuliwa na ujinga wa ujamaa na huzuni. Lakini kuna habari njema!

### I. Jinsi ya Kukabiliana na Kifo? (Yohana 11:1-4)

#### A. Kusudi la Kifo Cha Lazaro

Yesu alipopokea habari kwamba rafiki yake Lazaro alikuwa mgonjwa, alisema kwamba ugonjwa wake hautamwelekeza kwa kifo (mstari wa 4). Kwa hayo, alikuwa anamaanisha kwamba kifo hakitakuwa matokeo ya ugonjwa kwa sababu ingawa ilikuwa kweli kwamba Lazaro alikuwa anaenda kufa, kaburi halingeweza kukaa na mwili wa rafiki yake kwa muda mrefu. Tunapaswa kuelewa, kwa hivyo, kwamba Bwana alikuwa anatarajia kuwa kifo hakingekuwa cha ushindi, lakini tungeshindwa wakati alimfufua rafiki yake kutoka kwa wafu.

Maelezo *"utukufu wa Mungu"* katika injili yanatumiwa kumaanisha sifa za Mungu ambazo zinaonyeshwa kwa watu. Na siku hiyo, Bwana Yesu Kristo alitokea kama *"ufufuo na uhai"* (mstari wa 25), kati ya sifa zake mbili zinahusiana sana kwa mahitaji ya msingi ya mwanadamu.

#### B. "Bwana, Unayempenda ni Mgonjwa" (mstari wa 3)

Hapa tunao mfano mzuri wa jambo la kwanza ambalo sisi Wakristo tunapaswa kufanya tunapokuwa wagonjwa au tunapitia magumu yoyote, tunapaswa kumtafuta Bwana. Ni kweli kwamba hatuwezi kufanya hivyo kwa njia ya kimwili, kama vile Mariamu na Martha walifanya, lakini tunaweza kuja kwake kila wakati kupitia maombi yetu. Hakika, hii haimaanishi kwamba tusitumie njia zingine za kurejesha afya yetu. Kwanza, tunapaswa kuleta magonjwa yetu kwa Bwana kupitia maombi na kumtumaini kabisa, na pia kuwashukuru ndugu na dada zetu kwa kutuombea. Na kwa ujumbe ambao dada wa Lazaro walikuwa nao kwa Yesu, kulikuwa na maelezo muhimu na nzuri sana ambayo tunaona: *"Bwana, umpendaye ni mgonjwa…"* (mstari wa 3) Hawakuongeza jambo lingine lolote, hakufanya ombi la hitaji yoyote. Walikuwa na ujasiri mkubwa kwamba Bwana angefanya kile walifikiria ni bora.

### II. Hitaji la Kuomboleza (Yohana 11:5-16)

#### A. Uchungu Kadhaa

Katika ulimwengu huu, kila kiumbe kinafuka. Ni wale tu ambao hawaishi ndio hawatakufa, kwa kuwa kifo ni sehemu ya maisha isiyotenganishwa. Tunakibeba pamoja nasi kila wakati na hakika ni lazima. Tunajua na hukakika kwamba tutakufa. Lakini hapa tunahitaji kujiuliza: Je, tutakabilianaje na ukweli? Je, utahisije juu ya kifo cha mpendwa? Hakika…Uchungu! Huzuni! Mateso machungu zaidi!

#### B. Uchungu ni Sehemu Ya Maisha

Kifo husababisha uchungu! Ni Kawaida … Hakuna mtu anayetaka mpendwa wao kufa. Ni jambo la huzuni na uchungu zaidi linaoweza kutendeka. Yohana anatueleza kwamba wakati Yesu aliwafika katika nyumba ya familia ya wapenwa, dada zake Lazaro walikuwa na huzuni mkubwa sana, wakilia wasitaka kufarijiwa. Katika mstari mfupi wa maneno mawili tu, Biblia inaeleza jinsi Yesu, ambaye ni Mungu na mtu wa kweli

aliguzwa:: *"Yesu alilia"* (Yohana 11:35).

C. Wakati wa Kuomboleza

Ni sawa kulia wakati tunateseka na machungu ya kumpoteza mpendwa. Tunaweza kulia kwa ajili ya machungu yetu, na tunaweza kulia kwa ajili ya machungu yaw engine. Acha tuondoe huzuni na msaada na tufarijiane katika hali kali ya kifo. Lakini baada ya muda mkali wa wakati huo, baada ya siku au miezi za asili na zilizo muhimu za kuomboleza, acha tuendelee kuishi!

## III. "Mimi Ndimi Ufufuo na Uzima" (Yohana 11:17-44)

A. "... Ungelikuwa Hapa..."

Mara tu dada zake Lazaro waliposikia kwamba Yesu anakuja kuwaona, Martha aliondoka kwa haraka kukutana na Yeye, ambapo Mariamu alibaki (mstari wa 20). Mara tena, dada hawa walionyesha jinsi walivyokuwa tofauti. Martha kila wakati alikuwa mtendaji, kukasirika hara, kutkuwa na uvumilivu, ambapo Mariamu alikuwa mpole, wa kufikiria, kutafakari. Hata hivyo, wakati dada wote walikutana na Yesu, wote wawili walisema kitu kimoja: *"Bwana, kama ungalikuwa hapa, kaka yangu hangalikufa!"* (mistari ya 21, 32). Hakika, haya ndio yale wawili wangesemezana wakati wa machungu ya ndugu yao Walionyesha imani, bali wakati huo huo kutoamini kunaonekana. Wanawake hawa hawakuwa na shaka za nguvu za Bwana za kumponya ndugu yao, kama angelikuwepo.

B. "Lakini najua kwamba hata sasa chochote utakachomwomba Mungu, atakupa" (mstari wa 22)

Licha ya machungu yake yote, Martha bado aliamini kwamba Mungu alifanya kazi kwa nguvu kupitia Yesu. Tumaini lake ndani yake lilibaki bila kutingizika. Kwa kweli, alitumaini kwamba bado angefanya jambo kwa sababu alijua kwamba Mungu alisikia maombi yake (mstari wa 22). Lakini hapa tunaona mawazo ya kuyumbayumba na ya kuchanganya ambayo Martha alikuwa nayo juu ya Yesu. Alizungumza kana kwa Yesu alikuwa tu nabii mwanadamu ambaye hakuwa na nguvu za kutegemea, kana kwamba hangeweza kuamrisha uponyaji yeye mwenywe bila kumuomba Mungu. Kwa upande mwingine, ingawa alisema kwamba Mungu angempa "kila kitu" alichokiomba, ilionekana kwamba kwake Martha, suala la ufuffuo wa nduguye Lazaro halikuhusushiwa.

C. "Ndugu Yako Atafufuka Tena" (mstari wa 23)

Maneno ya kwanza Bwana wetu alitangaza pake Bethania ni ya kipekee. Alimwahidi Martha kwamba ndugu yake Lazaro atafufuka kutoka kwa wafu. Lakini Martha bado alikuwa anapambana na imani yake na hangeweza kutafsiri ufufuo ulioahidiwa Yesu kama ukweli wa wakati huu. Aliutafsiri tu kuwa wa siku ya mwisho (mstari wa 24). Kwa kweli, muda mchache baada ya Yesu kuagiza jiwe liondolewe kwenye lango la kaburi, Martha alioneka kuwa bado hakuamini kwamba Yesu alikuwa anaenda kumfufua ndugu yake, na yote angesema ilikuwa kwamba alikuwa tayari ananuka uvundo kwa sababu alikuwa amekufa kwa siku nne (mstari wa 39).

"Mimi ndimi Ufufuo na Uhai …" (mstari wa 25)

Martha aliamini kwamba Mungu angempa Yesu kila kitu alichoomba, lakini muda huo, Bwana alimwambia kwamba Yeye mwenyewe alikuwa na mamlaka na nguvu za kupeana uhai na kuurejesha kwa njia ya ufufuo (mistari ya 25-26). Yeye ndiye *"Mwandishi wa uhai"* (Matendo ya Mitume 3:15), Mungu wa mwili, chanzo cha uhai, uwe wa kiroho au kimwili. Kwa hivyo, hakuna mtu mwingine ila yeye tu angesema maneno kama haya: *"... Mimi ndimi ufufuo na uhai ..."* (mstari wa 25). Katika mstari wa 26, Yesu alisema: *"na kila anayeishi na kuniamini hatakufa kamwe."* Waumini watakumbolewa kutoka kwa kifo au uharibifu wa milele kwa nguvu za Bwana.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, Bwana ana kusudi la maisha yetu katika hali ngumu tunayokutana nayo? Eleza
- Kwa ufupi eleza hapa kama ilivyo na kulia kwa Yesu (mstari wa 35)
- Kwa ufupi jadili matokeo ya maneno ya Yesu kwamba yeye ni uhai wa imani yako binafsi..

## HITIMISHO

Wakati tuko katikati ya uchungu mkali usioweza kueleweka wa kifo cha mpendwa, tunahitaji kuweka imani yetu katika vitendo. Bwana yuko tayari kila wakati kutufariji kupitia Roho wake Mtakatifu! Tunahitaji kutumaini katika nguvu za ahadi za Bwana Yesu Kristo, na kuendelea kuishi na yeye, tukijua kwamba kifo hakikomeshi kila kitu. Yeye ni ufufo na uhai!

**Somo la** 25

## TUMAINI LETU KUU

**Lengo la somo:** Kujifunza jinsi ya kuiweka Imani yetu kwa vitendo na kutegemea Mungu kwa Matokeo

**Methali:** Mungu Hachelewi

**Kifungu cha Kusoma:** Yohana 11:1-44

**Mstari wa kumbukumbu:** Yesu akamwambia, "Mimi ndimi ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, ataishi tena" - Yohana 11:25

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?


Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?

Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?

Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?

Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Imani yetu katika Kristo inaleta tumaini la sasa na la uzima wa milele"



| Somo la 26 | KUISHI NA MAGONJWA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Yohana 11:1-44 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza kwamba tunahitaji kukubali kwa moyo mzuri mapenzi ya Mungu katikati ya magonjwa yasiyopona. | "…Neema yangu yatosha kwa ajili yako, maana uwezo wangu hukamilishwa zaidi katika Yeye." **2 Wakorintho 12:9** |

## UTANGULIZI

Mara nyingi, tumeamini kwamba tukigonjeka, lazima Mungu atuponye kwa sababu tunaomba na kukiri uponyaji. Yeye atatenda. Ingawa kama Wanazareni tunaamini katika uponyaji wa kiungu kupitia maombi ya imani au sayansi ya madawa, si lazima Mungu atuponye. Kama anvyopenda, atamponya mtu, na kumwambia mwingie: *"Neema yangu yakutosha"* (2 Wakorintho 12:9).

### I. Mwiba Wa Paulo Ndani ya Nyama (2 Wakorintho 12:1-7)

#### A. Mwiba wa Paulo

Watoa maoni wanasema kwamba Paulo awezekana alipatwa na maradhi mengi kwa muda mrefu. Wengine wanafikiria kwamba yaweza uwa ni macho yake. Alifanywa kipofu kwenye barabara ya Dameski kwa sababu ya mwakazi mkubwa wa nuru kutoka mbinguni (Matendo ya Mitume 9:3, 8), na hata kama aliponywa hapo mwanzoni, na kitu kama maganda yalikuwa yameanguka kutoka kwenye jicho (Matendo ya Mitume 9:18), kuona kwake hakika hakukuwa kuzuri. (Wagalatia 4:13-14) Pengine alihitaji mewani, ambayo haikuwa imebuniwa wakati huo. Macho yake yamekuwa yakimpa uchungu. Ugonjwa mwingine ambao anaweza kuwa aliumia ni kifafa, bidhaa labda ya kupigwa mara kwa mara aliyopata, kama vile wale alipokea katika mji wa Lustra (Matendo ya Mitume 14:19). Hatujui hakika kile Paulo alikuwa anaumia nini. Lakini mwiba huo ndani ya mwili ulionekana kuwa ugonjwa wa mwili.

#### B. Mjumbe wa Shetani

Katika dhana ya 7, Paulo aliwasilisha mwiba ndani ya mwili wake kama mjumbe wa Shetani. Inafaa kutaja kwamba katika mstari huu neno *'mjumbe'* linamaanisha *'malaika.'* Kile Paulo alikuwa anapendekeza ni kwamba kitu hiki ambacho kilikuwa kinamdunga kilikuwa cha kiroho, mjumbe wa maangamizo na kifo, asiyekuwa wa viwango wa Mungu. Chochote kilichokuwa, kilikuwa chini ya amri ya Shetani (Mathayo 25:41, Ufunuo wa Yohana 12:7). Kwa hivyo, mjumbe wa Shetani alikuwa adui na mpinzani wa Paulo. Shambulio hilo lilikuwa la mwili lililoleta usumbufu mwilini mwake. Mjumbe wa Shetani alionenaka kila wakati katika maisha ya Paulo.

#### C. Kofi Usoni

Wakati mtu anagonjeka ugonjwa usiotibiwa, ni kwa sababu Mungu ameruhusu. Anajua mtu huyo anaweza kuvumilia pigo hilo ngumu (1 Wakorintho 10:13). Hata katikati ya ugonjwa, Mungu anapima ukomavu wetu na uwezo wetu wa kupinga. Kwa hivyo, tukumbuke tusiwahukumu wale walio na ugonjwa sugu kwa kuwataja kama wenye dhambi (kumbuka yale tulijifunza katika masomo yaliyopita). Mwombaji Lazaro ni mfano mzuri kwa vile alikufa maskini, mgonjwa na peke yake. Hata hivyo, alipokufa, aliende moja kwa moja katika uzima wa milele, kinyume na tajiri alikufa katika utariji wa uchumi na marafiki zake na familia wakiwa karibu naye na akiwa katika afya nzuri, lakini mwisho wake ulikuwa mauti ya milele (Luka 16:19- 31). Licha ya mapigo magumu yanayosababishwa na ugonjwa huo, unaruhusiwa kwa kusudi la uungu.

### II. Kukumbatia Mapenzi ya Uungu (2 Wakorintho 12:8-9)

#### A. Ili Tusijivune au Kujiinua

Inashangaza kwamba Paulo alisema sababu ya mwiba wake ilikuwa uwezekano wa kujivuna (2 Wakorintho 12:7). Alikuwa mmishenari mkuu na mtume, lakini ilionekana kwamba alijaribiwa kuwa na kiburi. Kumbukua, alikuwa Mfarisayo aliyebadilishwa. Luka, mmoja wa wanafunzi wa Paulo, anaota picha katika injili yake ya Mfarisayo (Luka 18:11-12). Ukichambua Mafarisayo, hawakuwa wabaya kwa sababu hawakuwa walevi, walikuwa wazuri, hawakuwa walevi, hawakuzini,

walifunga na kutoa zaka. Lakini Mafarisayo walikuwa wamesahau jambo, kwa vile walikuwa wamejiinua na kuwapuuza wenzao (Luka 18:11).

B. "…Mara Tatu Nalimuomba Bwana …"

Je, Paulo alikosa imani? Je, Paulo alikuwa mtenda dhambi mbaya? Haikutosha kuwa alikuwa amemkubali Kristo? Je, Wakristo hawapaswi kuteseka? Kwa kuwa sisi ni Wakristo si jambo la hakika kwamba kila kitu maishani kitakuwa kamili. Si mahitaji yetu yote yanayotimizwa, lakini Bwana huwa anatuahidi uzima wa milele. Hakikisho liko, na ndio maana tunaishi kwa imani. Wakati tu tutavuka kizingi cha kifo ndivyo atapanguza machozi yetu (Ufunuo wa Yohana 21:4). Omba kwa ajili ya uponyaji, lakini tusipopona, fuata mtazamo mzuri wa Paulo.

C. "... Neema Yangu Yatosha"

Bwana wetu alimwambia mtume wake: *"...Neema yangu Yatosha..."* (2 Wakorintho 12:9). Paulo hakuhitaji kukata tamaa. Mungu hakuwa amemwacha kwa janga lake. Ametoa neema Yake. Wakati Mungu alimwambia, *"Neema yangu yatosha,"* pia anasema *"Mimi ninatosha kwa ajili yako."* Katika hali nyingine, neema ya Mungu italeta uponyaji, na kwa wengine, neema hii hii italeta nguvu za kuweza kupinga kwa matumaini ya ugonjwa huo kwa siku zao zote.

Hatupaswi kupoteza imani yetu Kwake, bali, tufuate mtazamo wa Paulo. Hakuna mwiba mwilini mwake, bali alikubali tabia ya unyenyekevu na kumtukuza Mungu kwa hilo (mstari wa 9). Tunaweza kupumzika ndani ya Mungu, kwa kuwa ametuambia kwamba wale wanaompenda, kila kitu (hata magonjwa yasiyoweza kupona) kitakuwa kizuri kwetu (Warumi 8:28). Katikati ya magonjwa yetu, tunapaswa kutegemea neema ya Mungu, na tuwe na hakika kwamba kama si mapenzi yake kutuponya.

### III. **Kumtukuza Mungu Katikati Ya Magonjwa (2 Wakorintho 12:9-11)**

A. "…Maana Uwezo Wangu Hukamilishwa Zaidi."

Je, Mungu anatahiji kukamilisha nini ndani yako? Wengine wanasema Waebrania yaweza kuwa iliandikwa na Paulo, na katika Waebrania 12:5-11, tunaambiwa kuhusu nidhamu ya uungu. Hivyo Mungu anayependa watoto wake, hututia nidhamu (Waebrania 12:6). Kama angetutia nidhamu, hatungekuwa watoto wa kweli (Waebrania 12:8). Kusudi la nidhamu ni kwamba tuhusike katika utakatifu wa Mungu (Waebrania 12:10), ambapo hakuna atakayeweza kumuona (Waebrania 12:14). Kwa hivyo, inaweza kusemwa kwamba magonjwa ni nidhamu, kwa sababu kupitia hayo, tumefundishwa na kukosolewa.

B. Kupumzika kwa Nguvu ya Kristo

Katikati ya magonjwa, nguvu za Kristo zitakuwa juu yetu. Alijeruhiwa kwa sababu ya maovu yetu, Kwa kuadhibiwa kwake sisi tumepata uhai (Isaya 53:5). Nguvu yake inaweza kutuponya papo hapo, au anaweza kuchagua kutuponya pole pole, au nguvu zake zitatusaidia kustahimili ugonjwa hadi siku tutakapofunga macho yetu. Sisi ambao tuko wazima na hatuna magonjwa sugu tunahitaji kujifunza aina ya vita ambavyo watu wagonjwa wanakabiliana nayo. Vita hivyo vinaweza kukosa tiba, na wema wetu waweza kutumiwa na Bwana kuwatia moyo ili wawe na ujasiri wa kukabiliana na ugonjwa.

## MASWALI YA ZIADA

- Kama Paulo, akiwa mmoja wa mitume wakuu wa Mungu, alipitia magonjwa, je unafikiri nini kuhusu mateso ya Wakristo kutokana na magonjwa sugu?
- Je, unaamini kwamba kama Mungu ni mwenye enzi, pia anatumia magonjwa kutuweka wakfu kwake zaidi? Eleza?
- Je, tutakabilianaje na utambuzi wa ugonjwa sugu usiotibika

## HITIMISHO

Nguvu za Kristo ziwe juu yetu na miili yetu inayodhoofishwa na magonjwa. Mungu atatudumisha na kuendelea kututumia kwa mambo makubwa (1 Wakorintho 1:27).

**<u>Somo la 26</u>:**

## KUISHI NA MAGONJWA

**Lengo la somo:** Kujifunza kukubali kwa moyo mweupe mapenzi ya Mungu tunapougua magonjwa yasiopona

**Methali:** Hata yule tai wa nguvu nyingi hutua mtini kupumzika

**Kifungu cha Kusoma:** 2 Wakorintho 12:1-9

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Neema yangu inatosha kwa ajili yako, maana uwezo wangu hukamilishwa zaidi katika udhaifu." 2 Wakorintho 12:9

**Maswali ya Kujadili**: Swali la 1. Je, ni nini kilichotendeka katika hadithi ambacho unakipa kipaumbele?
Swali la 2. Je, Kristo amekufunza nini kupitia hadithi hii?
Swali la 3. Je, Ni wapi tunaona huduma au kujali kwa Kristo katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, ni kwa njia gani muumini anafaa kujibu?
Swali la 5. Je, utashirikiaje ukweli uliochukua kwenye hadithi na mwingine wiki hii?

**Himizo la Hadithi**: Imani inatusaidia kufurahia Neema ya Mungu hata katika mapito magumu



| Somo la 27 | # JINSI YA KUHESHIMU UWEPO WA MUNGU |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Mambo ya Walawi 13-16 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba Biblia inatueleza kuheshimu uwepo wa Mungu. | "Aliwateua baadhi ya Walawi wawe wahuhdumu wa sanduku la Mwenyezi Mungu, wamtukuze, wamtolee shukrani na wamsifu Mwenyezi-Mungu, Mungu wa Israeli" **1 Mambo ya Nyakati 16:4** |

## UTANGULIZI

Licha ya maoni yetu binafsi juu ya suala, Biblia inafundisha ukweli fulani muhimu ambao Wakristo ni lazima wajifunze. Mmoja wa wahusika wa kibiblia wanaoweza kutufundisha juu ya uwepo wa Mungu ni Mfalme Daudi. Kama vile tunaona katika wimbo wa Zaburi, alimwabudu Mungu kila wakati. Somo hili linatoka kwa 1 Mambo ya Nyakati chapters 13- 16, linatufundisha jinsi tunaweza kuendea uwepo wa Mungu kulingana na amri za Neno Lake.

### I. Uwepo wa Mungu (1 Mambo ya Nyakati 13)

Moja ya maamuzi Daudi alifanya kama mfalme ilikuwa kuleta sanduku la Mungu Yerusalemu. Lilikuwa limetekwa nyara na Wafilisti (1 Samweli 4). Baadhi ya watoa maoni wanasema kwamba baada ya kusimamisha Yerusalemu kama mji wa Israeli, huu ulikuwa uamuzi muhimu zaidi wa Mfalme Daudi. Daudi alitaka kurejesha ibada sawa na hivyo kuongeza maisha ya kidini ya watu. Hii imesimuliwa katika 1 Mambo ya Nyakati 13. Zaidi ya nyingine yeyote, uamuzi huu ungemalizia hatima ya taifa la Israeli.

A. Kipaumbele Kwa Kutaniko Lote (mistari ya 1-4)

Uwepo wa Mungu ndiko hitaji muhimu ambalo watu wanalo. Mtu, kanisa au taifa linaweza kupata vitu vingi, lakini wako mbali na uwepo wa Mungu, hakika wanakosa uzuri mkuu (1 Yohana 5:12). Hata hivyo kuheshimu uwepo wa Mungu si juu ya kuonyesha hisia za kawaida na hoja tu kupitia maneno. Heshima yetu kwa uwepo wa Mungu hakika zinadhihirishwa kwa vitendo vya upendo na utiifu kwa amri zake (Yohana 14:23). Kwa nini Daudi aliamua kuleta sanduku kwenye mji mkuu? Lilikuwa tendo la utiifu wa upendo kwa amri ya uungu. Alitaka kufanya lililo bara zaidi kwa Mungu. Si uanaharakati ambao tunapaswa kutafuta kanisani, lakini uwepo wa Mungu mtakatifu. Hiki ni kipaumbele cha juu zaidi cha viongozi na umati wote.

B. Njia Mbaya (mistari ya 5-13)

Katika 1 Mambo ya Nyakati 13:5-14, sehemu ya masumbuko ya Daudi kujaribu kulete sanduku Yerusalemu inaangaziwa (mstari wa 10).

Kumbuka kwamba Uza alikuwa na nia zuri wakati alijaribu kuzuia sanduku la Mungu kuanguka, lakini si yeye aliyepewa jukumu la kufanya hivyo. Ni Walawi tu ndio walipewa mamlaka ya kulisongeza sanduku, na hili lilikuwa litendeke kulingana na ilivyoelezwa kwa sheria (Hesabu 4:5-6). Tunahitaji kueleza kwamba utaratibu huu ulikuwa mkali sana kwa sababu sanduku lilikuwa moja ya vitu vitakatifu sana vya Mungu (Hesabu 4:1 Mambo ya Nyakati 15:12-15).

Hili linatuekekeza kufikiria jinsi utakatifu wa vitu vya Mungu vilivyo! Katika kazi ya Mungu, mtu hawezi tu kuendelea na nia nzuri, lakini kuwa utiifu mkali wa amri zake. Katika jaribio la kufanyia Mungu jambo *'nzuri'*, tunaweza kujipata katika upinzani mkubwa kwa Neno lake takatifu. Kwa hivyo, njia pekee ya kumtumikia vyema ni kupokea kwa imani neema ya utakaso inayoturuhusu kutii Neno lake (Waebrania 10:19-25).

### II. Uwepo wa Mungu Huleta Baraka (1 Mambo ya Nyakati 14)

A. Mungu Hutimiza Ahadi Yake Kwetu (mistari ya 1-7)

Uwepo wa Mungu unaleta ustawi na baraka za kibinafsi. Mistari ya 1 hadi 7 inatueleza umuhimu wa matendo ambayo yanathibitisha kwamba Mungu alifurahishwa na uamuzi wa Daudi wa kuheshimu uwepo wake. Moja ya thibitisho la baraka za Mungu ilikuwa kutambuliwa kwa utawala wa Hiramu, mfalme wa Finishia ambaye alianzisha muungano wa kisiana na urafiki wa kudumu, ukileta faida kubwa kwa mataifa yote mawili.

Hapa tunaweza kuona utimilizo wa ahadi ya Mungu kwa Daudi wa kumjengea familia yenye nguvu ambayo Mungu angemteua Mfalme wa milele, Bwana wetu Yesu Kristo (1 Mambo ya Nyakati 17:2 Samweli 7:11-16). Katika sehemu hii ya somo, tunajifunza moja ya baraka kuu za Mungu katika maisha ya muumini, wakati tunaheshimu uwepo wake, ndipo utimizo wa ahadi zake za thamani.

B. Mungu Huonyesha Nguvu Zake kwetu (mistari ya 8-17)

Kama mfalme, Daudi mara nyingi alitambua uwepo wa enzi wa Mungu. Ushindi wake mkubwa ulikuwa kwa sababu ya tegemeo lake kwa uweza wa kimungu. Mistari ya 8 hadi 17 inaonyesha ushindi wake mkuu juu ya Wafilisti, maadui thabiti wa kihistoria wa watu wa Mungu. Tunaweza kusema kwamba huu ulikuwa ushinid kamili na wa hakika.

Kwa kumtumainia Mungu, tunapata ushindi wa uamuzi na dhahiri juu ya shida kubwa za maisha. Wakati mwingine, ushindi kama huo hauelezeki kutoka kwa maoni ya mwanadamu. Zinalingana peke na uingiliaji wa mkono wa Mungu mwenye nguvu zote: "*Kwake yeye ambaye kwa nguvu yake ifanyayo kazi ndani yetu aweza kufanya mambo makuu zaidi yay ale tuwezayo kuomba au kufikiria.*" (Waefeso 3:20)

**III. Tufurahie Katika Uwepo wa Mungu (1 Mambo ya Nyakati 15-16)**

A. Utakatifu Ulitakiwa Katika Uwepo wa Mungu (mistari ya 1-15)

Jaribio mpya la Daudi la kusongeza sanduku la Mungu Yerusalemu lilifanywa kwa kudai utiifu mkali kwa mahtiaji ya maadili na sherehe zilizowekwa wazi katika nambari ya Musa. 1 Mambo ya Nyakati 15:1-15 inatuonyesha kutimizwa kwa mambo haya mawili ya kimsingi. Daudi aliamrisha kwamba sanduku lisongezwe na Walawi na kwa utaratibu sahihi uliowekwa (Kutoka 25:10-22, Hesabu 4, Kumbukumbu la Torati 10:8).

Wacha tuangalie utimilifu wa mahitaji ya utakaso (1 Mambo ya Nyakati 15:12-14). Mzabibu, katika "Kamusi ya Agano la Kale na Agano Jipya" inasema: *"Maelezo "takasa" yanatoka kwa 'kadosh' (takasa, mwe watakatifu) na linatumika katika hali ya kufanya jambo au kuwa msafi na kukutana na mahitaji yote ya Mungu suala la usafi katika watu au vitu. Linatumika katika ibada rasmi ya Mungu ...Hata kama katika hali hii sisitizo kuu ni ibada, kuna pia viwango vya maadili na uadilifu"* (ukurasa wa 307).

B. Kufurahi Katika Uwepo wa Mungu (1 Mambo ya Nyakati 15:16-16:43)

Sehemu ya somo hili ya mwisho inasimulia sherehe kubwa ya kitaifa wakati wa uhamishaji wa sanduku na urejesho wa ibada ya Walawi. Tutazame jinsi Walawi walitambuliwa vizuri kulingana na uwezo wao tofauti wa ibada na huduma (zawadi na huduma): wasafirishaji wa sanduku, waimbaji na wana muziki, mabawabu, na Makuhani waliosimamia utendaji wa dhabihu.

Mwishowe, tunapata Zaburi ya shukrani kutoka kwa Daudi. Huu ulikuwa wimbo mpya wa Mungu siku hiyo ya sherehe. Inawezekana kwamba Zaburi hii iliundwa Daudi mbeleni kwa wakati huu maalum. Daudi alimteua Asafu na wenzake kuongoza ibada wakitumia Zaburi hii kuu (1 Mambo ya Nyakati 16:7-36). Shairi lilishirikisha kumbukumbu juu ya baadhi ya matukio muhimu ya Mungu akiwaokoa watu wa Israeli, na sehemu fulani zimeweka katika Zaburi zingine za Maandiko (Zaburi 96:1- 13, 105:1-15, 106:47-48).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, kwa nini Uza alipigwa na uwepo wa Mungu alipokuwa akijaribu kushikilia sanduku? Je, hiyo inatufundisha nini leo?
- Je, I Mambo ya Nyakati:10, 14 na 16 zinatufundisha nini na tunaweza kuzitumiaje leo?
- Je, ni vitu gani tunaweza kutaja katika maisha yetu ambavyo vitatuongoza kufurahia katika Bwana?

## HITIMISHO

Kuna njia nyingi ambazo waumini wanaweza kuheshimu uwepo wa Mungu; kila wakati ni lazima iwe kulingana na amri zilizotajwa katika Biblia. Kuheshimu uwepo wa Bwana inamaansiha kumpa kipaumbele katika maisha yetu na kumwendea kwa mioyo iliyowekwa wakfu na ya kushukuru.

**Somo la 27:**

## JINSI YA KUHESHIMU UWEPO WA MUNGU

**Lengo la somo:** Kuelewa kuwa Biblia inatueleza kuhusu kuheshimu uwepo wa Mungu

**Methali:** Amuabuduye mfalme hufanyika kuwa mfalme

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Mambo ya Nyakati 13-16

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mshukuruni Bwana, liiteni jina lake. Ambieni mataifa yale aliyoyatenda" 1 Mambo ya Nyakati 16:8

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?


Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?

Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?

Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?

Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** Mtukuze na mheshimu Mungu kwa yote unayoyafanya maishani



| Somo la 28 | KUJENGA NYUMBA YA MUNGU |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Mambo ya Nyakati 17 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza juu ya furaha ya kuwa sehemu ya kanisa la Mungu kupitia Roho wake Mtakatifu. | "Yeye ndiye atakayenijenge nyumba, name nitahakikisha kwamba ufalme wake unadumu milele." **1 Mambo ya Nyakati 17:12** |

## UTANGULIZI

Makanisa, kama sehemu tunayomwabudia Mungu na kutekeleza sehemu kubwa ya maisha ya kanisa, ni muhimu sana. Lakini Biblia inatufundisha kwamba *"...Mungu ...haishi ndani ya hekalu lililojenwa kwa mikono ya wanadamu."* (Matendo ya Mitume 17:24) Vivyo hivyo, Mfalme Sulemani alisema *"Lakini, ee Mungu kweli utakaa humu duniani na binadamu? Hata mbingu zenyewe, wala mbingu za mbingu za juu sana hazikutoshi, itakutoshaje nyumba hii ambayo nimeijenga!"* (2 Mambo ya Nyakati 6:18). Mahali pa Mungu pa kweli kukaa katika mioyo yetu, iliyotakaswa kupitia uwepo wa Roho Wake Mtakatifu. Kwa hivyo, haja yetu kubwa kila siku inapaswa kuwa kwamba maisha yetu ni hekalu takatifu kwa Bwana.

### I. Nyumba Ambayo Mungu Anakaa: Watu Wake (1 Mambo ya Nyakati 17:1-10)

Je, makanisa yetu yana umuhimu kiasi gani kwetu kama Wakristo?

A. Wasiwasi Juu ya Nyumba ya Mungu (mistari ya 1-4)

Alipokuwa akitembea ndani ya vyumba vya kifahari vya ikulu yake mpya huko Yerusalemu, Mfalme Daudi alikuwa na wasiwasi. Sanduku la Mungu lilikuwa mahali pa chini sana, wakati alifurahia ikulu nzuri na ya starehe. Daudi alichukizwa na wazo hilo kwamba Mungu angekuwa na nyumba isiyostahili kuliko yeye Kwa hivyo, aliamua kumjengea Mungu hekalu nzuri, na aliwaeleza washauri wake wa kweli, nabii Nathani (mstari wa 1). Mistari ya 1-4 inatueleza kwamba nabii wasiwsi hiyo kama Mfalme Daudi, na akafikria kwamba hili lilikuwa jambo la busara, na hata la mwanzo wa kimungu (mstari wa 2).

Daudi alifikiria kwamba mjengo huo uliojaa kutu haukustahili uwepo wa Mungu, na kujenga hekalu nzuri lilikuwa wazo njema. Lakini Mungu alikuwa na mpango bora zaid, ambao ungekamilishwa kwa wakati wake na kwa njia yake. Kama vile mtoa maoni alisema, *Kusudi la Daudi lilikuwa sahihi, lakini la mapema"* (Kanusi ya Thiolojia ya Beacon, nakala ya II . ukurasa wa 54).

B. Maisha ya Mungu na Watu Wake (mistari ya 5-10)

Ukosefu wa hekalu haukuwa kizuizi kwa Mungu la kuishi na watu wake. Mistari ya 5 hadi 10 inasema maendeleo ya kusudi la kimungu ya neema katika historia ya Israeli tangu uhuru wao kutoka Misri, ulifuatwa na kipindi cha waamuzi, hadi kuanzishwa kwa serikali ya kifalme. Mungu hakukosa kutimiza ahadi yake aliyofanya na Musa ya kuambatana na watu wake kwa uwepo wake (Kutoka 33:14-15). Ahadi zake zote zilitimizwa kwa uaminifu (Yoshua 23:14).

Hapa tunaona kwamba kama tu vile Mungu, kwa uaminifu wake mkuu na upendo, alibariki kizazi cha Daudi kupitia Yesu Kristo, nasi pia tumebarikia kwa neema ndani yake, pamoja na watoto wetu (Matendo ya Mitume 16:31, 1 Wakorintho 7:14). Hata hivyo, katika mwangaza kwa neema yake ya ajabu sana, ni lazima kila mmoja aamini binafsi na kuwa kabisa ndani ya Yesu ili kuwa sehemu ya nyumba yake na Ufalme, na hivyo aweze kufurahia ahadi zote zilizopewa na Mungu kwa kanisa lake.

### II. Mfalme Aliyejenga Nyumba ya: Yesu (1 Mambo ya Nyakati 17:11-14)

Mfalme Kama Daudi: Bali Mkuu Kuliko Wengine Wote

Mungu alimfunulia Daudi kwamba kutoka kwa uzao wake angemwinua Mfalme mkuu katika Historia, Bwana Wetu Yesu Kristo. Mistari ya 11-14 ina kumbukumbu mara mbili ya unabii huu, wa sasa na wa baadaye. *"...Nitamfanya mmoja wa watoto wako, wewe mwenyewe*

*awe mfalme, name ntauimarisha ufalme wake"* (mstari wa 11b), inamaanisha utawala wa mwana wa Daudi, Sulemani, ambaye alimrithi kwenye kiti cha enzi. Lakini kwa siku za baada ye za unabii huu alimaanisha Yesu Kristo, katika maneno ya kibinadamu, uzao wa Daudi. Katika vifungi kadhaa vya Agano Jipya, Yesu aliitwa *'Mwana wa Daudi'* (Mathayo. 9:27, 12:23, 15:22, Luka 1:32; Yohana 7:42, Warumi 1:3). Watafsiri wa Kiyahudi waliamini kwamba mwana wa Daudi angekuja ambaye angekuwa Masihi, Mwokozi aliyetangazwa katika Agano la Kale.

Hata leo, Wayahudi wanasubiri kwa makosa kuja kwa Masihi, na moja ya mahitaji ya kusubiri huju ni kwamba awe wa uzao wa familia ya Daudi. Unabii zote zinamtambua Yesu wazi na Mfale ule wa uzima ambaye angekuja, akitimiza agano la Daudi. Yesu pia alijieleza kama *'Mwana wa Mungu'*. Yesu alibishana na Marafisayo kuhusu yale Maandiko yanafundisha juu ya Masihi, na akawaonyesha kwamba Daudi chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, alimtabua kama Bwana (Zaburi 110:1, Mathayo 22:41-46). Yesu ni Mfale wa Utukufu!

A. Watu Na Ufalme wa Milele

Tangazo la umasihi lililokuwa na ujumbe wa nabii Nathani lilieleza kwamba Mfalme huyu mtukufu na wa milele angejenga nyumba ya Mungu: *"Yeye ndiye atakayenijenge nyumba, name nitahakikisha kwamba ufalme wake unadumu milele."* (1Mambo ya Nyakati 17:12)

Nyumba hiyo inahusu, zaidi ya familia ya damu ya Daudi mwenyewe, watu wa Mungu, kanisa. The church is called the '*House of Mungu'* (1 Timotheo 3:15) na *'hekalu takatifu'* (Waefeso 2:19-21), na imepatikana kwenye *'mwamba'* ambao ni mtu wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu (Mathayo 16:18) Yeye tu ndiye msingi usiobadilika wa kanisa (1 Wakorintho 3:11).

### III. Kusudi la Mungu kwa 'Nyumba' Yake (Kanisa) (1 Mambo ya Nyakati 17:15-27)

A. Kusudi la Neema

Mstari wa 16 unasema: *"Kisha mfalme Daudi akaingia ndani ya hema na kuketi mbele ya Mwenyezi-Mungu…"* (mstari wa 16a). Tangazo la umabii lilisababisha athari kubwa juu ya Daudi, kubwa sana hata papo hapo alihisi kuvutiwa kumwendea Mungu kupitia maombi. Ombi lake hapa ni moja wapo ya ombi bora zaidi katika Biblia nzima. Ni ombi linaoangazia hesima na shukrani kwa Mungu.

Je, Daudi alikuwa nani kabla ya kuitwa na kupakwa mafuta na Mungu kuwa mfalme wa watu wa Israeli? Mchungaji mdogo wa kondoo (mstari wa 7). Lakini Mungu alimwinua kufanya mambo makubwa, ili baada ya kutojulikana kabisa, kujulikana kwake kama mfalme kulienea katika mataifa yote yaliyozunguka Israeli (1 Mambo ya Nyakati 14:17).

Wakati kila mmoja watu anatazama nyuma kwa maisha yao, akiangazia mahali alikuwa kabla ya kumjua Mungu, tunaweza kutambua mambo makuu Bwana ametutendea!

B. Kusudi la Milele

Mwisho wa ombi lake nzuri, ambalo linaanza katika 1 Mambo ya Nyakati 17:16, Daudi anasisitiza kutimizwa kwa kusudi la Mungu kwa watu wake. Kile kilichofanya kusudi hili la Mungu kutovunjika kilikuwa uaminifu wake na chafuo la watu wake kwa mapenzi yake ya enzi (mstari wa 19). Kwa hivyo, tunawea kuwa na uhakika kabisa kwamba Mungu ataelekeza matukio ya maisha yetu hadi utambuzi wote wa kusudi lake, licha ya magumu yoyote, kama tu ilivyotendeka na Daudi na watu wa Israeli (mstari wa 21 Warumi 8:28-39).

Mwishowe, ombi la Mfalme Daudi linaangazia shukrani ya muumini. Kama watu wa Mungu, ni lazima tukae katika nia ya shukrani kwa Mungu kwa wokovu wa milele na baraka zake zote (mstari wa 24).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, unafikiri kipaumbele cha Mungu kwa watu wake ni kipi leo?
- Je, neno *'nyumba'* linamaanisha nini katika ahadi ya masihi?
- Je, ombi la Mfalme Daudi linaangazia nini?

## HITIMISHO

Kutoka kwa msingi wa dunia, Mungu alikuwa na kusudi ndani ya Kristo, kujenga nyumba na Ufalme wa milele. Kila Mkristo ni sehemu ya nyumba kuu ya Mungu ya kiroho, yaani watu wake, kanisa. Hii inamaanisha pia kwamba sisi ni raia na warithi wa Ufalme wake wa milele. Ukweli huu wa ajbu lazima utuweka kila wakati katika nia ya shukrani na kumtumikia na maisha matakatifu.

Somo la 28:

## KUJENGA NYUMBA YA MUNGU AU AHADI YA MUNGU KWA DAUDI

**Lengo la somo:** Kujifunza umuhimu wa kuwa sehemu ya Kanisa la Mungu

**Methali:** Ndege anapojenga kiota, anatumia manyoya ya ndege wengine

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Mambo ya Nyakati 17

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Bwana umenifanyia jambo hili jema kwangu kwa sababu ulitaka lifanyike. Umeniruhusu kuzijua ahadi zako za ajabu." 1 Mambo ya Nyakati 17:19

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?


Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?

Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini unyeyafanya kwa njia hiyo?

Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?

Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** Mungu hupeana furaha, furaha ipatikanayo kwa watu wa Mungu.



| Somo la **29** | **MUNGU NI MWAMINIFU, HATA KAMA SISI HATUWI WAAMINIFU** |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Mambo ya Walawi 18, 19, 20, 21 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba kila wakati tunapata ushindi katika maisha yetu, heshima na utukufu zinapaswa kuwa za Mungu, kwa vile ni Yeye ndiye anatupatia nguvu na hekima ya kuupata. | "Basi jipe moyo! Tupigane kwa kiume kwa ajili ya watu wetu, na kwa ajili ya Mungu wetu; na Mwenyezi Mungu atutendee lile analoona ni jema kwake." **1 Mambo ya Nyakati 19:13** |

## UTANGULIZI

Ni wazi kwamba that Mambo ya Nyakati 1 na 2 ziliandikwa kupeana mtazamo na kuendelea kwa kihistoria kwa Waebrania, jamii ya wana wa uhamisho ambayo ilihitaji sana kujua kwamba Mungu wa agano alikuwa bado ni Mungu wao. Historia ya Israeli ya zamani inaonyesha upendo Mungu mwaminifu kwa watu wake.

Mambo ya Nyakati inaonyesha mtazamo wa kikuhani, na haijapunguzwa tu kuridia ua kuongeza baadhi ya maelezo ya kizazi. Badala yake, kwa sababu ya mtazamo wao, maelezo juu ya hekalu na masilahi ya kiliturujia hutolea, na kuondolewa na nyongeza ni muhimu kwa uelewa kamili wa Wayahudi na mpango wa uungu wa wokovu. Kifungu cha kibiblia cha masomo yetu ya sasa kiko katika dhana ya utawala wa Daudi, ambacho kinaanzia 1 Mambo ya Nyakati 11:1 hadi 1 Mambo ya Nyakati 29:30.

### I. Daudi, Kama Shujaa, Anaongeza Ufalme (1 Mambo ya Nyakati 18-20)

Sura hizi zinafupisha vita vya kukera vya Daudi dhidi ya maadui wa watu wa Mungu (2 Samweli 8). Daudi alipata ushindi muhimu ambao ulimfanya akafahamika miongoni mwa watu wake na miongoni mwa taifa lililo karibu naye (1 Mambo ya Nyakati 14:17). Vivyo hivyo, nyara za vita na ushuru zilimetea utajiri mkuu.

#### A. Ushindi wa Daudi (1 Mambo ya Nyakati 18:1-13)

Daudi, katika utiifu wa Mungu, aliendelea katika biashara zake na uamuzi wa ajabu na nguvu. Maelezo yaliyotolewa juu ya Wafilisti, hapa na katika 1 Mambo ya Nyakati 20:4-8, yanaeleza kwamba walikuwa maadui walio na nguvu. Wafilisti walikuwa wamewadhulumu Waisraeli kwa vizazi kadhaa; lakini Daudi aliwashinda na kuwadhalilisha (2 Samweli 8:1-14). Hata alilemaza farasi zao (2 Samweli 8:4). Mashirika ya sasa ya kulinda wanyama hayangefurahia na matendo ya Daudi kwa farasi. Hata hivyo, hili lilikuwa tendo la kawaida la wakati huo, hasa kuzuia farasi kutumiwa viaha na adui.

#### B. Utajiri wa Daudi (mistari ya 7-11)

Tunapaswa kumheshimu Mungu na vile vitu ametubariki navyo. Kama kamanda mkuu wa jeshi, Daudi alimpa Mungu utukufu kwa kila ushindi. Alimtolea Mungu shaba iliyotekwa nyara Dameski na akaileta kwa mfalme Hamathi, akamtumia (mistari wa10-11).

1 Mambo ya Nyakati 18:6 na 13 zinarudia maneno haya: *"Bwana alimpa Daudi ushindi kokote alikokwenda."* Wakati huu, ni lazima tukumbuke kwamba Mungu anawapa watu nguvu, si za kuwafanya wajitukuze bali kutenda wema.

### II. Daudi Aamuru Hesabu ya Watu (1 Mambo ya Nyakati 21)

Mstari wa 1 unasema states: *"Shetani akajitokeza kuwataabisha Waisraeli, akamshawishi Daudi awahesabu watu."*

Yoabu, mkuu wa jeshi, alisema kwa nguvu dhidi ya hesabu hii. Katika mstari wa 4, tunaona kwamba mazungumzo kati ya wahusika wakuu wote walihitimishwa, na Yoabu akiwa katika utiifu kwa Daudi, na kuanza hesabu.

Pengine tunafikiria kwamba hapakuwa na jambo lolote libaya na hesabu. Tunajiuliza, Je, ni kwa nini mchungaji asijue idaya ya kondoo wake? Lakini tunahitaji kuona kwamba Daudi alitenda kwa msukumo wa kiburi chake,

ambacho kilimwudhi Mungu. Kwa maneno yaliyosemwa katika mstari 1, inaweza kuonekana kwamba Mambo ya Nyakati ilimlaumu Shetani, ambaye akiomba kiburi cha mfalme, alimshawishi kuwahesabu watu. Hakika, Daudi alitaka kuhesabu nguvu zake za kijeshi. Hata hivyo, mfalme alipoamuru hesabu, alionyesha ukosefu wa wa ujasiri katika ahadi ya Mungu.

A. Dhambi ya Daudi Na Tauni (1 Mambo ya Nyakati 21:1-22:1)

1. Hesabu (mistari ya 1-6)

Neno la asili ni *"kurejelea"*. Hesabu hiyo ilikuwa ya malengo ya kijeshi. Uhusiano wa Daudi na Mungu haukuwa sawa; alimkasirisha Mungu, akijiweka upande wa adui wa kiroho. Wakati uhusiano wa Daudi na Mungu haukuwa mzuri, uliathiri pia uhusiano wake na watu. Hakika, Mfalme Daudi alikuwa ameacha ibada yake na kumtegemea Mungu. Katika kutafakari juu ya kiwango cha utawala wake, alipuuza kwamba Mungu alikuwa ameahidi kwamba Israeli ingekuwa nyingi kama mchanga wa bahari. Ushindi aliokuwa nao haukuwa uwe tunda la mikakati au nguvu yake, bali nguvu za Mungu. Ni muhimu kiasi gani kukosa kupoteza ushirikiano wetu na Mungu! Tukumbuke, tunapofika mahali Bwana anatuelekeza, tegemeo letu kwake linapaswa kuwa taa inayoongoza hatua zetu.

2. Marekebisho na Ukombozi (mistari ya 7-13)

Daudi alitambua dhambi yake na hitaji mbele ya Mungu, na kuomba kwamba hatia yake iondolewe (mstari wa 8). Lakini Mungu alikuwa tayari ameamua kumuadhibu kwa uamuzi wake mbaya. Adhabu ya uungu juu ya watu wa Israeli inaangazia ushawishi ambao maamuzi ya mtu yanaweza kuwa nayo kwa wale walio karibu naye. Daudi angechagua katika miaka mitatu ya njaa, miezi mitatu ya ushindi wa dhuluma vitani, au siku tatu za tauni duniani. Alichagua ya mwisho (mistari ya 12-14). Ingawa msamaha wa Mungu ulikuwa njiani, Daudi hangeweza kuondoa nchi yake kwa matokeo ya kukosa kupata ushauri wa Mungu katika kufanya maamuzi. Ni muhimu jinsi gani kuomba na kutotenda kwa hali ya kukosa hekima katika maisha yetu au huduma! Ni lazima tukumbuke kwamba kuna watu karibu nasi ambao wanaweza kuathirika na matokeo ya matendo. Tauni (mistari ya 14-17)

Mstari wa 12 unataja chaguzi tatu zilizowasilishwa kwa Daudi kwa sababu ya kumuasi Bwana: Njaa kubwa (kupanda mbegu bure), kukimbia mbele ya maadui, au siku tatu za tauni. Daudi aliamua kuchagua tauni, kwa vile alijua kwamba mkono wa Mungu ulikuwa afadhali kuliko mkono wa mwanadamu. Na hakika, Mungu alieneza rehema yake na akaamuru malaika asimamishe uharibifu (mstari wa 15). Daudi alitambua hatia yake na kwamba ghadhabu ya Mungu ilikuwa kwa sababuya uamuzi wake mbaya (mstari wa 17).

3. Madhabahu na Dhabihu (mistari ya 18-27)

Daudi aliagizwa kujenga madhabahu kwenye kiwanja cha kupuria nafaka cha Ornani Myebusi (mstari wa 18) kama ishara ya mapatano. Ornami alipeana matumizi ya kiwanja chake bure, lakini Daudi alikataa kumtolea Daudi Mungu ibada rahisi. Daudi alisema: *"La, hasha; nitavinunua kwa thamani yake kamili; sitamchukulia Mwenyezi-Mungu kitu kilicho chako au kumtolea tambiko za kuteketezwa ambazo hazijanigharimu kitu."* (mstari wa 24) Mungu alionyesha kukubali kwake kwa dhabihu kwa kujibu kwa moto kutoka mbinguni kwenye madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa (mstari wa 26). Mungu alisimamisha ghadhabu (mstari wa 27).

4. Mahali pa Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 21:28-22:1)

Madhabahu ya shaba ambayo Musa alikuwa amejenga ilikuwa Gibeoni (mstari wa 29), na hapo ndipo dhabihu zote za Israeli zilikuwa zinatolewa. Lakini Daudi aliogopa silaha ya malaika wa Bwana, hivyo hangeenda huko (mstari wa 30). Daudi alishangazwa na mahali pa kupuria nafaka pa Ornami Myebusi hata akaamua kulijenga hekalu pale. (1 Mambo ya Nyakati 22:1)

## MASWALI YA ZIADA

- Je, tunajifunza nini kutoka kwa ushindi wa kijeshi wa Daudi? (1 Mambo ya Walawi 18:1-13;20:4-8).
- Kwa ufupi jadili jinsi unavyohisi somo hili litakusaidia katika kutembea kwako kwa Kikristo.

## HITIMISHO

Mkono wa Mungu kila wakati una kibali juu ya watu Wake, na anaahidi kuwabariki wale wanaomtii. Kwa hivyo, haijalishi magumu vile yalivyo ambayo tutapatana nayo, mkono wa mara nyingi uko tayari kubariki bidii ya watoto wake. Hata hivyo, kila tabia ya kiburi itaudhi moyo wa Mungu, na ingawa Mungu, katika Kristo, anaeneza rehema yake, matokeo machungu ya kutotii lazima yatapatikana.

**Somo la** 29:

## MUNGU NI MWAMINIFU, HATA KAMA SISI HATUWI WAAMINIFU

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba ushindi wetu watoka kwa uwaminifu wa Mungu

**Methali:** Kumpenda mfalme si vibaya; lakini mfalme akupendaye ni bora zaidi.

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Mambo ya Nyakati 18-21

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Uwe hodari, tukajitie moyo mkuu kwa ajili ya watu wetu, na kwa ajili ya miji ya Mungu wetu. Bwana afanye yaliyo mema machoni pake." 1 Mambo ya Nyakati 19:13


**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?

Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?

Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?

Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii? Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** Ushindi wetu Hautegemei idadi ya majeshi yetu



| Somo la 30 | MRADI MUHIMU ZAIDI WA MFALME DAUDI<br>**Maandiko:** 1 Mambo ya Nyakati 22:1-13 |
|---|---|

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kutambua, kuhusika, kuchambua, na kutumia tabia tofauti na matendo ya alipoendelea kutekeleza mradi mkubwa. | "Sasa, mtumikieni Bwana, Mungu wenu, kwa nia na moyo wote. Anzeni kumjengea Bwana Mungu mahali patakatifu …" **1 Mambo ya Nyakati 22:19** |

## UTANGULIZI

Kulingana na mstari wa kumbukumbu, wachukue wanafunzi waangazie umuhimu wa kuwa na mahali maalum palipotengwa kwa ajili ya kumwabudu Mungu nyakati za Daudi. Kulingana na maelezo yanafahamika, kile wanadamu wote wanapaswa kufanya maishani ni kuwa mtoto, waandike kitabu na kupanda mti. Lakini hakuna kimoja baadhi ya vitu hivi ambacho ni rahisi kufanya. Pengine hatuna watoto, hatujawahi kupanda mti na/au kuandika kitabu, lakini ni urithi gani ambao tutaacha tukifa? Waambie baadhi ya wanafunzi wajadili swali hili.

### I. Matayarisho ya Mradi (1 Mambo ya Walawi 22:1-9)

Mungu alimwambia Daudi amjengee madhabahu na kumtolea dhabihu, ambayo ilikubalika na Bwana (2 Samweli, 24:1-25; 1 Mambo ya Nyakati 21:2- 27). Daudi kisha, kwa kushukuru kwa rehema za Mungu, aliamua yafuatayo: *"Hapa ndipo mahali ambapo nyumba ya Bwana Mungu itakuwa, na pia madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa ya Israeli"* (1 Mambo ya Nyakati 22:1).

#### A. Mwito wa Wafanyikazi (mistari ya 2, 15)

Daudi aliwaamuru wageni walioishi kati yao kufanya kazi katika machimbo na kukata mawe kwa mradi huo. Pengine, kulikuwa na watu waliotekwa nyara wakati wa vita juu ya mataifa mengine. Mfalme hakujitahidi kupata idadi kubwa ya wafanyikazi: waashi, waashi wa mawe, seremala na watu wengi waliobobea kwa kila eneo la kazi. Hii ilijumuisha mafundi waliobobea katika kuni, na mafundi wa dhahabu ambao walitengeneza vipande vya kipekee vya kisanii na metali za thamani.

#### B. Vifaa vya Kujenga (mistari ya 3-4)

Daudi alikuwa mwadilifu katika kupanga, pamoja na kutoa vifaa muhimu kama vile mawe, chuma, shaba mbao, dhahabu na fedha. Alipanga kila kitu, lakini jambo ambalo hangeweza kufanya lilikuwa ujenzi wa hekalu lenyewe. Wafalme wa Tiro na Sidoni walitoa idadi kubwa ya mti wa Mwerezi, ambao unadumu sana, hauozi na una harufu ya kupendeza. Inavutia kutambua kurudia kwa maneno kadhaa yanayohusiana na ukarimu na uzuri wa rasilimali: kiasi kikubwa cha misumari, na shaba zaidi kuliko vile ingetumika (mstari wa 3); idadi isiyohesabika ya mti wa (mstari wa 4); elfu mia moja ya talanta za dhahabu, milioni moja ya talanta za fedha, chuma na shaba zisizokuwa na kipimo (mstari wa 14). Hii inatufundisha juu ya kutoa kwa ukarimu. Hatuhitaji kuwa matajiri ili kutoa. Kilicho muhimu ni mwelekeo wa mioyo yetu. Kwa kweli, mara nyingi maskini ni wakarimu zaidi na matajiri wachoyo.

### II. Maagizo na Mahitaji ya Sulemani (1 Mambo ya Walawi 22:10-16)

#### A. Ufalme Unaodumu (mstari wa 10)

Mstari huu ni wa muhimu sana kuhusu uhusiano ambao Mungu alitaka kuwa nao na Sulemani, mrithi wa Daudi. Mungu alitaka kuwa na uhusiano wa karibu kama ule wa baba na mwanawe. Hiyo inamaanisha uhusiano wa kila siku wa uaminifu, lakini pia wa utiifu. Zaidi, Bwana alimuahidi Daudi kwamba ukoo wake utakuwa wa milele *"Na wazawa wake wataitawala Israeli milele."* (mstari wa 10) Sulemani alimaliza siku zake akitawala kwa amani, kama tu vile Mungu alikuwa ameahidi. Hata hivyo, ahadi hiyo ilishinda utawala wa Sulemani. Ilikuwa ahadi ya masihi iliyotimizwa kwa kuja kwa Bwana Yesu Kristo, kama tu vile malaika alimwambia Mariamu (Luka 1:33).

#### B. Uwepo wa Mungu Ulio Muhimu (mstari wa 11)

Je, tunapaswa kufanya nini ili tuwe watu waliofanikiwa? Hili ni swali nzuri sana ambalo

tunaweza kujiuliza. Daudi alimwambia Sulemani kwamba uwepo wa Mungu ulikuwa muhimu kama alikuwa anaenda kufanikiwa, na kwamba alihitaji kujenga nyumba ya Mungu. Hivyo, uwepo huo wa kimungu ingeongoza ufahamu wa Sulemani na kumfanya mtawala mwenye busara wa Israeli. Leo tunahitaji viongozi wenye busara walio karibu na Mungu kuyatawala mataifa yetu kwa hekima! Katika hali nyingi, wanasiasa wetu hutafuta vyeo vya nguvu ili kuongezea mali yao binafsi. Zaid, wengi wao hupora hazi ya serikali kwa ghara ya mateso ya wengine. Hili ni jambo la huzuni!

C. Hitaji la Kufuata Sheria ya Mungu (mstari wa 13)

Ukosefu wa mazoezi ya kanuni zilizanzishwa katika sheria ya Mungu ndio sababu kwa nini maovu mengi katika jamii yetu, kama vile ufisadi, ukosefu wa ajira, uhalifu, umaskini, ukosefu wa kazi, ukosefu wa haki, ukosefu wa usalama, ulevi na matumizi mabaya ya nguvu katika nyanja tofauti ya maisha yetu ya kila siku. Ushauri wa Daudi kwa Sulemani ulikuwa sawa na ule Mungu alimpa Yoshua kabla ya kuchukua uongozi wa taifa (Yoshua 1:8). Hii pia inaenda kwa viongozi wote na wananchi leo: Ni lazima tufuate, tuzingatie na kutimiza sheria ya Mungu ili kuwe na jamii yenye haki na afya. Kwa hivyo, ufunuo wa mafanikio ya kibinafsi si kufanya mikataba ya kiuchumi, bali kupenda sheria ya Mungu na kuiweka katika matendo (mstari wa 13).

D. Bidii, Ujasiri Na Uhodari (mistari ya 14-16)

Daudi alimwambia mwanawe Sulemani: *"Haya, Anza kazi! Bwana na awe pamoja nawe…"* (mstari wa 16). Mafunzo ya Sulemani yalikuwa tofauti sana na ya babake Daudi. Kiongozi wa sasa alilelewa katika uwanja wa michezo ya kufanya mazoezi ya hatari, na hata alilazimika kukutana na wanyama wa mwituni (1 Samweli 17:34-36). Sulemani, kwa upande mwingine, alikuwa miongoni mwa matajiri ambapo watumishi walimpa mahitahi yake yote. Alizoea kutumikiwa, na wala sio kutumika. Kwa sababu hiyo, Daudi alimtia moyo asibaki tu ametulia, bali afanye kazi ya kutekeleza mradi mkuu wa mfalme: Nyumba ya Mungu.

### III. Msaada Kutoka Kwa Viongozi wa Nchi (1 Mambo ya Nyakati 22:17-19)

A. Mradi wa Shukrani (mistari ya 17-18)

Taifa la Israeli lilikuwa limekumbana na vifo vikuba kwa sababu ya hesabu ya watu, na Daudi, kwa shukrani zake za rehema kwa Bwana, alitaka kutayarisha chochote kilicho muhimu kwa ujenzi wa hekalu. Lakini Sulemani hangefanya peke yake, aliwahitaji viongozi wake wahusike kwenye mradi. Mungu alikuwa amelikomboa taifa kutoka kwa kifo. Kwa hivyo, Waisraeli wanapaswa kuhusika katika mradi huu wa shukrani ili kutengeneza mahali pa utukufu pa ibada ya Bwana. Kiongozi mzuri uwahusisha wengine katika huduma ya Mungu.

B. Kusudi thabiti (mstari wa 19)

Tunahitaji viongo wa taifa letu na makanisa yetu kujitolea thabiti kuutafuta uso wa Bwana ili awape hekima na ufahamu wa kutawala kwa haki. Tunahitaji katika siku hizi dhamira thabiti ya kumtafuta Bwana! Lakini wengi wamenaswa na wasiwasi wa maisha haya na usiwe na moyo au muda wa kuwa na ushirika na Mungu. Je, uamuzi wetu wa kutafuta Mungu uko thabiti kiasi gani, hasa wakati kazi nyingi zinatuzunguka?

## MASWALI YA ZIADA

- Kuhusu maandalizi ya ujenzi wa hekalu, orodhesha tabia za kipekee za Daudi (mistari ya 1-5,14,16).
- Je, Sulemani alihitaji nini ili kufanikiwa?
- Je, ni muhimu kiasi gani kwama sisi kama viongozi wa Kikristo tuwatie motisha na kuwahusisha ndugu na dada wengine katika huduma ya Bwana?

## HITIMISHO

Daudi alikuwa na watoto wengi, aliandika Zaburi nyingi na kuacha alama nyingi juu ya maisha ya raia wenzake kwa kutoa kwa ajili ya ujenzi wa hekalu la Bwana kama mahali ambapo taifa lote lingeweza kumwabudu Mungu wa vizazi. Nasi pia tunahitaji kutafuta uwepo wa Mungu, tukitii amri zake, na kutafuta mwongozo wake wa uungu wa kila siku ya maisha yetu. Mungu yule yule wa mani ambaye alikuwa na Daudi na Sulemani ndiye aliye na sisi kutusaidia leo!

**Somo la** 30:

**MRADI MUHIMU ZAIDI WA MFALME DAUDI**

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba Daudi alimsaidia Sulemani kufanikiwa katika ujenzi wa Hekal

**Methali:** Bangili moja haitoi mlio

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Mambo ya Nyakati 22:1-13

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Ndipo utakapofanikiwa, ukiangalia kuzitenda amri na hukumu Bwana alizomwagizia Musa juu ya Israeli. Uwe hodari, na wa moyo mkuu. Usiogope wala usifadhaike." 1 Mambo ya Nyakati 22:1-13

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?


Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?

Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?

Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?

Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** Tunafaa kuupitisha utakatifu wetu kwa vizazi vijavyo kupitia maneno na matendo



| Somo la **31** | **MAANDILIZI NA MGAWO WA RASLIMALI ZA WANADAMU/MWANADAMU** |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Mambo ya Nyakati 23:6, 24-27 |

| Lengo | Memory Verse |
|---|---|
| Kutumia kanuni za kibiblia za maandilizi na mgawo wa raslimali za mwanadamu tulizopewa na Mungu kusimamia. | "Daudi alipokuwa mzee wa miaka mingi, alimtawaza Sulemani mwanawe awe mfalme wa Israeli." **1 Mambo ya Nyakati 23:1** |

## UTANGULIZI

Katika miaka ya mwisho ya maisha yake, watu walifanya mipango na maagizo Fulani juu ya fedha zao, bidhaa, mahusiano, nk. Mfalme Daudi alifanya hivi kwa kuacha ufalme wake, kuacha maagizo yake na mwanawe Sulemani. Alifanya mipango ya raslimali yote iliyokuwepo katika ufalme, hata raslimali ya mwanadamu. Hili ni somo nzuri sana kwetu! Hata tunaweza kuwa hatuna maelfu ya watu wa kulinda, hilo si kitu, kanuni ni ile ile: tuwe wasimamizi waaminifu wa raslimali yote ambayo Mungu ametuaminia. Lengo letu na liwe siku moja tuweze kusikia sauti ya Bwana ikituambia: *"…Vema, mtumishi mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu katika mambo madogo, nitakukabidhi makubwa. Njoo ufurahi pamoja na bwana wako!"* (Mathayo 25:23)

### I. Walawi Katika Utumishi Wa Nyumba ya Mungu (1 Mambo ya Nyakati 23)

A. Daudi Alikuwa Mzee na Miaka Nyingi (mistari ya 1-3)

Biblia inatueleza kwamba Mfalme Daudi alikuwa mzee. Aliamua kuanza kufanya mipango fulani muhimu kabla ya kuondoka kwake (mistari ya 1-3). Nasi pia tunaweza kuanza kupanga katika maisha yetu, tukigawa na kuangalia baraka Mungu ametupatia.

B. Usimamizi Wa Walawi (mistari ya 4-5)

Katika mistari hii, tunatambua umuhimu wa usahihi. Daudi na Sulemani hakuwa tu wajue ni Walawi wangapi waliokuwepo, bali walihitaji kugawa katika majukumu na kazi tofauti. Hili lazima liwe lilikuwa somo kubwa katika utumishi na usimamizi. Daudi alisema, *"Kati yao, elfu ishirini nan ne wawe wasimamizi wa kazi ya nyumba ya Bwana na elfu sita wawe maofisa na waamuzi. Elfu nne wawe mabawabu na elfu nne wamsifu Bwana kwa ala za muziki nilizotoa kwa ajili ya kusudi hili."* (mistari ya 4-5)

C. Usimamizi Mwangalifu na Wa Maelezo (mistari ya 6-12)

Kile tunapata katika mistari ya 6-12 ni mgawo wa umakini wa majina na umri (inapaswa kukumbukwa kwamba wakati huo, hakukuwa na teknolojia ya kompyuta). Hii inatufundisha kwamba tunaweza na tuwe waangalifu na mali yetu, hasa katika uhusiano unaohusishwa watu chini ya ulinzi wetu na kusimamiwa kwetu. Nyuma ya kila jina, kuna uso na moyo. Labda kwa mifumo mingi, haswa katika enzi ya sasa ya kompyuta na teknolojia, kila mmoja wetu haendi zaidi ya kuwa tu *'idadi'* katika takwimu. Hata hivyo, kwake Mungu sisi ni zaidi ya idadi.

D. Jukumu Kubwa (mistari ya 13-15)

Huduma zote kwa Bwana ni takatifu, na ni lazima ziwe takatiuf kwa sababu Mungu ni mtakatifu. Mambo mengine uhitaji hisia wazi ya utakatifu, au ya utakatifu, au ya jukumu linalokuja na majukumu fulani. Kwa mfano, katika Agano la Kale tuligundua kwamba kuhudumia meza kulihitaji viongozi waliojaa Roho Mtakatifu: *"Ndugu zetu, chagueni miongoni mwenu watu saba wenye sifa njema, waliojawa na Roho na wenye hekima. Nasi tutawakabidhi jukumu hilo."* (Matendo ya Mitume 6:3) Kwa hivyo, kila jukumu lililofanywa kwa Bwana ni kazi kubwa.

### II. Wana Wa Haruni Kama Makuhani (1 Mambo ya Nyakati 24)

A. Kazi za Makuhani (mistari ya 1-6)

Majukumu ya makuhani ya makuhani kimsingi yalikuwa mara mbili: kutekeleza ibada za kidini na kuwasiliana na

Mungu. Katika hali hii, walitumika kama wapatanishi kati ya Mungu na watu Wake. Mungu alikuwa amekusudia hapo awali kwamba watu wa familia ya Haruni wanapaswa kuwa makuhani: *"Nawe Musa umlete kwangu Haruni ndugu yako, pamoja na wanawe, nadabu na Abihu, Eleazari na Ithamani utawateua miongoni mwa Waisraeli ili wanitumikie kama makuhani."* (Kutoka 28:1) Makuhani walikuwa kama daraja ya Mungu wakiwasaidia watoto kuwasiliana na Mungu.

B. Makuhani Walifanya Kazi Kwa Zamu (mistari ya 7-31)

Katika mistari hii, Daudi aliwapanga makuhani katika vikundi 24. Hakuwagawa tu, bali pia aliwapatia zamu katika huduma.

### III. Mgawo wa Wanamuziki Na Waimbaji (1 Mambo ya Nyakati 25)

A. "Wote Waliofundishwa Kumwimbia Bwana" (mstari wa 7)

Liapokuja suala la kumtumikia Bwana na watu wake, hatupaswi kutegemea tu ustadi wa asili, uwezo, zawad au talanta. Hakika, lazima kuwe na hali ya kujitolea na maandalizi endelevu. Mwanamuziki mzuri, kama tu sehemu zingine nyingi, lazima aendelee kukua kila wakati katika zile sehemu zinazohusu huduma. Kumtumikia Mungu kupitia muziki lazima kuonyeshe maandalizi mazuri, kiufundi na vitendo, na juu ya yote, maandalizi mazito ya kiroho.

B. "Wote Wakubwa Kwa Wadogo, Waalimu Kwa Wanafunzi, Walitumia Kura Katika Kupanga Kazi Zao" (mistari ya 8)

Kipengele kingine muhimu sana katika shirika na mgawo wa makujumu ya kuhusika ilikuwa nafasi ambayo kila mtu alipokea. Walitumika kwa zamu, na kila mtu alihusika. Je, na masomo mangapi ya vitendo ambayou tunajifunza hapa kwa ajili ya siku zetu? Katika huduma ya Bwana, hakuna mtu wa lazima, yote ni muhimu: wadogo, wazee, wanafunzi na waalimu. Mshukuru Mungu kwamba kanisa humpa kila mtu na watu wote nafasi ya kuhusuka kulingana na uwezo wao, talanta na majukumu!

### IV. Mabawabu Na Maafisa (1 Mambo ya Nyakati 26-27)

Katika sura ya 26, tunapata yafuatayo: taratibu ya mabawabu (mistari ya 1-19); taratibu ya waweka hazina (mistari ya 20-28); na taratibu ya maafisa na waamuzi (mistari ya 29-32). Katika sura ya 27, tunaweza kuona yafuatayo: taratibu ya majeshi (mistari ya 1-15); taratibu ya makabila ya Israeli (mistari ya 16-24), na usimamizi wa Mfalme Daudi (mistari ya 23-34).

A. Mabawabu wa Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 26)

Mabawabu wa familia ya Kora walikuwa makuhani waliopewa usimamizi wa kulinda malango ya hekalu la Mungu (mstari wa 1). Neno bawabu linamaanisha *'kusimamia, au kulinda.'* Ofisi hii ilikuwa ya umuhimu mkubwa; na hata tangu wakati wa Musa, mabawabu walikuwa tayari wameanzishwa. Walihitaji kuwa Walawi (1 Mambo ya Nyakati 9:26). Walawi walikuwa na kazi kadhaa katika usimamizi wao: kulilinda hekalu (2 Mambo ya Nyakati 23:19); kulilinda sanduku kutoka kwa wezi (1 Mambo ya Nyakati 15:23); kuchunga sadaka (2 Wafalme 12:9).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, tunapaswa kusubiri hadi tuwe wazaee ili kufanya mipango ya utaratibu wa raslimali ambao tumekabidhiwa wakati wa maisha yetu?
- Eleza kazi ya mabawabu.
- Je, kazi hii iko vipi kanisani mwako? Je, ni wapi na unatumika kwa njia gani?

## HITIMISHO

Mungu anatuita kuwa bora na kujitolea katika usimamizi wa raslilimali za kibinafsi, familia na kanisa, u anatuita calls us to be excellent and dedicated in the administration of personal, family and church resources, mgawo mzuri wa rasilimali za huduma ya Kikristo, na maandalizi na utekelezaji wa majukumu tofauti ya huduma. Tukumbue kila wakati: Mungu wetu na watu wake wanastahili huduma yetu bora!

**Somo la 31:**

MAANDILIZI NA MGAO WA RASLIMALI ZA WANADAMU/MWANADAMU

**Lengo la Somo:** Kutumia kwa hekima raslimali ambayo Mungu ametujalia

**Methali:** Kichwa kimoja hakiwezi kubeba paa.

**Kifungu cha Kusoma:** 1 Mambo ya Nyakati 23-27

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Katika hao zilikuwa zamu za mabawabu, yaani katika hao wakuu, wenye ulinzi sawa sawa na ndugu zao, wa kutumika katika nyumba ya Bwana." 1 Mambo ya Nyakati 26:12

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?
Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?
Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii? Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** "Katika hao zilikuwa zamu za mabawabu, yaani katika hao wakuu, wenyee ulinzi sawa sawa na ndugu zao, wa kutumika katika nyumba ya Bwana." 1 Mambo ya Nyakati 26:12



| Somo la 32 | MAANDALIZI YA KUJENGA HEKALU |
|---|---|
| | **Maandiko:** 1 Mambo ya Nyakati 28:1- 29:21 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujifunza kutoka kwa ushauri wenye hekima ambao Daudi alimpa Sulemani, kanuni zake za haki na ukarimu wake wa hekalu ambapo watu wangemwabudu Mungu. | "'Hayo yote,' Daudi alisema, 'Nimeyaweka kwa maandishi kama nilivyopewa na Bwana, na ameniwezesha kuyaelewa maelezo yote ya mpango." **1 Mambo ya Nyakati 28:19** |

## UTANGULIZI

Daudi alikuwa mfalme wa pekee wa Israeli ambaye kwa mamlaka yake na kiasi aliweza kufanikisha mambo mengi. Kama mtoto wa mwisho wa Yese, alijifunza jinsi ya kuwa mchungaji mzuri hodari ambaye alilinda kondoo wake kutokana na kuvamiwa na dubu na simba. Katika ujana wake, aliwaokoa watu wa Israeli kutokana na vita juu ya Wafilisti ambavyo vilionekana kutowezekana. Mfalme Sauli hangeweza kuona jinsi ya kushinda kile kilichoonekana kuwa shida isiyoweza kushindwa – jitu Goliathi. Kijana Daudi pamoja na kombeo lake na mawe yake 5 aliweza kumshusha adui mara tatu ya ukubwa wake. Zaidi, alikuwa mwanamuziki na mwimbaji, na mtunzi wa nyimbo nyingi.

### I. Mpango wa Mungu Kupitia kwa Daudi (1 Mambo ya Nyakati 28:1-8)

Baada ya miaka nyingi, Daudi alitaka kujenga hekalu kwa heshima ya Mungu. Tunaweza kuona haya katika sura zilizo mbele ya 1 Mambo ya Nyakati 28: "*Wakati Daudi alikuwa akikaa katika ikulu, alimwambia nabii Nathani, 'Hebu tazama, mimi ninakaa kwenye nyumba nzuri iliyojengwa kwa mwerezi, lakini sanduku la Bwana linakaa hemani.'*" (1 Mambo ya Nyakati 17:1) Daudi alishangazwa na utofauti katika ya ukuu wa nyumba yake na ukweli kwamba Sanduku la Bwana lilikuwa bado kati ya mapazia, vitambaa, na ngozi za wanyama zilizoponywa ambazo zilitengenezwa. Daudi alikusudia kujenga hekalu ambalo Sanduku la Mungu linaweza kuwekwa kwa heshima.

Halafu, tayari akiwa mzee sana, Mfalme Daudi aliwaita watu kwenye mkutano (1 Mambo ya Nyakati 28:1). Aliwafunulia tamaa yake ya asili ya kujenga hekalu la Mungu na kushiriki nao kwamba hakuwa anaenda kujenga hekalu, kwa sababu Mungu alikuwa na mpango bora (mistari ya 2-3) Alikuwa anafanya mipango ambayo mwanawe Sulemani angeweza kutekeleza na watu (mistari ya 11-19). Mungu alikuwa amemwambia kwa sababu ya damu yote alikuwa amemwaga katika vita vyake vya kijeshi, hangemjengea hekalu. Lakini Mungu alimfurahisha Daudi kwa kumpa Sulemani jukumu hilo (mistari ya 5-6). Kupitia Sulemani, Mungu angeleta baraka maradufu kwa Daudi, ambayo ingewapa pia kibali watu wa Israeli. Kwanza, angekuwa mfalme angeendeleza ukoo wake; na pili, angejenga hekalu la kuabudu jina la Mungu.

Lazima Mfalme Daudi awe kielelezo chetu katika kupenda na kutumaini uwepo wa Mungu (Zaburi 27:4, 122:1, 84). Leo, sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 6:19), lakini kama watoto wa Mungu, hakupaswi kuwa na mahali pazuri pa kuwa kuliko kukusanyika kwa kuhusika katika ibada ya Mungu wetu katika jamii.

### II. Mapendekezo ya Daudi kwa Mfalme Wa Baadaye (1 Mambo ya Nyakati 28:9-10)

Kwa kuchagua mfalme wa Baadaye wa Israeli, Daudi, kutokana na ujuzi wake, alimpa Sulemani mapendekezo tano. Kama Sulemani angemtii Mungu, angefanikiwa. Sasa, tutajifunza kila moja ya mapendekezo hayo.

A. "…Nawe, Sulemani Mwanangu, Umjue Mungu Wa Baba Yako… …" (mstari wa 9)

Daudi alimwomba mwanawe asisahau kwamba Mungu anataka heshima na uaminifu. Sulemani alikuwa na nafasi ya kusikia ujuzi nyingi za kihistoria mwanzo, kama wakati babu na bibi wanatueleza hadithi zao za kusimulia. Hadithi za Daudi zilikuwa za kusimulia kwa sababu ya uzito wa kiroho ambao zilikuwa nazo. Hii inaonyesha kwamba kama wazazi, tunalo jukumu la kuishi katika njia ambayo watoto wetu wanaweza kumuona Mungu katika kila sehemu ya maisha yetu. Kama wazazi, tunaweza pia kueleza watoto

wetu kwa ushawishi pendekezo hili hili la kuheshimu na kuwa waaminifu kwa Mungu.

B. "Mtumikie Kwa Moyo Wako Wote" (mstari wa 9)
Ushauri mwingine uliopewa Sulemani ulikuwa amtumikie Mungu kwa audilifu na nia. Utakatifu wa moyo ni muhuri na ushuhuda wa huduma ya uaminifu kwa Mungu. Mungu ana haja na huduma zetu, lakini zaidi ya yote, hali ya moyo wetu, roho yetu na nia zetu. Tumeitwa kama Sulemani kutumika *"na nia thabiti…"* Kwa pendekezo hili, Daudi alimwambia Sulemani asiwe na utawala ulio hai tu, bali huduma iliyowekwa wakfu kutoka kwa moyo kwa Mungu. Huduma ni lazima iwe na furaha, kwa sababu Mungu anajua motisha na nia tunayohudumu nayo. Hivyo leo, ni lazima ukombozi wa Kristo uwe motisha yetu ya juu katika kuhudumu. Daudi alimwambia mwanawe: *"Ukimtafuta yeye, utamwona; lakini ukimwacha, atakutupilia mbali milele."*

C. "…Bwana Amekuchagua Wewe Umjengee Nyumba ya Ibada …" (mstari wa 10)
Kipaumbele cha kwanza cha Sulemani kama mfalme kilikuwa kumjengea Bwana hekalu. Kujenga hekalu halikuwa suala rahisi kwa vile kulikuwa kunaenda kuwa na vizuizi vingi. Kwa hivyo, katika 1 Mambo ya Nyakati 28:20, Mfalme Daudi alimpa Sulemani maneno ya kumtia moyo. Wakati tunaanza mradi mkubwa, ni lazima tuhesabu gharama ili itusaidie kukamilisha mradi. Mtu alisema wakati mmoja: *"Ili kuanza mradi mkubwa, unahitaji ujasiri. Ili kukamilisha mradi mkubwa, unahitaji uvumilivu."* Je, ni miradi mingapi huisha kama hisia au udaganyifu? Pengine tuneanza kusoma kitabu cha Biblia na hatujawahi kamilisha. Pengine tumeanza kuomba kila asubuhi kisha tukakata tama, n.k. Haijalishi suala ni gani, ni lazima tuwe wajasiri na kuvumilia, tukimtumainia Bwana kabisa.

**III. Mapendekezo Ya Taifa (1 Mambo ya Nyakati 29:1-5)**

A. Sadaka Ya Ukarimu Ya Watu (1 Mambo ya Nyakati 29:6-9)
Daudi, baada ya kutoa sadaka yake ya ukarimu, alikamilisha na maneno yafuatayo: *"Ni nani basi atakayemtolea Bwana kwa hiari ili ajiweke wakfu hivi leo kwa Bwana?"* (mstari wa 5). Hadi wakati huu, Daudi alihubiri kwa mifano; na tangu wakati huo, angesubiri jibu kutoka kwa watu. Kazi ya Mungu inahitajibidii ya wote, wala si wachache tu. Ingawa kujitolea ni lazima kila wakati kuanze na wale wanaoongoza kazi ya Bwana, yaani, wachungaji, rais, waalimu, n.k., kila mtu anahitaji kuhusika. Tunaona haya katika mwisho wake, *"Ndipo watu wakafurahi kwa sababu walitoa kwa hiari, maana kwa moyo wao wote walimtolea Bwana. Daudi mfalme alifurahi sana."* (1 Mambo ya Nyakati 29:9)

B. Ombi la Daudi (1 Mambo ya Nyakati 29:10-25)
Kwa furaha, Daudi aliomba mbele ya Mungu. Lilikuwa ombi la unyenyekevu na la kutoka moyoni ambalo lilihusu hatua tano zinazohusika:

1. Kuabudu Mungu, kumpa heshima na utukufu (mistari ya 10-13).
2. Kudhalilika na kutambuliwa kwamba neema yake ndiyo inayotuwezesha kushiriki naye (mistari ya 14-15).
3. Shukrani kwa kujenga nyumba kwa jina la Bwana (v. 16).
4. Kukiri wazi na nia ya kuishi kwa uaminifu na uwazi (mistari ya 17-19).
5. Ombi kwa Mungu kwa moyo unaodumu katika ukarimu (mstari wa 17).

Watu walimbariki Mungu na kumtolea sadaka za wanyama kwa furaha (mistari ya 20-22). Leo sisi ni dhabihu ya ibada ya kweli kwa Mungu (Warumi 12:1-2). Mistari ya mwisho ya 1 Mambo ya Nyakati inathibitisha uaminifu wa Bwana (mistari ya 23-25).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, kwa nini Mungu hakumruhusu Daudi ajenge hekalu (mistari ya 2-3)?
- Je, kwa nini viongozi au ndugu wakubwa na dada katika imani wanaitwa kuwasaidia viongozi wadogo sasa?
- Je, ukarimu tunaojifunza katika kifungu hiki unatufundisha nini (1 Mambo ya Nyakati 29:6-9)?


## HITIMISHO

Daudi alikuwa mtiifu kwa Mungu. Ingawa kulikuwa na mateso maishani mwake kwa sababu ya maamuzi mabaya, mwisho wa siku zake, Mungu alimpa umri wa uzee kwa amani. Alitimiza tamaa yaek, na kupitia kwake aliaacha mfano wa maisha yanayostahili kuigwa kwa ukarimu wa kweli na kumuabudu Bwana wetu.

**Somo la** 32:

## MAANDALIZI YA KUJENGA HEKALU

**Lengo la Somo:** Kujifunza kwamba kazi ya Mungu inahitaji matayarisho mazuri.
**Methali:** Unapofuata nyayo za baba yako, unajifunza kutembea kama yeye.
**Kifungu cha Kusoma:** 1 Mambo ya Nyakati 28-29
**Mstari wa Kumbukumbu:** "...Kwa kuwa Bwana hutafuta-tafuta mioyo yote, na kuyatambua mawazo yote na f ikira. Ukimtafuta, ataonekana nawe, ukimwacha, atakutupa milele." 1 Mambo ya Nyakati 28:9
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?
Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?
Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.
**Himizo la Hadithi:** Dhabihu iliyo nzuri zaidi ni maisha yetu ya ibada kwa Mungu.



| Somo la 33 | OMBI MUHIMU |
|---|---|
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati 1:1-13 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kujua kwamba hakuna hazina kuu kuliko hekima inayotoka mbinguni, ambayo uamuzi wetu unapaswa kusimamia. | "Heri mtu anayegundua hekima, mtu yule anayepata ufahamu." **Mithali 3:13** |

## UTANGULIZI

Je, ni kufanana na tofauti gani ambayo iko kati ya Kijana Tomaso na Sulemani? Mfalme Sulemani anachukuliwa kuwa mtu wa hekima zaidi wa wakati wote; na Kijana Tomaso alijulikana kuwa mtu wa mwisho kujua kila kitu. Wa mwisho alizaliwa katika karne ya kumi na nane. Akiwa na miaka miwili alijifunza kusoma Biblia mara mbili. Akiwa na miaka 14, angesoma lugha 10, ikiwa ni pamoja na Waebrania. Pamoja na kusoma maandishi na picha za Kimisri, alifanya pia uvumbuzi nyingi za kisayansi. Akili na hekima ni vitu tofauti. Akili inapendeza maarifa ya kisayansi lakini hekima ni uwezo wa kutofautisha kati ya mema na mabaya. Ya kwanza inapatikana kupitia masomo, na ya pili ni zawadi kutoka kwa Mungu ya kutuwezesha tusijikwae na kuishi milele. Lakini je, Sulemani alipataje hekima nyingi akiwa na umri mdogo? Hebu tuone kile 2 Mambo ya Nyakati 1:1-13 inasema.

### I. Ombi la Hekima (2 Mambo ya Nyakati 2:1-10)

Kulingana na watoa maoni, Sulemani alianza utawala wake akiwa na miaka kati ya 16-18. Alipokuwa mdogo, alikuwa tayari mara tu Daudi babake alimthibitisha kuwa mfalme wa baadaye wa Israeli: *"Mfalme Daudi akaumbia ule mkutano wote uliojumuika, 'Sulemani mwanagu, ambaye peke yake amechaguliwa na Mungu. Kazi hii ni kubwa, kwa sababu nyumba atakayoijenga si ya mwanadamu, bali ni ya Mungu'"* (1 Mambo ya Nyakati 29:1) Utawala wa taifa haukuwa rahisi kusimamia, ikiwa ni pamoja na pendekezo muhimu la kujenga nyumba ya Mungu, jambao ambalo Daudi hangefanya kwa amri ya uungu (1 Mambo ya Nyakati 28:2-3).

Mwandishi wa 1 Wafalme sura ya 2 inaeleza jinsi Daudi alimshauri Sulemani atende kwa hekima. Hii inaonyesha mambo mawili ambayo baba anatarajia kutoka kwa mtoto wake: kufanya na kutenda kwa hekima: *"Basi wewe fanya kadiri ya hekima yako, ila tu usimwache afe kwa amani"* (1 Wafalme 2:6); *"…Wewe una hekima…"* (1 Wafalme 2:9). Daudi alitarajia mwanawe Sulemani atende kwa hekima, na alikuwa na uhakika kwamba atafanya hivyo. Hii inadhihirisha mapenzi ya Mungu kwa Sulemani kutawala ufalme na kujenga hekalu lililotarajiwa, jambo ambalo Adoniya nduguye, ambaye alitaka cheo, hangeweza kufanya (1 Wafalme 1:5-27).

Kwa sababu ya kila kitu kilichotajwa katika aya, Sulemani hakuhitaji chochote kuliko moyo wa hekima. Sulemani alitaka kuhimiza moyo wa babake ambaye alimtumainia kuwa mfalme mpya licha ya ukweli kwamba alikuwa na ndugu kadhaa ambao walikuwa wameteuliwa kama mfalme. Kila mtoto anapaswa kulenga kuleta furaha kwa wazazi wake. Baadaye, katika hekima yake, Sulemani aliandika maneno haya kwa hafla tatu: *"Mtoto mwenye hekima ni furaha ya babake…"* (Mithali 10:1, 15:20, 29:3). Kinyume chake: *"Mtoto mpumbavu ni huzuni kwa baba yake"* (Mithali 17:25, 19:13). Ili kupata hekima kutoka juu, Sulemani alianza kwa kumpa Mungu nafasi katika maisha yake: *"Sulemani alipanda mbele ya madhabahu ya shaba iliyokuwa mbele ya Bwana iliyokuwa kwenye hema la mkutano akatoa tambiko elfu moja za kuteketezwa."* (2 Mambo ya Nyakati 1:6)

Katika matendo ya kujitoa kwake na ukarimu katika ibada, Mungu alijitokeza na kusema: *"Omba chochote utakacho name nitakupa"* (mstari wa 7). Njia pekee inayoonekana ya kupata uwepo wa Mungu ni wakati tunaingia katika ushirika Naye katika roho na kweli. Leo, Mungu ametuachia Neno Lake lizungumze kwa mahitaji yetu. Kwa toleo la Mungu Sulemani alikumbuka maneno yote ya babake Daudi juu ya jukumu la kuongoza taifa la (mistari ya 8-9). Hiyo ndio sababu katika ujana wake, alimwambia Bwana: *"Unipe hekima na maarifa ili niweze kuwatawala watu wako vizuri."* (mstari wa 10). Kama mkuu, Sulemani hakika alikuwa ameagizwa vyema na kuelimishwa. Hata hivyo, hiyo haikutosha kulitawala taifa la Israeli. Baba yake alimtia moyo, na akatafuta hekima hiyo mahali

panapofaa: Katika uwepo wa Mungu.

Ingawa sisi si wafalme, tunapaswa kufanya maamuzi bora katika maisha yetu. Wengi wameanguka katika ukomo wa makosa na, kama usemi unavyosema, bado wanajikwaa juu ya jiwe moja. Sababu ya hii ni kwamba hawamuombi Mungu awape hekima. Mtume Yakobo anatufundisha yafuatayo: *"Kama mmoja wenu ametindikiwa hekima, basi, anapaswa kumwomba Mungu ambaye atampatia, kwani Mungu huwapa wote kwa wingi na kwa ukarimu."* (Yakobo 1:5) Tunahitaji kufanya uchambuzi wa kibinafsi katika maisha yetu: Ni vile tulivyo kwa sababu Mungu alitaka iwe hivyo; au je, ni kwa sababu imekuwa matokeo ya upumbavu? Tufanye yale Sulemani alifanya: Tumuombe Mungu hekima.

## II. Zawadi ya Uungu (2 Mambo ya Nyakati 1:11-12)

Tunaye Mungu anayetoa, na wakati tunaomba vitu vinavyofaidi maisha yetu ya kiroho na ya ndani, Yeye yuko tayari kutusaidia. Kumbuka yale Bwana Yesu alituambia: *"Ombeni nanyi mtapata ili furaha yenu ikamilike."* (Yohana 16:24) Tunapaswa tukumbuke kwamba wakati Bwana alisema hivi, hakumaanisha tuombe mambo ya mwili, kwa sababu katika kweli mambo ya mwili hayaridhishi. Badala yake yanaelekeza hata kwa mengi zaidi. Hata hivyo, kuomba uwepo wake unaoendelea kupitia Roho Wake Mtakatifu ni kuwa na furaha ya milele; na *"... hakuna mtu atakayeiondoa kwenu"* (Yohana 16:22). Furaha ni tiba ya huzuni, hofu na upweke.

Sulemani hakuweza tu kuhukumu kwa hekima, lakini pia kupitia utawala wake katika Israeli, aliweza kufanya mambo matatu ambayo wafalme wengine hawangeweza kutimiza: Kwanza, alijenga hekalu maridadi na nzuri sana ambayo imewahi kuwepo, pamoja na vipimo na maeneo maalum ambayo Mungu alikuwa ameonyesha kupitia kwa Daudi. Pili, alipanua eneo la kitaifa bila hitaji la vita au vifo kama wafalme wengine walivyofanya. Hii ilileta amani na kujulikana kwa taifa la Israeli. Aliheshimu maana ya jina lake: *"amani."* Mataifa yaliyowazunguka yalikuwa tayari kufanya urafiki na Sulemani ili kupata faida fulani. Mfano mmoja wa hii ulikuwa kuzuru kwa malkia wa Sheba (2 Mambo ya Nyakati 9:1-12).

Alikuwa na uwezo wa kufanya biashara na nchi tofauti. Hiyo ndio sababu aliweza kuagiza rasilimali nying na vifaa vilivyotumika kwa ujenzi wa hekalu. Udhaifu wake ulikuwa farasi, ambayo alibadilishana na nchi za kaskazini na kusini (2 Mambo ya Nyakati 1:16, 9:24). Hekima yake ilileta utajiri kwa taifa la Israeli. Zaidi, Sulemani alifahamika kupitia ushauri na maandishi yake. Kama mwandishi wa mashairi, aliandika mithali elfu tatu na nyimba elfu moja na (1 Wafalme 4:32); kama mwanafilosofia, aliweza kufundisha juu ya miti, wanyama, ndege, wanyama watambaao na samaki (1 Wafalme 4:33). Mfalme huyu aweza kuwa alikuwa mwandishi wa vitabu vitatu vya kanuni: Mithali, Wimbo Ulio Bora na Mhubiri.

## III. Tuzo Lililoongezeka (2 Mambo ya Nyakati 1:12-13)

2 Mambo ya Nyakati 1:12 inasema: *"...ninakupa hekima na maarifa. Pia, nitakupa utajiri, amli na heshima zaidi ya mfalme mwingine yeyote aliyekuweako kabla yako na mfalme mwingine yeyote atakayetawala baada yako."* Wakati Sulemani alifanya ombi lake kwa Mungu, hakujifikiria yeye mwenyewe, lakini alifikiria zaidi juu ya jukumu alilokuwa nalo kama mfalme wa taifa lake, yaani, katika misheni ambayo alikuwa amechaguliwa. Kipaumbele chake hakikuwa kupata utajiri, kupata vitu vingi vizuri zaidi, au utukufu au kujulinana ambako dunia ingempatia. Mungu alitaja vitu hivi ambavyo havikuwa kipaumbele au furaha yake. Hata hivyo, Mungu alitaka kuongeza vitu hivi kama tuzo ya kuomba tu kwa unyenyekevu hekima na maarifa ya kutawala Israeli.

Kila kitu ambayo Mungu alimhaidi Sulemani kilitimia. Hata hivyo, alimuonya pia katika 2Mambo ya Nyakati 7:17-18 kwamba vitu hivi alivyoongezewa visiwe chombo cha kuabudu, bali awe mwaminifu kwa Mungu ili maovu yasimjie.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, unatarajia nini kutoka kwa watoto wako?
- Je, Sulemani alimuomba nini Mungu ambacho kilifurahisha moyo wa babake? (2 Mambo ya Nyakati 1:10).
- Je, ni majaribu gani yanayoweza kuja pamoja na utajiri na utukufu wa dunia hii?

## HITIMISHO

Hekima ni bora kuliko dhahabu na fedha zikiwekwa pamoja, na kila jiwe la thamani. Wenye kiburi hufanya makosa ya kufyata utajiri; mwisho wao utakuwa mbaya (Mithali 8). Kristo ndiye chanzo cha hekima ya kweli; kumpokea ndio utajiri mkuu ambao unaweza kupatikana. Tukikaa ndani yake na maneno yake yakae nasi, tunaweza kuomba chochote tutakacho nasi tutapewa (Yohana 15:7).

**Somo la** 33:

## OMBI MUHIMU

**Lengo la Somo:** Kujua kwamba hamna mtu awezaye kutawala bila hekima na maarifa kutoka kwa Mungu.

**Methali:** Maarifa ni kama bustani: Isipopaliliwa, haiwezi kuvunwa.

**Kifungu cha Somo** 2 Mambo ya Nyakati 1:1-13

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?
Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?
Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii? Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Mstari wa Kumbukumbu:** Basi sasa nipe hekima na maarifa, nijue kutoka na kuingia mbele ya watu hawa. Kwa kuwa ni nani awezaye kuwahukumu watu wako hawa walio wengi? 2 Mambo ya Nyakati 1:10

**Himizo la Hadithi:** Tafuata hekima na maarifa ya Mungu naye atakuinua.



| Somo la 34 | # NYUMBA INAYOSTAHILI MUNGU |
|---|---|
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati sura ya 3 hadi 7 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kutambua kwamba sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu na kutambua maana ya hii. | "Ichunge nyumba hii mchana na usiku, mahali ambapo umechagua watu wako waliabudu jina lako. Unisikie mimi mtumishi wako ninapokuja mahali hapa kuomba." **2 Mambo ya Nyakati 6:20** |

## UTANGULIZI

Mfalme Daudi alitaka kujenga hekalu, ambayo ingekuwa ya kipekee na mahali maalum kwa Mungu. Hata hivyo, yake ilitimia kwa sababu tumeona katika masomo yaliyopita, alikuwa mfalme wa vita na kazi ilikuwa itekelezwe na mwanawe Sulemani. Tunapojifunza somo hili, tunaweza kugundua mambo muhimu ya ujenzi wa hekalu hilo ambayo yanaweza kutumiwa kwa maisha yetu ya Kikristo ya kila siku.

Ujenzi wa Hekalu (2 Mambo ya Nyakati 3:1-17)
Hekalu la Yerusalemu, linalojulikana kama hekalu la Sulemani, lilikuwa liwe mahali pa kuabudu ambapo pangechukua nafasi ya hema ilikuwa pamoja na watu wa Israeli katika safari yao jangwani, na ilikaa juu ya vilima vya Gibeoni: *"Hema ya Bwana, ambayo Musa alikuwa ametengeneza nyikani, na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa wakati huo vilikuwa bado pale mahali pa kuabudia huo Gibeoni."* (1 Mambo ya Nyakati 21:29)

A. Mahali pa Ujezi
Katika 2 Mambo ya Nyakati 3:1-2, tunasoma kwamba Sulemani alianza kujenga nyumba ya Bwana katika Yerusalemu, kwenye Mlima Moria. Tamaduni ya Kiyahudi inatambua Moria kuwa sehemu ile ile ambayo Mungu alimwagiza Abrahamu kumtoa dhabihu ya mwanawe Isaka (Mwanzo 22:2). Ardhi ilipatikana na Daudi wakati alimtengenezea Yehova madhabahu ambapo alitoa sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya amani, na Bwana alijibu kwa kutuma moto kutoka mbinguni kwenye madhabahu kama jibu la dhabihu yake (1 Mambo ya Nyakati 21:22-26).

B. Vipimo (2 Mambo ya Nyakati 3:3-4)
Vipimo vya hekalu lililojengwa na Mfalme Sulemani kwa ajili ya Bwana vilikuwa hivi: Urefu wa dhiraa sitini, upana wa dhiraa ishirini, na urefu wa miko mia na ishirini (2 Mambo ya Walawi 3:3-4). Katika mita, *"mjengo unapaswa kuwa na urefu wa mita na upana mita 9 na urefu wa mita 13.5 (dhiraa 60×20×30)."* (https:// en.wikipedia.org/wiki/Temple_of_Jerusalem).

C. Vifaa
Katika ujenzi wa hekalu, vifa bora zaidi na vya manufaa wakati wa Sulemani vilitumika, kama vile: Dhahabu safi na nyororo; jasi na mti wa mwerezi; vitambaa kwa pazia, kama vile rangi ya samawati, zambarau, nyekundu na kitani; shaba, mawe ya kuchongwa ya kuta na vito vya thamani.

Katika 1 Wakorintho 3:9, Paulo aliandika: *"...Maana sisi ni ndugu wafanyakazi pamoja na Mungu na nyinyi ni shamba lake, jengo la Mungu.* Katika ujenzi, mtu huweka misingi, mwingine anajenga, lakini kila mmoja hujijengea maisha ya wale wanaotunga hekalu la Mungu. Kila mmoja lazima achague vifaa ambavyo anataka kutumia, ambayo inaweza kuwa dhahabu, fedha, mawe ya thamani, au kuni, vifaa vya ubora duni, kama nyasi na mabua. Katika siku za mwisho, vifaa tulivyotumia vitajaribiwa kwa moto.

D. Kumalizia
Kila kitu kilifunikwa na dhahabu nyororo. Nguzo mbili ziliwekwa mbele ya hekalu, ambazo kila moja ilipewa jina. Nguzo iliyokuwa upande wa kulia iliitwa Yakini na ile iliyokuwa upande wa kushoto, Boazi (1 Wafalme 7:21). Mawe ya ujenzi yalifunikwa na mierezi, kuni kwa njia ambayo hazikuonekana. Vivyo hivyo, mti wa mwerezi ulikuwa na nakshi za maboga

ya mwituni na maua, na vyote vilifunikwa na dhahabu (1 Wafalme 6:15,18).

## I. Samani za Hekalu (2 Mambo ya Nyakati 4:1-5:10)

Hekalu lilijumuisha vifaa na vyombo vilivyohitajika kutekeleza sherehe na matambiko (dhabihu na sadaka za kuteketezwa). Hekalu jipya lilihitajika kuwa na vifaa ambavyo Mungu alikuwa amemwambia Musa avijumuishe. Lakini hekalu hili jipya lilikuwa lifafanuliwe sana. Walitengeneza vinara vya taa kumi vya dhahabu, meza kumi, bakulimia za kunyunyizia dhahabu nan a maji mengi. Mchoro ulifanya vizuri. Makomamanga mia nne yalichongwa juu ya minara. Vitu vingi vilitengenezwa kwa shaba iliyosuguliwa. Kulikuwa na madhabahu ya dhahabu, There was a golden altar, viti vya taa vya dhahabu safi ili kuwaka ya mahali patakatifu palioelezewa. Waliweka sanduku la agano mahali patakatifu sana, ambapo wakati huu ndani yake lilikuwa tu na mbao za mawa zilizo na zile amri kumi. *"Hakukuwa na kitu ndani ya sanduku la agano, ila vile vibao viwili vya mawe ambavyo Musa aliviweka humo kule Horebu, mahali Bwana alifanya ahadi na watu wa Israeli walipotoka Misri."* (2 Mambo ya Nyakati 5:10) Mungu anataka tupambwe kwa moyo mtakatifu na safi. Anatafuta ukweli wetu na usafi wa nia (1 Samweli 16:7 na 1 Petro 3:3).

## II. Kuwekwa Wakfu kwa Hekalu (2 Mambo ya Nyakati 6:1-7:10)

### A. Sherehe

Sulemani alipokamilisha kujenga hekalu, aliwaita watu kwa sherehe kubwa kwa ajili ya kuwekwa wakfu kwa hekalu. Mfalme Sulemani, pamoja na mkutano wote wa Israeli, walikusanyika mbele ya Sanduku la Agano na kutoa sadaka za kondoo na ng'ombe wasiohesabika (2 Mambo ya Nyakati 5:6). Pamoja na dhabihu ambayo watu walitoa, Sulemani pia alitoa dhabihu ya ng'ombe elfu ishirini na mbili na kondoo elfu mia moja na ishirini. Wakati huo wa kuweka wakfu, mfalme alimuomba Bwana akimwuliza msamaha wa dhambi za watu na kutoa dhabihu, sadaka za kuteketezwa, na sadaka za amani: *"Sulemani alipomaliza sala yake, moto ulishuka kutoka mbinguni na kuchoma sadaka na tambiko za kuteketeza zilizotolewa, kisha utukufu wa Bwana ukaijaza nyumba."* (2 Mambo ya Nyakati 7:1) Uwepo wa Mungu ulikuwa mkuu kwamba mahakuhani hawangeweza kubaki mahali pale kwa vile wingu lilikuwa limefunika kila kitu. Uwepo huo huo wa Mungu bado unajidhihirisha kwetu sisi ambao tunamwamini Mwana wa Mungu, kupitia Roho Mtakatifu, kama vile anavysema katika Mathayo 18:20 *"Kwa maana pale wanapokusanyika wawili au watatu kwa jina langu nipo hapo mimi kati yao."*

### B. Sherehe Kubwa

Mbali na sherehe ya kuwekwa wakfu kwa hekalu, kulikuwa na siku saba za sherehe pamoja na taifa lote la Israeli. *"Walawi wote waimbaji— wakiwamo Asafu, Hemani, na Yeduthuni pamona na wanao na watu wa jamii – walisimama upande wa kushoto wa madhabahu, wakiwa wamevalia nguo za kitano na wakicheza na matoazi, vinana na vinubi. Walifuata makuhani 120 wapiga tarumbeta. Wapiga tarumbeta na wanamuziki walijiunga nao kwa umoja ili kutoa shukrani na kumwambwa Bwana asante. Pamoja na tarumbeta, kulikuwa na matoazi na vyombo vingine, waimbaji walisifu sauti zao kwa kumshukuru Bwana."* (2 Mambo ya Nyakati 5:12-13)

Kulinda kwa Daudi na Sulemani kwa ujenzi wa hekalu la Mungu kunapaswa kuigwa katika maisha yetu, tukikumubka yale Paulo alisema: *"Je, hamjue nyinyi ni hekalu la Mungu na Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?"* (1 Wakorintho 3:16) Na tuna uhakika kwambe hata kama nyumba hii itaangamizwa, tunayo ahadi ya milele *"Maana tunajua kwamba hema hii ambamo tunaishi sasa hapa duniani yaaani mwili wetu, itakapong'olewa, Mungu atatupa makao mengine mbinguni, nyumba ya milele isiyotengenezwa kwa mikono."* (2 Wakorintho 5:1)

## MASWALI YA ZIADA

- Kama hekalu la Roho Mtakatifu, je, tunawezaje kuchangia kumtii Mungu nalo?
- Leo sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu. Je, vyombo hivyo ni gani leo?
- Je, ni nani walikuwepo wakati wa kuwekwa wakfu kwa hekalu? (2 Mambo ya Nyakati 5:2,12)

## HITIMISHO

Sulemani, kwa utiifu wake kwa Mungu, alijenga hekalu na vitu bora zaidi ambavyo angepata, akilifanya kuwa jengo nzuri na la kupendeza. Leo, Mungu, ambaye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, anastahili kukaaa katika hekalu bora. Biblia inatufundisha kwamba anachagua kuishi nasi leo, kanisani mwake. Kama hekalu la Roho Mtakatifu, tuishi maisha matakatifu yanayomheshimu Mungu.

**Somo la 34:**

**NYUMBA INAYOSTAHILI MUNGU**

**Lengo la Somo:** Kutambua kwamba sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu.


**Methali:** Nyumba ndogo inaweza kuweka marafiki wengi.

**Kifungu cha Kusoma:** 2 Mambo ya Nyakati 3-7

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Sikia maombi yangu mimi mtumishi wako na ya watu wako Israeli wanapoomba wakielekea mahali hapa. Usikie maombi kutoka huko mbinguni na ukishasikia, utusamehe." 2 Mambo ya Nyakati 6:21b

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?
Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?
Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii? Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** Sisi ni Hekalu kwa sababu Mungu amechagua kuishi katika maisha yetu leo.



| Somo la **35** | **MFALME ALIYE NA HEKIMA YA KIPEKEE** |
|---|---|
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati 7:11-9:28 |

| **Lengo** | **Mstari wa Kumbukumbu** |
|---|---|
| Kujifunza jinsi ya kutafuta hekima ya Mungu kwa kila muda wa maisha yetu, na hivyo kufanikiwa kabisa. | "Nao wafalme wote nchi zote walikuwa na hamu ya kumwendea Sulemani ili kusikiliza hekima yake ambayo Mungu alikuwa amemjalia." **2 Mambo ya Nyakati 9:23** |

## UTANGULIZI

Mfalme Sulemani alikuwa mmoja wa wafalme wa Israli waliobaki kwenye kiti cha enzi kwa miaka 40 (2 Mambo ya Nyakati 9:30). Kwa wafalme wote waliotawala Israeli, aliwacha alama kubwa ya heshima yake, hasa hekima ambayo alitambuliwa nayo pakubwa (2 Mambo ya Nyakati 9:23). Vifungu vya kibiblia katika masomo haya vinatuonyesha kile Mfalme Sulemani alipata kwa sababu ya hekima ambayo Bwana alimpa, ikiwa ni pamoja na utajiri mwingi.

Wakati huo, hapakuwa na mfalme wa ufalme ambaye alikuwa hajasikia juu ya Mfalme mkuu Sulemani, na walitaka kuwa kama yeye na kufurahia utajiri kama wake. Kwa sababu ya hii, Mfalme Sulemani alipokea wageni wengi kutoka kwa viongozi wa kimataifa ambao walitaka sana kujua jinsi alifika mahali alikuwa.

### I. Agano la Mungu na Sulemani (2 Mambo ya Nyakati 7:11-22)

A. Moyo Wenye Mtazamo Sawa (mistari ya 11-12)

1. Neno *'moyo'* katika Biblia ni zaidi ya chombo muhimu cha mwili kwa maisha. Ingawa katika Maandiko neno 'moyo' linaonekana zaidi ya 900, idadi kubwa ya hafla hizi ni karibu kamwe kwa maana halisi. 'Moyo' katika Biblia unahusu mwendo wa ndani wa kuishi kwetu ambapo hisia inakaa (Zaburi 62:10); mawazo (Mwanzo 6:5); hiari (Zaburi 119:2); na mara nyingi, unawakilisha sehemu ya ndani ya utu wetu (Mwanzo 6:6).

2. Bwana alimtokea Sulemani, na maneno aliyonena juu yake (2 Mambo ya Nyakati 7:11-12), ni dhihirisho kwamba anasikia maombi ya watoto wake kila wakati, na anafurahia wale wanaomtafuta ili awape yaliyo mema (Zaburi 145:18-19), na wanayatafuta kwa mioyo yao yote (Yeremia 29:13).

B. Ahadi Nzuri Juu ya Watu Wake (mistari ya13-22)

1. Mtazamo Wake Umejaa Upendo.

Mtazamo wa Mungu ulikuwa kwa Sulemani, lakini pia, hasa kwa watu wake. Mungu alijua yale yalikuwa katika mioyo ya Waisraeli, na ingawa mtazamo wake umejaa upendo, Yeye anapendezwa na yaliyo ya haki na takatifu; hivyo uasi hule huku yake (mstari wa 13).

Kuwa na wakati wa kutafakari na wanafunzi wako na uwaulize: Je, watu duniani wanaishi aje leo? Je, ni kwa nini kuna uhalifu mwingi, uhaba, ukosefu wa haki, kutojali, kuchanganyikiwaWhy is there so much crime, scarcity, injustice, indiffer, maumivu na hofu? Je, ni uhusiano gani ambao matatizo haya yote ya hisia yanayo kwa suala la utiifu kwa amri za Mungu?

2. Masharti ya Kupata Ahadi.

Hata katikati ya ukweli huu wote, kulikuwa na ahadi nzuri ya uponyaji kwetu sisi ambao tulitubu kwa kweli na kujinyenyekea mbele ya enzi yake. Mungu aliwaahidi Waisraeli vitu vitatu wakinyenyekea wenyewe, waomb, na kumtafuta na kuacha njia zao mbaya: i) Angesikika maombi yao; ii) Angewasamehe, na iii) Angerejesha utajiri wa nchi yao. Hata hivyo, ili kupata ahadi hizi zote, Mungu aliweka chini masharti magumu (mstari wa 14). Walihitaji kufanya yafuatayo:

- Mungu anataka watu wake wawe wanyenyekevu (Waefeso 4:1-2).
- Mungu anataka watu wake waombe (Waefeso 6:18) na kutafuta uso wake (Wakolosai 3:1- 2).
- Mungu anataka watu wake waachane na njia zao mbaya (Ufunuo wa Yohana 3:19).

Ahadi ya Bwana inaendelea kwa watu wake, na anaahidi

kusikiliza hali ambayo tunapitia; na utiifu unabaki sharti muhimu kwa ajili ya baraka za Bwana (2 Mambo ya Nyakati 7:15).

Katika kifungu hiki, Sulemani anahimizwa kuenenda kama baba yake: kuishi katika utiifu na unyenyekevu kwa Mungu, ili utawala wake ufanikiwe (mistari ya 17-18). Waambie wanafunzi washiriki baadhi ya uzoefu au hadithi ambapo, kwa sababu ya nia nzuri na kuwa watiifu kwa Mungu, walipokea tuzi nzuri.

3. Matokeo ya Kutotii

Kumweka Mungu katika nafasi ya pili au ya tatu maishani mwetu mara nyingi kutatuanika kwa mateso mengi, ambayo yanaweza kutuelekeza kwa kutenganishwa naye milele (mistari ya 19-20). Hekalu lililojengwa na Sulemani lilikuwa patakatifu pazuri ambapo jina la Mungu lilisifiwa na uwepo wake ulionekana. Hata hivyo, baada ya watu wa Mungu kuacha njia ya utiifu, hali ilibadilika. Leo, msikiti wa Waislamu kwenye tovuti ya hekalu.

## II. Mungu Alimpa Mafanikio Makubwa (2 Mambo ya Nyakati 8:1-18)

Mungu alikuwa mwaminifu kwa ahadi yake kwa Mfalme Sulemani Kwa sehemu yake, Mfalme Sulemani alitimiza utiifu wake kwa Mungu. Katika kipindi hiki cha utawala wake, Mfalme Sulemani alipata yafuatayo:

A. Alikamilisha Ujenzi wa Hekalu (mstari wa 1)

Hekalu ulikuwa mradi wa muda mrefu. Ilimchukua Sulemani nusu ya muda wa utawala wake kulikamilisha. Mungu alikuwa makini kwa hayao yote. Kutajwa kumefanywa juu ya vita vya pekee ambavyo vilitokea katika Biblia wakati wa utawala wa Sulemani. Vifungu hivi pia vilitaja miradi ingine ya mjengo katika miji mpya na kuimarisha ile ya zamani, kupanuliwakwa miradi kama vile maghala, ngome, mahali pa farasi na magari Kwa kweli, Mfalme Sulemani alikuwa mjenzi bora (mistari ya 2-6).

B. Hotuba Yake Ya Ibada ya Umma (mistari ya 11-16)

Huu ulikuwa uamuzi wa kufurahisha ambao Sulemani alifanya kuhusiana na mkewe, binti wa Farao. Alimjengea jumba la kifalme, mbali na mji wa Daudi. *"Huu ulikuwa mchanganyiko wa umoja kati ya malkia wa Wamisri na mfalme wa Wahebrania, mwabudu wa miungu nyingi aliyeungana kumwabudu Yehova. Angalau, busara na unyeti wake wa kiroho bado ulimwelekeza kufikiria juu ya maoni ya Yehova ya muungano huu, kwa kumjengea mke wake makao mbali na mahali patakatifu (mstari wa 11)."* (op. cit. 2000, p. 335).

Tafsiri inayowezekana kwa nini Sulemani aliwaoa wanawake kutoka mataifa tofauti ilikuwa ni kupata nafasi ya siasa. Wakati alioa binti wa mtawala fulani, pengine hawangemvamia kama mmoja wa binti wao alikuwa malkia. Hatujui hakika kama maelezo hayo ni ya kweli au la. Ukweli ni kwamba Sulemani alikuwa na wanawake wengi. Tabia kama hiyo ilikuwa kinyume na maagizo ya Mungu.

C. Mafanikio ya Kibiashara (mistari ya 17-18)

Mwishowe, sura hii inakamilika na hadithi juu ya Hiramu, ambaye alituma dhahabu kwa Sulemani. Halikuwa jambo la kawaida kwa mtu wa Israeli kwenda Esion-geberi kwa vile Waisraeli hawakuwa mabaharia na hawakufanya kazi baharini (mstari wa 17). Hii ilikuwa bandari karibu na kaskazini mwa Bahari ya Shamu. Kitendo cha Sulemani kinatuonyesha maono makubwa ambayo Sulemani alikuwa nayo kwa biashara, kwa kuwatuma watumishi wake kwenda Ofiri, sehemu iliyokuwa na dhahabu nyingi (mstari wa 18, 2 Mambo ya Nyakati 9:10; Isaya 13:12). Ingawa Mfalme Sulemani alikuwa mtu mashuhuri wa biashara, bahati mbaya hilo lilimwelekeza kuacha uhusiano wake na Mungu.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, unafikiri Mungu alitaka kumfanya Mfalme Sulemani kufahamika?
- Je, kitu gani kilicho na thamani zaidi Utajiri au hekima?
- Wakati Biblia inataja neno "moyo" je, inamaanisha nini?

## HITIMISHO


Wafalme wengi na mataifa walitambua jininsi Mungu alikuwa kupitia kwa hekima na ushindi wa Sulemani. Ni muhimu kuwa na moyo ambao ni mtiifu kwa amri za Mungu. Hii inafaa kuwa juu ya tamaa ya binafsi, kujiridhisha na tamaa za mwili.

**<u>Somo la 35</u>:**

**MFALME ALIYE NA HEKIMA YA KIPEKEE**

**Lengo la Somo:** Kujifunza jinsi ya kutafuta hekima ya Mungu kwa kila hali.
**Methali:** Mafundo ya hekima hufunguliwa na watu walio na hekima
**Kifungu cha Kusoma:** 2 Mambo ya Nyakati 7-9
**Mstari wa Kumbukumbu:** "Wafalme wote wa duniani wakamtafuta Sulemani uso wake. Walitaka kusikia hekima ambayo Mungu alikuwa ametia moyoni mwake." 2 Mambo ya Nyakati 9:23
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, Mungu anaheshimiwa au kutoheshimiwa kwa njia gani katika hadithi hii?
Swali la 3. Kama ungekuwa katika hadithi hii, je, ni mambo yapi ungeyafanya tofauti? Je, kwa nini ungeyafanya kwa njia hiyo?
Swali la 4. Je, utajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi hii katika wiki hii.

**Himizo la Hadithi:** Wakati tunatafuta hekima ya Mungu, watu watatambua jinsi Mungu alivyo mkuu.



| Somo la<br>**36** | **KUCHAGUA TIMU INAYOFAA** |
|---|---|
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati 10:6-14 |

| **Lengo** | **Mstari wa Kumbukumbu** "Ukiwahurumia watu hawa, ukiwafurahisha na kusema nao maneno mazuri, hapo watakuwa watumishi wako daima." **2 Mambo ya Nyakati 10:7** |
|---|---|
| Kukubali kwamba kuna hitaji la kusawazisha ushauri wa watu wazee na ule wa vijana kabla ya kufanya maamuzi. | |

## UTANGULIZI

Rehoboamu alikuwa mrithi wa moja kwa moja wa kifalme mwenye hekima zaidi ambaye aliwahi kuwako juu ya uso wa dunia. Kama mwana wa Sulemani, mwanzo, alionyesha hekima ambayo baba yake alikuwa amemrithi. Alitafuta ushauri kutoka kwa wazee wa watu wake na hakuwapuuza vijana wa wakati wake ambao pia alitaka ushauri wao. Hata hivyo, tatizo lililotokea baadaye lilikuwa kwamba Rehoboamu hakusawazisha ushauri kwa hekima; na aliamua kutegemea ushauri mmoja. Suala halikuwa ukweli kwamba alikuwa amewauliza vijana, lakini badala yake, kwamba alipuuza ushauri wa wale ambao wana uzoefu, na hili lilisababisha makosa mabaya. Hii haimaanishi kwamba katika makanisa yetu na jamii wasitafute ushauri kutoka kwa vijana; tunapaswa kuzingatia maoni yao.

### 1. Ushauri wa Jimbo la Uzoefu (2 Mambo ya Nyakati 10:6-7)

Katika watu wa Mungu, wazee waliheshimiwa sana; walikuwa halisi kabisa. Wakati huo, mwanamume anaweza kuzingatia kuwa mzee wakati alikuwa na miaka 50au zaidi, wakati kwa upande wa wanawake, walihitaji kuwa 60 au zaidi (Hesabu 8:25, 1 Timotheo 5:9). Katika mataifa yote, walitawala pamoja na mfalme wao au waliwaendea kwa ushauri kabla uamuzi wowote mkubwa wa kitaifa, na Israeli haikuwa ubaguzi. Kwa hivyo, Mfalme Rehoboamu kwa hekima alirudi kwa wazee wa taifa kutafuta ushauri. Katika hali hii, wazee wa utawala wa Rehoboamu walipeana ushauri mzuri na mfupi.

Wazee walimpa maoni mazuri matatu. Hebu tuzitazame:

*i.) "Ukwaruhurmia watu hawa…"* (mstari wa 7): Hii inamaanisha kuwatendea kama wanadamu, kuwatendea kwa ukarimu, kuwaletea ustawi, kwa furaha, na rehema na zaidi ya yote, kutafuta mafanikio yao. Mfalme alihitaji kukumbuka kwamba sisi wote tumeumbwa katika mfano wa Mungu, na hivyo kuwatendea watu wa chini vyema.

ii.) Kama mfalme aliwatendea watu wake vizuri, *"… watakuwa watumishi wako daima."* (mstari wa 7).

iii.) Walimwambia mfalme *"…awape maneno mazuri"* (mstari wa 7). Washauri hawa walikuwa wanamkumbusha mfalme kwamba alihitaji kuwasikilisa watu wake na kuwatendea vyema na kusema nao kwa ukarimu.

Ushauri ulitolewa na wazee wa hekima unaelekeza jinsi Masihi atatawala. Hakika itakuwa utawala wa aina tofauti kabisa ambapo upendo ni kiini cha kila kitu, na watu wa Mungu, watu wake waliokombolewa, watafurahia mafanikio, ustawi na furaha. Itakuwa bora zaidi. Atasema na kila mtu kwa maneno ya wema, ya baraka na wala si ya laana (Ufunuo wa Yohana 22:3).

### II. Ushauri Wa Vijana (2 Mambo ya Nyakati 10:8-11)

Baada ya kusikiliza wenye hekima na wazoefu, Mfalme Rehoboamu alitafuta ushauri wa vijana. Je, alifanya hivyo kwa nini? Mstari wa 8 unasema: *"Lakini Rehoboamu alipuuza shauri la wazee na badala yake akashauriana na vijana wa rika lake ambao walikuwa washauri wake"* Waulize wanafunzi wako: "Je, uko na rafiki (au marafiki) ambao umewafahamu tangu utotoni? Kumbuka vichekesho mlifanya nyinyi nyote? Kumbuka ni nani aliyewashauri? Je, unakumbuka ni nani mliunda naye timu katika michezo yenu nyingi ya utotoni na ujana?"

Tunaelewa kwamba chaguo la Rehoboamu lilikuwa la busara, kwa sababu vijana walikua pamoja na yeye. Labda walikuwa jamaa, wakuu kama yeye, watumishi, n.k. Hata hivyo, zaidi ya washauri, hawa walikuwa marafiki na kaka katika kila njia, na ambao labda alikuwa amefanya ufisadi tangu utoto, ambaye alikuwa na uzoefu wa maendeleo ya ujana. Labda waliishi pamoja utotoni na ujana, hasa malezi yao katika sheria ya

Mungu. Tunaweza kuwazia kwamba huenda walienda hekaluni pamoja na kuishi kupitia uzoefu mwingi kama vile tulifanya tunapowakumbuka wale marafiki tulikua pamoja. Mungu alijua Rehoboamu angechagua ushauri wa marafiki wake kwa sababu aliwapenda na alitaka kuwa nao. (2 Mambo ya Nyakati 10:15, 1 Kings 11:29-33).

Huu ni ushauri ambao rafiki zake walimpa: *"Watu hao waliokuambia 'Baba yako alitutwika mzigo mzito, lakini wewe utupunguzie,' wewe waambie hivi: 'Kidole change kidogo cha mwisho ni kinene zaidi kuliko kiuno cha baba yangu. Mzigo wa baba yangu ulikuwa mzito, lakini wangu utakuwa mzito zaidi. Baba yangu aliwapiga kwa mijeledi, lakini mimi nitawapiga kwa mijeledi yenye miiba.'"* (mistari ya 10-11) Inavyoonekana, Rehoboamu aliona ugumu tu wa kutawala nchi, sio fursa. Alitaja tu mambo mabaya zaidi ya utawala wa Sulemani, na akaamua kuwa mkali kwa watu.

Jambo la busara lilikuwa kuendelea na aina hii ya uongozi, ambayo waliifahamu. Walikuwa wamefundishwa hivi, na uongozi mgumu. Hii ilimaanisha kwamba kila utawala au usimamizi ni lazima utafute mfano wake wa uongozi na wala sio kuendelea katika njia sawa na utawala wa awali, au kwa upande wa kanisa, uchangaji wa hapo awali.

Kazi ya Rehoboamu kama mfalme ilikuwa kurahisisha mzigo wa kizazi cha wakati huo ambacho kilikuwa kimefanya kazi kwa bidii katika kujenga hekalu na jumba la kifalme kwa miaka (2 Mambo ya Nyakati 8:1). Alihitaji kulea kizazi kipya cha vijana ambacho angefanya nao kazi.

Alilazimika kufanya kazi na watu wa wakati wake, akiwashirikisha katika kazi ngumu, bila kupuuza ushauri wa wazee. Kila kijana ni lazima asikilize hekima ya wale walio na uzoefu, akisikiliza ushauri wao mzuri ili kuweza kufanya maamuzi mazuri.

### III. Uamuzi Mbaya wa Mfalme Rehoboamu (2 Mambo ya Nyakati 10:12-14)

Maneno ya mfalme yalikuwa haya: *"Mzigo wa baba yangu ulikuwa mzito; lakini wangu utakuwa mzito zaidi. Baba yangu aliwapiga kwa mijeledi, lakini mimi nitawapiga kwa mijeledi yenye miiba."* (2 Mambo ya Nyakati 10:11-15a).

Vijana walikuwa wameona kwamba Sulemani alikuwa mkali kwa watu, akitaka ushuru wa juu kutoka kwao. Litakuwa jambo la busara kufikiria kwamba Sulemani alikuwa mfalme mwenye hekima, ushuru huu mzito ulikuwa jambo zuri na mfalme mchanga anapaswa kuendelea lakini kwa nguvu zaidi. Kila uamuzi, kila tendo, lina matokeo. Mfalme Rehoboamu alichagua ushauri wa vijana ambao alikua pamoja nao, na watu wa Mungu wakaasi (2 Mambo ya Nyakati 10:16). Tatizo halikuwa ugumu wa utumwa yenyewe, lakini vijana hawalijivunia nguvu zao (Mithali 20:29), na walitaka kuongenza ugumu zaidi kuliko ule Mfalme Sulemani aliwekwa kwa watu wa Mungu (2 Mambo ya Nyakati 10:10- 11, 13-14).

Wakati wa kujivunia nguvu zao, vijana walikosea katika ushauri wao. Hii inatufundisha kuwa jamii inaundwa na vijana na watu wazima wazee. Kwa uongozi wenye mafanikio na utawala, ustawi wa wote unapaswa kuzingatiwa. Ili kuwa na usawa wa jamii au jamii ya kanisa, vijana wote kwa shauku na nguvu, na pia hekima na uzoefu wa wale walioishi muda mrefu, unahitajika. Hivyo, kundi moja linaongoza kwa nguvu, na lingine linaongoza kwa ushauri.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni nini kinaweza kuwa kingetendeka kama mfalme angesikiliza washauri wake wazee?
- Je, kwa nini vijana hawa walimpa mfalme ushauri huu?
- Je, jukumu la washirika wazee katika umati ni lipi?

## HITIMISHO

Tunahitaji kila mmoja. Tunahitaji kusikiliza ushauri wa watu wakubwa katika taifa na wachungaji walio na uzoefu mwingi wa kutufundisha. Wakati huo huo, ikizingatiwa kuwa jamii na hata makanisa yetu yanabadilika milele, tunahitaji kusikiliza sauti ya miaka elfu na ile ya Kizazi cha sasa. Pamoja, kwa umoja, tunaweza kujenga kanisa la Yesu la karne ya ishiri na moja kwa ajili ya utukufu wake.

**Somo la 36:**

## KUCHAGUA TIMU INAYOFAA

**Lengo la somo:** Kukubali kwamba tunahitaji kusawazisha ushauri wa wakubwa kwa wadogo kabla ya kufanya maamuzi


**Methali:** Mfalme akiwa na washauri wazuri utawala wake huwa na amani

**Kifungu cha kusoma:** 2 Mambo ya Nyakati 10:6-14

**Mstari wa Kumbukumbu:** Wakamwambia, wakasema, "Ukiwa mwema kwao watu hawa, na kuwapendeza, na kuwambia maneno mazuri, ndipo watakapokuwa watumishi wako siku zote" 2 Mambo ya Nyakati 10:7

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utashirikiaje hili somo kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Wakubwa kwa wadogo wanaweza kuwa na hekima, hebu tuwasikilize!



| Somo la 37 | # IMANI INAJARIBIWA |
| --- | --- |
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati 20:1-30 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
| --- | --- |
| Kutiwa changamoto kutumia nidhamu za kiroho kama zoezi ambalo Mungu ametupatia kuimarisha imani yetu, na kuibuka washindi machoni pa maadui. | "Wewe ndiwe Mungu wetu! Waadhibu, kwani sisi hunata uwezo wowote mbele ya jeshi kubwa kama hili linalotujia. Hatujui la kufanya ila tunatazamia msaada kutoka kwako." **1 Mambo ya Nyakati 20:12** |

## UTANGULIZI

Katika sura zilizopita za masomo yetu, tunampata Yehu nabii akimshauri mfalme wa Yuda kutofanya ushirikiano na nguvu za adui (2 Mambo ya Nyakati 19:1-27). Lakini Mfalme Yehoshefati hakusikia na kufanya ushirikiano na maadui wa Mungu (mstari wa 2). Hata hivyo, alifanya mambo mema pia (mstari wa 3). Aliwaongoza watu kurudi kwa Bwana na kutafuta haki (mistari ya 6-7). Aliwaongoza watu katika ukweli kwa moyo mweupe (mstari wa 9).

Tunaposoma 2 Mambo ya Nyakati 20, tutaona kwamba wakati Mfalme Yehoshefati alikuwa hatarini, yeye pamoja na watu wake walimwomba Bwana msaada na Alijibu maombi yao. Tutatambua jinsi matumizi ya nidhamu tofauti za kiroho ilikuwa njia ya neema ambayo ilitia nguvu imani ya Mfalme Yehoshefati na watu wa Yuda wakati wa uadui.

### I. Wakati wa Majaribio (2 Mambo ya Nyakati 20:1-3)

Kamusi ya mtandao inaeleza "hofu" kama: *"hisia isiyopendeza inayosababishwa na imani kwamba mtu au kitu kiko katika hatari, hasa kinachoweza kusababisha uchungu, au tishio."* Kulikuwa na sababu asili ya hofu. Mstari wa 2 unasema kwamba jeshi kubwa lilikuwa linawajia kutoka Edomu. Walishangaa.

Suala ni kwamba hali fulani maishani ambazo zinaonekana kwetu kuwa hatari, ajali au tishio, kawaida tunatenda kwa hofu au wasiwasi. Yehoshafati hakuwa tofauti kwa haya. Watu wengi katika Biblia walihisi hivyo. Musa alihisi hofu walipovamiwa na Ogu, mfalme wa Bashani (Hesabu 21:33-34). Zakaria aliogopa wakati malaika alitangaza kwamba alikuwa anaenda kuwa baba katika umri wake wa uzee (Luka 1:12-13). Wanafunzi walipomwona Yesy akitembea juu ya maji, waliogopa (Mathayo 14:26).

Mfalme Yehoshafati alikuwa na tishio la kukabiliana nalo: Mataifa matatu yalikuwa yanamjia (2 Mambo ya Nyakati 20:1). Kama mfalme, Yehoshafati alijua jeshi lake halingeweza kushinda katika vita juu ya majeshi, na alihisi kuishiwa na nguvu kwa vile hangewapa watu wake jibu la kuridhisha kwa tishio kama hilo.

Hofu hutuvamia wakati wa majaribio na kutuonyesha kwamba hatuwezi kupata kila kitu kupitia kujitosheleza kwetu. Pia inatukumbusha kwamba ni lazima tutegemeane, na zaidi, tunahitaji kuweka tumaini letu kwa Mungu!

Hivi ndivyo Yehoshafati alifanya katika hali hii (mstari wa 3b). Hata kama hofu ilikuwa imevamia moyo wa Yehoshafati, alijua kwamba kulikuwa tu na njia moja ambayo ingeondoa hofu: alihitajika kumgeukia Mungu kwa moyo wake wote na kutafuta uongozi na ushauri Wake.

### II. Kutumia Imani (2 Mambo ya Nyakati 20:3-19)

#### A. Ibada (mstari wa 3, 6)

Ibada ni tendo la kutoa heshima na utukufu kwa Mungu. Uamuzi wa kwanza ambao Yehoshafati alifanya, baada ya kupokea habari za vita, ulikuwa kuabudu: *"…Yehoshafati aliamua kumtafuta Bwana…"* (mstari wa 3). Kamusi ya Beacon inafafanua "Ibada" kama *"mwitikio wa kibinadamu kwa asili ya uungu"* (ukurasa 32). Yehoshafati aliinua sifa za Mungu kama tendo la ibada (mstari wa 6).

#### B. Maombi (mstari wa 4a)

Katika maombi, tunaungana na Mungu kwa uangalifu, tukiwasiliana na yeye, au tukitafuta msaada wake wakati wa hitaji. Kwa kutumia nidhamu hii ya kiroho, Yehoshafati hakujizuia kuabudu na kutafuta ushauri wa Mungu, aliwaita pia watu wa Israeli pamoja kuomba

msaada wao (mstari wa 4a).

C. Sifa (mstari wa 7)

Sifa humtukuza Mungu kwa yale ametenda. Sehemu moja ya ibada ya Yehoshafati ilikuwa kutambua jinsi Mungu alikuwa ametenda kwa niaba yao katika historia (mstari wa 7).

D. Ushirika (mistari ya 9-13)

Tunaweza kuvutiwa tu tunaposoma katika kitabu cha Matendo ya Mitume kwamba wanafunzi wa kwanza: *"...walikuwa kitu kimoja"* (Matendo ya Mitume 2:44, 4:32). Ingawa walikuwa katika hali ngumu, wakiangazia mateso yaliyoanzishwa juu ya Wakristo, waliungana kwa amani (Matendo ya Mitume 2:1). Ushirika huu wa karibu ulipata heshima ya wale waliowaona (Matendo ya Mitume 2:47).

E. Neno la Mungu (mstari wa 15)

Moja ya nidhamu za kiroho au njia ya imani ambayo inatia nguvu imani yetu na kutupa tumaini ni kukimbilia ahadi za Mungu. Watu wa Israeli walipokea neno kutoka kwa Mungu lililowatia moyo na tumaini (mstari wa 15), Ushirika na Mungu hutusaidia kurekebisha mtazamo wetu. Yehoshafati alikumbuka kwamba maisha yake na ile ya watu hayakumtegemea yeye, au jeshi lake. Mungu mwenye Enzi alimwambia asiogope, lakini amtumaine. Mungu akasema: *"Nisikilizeni, enyi watu wa Yuda na wakazi wa Yerusalemu! Mwaminini Bwana Mungu wenu, nanyi mtakuwa imara; muwe na imani na manabii wake, nanyi mtafaulu."* (mstari wa 20).

### III. Tendo la Imani (2 Mambo ya Nyakati 20:20-22)

Watu wa Israeli walianza kutenda kwa imani: *"Kesho yake, wakaamka asubuhi na mapema, wakaenda mpaka katika jangwa la Tekoa. Walipokuwa wanaondoka, Yehoshafati alisimama, akawaambia, 'Nisikilizeni, enyi watu wa Yuda na wakati wa Yerusalemu! Mwaminini Bwana Mungu wenu, nanyi mtakuwa imara; muwe na imani na manabii wake, nanyi mtafaulu.'"* (mstari wa 20) Imani inahitaji tumaini kamili katika Mungu na utiifu wote kwake. Tunapotenda kwa imani, mtazamo wa hali ya maisha yetu unabadilika (mstari wa 21). Yehoshafati alikutana na majaribu kwa sifa. Imani yake ilitiwa nguvu wakati alijitoa kwa Mungu, akatafuta ushauri wake kwa maombi, pamoja na watu, akikumbuka matendo makubwa ya Mungu na tabia yake. Aliwakumbusha wastu kwamba Mungu ni wa rehema na atawaongoza. Hii ni IMANI.

### IV. Ushindi Wa Kiasili (2 Mambo ya Nyakati 20:23-25)

Yehoshafati hakuwa tofauti kwa viongozi ambao Mungu amechagua mbeleni. Alikuwa akiongoza jeshi lake ndogo juu ya falme tatu zilizoungana. Alifanya hivyo kwa sababu alitumaini katika ahadi ya Mungu: *"Hamtahitaji kupigana vita hivi. Nyinyi jipangeni tu halafu mngojee, na mtaona Bwana akiwashinda kwa niaba yenu. Enyi watu wa Yuda na Yerusalemu. Msiogope; wala msifadhaike. Nendeni vitani, naye Bwana atakuwa pamoja nanyi."* (2 Mambo ya Nyakati 20:17)

Muda ulipowadia wa kuchukua silaha na kushambulia, Yehoshafati alitoa agizo ambalo hatukufikiria kusikia katika dhana ya vita. Yehoshafati aliliambia kundi lake la Walawi waimbe (2 Mambo ya Nyakti 20:21). Ujasiri wa Yehoshafati kwa Mungu ulilipwa fidia kwa njia isiyo ya kawaida: *"Wakati walianza kuimba na kusifu, Bwana aliwavuruga akili wanajeshi wa Amoni, Moabu na Mlima Seiri waliokuja kupigana na Yuda, na wakashindwa."* (mstari wa 22)

Yehoshafati, kama Musa na Yoshua walitenda kwa imani, wakijua kwamba Mungu ni wa kweli Waisraeli wangeone tendo lisilo la kawaida la Mungu, ambaye aliwaahidi ushindi.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni nidhambu gani ya kiroho inayoangaziwa katika 2 Mambo ya Nyakati 20?
- Je, tunawezaje kuonyesha shukrani yetu na furaha kwa njia za ajabu ambazo Mungu anajionyesha na kutenda kwa niaba yetu?

## HITIMISHO


Nidhamu ya kiroho kama vile maombi, masomo ya Biblia, kufunga, miongoni mwa zingine ni muhimu kwa ukuaji wetu wa kiroho na ushindi. Mungu ametupa nidhamu hizi kama mazoezi ambayo tunaweza kupata nguvu ya imani yetu na kukutana mashambulizi ya maisha. Tusiache kuzifanya!

**<u>Somo la  37</u>:**

## IMANI INAJARIBIWA

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba nidhamu za kiroho ingawa inazo changamoto lakini ni muhimu
**Methali:** Mti hauanguki kwa kiharusi cha kwanza
**Kifungu cha kusoma:** 2 Mambo ya Nyakati 20
**Mstari wa Kumbukumbu:** "Maana sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu, wala hatujui tufanyeje; lakini macho yetu yatazama kwako." 2 Mambo ya Nyakati 20:12b
**Maswali ya kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Unapopatwa na changamoto, tulia, uliza na uombe kwa Imani!



| Somo la 38 | MABADILIKO YANAYOHITAJIKA |
| --- | --- |
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati 29:3-31:21 |

| Lengo | Memory Verse |
| --- | --- |
| Kuonyesha kile kinachoweza kutokea wakati Mungu anawafufua watu wake wakati wamerudi nyuma. | "…Nisikieni enyi Walawai! Jitakaseni na itakaseni nyumba ya Bwana, Mungu wa babu zenu. Toeni uchafu wote uliomo patakatifu." **2 Mambo ya Nyakati 29:5** |

## UTANGULIZI

Uamsho umekuwa wa kawaida katika hadithi ya watu wa Mungu. Katika Agano la Kale, tunaona watu baada ya muda walipotea njia kutka kwa Mungu na alimwita kiongozi awasaidie kutubu na kufanya upya ushirikiano wao na ushirika pamoja naye kwa utiifu. Hadithi hii juu ya Mfalme Hezekia inawakilisha moja ya wakati huu wa uamnsho.

### I. Mfalme Hezekia Alisimamishwa Tena Upya Ushirikiano na Mungu (2 Mambo ya Nyakati 29:2-36)

A. Je, Mfalme Hezekia Alikuwaje? (mistari ya 2-5)

Mstari wa 2 unasoma: *"Alitenda mema mbele ya Bwana, kama vile alivyofanya Daudi, babu yake."* Kwa sababu alikuwa mfalme mcha Mungu na mwenye haki, aliona nja ambazo watu walikuwa wakimuasi Mungu. Aliona ibada yao ya sanamu. Katika utawala wa babake Ahazi, milango ya hekalu ilikuwa imefungwa kuondoa hamu yoyote ya kurudi kwenye ibada ya Mungu (2 Mambo ya Nyakati 28:24, 29:7). Aliona kwamba milango ya hekalu ilikuwa imefungwa. Mstari wa 3 ulizema kwamba alifungua milango ya hekalu na kuirekebisha.

Mfalme Hezekia alitambua kwamba taifa walihitaji kunyenyekea mbele ya Mungu. Alikubali kwamba baadhi ya mambo babu zake walifanya yalikuwa mabaya, na kwa haraka akasema kwamba watu walihitaji kumrudia Mungu. Jambo la kwanza alilofanya lilikuwa kuwakusanya Walawi na makuhani na kuwaalika kutubu kwa mazoea haramu ya kidini na kujitakasa mbele ya Mungu.

B. Uchambuzi wa Mfalme Hezekia Wa Hali Hiyo (mistari ya 6-9)

Mistari ya 8-9 inaeleza wazi matokeo ya kumuasi Mungu. Dhambi huleta matokeo. *"Hasira ya Bwana"* ilianguka juu ya Yuda na Yerusalemu. Mataifa mengine yalikuwa yakiwacheka. Kwa sababu ya dhambi za mababu, wengi *"walianguka kwa upanga"* na baadhi ya wana na binti wao na wake walikuawa katika mateka.

Je, Mungu angesema nini juu ya makanisa yetu leo? Je, tuko waaminifu kama inavyotupasa? Na je, mafundisho ya uongo kama vile thiolojia ya utajiri, viongozi na wachungaji wanaoanguka katika uzinzi, hesabu ya kanisa la uongo, kutowajali maskini na wahitaji, n.k?

C. Suluhisho la Mfalme Hezekia (mistari ya 10-36)

Mistari hii inasimulia yale Makuhani na Walawi walihitajika kufanya ili kusafisha hekalu. Wachukue wanafunzi watengeneze orodha ya yale yaliyofanywa. Katika mstari wa 10, mfalme alisema kwamba atafanya upya agano la Mungu. Anawaonya wasipuuze na watekeleze kazi walizopewa katika sheria ya Musa. Walawi walisikia, wakatubu na kuanza kufanya kazi wakisafisha wakitoa ndani ya hekalu kila uchafu wa ibada ya sanamu. Walipokuwa wamemaliza, walikuwa na sherehe ya ajabu pamoja na dhabihu, muziki na ibada (mstari wa 29). *"Hivyo basi, huduma za ibada zikaanzishwa tena hekaluni. Hezekia na watu wote wakajawa na furaha tele kwa sababu ya yote Mungu aliyowatendea watu; mana tukio hili lilitokea ghafla."* (mistari ya 35b- 36)

### II. Mfalme Hezekia Asherekea Pasaka (2 Mambo ya Nyakati 30:1-20)

A. Sherehe Ya Kuwaunganisha Watu Wa Mungu mistari ya 1-6)

Sherehe ya Pasaka ingesherehekewa kila mwaka kukumbuka vile malaika wa kifo *'alipita'* katika nyumba

za Waisraeli kule Misri. Kusherehekea huku muhimu kulipitishwa kutoka kizazi hadi kingine. 2 Mambo ya Nyakati 30:5 inataja kwamba hawakusherehekea vizuri sherehe hii muhimu ya kidini kwa muda mrefu.

Mfalme Hezekia na Walawi wote waliotakaswa walihisi tamaa kubwa ya kumtii Mungu. Kwa vile walihitaji muda wa kujitayarisha kwa ajili ya Pasaka, walifanya mipango ya kuisherehekea katika mwezi wa pili wa mwaka, na wala si wa kwanza, kama vile Mungu alikuwa ameamuru (2 Mambo ya Nyakati 30:13).

Hili lilikuwa liwe tukio kubwa. Watumishi walitumwa kwa Israeli yote (ufalme wa kaskazini) na Yuda wakiwaalika watu kwa sherehe kuu. Katika mistari ya 5 hadi 9, tunaweza kusoma barua ambayo mfalme alituma kwa Falme zote. Waambie wanafunzi wako waichambue.

B. Mwito wa Kutubu (mistari ya 7-20)
Sura iliyobaki inaeleza sherehe ya Pasaka ya ajabu ambapo wanakondoo wengi waliteketezwa na kulikuwa na kufurahia kwa wingi. Sura inakamilika na ombi la Hezekia na baraka ya mwisho ya Bwana. *"Bwana uliye mwema, msamehe yeyote yule atakayekuomba wa moyo wake wote wewe Bwana Mungu, Mungu wa babu zake, hata ingawa si msafi kulingana na sheria za utakaso. Bwana alikubali ombi la Hezekia, akawasamehe watu hao."* (mistari ya 18b-20)

**III. Je, toba inalo jukumu gani katika ushirika wetu na Mungu? Mfalme Hezekia Alianzisha Tena Huduma ya Kikuhani (2 Mambo ya Nyakati 31:1-21)**

A. Maangamizo ya Ibada ya Sanamu (mistari ya 1-2)
Kama matokeo ya kukutana na Mungu, watu walizunguka katika falme zote mbili wakiangamiza mambo ya kipagani ya ibada ya sanamu.

Hezekia aliwapanga makuhani katika vikundi kubadilishana kwenye ibada ndani ya Hekalu. Mfalme Hezekia alirudisha sehemu ya ibada, na makuhani na Walawi walianza kuona tena maana ya maisha na kazi ambayo waliachiwa (2 Mambo ya Nyakati 31:2).

Hezekia alitambua kwamba watu walikuwa mbali na Mungu. Alitambua pia kwamba yeye peke yake ndiye angebadilisha hali. Ilikuwa muhimu sana kuwatia changamoto Walawi watubu na kumrudia Mungu, kwa sababu kwa timu ya watu watakatifu, mfalme alikuwa anaenda kupata mengi.

B. Urejesho wa Zaka (mistari ya 3-21)
Timu yake ya wasaidizi ilihitaji msaada wa kifedha. Washiriki wa kabila la Lawi, tangu kuingia katika Nchi ya Ahadi, hawakuwa na nchi ambayo ya kupanda chakula na kuhifadhi wanyama. Makabila mengine kumi na moja walikuwa walete asimilia 10% ya mazao yao kwenye ghala kwa matumizi ya Walawi. Lakini ilionekana kwamba kwa muda mrefu, mambo hayakuwa hivi, kwa hivyo watu waliotengwa na Mungu kutumika ndani ya Hekalu walikuwa wamepuuza majukumu yao ya kidini ya kusaidia matakwa ya uchumu wao.

Watu waliokuwa wametubu na kubarikiwa na Bwana walikuwa wakarimu katika kuleta zaka zao. Kwa kweli, walikuwa wakarimu sana hata kulikuwa na lundo la bidhaa tofauti. Katika mstari wa 10 tunasoma kuwa Kuhani mkuu alimwambia mfalme kwamba: *"Tangu watu waanze kuleta matoleo yao ya hekaluni, tumekuwa na vyakula vya kutosha na hata tunayo akiba kubwa kwa sababu Bwana amewabariki watu wake, ndiyo maana tumepata vitu hivi vyote."* Familia zote za Walawi zililinswa na hivyo wangehudumu ndani ya Hekalu.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni jambo gani la kwanza Mfalme Hezekia alifanya ili kurudisha huduma hekalu? Kwa nini?
- Je, walikuwa wanakumbuka wakati wa Pasaka?
- Je, Hezekia alitayarishia timu yake ya Walawi?

## HITIMISHO

Wakati watu wa Mungu katika AGano la Kale na hata leo wanaanguka katika dhambi, wanamsahau, na kwenda mbali na njia zake, Mungu humchagua mtu wa kuongoza uamsho. Kila uamsho uanzi na hisia wazi ya dhambi, ikielekeza kwa toba na baraka. Hii ndio ilitendeka katika utawala wa mfalme huyu mwema. Aliwafundisha pia na kuwapa Walawi ili wawe vile aliwaita wawe – viongozi wa watu kuelekea utakatifu!

**Somo la** 38:

## BADILIKO MUHIMU

**Lengo la Somo:** Kuonyesha yanayotendeka watu wa Mungu wakitubu dhambi zao, kumrejea na kumheshimu Mungu

**Methali:** Usitazame mahali ulianguka bali tazama ni wapi uliteleza

**Kifungu cha Kusoma:** 2 Mambo ya Nyakati 29-31

**Mstari wa kumbukumbu:** "Mungu wenu ndiye mwenye neem na mwenye rehema, wala hatawageuzia bali uso wake mkimrudia" 2 Mambo ya Nyakati 30:9

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii?

**Himizo la somo:**



| Somo la 39 | FANYA YALIYO MEMA KILA WAKATI |
|---|---|
| | **Maandiko:** 2 Mambo ya Nyakati 33–35:19 |

| Lengo |
|---|
| Kujifunza kwamba Mungu ni wa neema na msamaha lakini anataka kila wakati tutende yaliyo mema. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Alitenda mema mbele ya Bwana na alifuata njia zake Daudi babu yake, na kushika amri za Bwana kwa dhati." **2 Mambo ya Nyakati 34:2** |

## UTANGULIZI

Wale wanaochukua nafasi ya uongozi, katika njia moja au nyingine, wataacha alama ya maisha yao. Kwa maneno mengine, mtindo wa maisha yao utaathiri vizuri au vibaya maisha ya watu wao ya sasa na baadaye. Watakumbukwa labada kama viongozi wazuri au wabaya. Katika darasa hili tutazungmza juu ya aina tatu za viongozi ambao waliacha alama ya historia kwa watu wa Bwana. Tunaweza kujifunza kutoka kwa mafanikio au kuanguka kwao, na tutatiwa changamoto kukumbukwa kwa maneno ya ajabu na yasiyoweza kusahaulika: *"Alitenda mema mbele za Bwana, bila kugeuka upande wa kulia au kushoto."*

### I. Mfalme Manase Alianza Vibaya na Kumaliza Vizuri (2 Mambo ya Nyakati 33:1-20)

Mambo ya Nyakati inatoa mistari 20 kwa Mfalme Manase. Yerusalemu miaka 55. Alikuwa na miaka 12 alipoanza kutawala (mstari wa 1). Katika mstari wa 2, inasema: *"Alitenda maovu mbele ya Bwana, kwa kuiga mienendo miovu ya mataifa ambayo Bwana aliyafukuza wakati watu wake wa Israeli walipokuwa wanaingia nchini."* Hata hivyo, mstari wa 13 unasema: *"Alimsihi Bwana, naye Bwana akapokea ombi lake na sala yake akamrudisha Yerusalemu katika ufalme wake. Ndipo Manase akatambua kuwa Bwana ndiye Mungu."*

#### A. Alifanya Sanamu Za Wapagani na Kuziabudu (mstari wa 3-7)

Mfalme Manase alimjengea Baali madhabahu na kutengeneza sanamu za Maashera na kuziabudu. Aliabudu nyota, akiitengenezea madhabahu ndani ya Hekalu. Pia alimtengenezea Ashera fungu la tambiko, na maana ya ngono, na kuliweka katika Hekalu. Hii ilikuwa chukizo kwa Mungu. Alishauriana na wachawi na hata akatoa dhabihu ya watoto wake wa kiume kwa moto. Kwa hivyo, mfalme huyu alikuwa mtaalam wa nyota wa kipagani na mazoea ya uchawi ambao walitafuta ishara, walipewa uganga, wakashauriana na watabiri na watangazaji.

#### B. Habari Njema Juu ya Mfalme Manase

Hakika katika utawala wake, Mfalme Manase alichukuliwa mateka Babeli. Katika seli nyeusi ya gereza baridi, mfalme huyu mwovu alimkumbuka Mungu na kutubu. Alimaliza utawala wake kama mfalme aliyetubu, lakini utawala wake ulimsababishia maangamizo mengi kwa taifa.

1. Alimwomba Mungu, Kwa Unyenyekevu Mkubwa (mstari wa12)
2. Alipanga na Kulinda Mji (mstari wa 14)
3. Aliondoa miungu na Kutengeneza Upya Madhabahu (mstari wa 15-16)

### II. Mfalme Amoni: Mfalme Mbaya (2 Mambo ya Nyakati 33:21-25)

Mfalme ambaye alianza vibaya na kumaliza vibaya alikuwa Mfalme Amoni. Biblia inatoa mistari mitano ya mfalme huyu. Alitawala Yerusalemu kwa miaka miwili. Ni muhimu kuwarejelea ili tusianguke katika makosa kama hayo. Biblia inaeleza kwamba Amoni alizidisha dhambi ambayo babake Mfalme Manase alitenda katika mwanzo wa utawala wake (mstari wa 23). Hakufayata mfano wa babake baada ya kunyenyekea mbele ya Mungu na kuacha dhambi. Amoni alikuwa na mwisho mbaya; aliuawa mahakamani (mstara wa 24). Mfalme Amoni alianza vibaya na kumaliza vibaya. Hii inatufundisha kwamba tukiishi

vibaya na kukosa kubadilika, hatatukumbukwa kamwe; au tutakuwa mfano mbaya.

### III. Mfalme Yosia Mfalme Mzuri wa Kweli (2 Mambo ya Nyakati 34-35:27)

*"Alitenda mema mbele ya Bwana na kufuata njia za babake Daudi; bila kugeuka upande wa kulia au kushoto."* Kisha alipokufa, tunasoma: *"Yeremia alitunga shairi la maombolezo kwa ajili ya kifo chake, na hadi leo waimbaji wote waume kwa wake humtaja Yosia katika maombolezo yao."* (2 Mambo ya Nyakati 35:25) Acha tuone alichopata katika maisha yake.

A. Alisafisha Nchi Kutokana na Sanamu Zote Za Ibada (2 Mambo ya Nyakati 34:3-7)

Yosia alianza kumtafuta Mungu kama vile Mfalme Daudi alifanya wakati wake. Aliondoa maeneo yote ya kipagani na sanamu za Ashera. Aliangamiza madhabahu yote ya Baali. Alivunja sanamu za jua. Alirarua na kusugua sanamu zote kuwa vumbi. Alichoma mifupa ya makuhani wa ibada ya sanamu. Katika hali hii, hakusafishia tu Yuda, lakini pia nchi za kabila lingine kama vile Manase, Efrahimu, Simeoni, na Naphtali. Haya yote yanaonyesha kwamba Yosia alitenda yaliyo memba mbele za Bwana. Mungu ana wivu na atawabariki wale wote wanaomwabudu.

B. Alitengeneza Upya Nyumba ya Bwana (2 Mambo ya Nyakati 34:8-17)

Yosia alifanya mchango mkubwa wa kutengeneza upya Hekalu. Mafundi seremala na waashi wa mawe na waliojitolea wengine wengi walifanya kazi kwa bidii hadi kazi hiyo ilipomalizika. Hii lazima iwe ilimpendeza Mungu na watu. Tunapaswa kuweka talanta zetu na vipawa kuwepo ili Kanisa la Mungu wetu mzuri litamaniwe na kuheshimiwa kama inavyostahili.

C. Alitawala na Kuhakikisha Kwamba Kila Mtu Anatii Neno la Mungu (2 Mambo ya Nyakati 34:18-33)

Mfalme Yosia alishangazwa na kusomwa kwa kitabu cha sheria ambacho Hilkia alipata (mistari ya 18-27). Alipokuwa anasikiliza Neno la Mungu lililoandikwa, Yosia alivutiwa sana moyoni mwake. Mfalme Yosia hakusikiliza tu na kuvutiwa na kulitii Neno la Mungu, bali alitoa amri kwamba watu wake wote watii Neno la Mungu (mstari wa 33). Hiyo ndio nafasi ya kiongozi anayetenda mema mbele ya Mungu. Alipokuwa mfalme, alijitahidi kadiri ya uwezo wake kuwaweka watu karibu na Mungu, akiwasaidia wasirudi tena kwenye ibada ya sanamu.

D. Alisherehekea Pasaka (2 Mambo ya Nyakati 35:1-19)

Inavyoonekana, kwa muda mrefu walikuwa wameacha kusherehekea sikukuu hii ya kila mwaka. Mfalme Yosia alihakikisha kwamba watu wote walihusika na maelezo yote yanayowahusu. Ulikuwa wakati wa kweli wa kusherehekea Mungu aliyekomboa na Mungu aliyetimiza ahadi. Mfalme aliwahimiza, aliwaamuru na kuwatia moyo makuhani na Walawi kutimiza ofisi yao vizuri:

i). Aliwakumbusha juu ya huduma ambayo walikuwa wamepewa na Musa (mstari wa 6), Daudi na Sulemani (mstari wa 4).

ii). Aliamuru Sanduku la Agano kuwekwa mahali pake (mstari wa 3).

iii). Aliagiza Walawi wamtumikie Bwana Mungu wao na watu wake (mstari wa 3);

iv). Aliwaagiza watu kuwa watakatifu na kuwafundisha washirika wa familia (mstari wa 6).

v). Aliwatia moyo Walawi katika huduma ya Hekalu la Bwana (mstari wa 2).

Makuhani na Walawi kwa uaminifu walitimiza huduma zao (mstari wa 10), na pia walimheshimu Mungu walipohusika kwenye Pasaka (mstari wa 14).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, mafunzo ambayo tunaweza kujifunza kwa Mfalme Manase?
- Je, ni nini kilitengeka wakati Mfalme Yosia alisoma kitabu cha sheria?
- Je, ni katika njia gani ambayo alimpendeza Mungu?

## HITIMISHO


Tunapaswa kukumbukwa kama wanaume na wanawake walioanza vyema na kumaliza vyema. Mfalme Manase anatufundisha kwamba Mungu ni mwingi wa neema na atawasamehe wale wanaomtafuta kwa unyenyekevu hata kama wamekuwa wabaya. Mfalme Amoni alikuwa mbaya, lakini mwanawe Mfalme Yosia alikuwa mmoja wa wafalme bora waliowarudisha watu kwa Mungu. Tangia umri mdogo, aliamua kila wakati kutenda mema mbele ya Mungu.

**Somo la** 39:

## FANYA YALIYO MEMA KILA WAKATI

**Lengo la Somo:** Kujifunaza kwamba Mungu ni wa neema na anasemehe, ila anataka sisi kutenda mema kila wakati.
**Methali:** Mahali utaishi ukiwa na umri wa kimo, panadhihirisha na mahali ulikuwa katika ujana.
**Kifungu cha Kusoma:** 2 Mambo ya Nyakati 33-34
**Mstari wa kumbukumbu:** "Akafanya yaliyo mema machoni pa Bwana, akaziendea njia za Daudi babaye, asigeuke kwa kuume wala Kushoto" 2 Mambo ya Nyakati 34:2
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hadithi wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Kufuata muongozo wa Mungu utuhakikishia mwisho mwema.



| Somo la 40 | IMANI NA KUJITOLEA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 1:1-7 |

| Lengo |
|---|
| Kutambua na kutumia imani na kujitoa katika maisha yetu ya kila siku. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Mungu aliwajalia vijana hao wanne maarifa na ujuzi katika elimu na hekima. Zaidi ya hayo, alimjalia Danieli kipawa cha kutafsiri maono na ndoto." **Danieli 1:17** |

## UTANGULIZI

Danieli ni kitabu cha kipekee katika Agano la Kale kinachochukuliwa kuwa sehemu ya fasihi ya maarifa ya Kiyahudi. Aina hii ya fasihi ilionekana wakati wa shida kali inayoonekana. Inafurahisha kutambua kuwa Wakristo wanaweka kitabu cha Daniel karibu na manabii wakuu. Pengine, hii ni kwa sababu Danieli alikuwa mtawala ambaye Mungu alitumia kama mnabii, hata kama cheo chake hakikuwa cha unabii.

Katika kifungu hiki tunachosoma leo, tunaona kwamba hata kama watu wa Kiyahudi waliadhibiwa kwa uasi wao wa mara kwa mara kwa Mungu, na idadi kubwa ya wakaazi wa Yerusalemu ilichukuliwa mateka huko Babiloni, Mungu hakuwaacha. Danieli na vijana wenzake katika hadithi hii ni mfano wa haya. Hapa kuna mwanzo wa hadithi ya kusimulia ya imani na kujitoa. Danieli na marafiki wake watatu walichaguliwa kwa kazi ya juu kwa sababu ya uaminifu wao kwa Mungu na kanuni ambazo walikuwa wamefundishwa katika Israeli.

### I. Je, Ni Nini Kilikuwa Kinatendeka Wakati Danieli na Marafiki Wake Waliishi? (Danieli 1:1-4)

Babiloni ilikuwa iko Mesopotamia (ambayo sasa ni Iraq), kwenye ukingo wa mashariki ya Mto Yufreti. Mji huu ulikuwa mji tajiri na mji mkuu wa ustaarabu ambao ulichangia kuundwa kwa unajimu, maendeleo ya dawa, ilianzisha sayansi ya lugha, iliandaa nambari za kwanza za kisheria, na kufundisha misingi wa hisabati ya Kigiriki, fizikia na falsafa. Vile vile, Mesopotamia ilipitisha mafundisho haya kwa Wayahudi, ambao nao pia waliwafundisha Waarabu. Mfano wa hii ni maarifa ya sayansi na usanifu.

Miaka hiyo ilikuwa wakati mgumu sana kwa ufalme wa Yuda. Walipitishwa kutoka kwa mshindi mmoja kwenda kwa mwingine, na ingawa manabii waliomtumikia Mungu wakati huo waliwaonya wakuu juu ya matokeo ya kumuasi Mungu, wale waliohusika watu hawakujali. Wakati wa utawala wa Yehoyakimu, nabii wa Mungu Yeremia alimshauri mfalme (Yeremia 25:1-11). Wakati Yehoyakimu alikuwa ametawala kwa miaka mitatu, katika mwaka wa 605 Kabla Kristo, Nebukadneza aliwashinda Wamisri katika Karkemishi (Yeremia 46:2), na kushinda sehemu kubwa ya Mashariki ya Karibu, ambayo ilikuwa ni pamoja na ufalme wa Yuda.

Wakati Yuda alishinda, idadi kubwa ya watu ilichukuliwa mateka huko Babiloni. Katika kundi kulikuwa na Danieli na marafiki wake. Walibaki mateka kwa utawala wote wa Nebukadneza, na miaka mitatu ya kwanza ya utawala wa Koreshi, wa Persia. Babiloni ilishindwa na Waperezi katika mwaka 539 Kabla Kristo.

### II. Je, Watu Waliamini Katika Sehemu Ile ya Ulimwengu? (Danieli 1:5-7)

Kila mvamizi alileta miungu yao na kujaribu kulazimisha ibada ya miungu hiyo. Kwa sababu ya mafanikio yake ya kijeshi, Nebukadneza aliona miungu wake kuwa yenye nguvu zaidi kuliko wengine wote. Kwa hivyo, idadi ya watu wa ufalme wa Yuda ilikuwa ililazimishwa rasmi kuabudu miungu ingine na kumwacha Bwana. Kwa hivyo kuwa mwaminifu kwa Mungu halikuwa jambo rahisi siku hizo, hasa wakati viongozi wa Kiyahudi walikuwa mfano wa Wayahudi wa ukafiri kwa Bwana. Kwa habari ya manabii, kumtumikia Mungu na kumwasilisha mbele ya watu halikuwa jambo rahisi. Kitabu cha Yeremia kinaelezea waziwazi shida ambazo Yeremia alipata.

Wababeli hawakuhusika sana katika sherehe za kirasmi, isipokuwa sherehe za mungu wa kike Ishta, mmoja wa miungu kuu ya ufalme, pamoja na Bel, aliyeitwa Merodak na Waebrania, also identified as Marduk,

mungu wa jua na mkuu wa uungu wa Wababeli. Sherehe za Ishta zilikuwa za kupendeza, pamoja na furaha, na ibada katika hekalu ikiwa ni pamoja na ukahaba takatifu. Sambamba na yaliyo hapo juu, dini maarufu ilikuwa na wingi wa miungu ya kibinafsi na ya familia; hadithi za uwongo ambazo ziliundwa kwa mdomo kwa muda. Vivyo hivyo, watu walitumia hirizi, vichaka na mila kusuluhisha hali tofauti za hali na magonjwa. Watu walihusika. Watu walishiriki kikamilifu katika sherehe hizi za kidini.

Mabadiliko ya majina tunayopata katika Danieli 1:7 yana maudhui ya kidini yenye nguvu, na yanathibitishwa tunapochunguza maana ya majina hayo. Kumbuka kwamba kwa Wayahudi, pia, majina yalikuwa muhimu na yalikuwa na maana ambayo mwenye jina aliibeba kwa uzito. Kwa maoni ya wanahistoria wengine, mabadiliko ya jina, ya mhusika wa utumishi wa jumba la kifalme, ilimaanisha kwamba vijana wangekuwa chini ya mamlaka mpya ya kiroho kuanzia wakati huo na kuendelea.

Nebukadneza, kulingana na historia ya kibiblia, alitumia wahenga wengi, watabiri na wachawi ambao aliwaendea alipowahitaji. Wakaldayo, waliotajwa katika kitabu cha Danieli, walikuwa wanasayansi wa wakati huo na walikuwa na uwezo wa kutafsiri aina zote za ndoto. Maarifa haya yalipatikana kupitia mafundisho, na mfalme alieleza kwamba mateka waliochaguliwa walipaswa kusoma kwa miaka mitatu ili kuweza kutumika katika jumba la kifalme (Danieli 1:4-5).

### Je, Tunaweza Kujifunza Nini Kutoka Kwa Hadithi Hii?

Tayari tumeona kufanana kati ya hali ya uhasama wa kimataifa ya wakati wa Danieli na mazingira ya dunia leo. Tunaweza pia kuona kufanana kati ya dhana ya kidini ya Wababeli na wingi wa dini za sasa. Tunaishi katika ulimwengu ambao umesumbuliwa na mizozo. Maneno mengine yanajitahidi kwa sababu wanataka uhuru wao. Katika mfumo wa uchumi wa ulimwengu, kuna ukosefu wa usawa mwingi na udhalimu ambapo idadi ngodo ya idadi ya watu ulimwenguni ina utajiri mwingi.

Kwa habari ya dini, ulimwengu wa magharibi umejaa chaguzi nyingi. Hata ndani ya ulimwengu wa Kikristo kuna mengi ya Ukristo bandia, ambapo wafuasi hawakubaliani na mafundisho ya Neno, hata kama wanatangaza kuwa kama Wakristo.

Baada ya kuona hali hii, tunatambua kwamba hadithi ya Danieli na marafiki wake inatufundisha umuhimu kabisa. Katika nafasi ya kwanza, Danieli na marafiki wake walikuwa wazi katika mawazo yao kwamba kando na uadui wa hali, Mungu alikuwa kwenye enzi Yake na kwa hivyo, walithibitisha uaminifu wake wa kibinafsi. Hukumu yao haikutokana na mazingira au walitarajia Mungu kuwabariki na ustawi wa mali. Neno kuu lilikuwa 'kujitoa" kwa Mungu ambaye wamempa maisha yao. Kumfuata Mungu ilikuwa wazi kipaumbele chao kwanza.

Danieli na marafiki wake waliamua kutii kanuni na matendo waliyokuwa wamefundishwa kule Yuda. Walitaka kumtii Mungu hata kwa vitendo kama mlo na kuhifadhi kitambulisho chao kama Wayahudi, ambapo wakati huo wawe wananchi wazuri, waaminifu katika mambo yote ya maisha.

Maamuzi yaliyofanywa na watu yanatufundisha kwamba katika njia moja au nyingine, ni vizuri kuangalia uchaguzi wa maisha yetu. Baadaye kidogo habari ya Danieli (Danieli 3:17-18), marafiki wake watatu, kwa ujasiri na unyenyekevu wakati huo, walisimama imara katika kujitoa walikojitoa mbele ya Mungu. Walikuwa wameamua kumheshimu Mungu kwa gharama yoyote. Walifanya maauzi hatari na hata ya kishujaa. Sisi pia, siku kwa siku, tunahitaji kufanya uchaguzi mzuri ambao utampendeza Mungu.

## MASWALI YA ZIADA

- Unganisha maneno yafutayo na maana yao yanayofaa.
  - ◊ Danieli - Bwana ni msaada wangu
  - ◊ Hanania - Mungu ni hakimu wangu
  - ◊ Mishaeli - Bwana amekuwa wa neema
  - ◊ Azaria - Mtu anayetoka kwa Mungu
- Je, tunawezaje kuwaiga vijana hawa katika maisha yetu ya kila siku?
- Je, umejifunza nini kutoka kwa masomo ambayo unaweza kutumia kwa maisha yako wiki hii?

## HITIMISHO


Tunahitaji kuhakikisha kwamba tumeweka tumaini letu kwa Mungu na kutumia mafundisho yake kila siku ya maisha yetu.

**Somo la** 40:

**IMANI NA KUJITOLEA**

**Lengo la Somo:** Matumizi ya Imani na kujitolea katika maisha ya yetu ya kila siku.
**Methali:** "Mvumilivu hula mbivu."
**Kifungu cha Kusoma:** Daniel 1:1-8
**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 1:7 – "Mkuu wa Matowashi akawapa majina: alimwita Danieli Belteshaza; na Hanania akamwita Shadraka; na Mishaeli akamwita Meshaki; na Azaria akamwita Abednego."
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** "Tunahitaji kuishi katika imani yetu hata kama wengine watabadilisha majina yetu"



| Somo la 41 | KUMTII MUNGU KULIKO KUMTII MWANADAMU |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 1:8-20 |

| Lengo |
|---|
| Kudumu katika imani zetu za Kikristo hali yoyote, tukikumbuka kwamba Mungu huwaheshimu wale wanaomheshimu. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Bwana atawapigania; nyinyi mnachotakiwa kufanya ni kutulia tu." **Kutoka 14:14** |

## UTANGULIZI

Mahali tunafanya kazi, au katika hali ya kijamii, shuleni, chuoni, hata katika mazingira ya familia, katika hafla fulani tunaweza kuwasilishwa na hali zinazopingana moja kwa moja na kanuni ambao Mungu anapeana kama sheria ya kanuni ya mwenendo kwa maisha ya wana na binti zake. Kwa hivyo, ni jukumu letu kuwa waangalifu katika hizo hali zote zinazotusababisha, sisi kama waumini katika Kristo, kutoa ushuhuda mbaya kwa neema ya Mungu, na hata kugeuka kutoka kwa imani yetu.

### I. Danieli Na Marafiki Wake Hawatiwa Unajisi (Danieli 1:8)

Kujiweka katika dhana ya somo la leo, tukumbuke kwamba Danieli alichaguliwa, pamoja na wenzake watatu (Hanani, Mishaeli na Azaria), kukaa katika ua wa Nebukdneza, ambapo alipata kibali nao katika njia kama ile ya Yusufu kule Misri.

Kama washirika wa ua la Mfalme Nebukadneza, Danieli na wenzake walikuwa na haki ya kushiriki chakula cha mfalme, vile vile vinywaji husika na vitoweo vyote vilivyojumuishwa kwenye menyu (Danieli 1:5). Kwa kuchambua nafasi zilitajwa hapo juu, tunastahili kuthibitisha kuwa kilikuwa chakula cha ua ambacho mfalme alikuwa anawapa. Hali hii ilileta shida kwa Danieli na wenzake kwa sababu walikuwa vijana wanne wa Kiyahudi ambao walikuwa na imani kali na walikuwa wameyatoa maisha yao kumtumikia Bwana katika hali yoyote aliwaweka ndani. Shida yao ilikuwa kama ifuatavyofuata: Kukubali nafasi ya kuhusika katika chakula cha mfalme kungechafua maisha yao, lakini kubaki waaminifu kwa Mungu wao na kukataa nafasi hiyo ingeleta kutokubaliwa kwao kwa kifalme, na hiyo ingekuwa hatari.

Kufuata sheria ya Bwana katika mawazo na moyo wake, Danieli alionyesha kusadikika kwake kwa uaminifu kwa Mungu mmoja wa kweli: *"...Danieli aliamua kutojitia unajisi kwa chakula cha kifalme na divai""* (Danieli 1:8). Lazima tuangazie hapa dhamira ya Danieli ya kubaki mwaminifu kwa imani yake katika hali ambayo hakusita kukataa pendeleo alilopewa au katika kuasi amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mfalme Nebukadneza. Zaidi, uamui ambao alikuwa ameufanya; kwa hivyo *"alimwomba towashi mkuu amruhusu asile vitu hivyo na kujitia unajizi."* (mstari wa 8)

Akikabiliwa na hali hii, Danieli na wenzake walikubali kujitolea huko kwa kupitia mtihani usiolingana wa kutojitia unajisi na chakula cha kifalme, wakiweza kuchagua chakula chao wenyewe (mboga na maji). Baada ya siku kumi, walionekana bora zaidi kama wale vijana waliokula chakula kama kile cha mfalme. Kwa kuwa hakukuwa na tofauti mbaya, waliruhusiwa kula chakula kilochoonekana bora kwao (Danieli 1:13).

Kama wana na binti wa Mungu, tunahitaji kusimama imara katika dhamira yetu na kuamua kabisa vile tutatenda katika hali fulani ambayo imani yetu kwa Mungu inajaribiwa au kachanganywa. Bwana wetu Yesu Kristo alituambia katika Mathayo 5:37 ambapo tunasoma: *"Unachohitaji kusema ni 'Ndiyo' au 'La'; chochote zaidi ya hayo hutoka kwa yume mwovu."*

### II. Mungu Alizawadi Uadilifu Wa Vijana (Danieli 1:14-20)

Danieli na wenzake walionyesha kujitoa na uaminifu wao kwa Mungu, wakati huo huo walionyesha hiari yao ya kufuata masharti ya wale waliokuwa juu yao. Wakati ambapo ni ukweli kwamba vijana hawa wa Kiyahudi waliamua kukataa chakula cha Mfalme Nebukadneza, walichukua ahadi kwamba hii haingepunguza uwezo wao wa mwili au kuwazuia kutimiza majukumu waliyopewa. Hivyo, waliendelea kusoma sayansi, lugha

na mambo mengine mengi (Danieli 1:4).

A. Mwonekano wa Kimwili (mstari wa 15)

Nyuso zao zilionekana bora zaidi na walikuwa hodari kuliko watu wengine wote waliokula chakula cha mfalme. Hii inatufundisha kwamba hata katika onyesho la kwanza tunalowapa watu, uwepo wa Mungu kwa watoto wake unaonekana.

B. Maarifa na Akili (mstari wa 17)

Mungu ndiye aliyewapa maarifa na akili vijana hawa, lakini si hivyo tu, walipokea pia uwezo wa kutafsiri ndogo na kuchangia sayansi ya ufalme wa Nebukadneza. Danieli pia alipokea ufahamu wa kutafsiri ndoto na maono; akithibitisha katika njia hii kile Maneno yanasema: *"Kumcha Bwana ndicho chanzo cha hekima, na maarifa ya Mtakatifu ni ufahamu."* (Mithali 9:10)

C. Kutambuliwa Kwa Mfalme (mstari wa 19)

Baada ya muda uliokuwa umekubaliwa kuonyesha kwamba kujitenga na chakula cha mfalme hakukuwa kunaenda kuwaadhiri katika njia yoyote, mkuu wa matowashi waliwapeleka vijana wanne mbele ya Nebukadneza kwa thibitisho lake. Matokeo yalikuwa kwamba mfalme, baada ya kusema nao, aliamua kwamba kati ya vijana katika ua lake hapakuwa na yeyote kama na wenzake. Nebukadneza alikamilisha haya baada ya kuwachunguza kwa mambo kadhaa ambayo hekima na akili zilihitajika. Walithibitika kuwa wa hali ya juu zaidi kuliko wagagna na wachawi waliokuweko katika ufalme wote.

III. Je, Mungu alizawadije uaminifu wa vijana hawa Wayahudi? Changamoto kama hizo leo

Suala nitakaloshiriki ambalo linafuata ni ushuhuda wa kweli wa Mkristo, ambaye kwa sababu zinazopita ufahamu wake, aliingizwa katika hali fulani na shida kama ile iliyowapata Danieli na rafiki zake watatu katika ua la Mfalme Nebukadneza.

Mahali ambapo Steven (jina bandia), anafanya kazi nafasi ya kupandishwa cheo cha kazi ilitangazwa ili waajiriwa waliotimiza mahitaji yaliyotajwa wangepandishwa kwa kazi ya juu, na kwa hivyo, wangepata ongezeko la mshahara. Wakati Steven aliwasilisha faili yake na nyaraka zinazohitajika, alijulishwa kwamba alihitaji uthibitisho wa semina ya mafunzo ambayo hakuhudhuria. Lakini mmoja wa wafanyikazi alimwambia kwamba hilo halikuwa tatizo, kwa vile stakabadhi hii ingepatikana, ingawa hakuhudhuria semina, kwa kiasi kidogo cha pesa. Kwa kukabiliwa na hali hii, Steven aliamua kwamba hatahusika katika kuinuliwa kwa kazi na atasubiri hadi kikao kingine ambacho atakuwa na stakabadhi zote kwa njia halali na ya uaminifu, akipeana ushuhuda kwamba watoto wa Mungu hutumainia jina la Bwana (Zaburi 20:7, 1 Mambo ya Nyakati 16:29).

Tuishi katika hali ambapo hatuigi mitindo ya dunia, bali sisi wenyewe tunabadilishwa kupitia kufanywa upya kwa mawazo yetu, ili tuthibitishe mapenzi mema ya Mungu yanayopendeza na masafi (Warumi 12:2). Tunapaswa kutumaini katika ahadi aliyofanya nasi katika Neno lake: *"...Msiogope! Kaeni Imara nanyi mtaona ukombozi Bwana atawaletea leo... mnachotakiwa ni kutulia tu."* (Kutoka 14:13-14)

## MASWAL YA ZIADA

- Je, ni aina gani ya vyakula ambavyo Danieli na rafiki zake waliitisha na kwa nini?
- Je, uadilifu ni nini?
- Wakati tunapitia hali ngumu katika maisha yetu, je, ni njia gani ambazo tunaweza kushuhudia uaminifu wa Mungu? Je, unaweza kuonyesha kwa njia gani tumaini lako kwake?

## HITIMISHO

Ni lazima kila wakati tuweke katika mawazo na mioyo yetu kwamba Mungu wetu ni Mungu mwenye nguvu zote, Muumba mbingu nan chi, ambaye hakuna jambo linalomshinda. Kwa hivyo, ni lazima tumtumaini Yeye pamoja na Neno Lake. Kwa mawazo na mioyo iliyobadilika, badala ya kuiga ulimwengu na vipimo vyake, matendo na itikadi, kwa mioyo ya shukrani, tuonyeshe kwamba Yesu Kristo anatawala ndani yetu.

## Somo la 41:

## KUMTII MUNGU KULIKO KUMTII MWANADAMU

**Lengo la Somo:** Kuendelea katika Kusadiki kwetu kwa Kikristo katika hali zote.


**Methali:** "Elimu ni Bahari/Hekima haijengeki kwa usiku mmoja."

**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 1:8-20

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 1:8 "Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa kwa sababu hiyo ingekuwa kinyume na sheria za Kiyahudi na kujitia unajisi. Kwa hivyo alimwomba Ashpenazi amruhusu asijitie unajisi kwa njia hii."

**Maswali ya Kujadili:**
Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** "Mungu hutusaidia kuendelea katika kumtii kwa hali zote."



| Somo la 42 | NDOTO YA MFALME NEBUKADNEZA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 2:1-48 |

| Lengo |
|---|
| Kuelewa kwamba Mungu mara nyingi hutafuta watu wanaomjua ili aonyeshe mapenzi Yake ulimwenguni. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "…Yuko Mungu mbinguni ambaye hufumbua mafumbo."" **Danieli 2:28** |

## UTANGULIZI

Kuonta ni sehemu ya maisha ya mwanadamu na, labda kwa sababu hii, tunavitaja vitu vingi kuwa ndoto. Kwa mfano, tunasema 'tunayo ndoto' ya jambo ambalo tunatumaini itatimia, au tunaeleza juu ya ndoto ambayo 'tuliota jana usiku', au tunaota juu ya mwenzi wa ndoa au ndoto ya kazi, n.k. Lakini 'kuwa na ndoto' na 'kuota' havifanani kamwe. Sisi sote tunayo 'ndoto'. Katika hadithi hii ya ndoto na ukweli, wa uhai na mauti, ya ukombozi wa sasa na ukamilifu wa baadaye, tunapaswa kutofautisha vipengele viwili muhumu katika ndoto zilizonyeshwa na Mungu kwa Mfalme Nebukadneza: Utafsiri na ufunuo. Tunajitahidi kutafsiri ndoto, lakini hii ni sifa ya Mungu ya kipekee. Mungu hufunua kusudi lake kwetu. Mungu alimtumia Danieli kama mjumbe wake kutafsiri ndoto ya mfalme.

### I. Ndoto ya Nebukadneza (Danieli 2:1-13)

#### A. Alikuwa Mfalme Wa Ushirikina (mistari ya 1-4)

Nebukadneza alikuwa kama kila kiongozi wa siasa wa wakati wake, mtu wa imani duni wa juu. Jambo la muhimu ambalo hadithi zilizochukuliwa katika kila moja ya falme zilizotajwa katika Biblia linajulikana vyema: *"Basi, mfalme akaamuru waganga, walozi na wachawi wa Wakaldayo waletwe ili wamfasirie ndoto yake."* (mstari wa 2) Walikuwa na vitabu ambavyo maana ya ndoto ilifafanuliwa, na wakati waliota jambo kama mkate, au mwezi, au mnyama, wangetafuta kitabu na kutafuta maana ya ndoto. Hii ni sawa na vile watu wengi wanafanya leo wakati wanachagua nambari ya bahati nasibu baada ya kuota kitu maalum. Watu wengine hata hutafuta shauri kwa kadi za uganga au unajimu. Lakini tunapaswa kujiuliza, "Je, haya humpendeza Mungu?"

#### B. Alikuwa Mfalme wa Donda (mistari ya 5-11)

Nebukadneza alikuwa mskirikina, lakini alikuwa mjanja pia. Yawezekana kwamba wakati mmoja hapo awali, baadhi ya waganga wake walijifanya ili kumdanganya na tafsiri za uongo. Pengine ndio maana aliamua wakati huu haitakuwa hivyo. Kwa hivyo, hakuwaomba tu utafsiri, bali pia aliwakumbusha ndoto aliyokuwa nayo. Hili lilikuwa jambo ngumu kwa vile njia pekee ya kutafsiri ndoto yake ilikuwa kujua maudhui yake, na mfalme alionekana kusahau.

#### C. Alikuwa Mfalme Asiyekata Tamaa (mistari ya 12-13)

Nebukadneza, kwa sababu ya tuhuma kwamba watu wake wenye busara walikuwa wakijaribu kumdanganya, alikasirika na akaamua kukatiza maisha yao. Huyu dikteta alikuwa na tabia ya mabadiliko ya hisia na hasira yake kali (sura ya 3, 4 na 6 zinaonyesha kipengele hiki cha utu wa Nebukadneza). Hata hivyo, uamuzi huu mkali unaonyesha pia kwamba bidii yake ya kupata maudhui ya ndoto yake, ambayo anaichukulia kuwa ya muhimu sana, ilikuwa imara.

### II. Danieli Afunua Ndoto (Danieli 2:14-23)

#### A. Mungu Huonyesha Kusudi Lake Kwa Wale Wanaosikiliza (mistari ya 15, 19)

Mungu alikuwa amempa Danieli uwezo wa kutafsiri ndoto. Alikuwa amechaguliwa miongoni mwa vijana bora wa Kiyahudi katika Yerusalemu kupelekwa Babeli. Danieli na rafiki zake walichaguliwa kwa sababu walikuwa: *"bila kasoro, wazuri kwa umbo, wenye uzoefu wa kila hekima, wenye akili na maarifa na wanaofaa kutoa huduma katika ikulu."* (Danieli 1:4) Lakini Danieli alifanya uamuzi muhimu tangu mwanzo wa kuingia katika mazingira ya wapagani ya Babeli. Kijana huyu Myahudi *"…aliamua*

*kutojitia unajisi kwa kula chakula bora cha mfalme na kunywa divai yake…"* (Danieli 1:8)

B. Mungu Huonyesha Kusudi Lake Kwa Wale Walio na Ujasiri (mstari wa 16)

Danieli alihitajika kuwa hodari baada ya kumwuliza nahodha wa kikosi cha Nebukadneza (mstari wa 15) ampeleke kwa mfalme ambaye alikuwa amewaamuru kabisa kuwaua wanaume na wanajimu wa ufalme wake (akiwemo na marafiki wake). Biblia inatueleza kwamba tangazo lilikuwa tayari limechapishwa (mstari wa 13) na, kama hadithi zingine tunazofahamu, toleo la tangazo lilimaanisha kwamba haingekuwa rahisi kulibatilisha (linganisha na Esta 3:14-15, 8:13, 9:1, 13, Danieli 6:8-9, 15, n.k.). Hivyo, kufuata amri hiyo kungeweza kuepukwa tu na kuchapishwa kwa mtu mwingine kulibatilisha (Esta 8:13-9:1). Kama vile ilivyokuwa na Daudi, Yoshua na wahusika wengine, ujasiri na nguvu zinatokana na kumjua Mungu mmoja wa kweli.

C. Mungu Huonyesha Kusudi Lake Kwa Wale Hunyenyekea Mbele Yake (mistari ya 17-18)

Danieli alikuwa mnyenyekevu pia wa kutosha kwenda nyumbani, kushiriki hitaji la dharura na marafiki wake Hanania, Mishaeli na Azaria. Tunahitaji kujiuliza kama imani yetu ni ya kweli na imara. Tutapata majibu tunapoomba pamoja na wengine katika umoja wa kusudi. Kwa hivyo, vijana hawa waliomba na kufunga kama vile Esta alivyofanya. Wanafunzi katika chumba cha juu waliomba pamoja kabla ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 1:14, 2:4). Tunapomtafuta Mungu pamoja, Yeye yuko pamoja nasi na anaweza kutubariki na kujibu maombi yetu. Zaidi, Danieli na wenzake walimwomba Mungu *"…aliyeumba ulimwengu …hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono ya wanadamu."* (Matendo ya Mitume 17:24), kwa *"Mungu wa mbinguni".* Na jambo la kushangaza katika ombo la utafsiri wa Danieli kwa rafiki zake lilikuwa kwamba hii haikuwa kuomba nguvu, ujasiri au ujuzi; lakini kuomba *"huruma ya Mungu wa mbinguni"* (mstari wa 18). Hii inaonyesha kwamba Danieli alijua vizuri ni misingi gani ambayo Mungu wanayemsubiri angetenda.

## III. Kufahamu Mapenzi ya Mungu (Danieli 2:24-49)

A. Weka Kando Kila Kitu Kinachotuangaisha

Tunahitaji kujua mwelekeo tunaotazama. Danieli alipoelewa ukubwa wa changamoto hiyo, alijua aelekee upande gani. Tunataka kuelewa mapenzi ya Mungu ni nini, ni lazima kama Danieli tumtazame *"Mungu wa mbinguni"* (mstari wa 18). Ili tuweze kumsikiliza Mungu, tunahitaji, kama Danieli, kutofatuisha kati ya hekima ya ulimwengu (watu wa hekima wa Babeli wakati wa Danieli, au Wagiriki wakati wa 1 Wakorintho Cor. 1:18-29) na hekima inayotoka mbinguni (Yakobo 3:17), ambayo inatoka kwa Mungu (Danieli 2:27-28). Ni Mungu wa Biblia peke yake ndiye chanzo cha *"nguvu na hekima"* (Daniei 2:20). Hakuna kitu kinachopaswa kutukengeusha.

B. Elewa Kwamba Historia Huelekea kwa Kukamilika Kwa Ufalme wa Mungu

Nebukadneza, mfalme aliye madakarani, aliitwa hapa *"mfalme wa wafalme"* (mstari wa 37), angefuatwa na falme zingine (mistari ya 38-42), wambayo wakati wake zingeangamizwa n.k. Mungu ataleta Ufalme Wake. Tuseiwa na shaka kwamba Atafanya hivyo. Kwa hivyo, Danieli alisema yafuatayo: *"…Ndoto ni ya kweli na maana yake ni halisi."* (mstari wa 45) Siku iliyotangazwa na Isaya itafika (Isaya 9:6-7, tazama pia Danieli 2:44). Yesu anatuhimiza tutafute ufalme wa Mungu juu ya vitu vingine (Mathayo 6:33). Ufalme huu utajumuisha kila kitu na mapenzi ya Mungu yatadhihirishwa juu ya kila kitu kilichoumbwa.

## MASWALI YA ZIADA

- Ukitazama Danieli 2:1-4 je, unafikiri haya yanaonekana hata leo? Kwa njia gani?
- Je, Mungu amekupa vipawa gani? Unavitumia ipasavyo?
- Kama sifa moja ya Danieli ilikuwa kwamba alisikiliza sauti ya Mungu, je nini kinatuzuia kuwa wasikilivu leo?

## HITIMISHO


Watu wengi wana aina mbali mbali za ndoto. Mungu alimtumia Danieli kufunua maana ya kweli ya ndoto ya Mfalme. Ingawa mawazo yake na njia zake ziko juu kuliko zetu, Mungu huwachagua watoto wake kushirikiana naye katika kazi ya kuumbusha ulimwengu hali ya muda mfupi na usiodumu wa falme zao, kinyume na ufalme wa Mungu wa kudumu na wa milele.

**Somo la 42:**

## NDOTO YA MFALME NEBUKADNEZA

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba Mungu hueleza mambo ya siri kwa ajili ya utukufu wake.
**Methali:** "Usipoziba ufa utajenga ukuta"
**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 2:1-48
**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 2:28 "...lakini yule Mungu wa mbinguni afunua siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadneza mambo yatakayokuwa siku za mwisho. Ndoto yako ni hii."
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** "Vipawa vyote tunavyopata kutoka kwa Mungu vinapaswa vitumiwe kwa utukufu wake."



| Somo la 43 | THAMANI YA UANIMIFU |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 3:1-30 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuhimizwa kuwa mwaminifu na muazi kwa Mungu katikati ya ibada ya uongo ya ulimwengu na kila wakati kutoa ushuhuda wa kweli wa nguvu za Mungu. | "Basi, mfalme Nebukadneza akasema, - Na asifiwe Mungu wa Shadraki, Meshaki na Abednego, kwa kuwa alimtuma malaika wake na kuwaokoa watumishi wake! Walimtumainia Yeye…" **Danieli 3:28** |

## UTANGULIZI

Hadithi ya Shadraki, Meshaki na Abednego pia ni mfano mkubwa wa nguvu ya Neno la Mungu katika maisha ya wale wanaoikubali. Kwa sababu ya uaminifu wao kwa Muumba wao, hata Mfalme Nebukadneza alimtukuza, na wengi walishuhudia nguvu za Mungu za ajabu. Sasa, Danieli 3 inatuonyesha yale Mungu anataka kutufundisha katika somo hili.

### I. Ibada Iliyoamriwa na Mfalme Nebukadneza (Danieli 3:1-7)

Kutoka mwanzo, wakati watu wa Israeli waliumbwa, Mungu aliwataka watu wake kuwa waaminifu Kwake, na hiyo ilimaanisha kukosa kuabudu miungu ingine (Kutoka 20:2-5). Hata hivyo, Waisraeli hawakufanya hivyo; badala yake walifanya kinyume. Kwa sababu hiyo, walishindwa na kuchukuliwa mateka katika Babeli. Wakati huo, na mbali na nchi hiyo, msukumo wa ibada ya sanamu ilikuwa nzito zaidi. Nebukadneza aliwakilisha nguvu za dunia za zamani na za sasa, kama vile Farao wa Misri au Herode walikuwa katika Agano Jipya. Hata hivyo, wote, pamoja na wale ambao waliinuka kwa kiburi na wakaidi katika kila karne hadi leo, watashindwa kwa nguvu za Mungu za ajabu (Kutoka 15:19, Matendo ya Mitume 12:21- 23).

Vivyo hivyo, inaweza kusemwa kwamba Nebukadneza ndiye mfalme wa kawaida ambaye alitumia dini kwa manufaa yake. Baada ya kupokea maana ya ndoto yake, alishawishiwa na nguvu za Mungu, lakini wakati hofu ilipita, alionyesha tena kiburi chake (Danieli 2:47). Nia ya Nebukadneza haikuwa ishara ya unyenyekevu, lakini kunufaika, kwa sababu katika Danieli 3, tunaona huyu mfalme, ambaye aliendelea na majivuno yake, akiamrisha ibada ya sanamu.

Kwa kuiweka wakfu sanamu hiyo (Danieli 3:2-3), mfalme huyu wa Babeli aliamuru kwamba watu wote waliokuwa katika ofisi za kisiasa katika ufalme wake wote wakutane, miongoni mwao walikuwa maafisa wapya: Shadraki, Meshakia na Abednego, kwa vile Danieli alikuwa amewaombea wasimamie shughuli za mkoa wa Babeli (Danieli 2:49). Kwa sauti ya mbiu ya kifalme, watu wote walihitajika kuinana na kuabudu sanamu ya dhahabu (Danieli 3:4-5).

### II. Mtazamo Thabiti Katikati ya Jaribio (Danieli 3:8-20)

Kwa kejeli, baadhi ya Wakaldayo waligundua kuwa marafiki watatu wa Danieli hawakuwa wakifuata agizo la mfalme Kwa hivyo, walitangaza kukataa na 'ukosefu wa heshima' kwa sanamu ya Nebukadneza (mistari ya 8, 12). Katika kifungu hiki, mafundisho mawili muhimu yanaweza kuonekana: Katika sehemu ya kwanza (Danieli 3:12, tunaona kufungwa macho ambapo Shadraki, Meshaki and Abednego walifanyiwa. Wakaldayo hawa waliamini kwamba kwa sababu vijana Wayahudi walifanyia serikali kazi, wangefanya kila kitu ambaho mfalme aliagiza. Hivi sasa tunaishi katika ulimwengu ambao unadai kwamba tuishi kulingana na viwango na sheria zake. Hata hivyo, ni juu yetu kujua jinsi ya kutambua kile ibilisi anapendekeza na kile Mungu anataka kwa watoto wake. Usaliti wa mali umewafanya Wakristo wengi kuacha imani yao. Hata hivyo, ni lazima tukumbuke kwamba ingawa kazi na biashara ni muhimu, haviko muhimu sana kuliko kutii, kuwa mwaminifu na muwazi kwa Mungu.

Ibilisi anajua kwamba kazi ni muhimu, na anaitumia kama njia ya kutusaliti. Kwa hivyo, onyo lifutalo ni muhimu: Jihadharini na kuabudu sanamu za sasa! Kumbuka kwamba tunapitia majaribu haya, na imani yetu inafaa kuwa ya ushindi, tukitumaini kabisa katika ahadi za Bwana. Kumbuka kwamba huduma na ibda zinapaswa tu kuwa za Mungu wetu; kisha atatupa yale tunakosa (Mathayo 6:25-33).
Katika sehemu ya pili, marafiki watatu wa Danieli wanatufundisha tusiige mazingira ya kijamii ambayo tunaishi. Waumini wengie, wanaoishi na thamani na

vipaumbele vya ulimwengu huu, wanaingia pole pole katika mazingira ya kuiga na ya udini. Labda mwanzoni walisema 'hapana' lakini walifahamu kile jamii hii inapeana hadi wakaikumbatia na kuiona kama jambo la kawaida. Hatua hizi zinafanyika na 'sanamu' za ulimwengu kama vile muziki, mitindo, michezo, nlk. Utiifu unatufanya tuwe wepesi kubadilika, na sio wakali dhidi ya mambo haya. Uvumilivu kama huo unaweza kutuongoza kufuata mtindo wa maisha wa kiulimwengu.

Kuzingatia ni uwezekano mdogo: unaanza katika mawazo yetu, na kisha huelekea kwa matendo yetu. Kwa sababu hii, mtume Paulo alipendekeza kwamba tuweke wakfu maisha yetu yote, bali kujifananisha na ulimwengu huu. Kama wanafunzi wa Kristo, ni lazima turuhusu Roho Mtakatifu abadilishe mawazo yetu ili tuishi kulingana na mapenzi ya Mungu (Warumi 12:1-2). Haya yanaweza kut kupatikana kwa kuwa mwaminifu kwa Bwana kwa kulifuata na kulitii Neno Lake. Marafiki wa Danieli hawakuiga nyakati au dhana za kijamii ambazo waliishi ndani. Maombi yao ya mara kwa mara yaliwaelekeza kusimama imara mbele ya majaribu, wakujua la kufanya, bila kujali yatayotendeka kwa maisha yao (Danieli 3:16- 18).

### III. Uaminifu na Kuinuliwa kwa Mungu (Danieli 3:21-30)

Shadraki, Meshaki na Abednego walikutana na adhabu kali ya Nebukadneza. Hawangeweza kutoroka. Kwa sababu ya uaminifu wao kwa Mungu, maisha ya watu hawa yalikuwa hatarini katika tanuru la moto lililokuwa limewashwa mara saba zaidi ya kawaida (Danieli 3:19), iliwaka sana hata watu waliowatupa ndani ya tanuru walikufa (mstari wa 22). Kwa hivyo mashujaa wetu wa Kiyahudi walifungwa na kutupwa kwenye shimo la moto (mstari wa 23).

Hata hivyo, jambo lisilotarajiwa na la kushangaza lilitendeka mbele ya macho ya mfalme mwenyewe. Akiwa na hofu nyingi aliuliza, *"Je, hatukuwafunga watu watatu na kuwatupa motoni?"* (mstari wa 24) Mara tu swali lake lilipothigitishwa, na bado kwa heshima, alisema: *"Tazama! Mbona ninaona watu wanne wakitembeatembea humo motoni bila kufungwa na wala hawadhuriki, na mtu wa nne anaonekana kama mwana wa miungu?"* (mstari wa 25) Kile Nebukadneza alikuwa akiona kilikuwa nguvu za Mungu za kutunza na kuwalinda watu wake.

Biblia imejaa miujiza inayoheshimu, nguvu, ukuu na enzi ya Mungu. Hadithi hii ni kati yake. Mungu ni mwaminifu kwa ahadi Zake, na kutimizwa kwake kwa ajili ya utukufu wake. Hata wakati taifa lote lilikuwa limeacha amri za Mungu, na kuelekea kwa utumwa, kulikuwa na mabaki ambao daima walibaki waaminifu kwa Mungu. Mabaki hayo yaliteseka kutoka kwa utumwa, hata hivyo, Mungu aliwalinda kutokana na maovuyote. Hivi ndivyo Mungu anawajali watu wake, wale hakika ni wafuasi wake waaminifu, wale wanaofanya tofauti katikati ya taifa lililokuwa la udini mwingi.

Uaminifu wa Mungu ulikuwa dhihirisho. Mungu anatutafuta, na anajua kwamba shuhuda za kweli zitaleta utukufu kwa jina lake na watu watafikiwa kwa ajili yake. Katika Agano Jipya, tunapata kwamba Paulo alikuwa tayari kufa ili injili iwafikie watu wengi. Hata hivyo, kulikuwa na Wakristo waliomshawishi asiende Yerusalemu kwa sababu hakika kifo kilimsubiri huko (Matendo ya Mitume 21:4-14). Lakini mtume alijua ni nani aliyemwamini (Matendo ya Mitume 21:13).

Kwa bahati mbaya, kuna waumini wengi wanaotafuta uaminifu wa Mungu kwa manufaa yao zaidi kuliko kumheshimu Mungu kama inavyostahili. Kwa hivyo, wanaomba ulinzi wa Mungu kwa ajili yao wenyewe, lakini ni wachach sana walio tayari kuteseka ili wengine wapate kumjua Kristo. Kuna imani potovu na ya bure inayosema kwamba watoto wa Mungu hapaswi kuteseka na wanapaswa kuwa na kila kitu wanachotaka. Hata hivyo, Biblia imejaa mifano ya wafuasi na wanafunzi wa Kristo walioishi katikati ya mahitaji na mateso. Hata Yesu mwenyewe hakuwa na mahali pa kuweka kichwa chake (Mathayo 8:20).

## MASWALI YA ZIADA

- Je, Nebukadneza aliamuru nini na aliomba nini?
- Je, nia ya vijana ilikuwa gani kulingana na Danieli 3:12?
- Je, mateso yangu ni juu ya ushuhuda wangu na Kristo, au kwa sababu ya upumbavu wangu wa maisha?


## HITIMISHO

Katika jamii yetu, pia tunazo sanamu, amri zisizo za Mungu na miungu kama ushahidi wa ibada ya uongo. Hata hivyo, kama tu vile vijana hao walibaki waaminifu kwa Mungu, hivyo nasi pia tunapaswa kuwa wajasiri na tuangazie kwa bidii, kuwa na ushuhuda kulingana na kanuni za kibiblia. Tutakuwa na ulinzi na usalama katika Mungu wakati tunafanya maamuzi ya hekima na yaliyo sawa kulingana na thamani za kweli za kibiblia na kanuni zake, kwa sababu Mungu ni mwaminifu.

**Somo la 43:**

## THAMANI YA UANIMIFU

**Lengo la Somo:** Kuhimizwa kuwa Wazi na waaminifu kwa Mungu.
**Methali:** "Uaminifu hupatikana siku kwa siku, wala sio kwa usiku mmoja."
**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 3:1-30
**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 3:28 "Nebukadneza akanena, akasema, 'Na ahimidwe Mungu wa Shadraka, na Meshaki, na Abednego. Aliyemtuma malaika wake, awaokoa watumishi wake waliomtumaini, wakaligeuza neno la mfalme, na kujitoa miili yao ili wasimtumikie mungu mwingine, wala kumwabudu, ila Mungu wao wenyewe."
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?
**Himizo la Hadithi**: Tunapaswa kuwa waadilifu na waaminifu kwa Mungu kwa sababu Yeye ni mwaminifu.



| Somo la 44 | KIBURI HUTANGULIA KUANGUKA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 4:1-37 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuangazia dhambi ya Nebukadneza ya kiburi; jinsi ya kuiepuka, na kama inawezekana , jinsi ya kukabiliana nayo. | "Naye huwashusha wenye kiburi" **Danieli 4:37b** |

## UTANGULIZI

Danieli 4 inatueleza juu ya kiburi cha Mfalme Nebukadneza. Watu wengi (wakiwemo Wakristo) wana tatizo na kiburi, kikiwaongoza kwa hali ya majivuni, nia isiyosamehe, kutokuwa na rehema, kuifanya mioyo yao kuwa migumu, n.k. Kiburi kimewaelekeza wengi kuanguka katika dhambi zisizo hesabika (Mithali 16:18). Tutaunda mada yakiburi.Kwa ajili ya haya, tunaweza kusema yafuatayo: kama hatungekuwa katika neema ya Mungu, kiburi kingetuangamiza kabisa. Ilikuwa na ni kwa neema ya Mungu ambayo inaingilia kati na kutuinua kutokana na kuanguka, na kutusaidia kuacha, na kutafuta kusafishwa na kiburi.

### I. Ndoto ya Nebukadneza na Tafsiri Yake (Danieli 4:1-27)

#### A. Mti, Mfalme na Ufalme Wake

Danieli alitangaza kwamba Mungu alikuwa amekabidhi kazi hii ya utawala wa kifalme kwa Nebukadneza kama mfalme. Mungu alimruhusu Nebukadneza kutawala mataifa yote, na hasa watu wa Mungu waliokuwa mateka katika mji mkuu wa ufalme wake. Mungu alikuwa amekabidhi ulinzi wa watu wake kwa wafalme wengi wa kizazi cha Wayahudi, lakini wengi walianguka. Sasa, alikuwa anapeana jukumu hili kwa mfalme wa kigeni, Nebukadneza (Yeremia 29:7,14). Hata hivyo, tunapaswa tukumbuke kwamba Bwana anatawala kila wakati, ili kwamba anaweza kutumia maadui kuwabariki watu wake.

#### B. Roho Wa Mungu Mtakatifu Au Uwepo wa MUNGU

Katika ndoto yake, mfalme alipokea ujumbe ufuatao: *"Hii ni hukumu iliyotangazwa na walinzi, ni uamuzi wa walio watakatifu, ili wanadamu wote kila mahali wapate kutambua kuwa Mungu Mkuu anayo mamlaka juu ya falme zote za wanadamu, yeye humpa ufalme mtu yeyote ampendaye, humfanya mfalme hata mtu duni wa mwisho."* (mstari wa 17) Danieli alijulikana kwa ucha Mungu wake. Alikuwa ametafsiri ndoto ya mfalme mbeleni. Kwa hivyo, mfalme alimwita kwa sababu alijua kwamba Danieli alikuwa na *"roho ya miungu mitakatifu"* (Danieli 4:18). Nebukadneza alitambua uwepo wa Mungu kwa Danieli, lakini alitunukia kipawa hiki kwa miungu wake, na wala si kwa yule Mungu mmoja wa kweli.

#### C. Marekebisho na Adhabu ya Kimungu

Mti ulikuwa unaenda kukatwa, hukumu ya uungu yaja mapema au baadaye. Tunayo nafasi ya kurekebisha njia zetu kabla ya Mungu kutenda Danieli anaota fursa hii kwa mfalme kwa uaminifu. Danieli 4:27 anasema: *"Kwa sababu hiyo, Ee Mfalme, sikiliza shauri langu. Acana na dhambi zako na maovu yako, utende haki na kuwaonea huruma waliodhulimiwa, huenda muda wako wa fanaka ukarefushwa."* Hata hivyo, adhabu ambayo Mungu anaahidi kutuma kwa mfalme ni nguvu kabisa. Tunaona katika historia ya watu wa Mungu kwamba Mungu hutusababisha tuteseke kwa matokeo ya dhambi zetu wenyewe.

### II. Matokeo ya Kiburi (Danieli 4:28- 33)

#### A. Kiburi, Shida ya Kila Mtu

Nebukadneza alikiri kwamba alikuwa amejenga ufalme wake, sio kwa makusudi ya kumtukuza Mungu, bali kutukuza ufalme wake. Hivyo, alikuwa amejitukuza na kuweka enzi ya nafsi yake mwenyewe kwa ksuema kwamba alikuwa amejenga yote kwa nguvu zake, wakati katika ukweli, jibu lake lingekuwa kwamba ilikuwa ni kwa neema ya Mungu kwamba aliweza kujenga na kutekeleza. Mungu alikuwa na ni yeye anayepeana na atapeana nguvu za kufikia mafanikio ya kawaida, mafanikio ya kitaaluma, familia, kazi au ajira, uongozi wa jamii au huduma, n.k. Kila kitu kisichomtukuza

Mungu, atakirekebisha, kwa kuwa kila kitu ni cha Mungu, na vyote vinavyoishi vinatoka Kwake (Warumi 11:36).

B. Nebukadneza Aliadhibiwa na Kurekebishwa

1. Ufalme Uliondolewa Kwake.

Danieli 4:31, 36 anathibitisha haya. Mfalme Nebukadneza aliondolewa kwa ufalme wake, lakini kwa muda mfupi. Hii inatufundisha kwamba nidhamu ya uungu katika maisha haya ni kali, lakini ya muda. Kwa Nebukadneza, ilidumu kwa muda wa miaka saba na baadaye, adhabu ilifikwa mwisho.

2. Aliishi Kama Mnyama wa Shambani (mistari ya 32-33)

Nebukadneza alionekana kupoteza akili yake. Alianza kula majani kutoka kwa shamba, mwili wake ulilowa kwa umande, nywele zake zikawa ndefu kama manyoya ya tai, na kucha zake kama za ndege. Hatujui kilichotendeka hakika, lakini tunaweza kusema kwamba dhambi humbadilisha mtu kimwili na kiroho kuwa mnyama, kuwa viumbe vinavyoudhi ambao wamepoteza fahamu zao kwa kufungua tamaa zao mbaya, kufanya giza na kuumiza hoja zao, wakifanya mioyo yao kuwa migumu.

III. **Toba Na Urejesho (Danieli 4:34-37)**

A. Neema Na Toba

Fahamu ya Nebukadneza ilirejeshwa (mstari wa 34). Alihisi bora na kuacha kuwa mnyama na kuwa mtu tena man tena katika umbo na mfano wa Mungu. Lakini Mungu kwanza alianza na afya yake ya kiroho, wakati mtu huyu alimtambua Mungu kama Mfalme wa pekee wa mbingu na nchi.

B. Kurejeshwa Kikamilifu

1. Utukufu wa ufalme wake ulirudishwa kwake (mstari wa 36). Mara nyingi tunapoanguka katika dhambi, tunapoteza baadhi ya kile tuligharamia. Kwa mfalme, ilikuwa ufalme wake, kazi, jamii, wateja, marafiki, nyumba, n.k. Uzinzi unaweza kusababisha kupasuka kwa familia, hata upotezaji wa mali. Hata hivyo, tunapotubu, Mungu ana uwezo wa kurejesha nyumba iliyotalakiwa, kazi iliyopotea, marafiki wa mbali, wateja wanaotuamini tena, na zaidi.

2. Heshima yake na ukuu vilirejeshwa kwake (mstari wa 36). Kuanguka katika dhambi kunaweza pia kusababisha kupoteza kwa heshima. Kwa mfano, wakati mchungaji au kiongozi ananguka, hapotezi mahali pake, bali pia jina lake au hadhi yake, uchungaji wake. Hata hivyo, wakati kuna moyo ulionyenyekea na kutubu, Mungu anaweza kurejesha kujistahi kwetu na hisia za utu.

3. Viongozi wake walimtafuta (mstari wa 36). Kutenda dhambi pia huathiri mduara wowote wa watu ambao sisi ni mali yao. Lakini kuna mwito kwa watu wa Mungu kumrejesha aliyeanguka, kwa vile mtu anapoponywa, wote wanapona (2 Wakorintho 2:10-11). Viongozi wanapaswa kuwatafuta walioanguka katika dhambi. Mungu anaweza kuwatumia katika hali ya urejesho. Watu wanaweza kurejeshwa wakati kuna moyo ambao umekiri dhambi zake na kuomba msamaha, sio tu kwa Mungu, bali pia watu waliohuzunika au kuathirika.

4. Ukuu mkubwa uliongezewa kwake. Mwishowe, tunaweza kuesma kwamba wakati Mungu anaumia, anaponya, wakati anaadhibu, anarejesha. Mungu ni wa haki. Hata hivyo, Mungu si wa haki tu, yeye pia ni mkaribu, kwa sababu mara nyingi anatubariki zaidi ya tunavyostahili. Huu ni utukufu wa neema yake. Mungu ni mwema na mkarimu kabisa.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, mfalme aliota nini?
- Je, matokeo ya kiburi leo ni gani?
- Je, urejesho wa mtu kanisa unahusu nini leo?

## HITIMISHO


Kama tu Nebukadneza, wengi wamejaribiwa na kiburi, lakini si wengi walioshinda. Hata hivyo, Mungu ni mwema na rehema zake ni mpya kila asubuhi, na zinafikia moyo unaotubu na kumtafuta.

**Somo la** 44:

**KIBURI HUTANGULIA KUANGUKA**

**Lengo la Somo:** Kujifunza kutoka kwa dhambi za Nebukadneza za kiburi.
**Methali:** "Kiburi huenda tu kwa urefu wa mate ya mtu."
**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 4:1-37
**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 4:37b - "Maana matendo yake yote ni ya haki, naye huwashusha wenye kiburi."
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii? Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi: "**Mioyo iliyotubu hupokea rehema na wema wa Bwana."



| Somo la 45 | MAANDISHI KWENYE UKUTA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 5:1-31 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kwamba dhambi huleta maangamizo kwa maisha yetu. Tunapaswa kukumbuka kwamba hatuwezi kuepuka kutoka kwa mikono ya Mungu mwenye enzi anayetawala kila kitu. | "Lakini alipoanza kuwa na kiburi, akawa na roho ngumu na mwenye majivuno. Aliondolewa katika kiti chake cha enzi akanyang'anywa utukufu wake." **Danieli 5:20** |

## UTANGULIZI

Danieli 5 inatueleza juu ya kuanguka kwa mfalme wa Babeli. Historia inatueleza kwamba Mfalme Belshaza alikuwa wa mwisho katika nasaba ya Nebukadneza. Baadaye, ufalme wa Babeli ulipewa Wamedi na Waperezi. Tabia inayoonekana katika kifungu hiki bila shaka ni Danieli kama mtu mzee. Alitokea kama kijana mmoja wa mateka wa Israeli, aliyechukuliwa kama mhamiaji na Nebukadneza. Alijitoa sana kwa Mungu, na kutoka kwa ujana wake alikuwa amekusudia moyoni mwake kutii sheria za Mungu na kuwa shahidi wa baraka kwa wale wote waliokuwa karibu naye katika ikulu ambayo waliishi.

Mungu ni mwenye enzi. Anamiliki mamlaka ya juu, kwa hivyo hakuna jambo au mtu yeyote anaweza kuwa juu ya mamlaka hayo. Yeye huweka na pia huondoa mamlaka (Danieli 4:25). Katika masomo yaliyopita, tuliona jinsi Mungu alionyesha enzi yake kwa Mfalme Nebukadneza, na katika siomo hili, tutaona vile alionyesha enzi yake kwa Mfalme Belshaza.

### I. Karamu Kubwa (Danieli 5:1)

Historia inatufundisha kwamba ingawa maneno yanamtaja 'baba' wa mfalme Belshaza, alikuwa kwa ukweli babu yake. Miaka nyingi ilipita tangu kuvamiwa na kuangamizwa kwa Yerusalemu. Sura hii inaeleza karamu kubwa au sherehe iliyotengwa kwa ajili ya miungu ya wapagani ya Babeli. Mfalme alikuwa amewaalika maelfu ya wakuu wake, wake wao na wanawake wao. Sherehe ilikuwa kwa kilele cha makelele na kusherehekea. Kila mtu alikuwa anakunywa divai wakisifu miungu ya wapagani. Kulikuwa na muziki wa sauti, kucheza, kunywa kwa wingi, meza zilienezwa na vyakula vitamu zaidi. Kila mtu alikuwa akilewa sana, na kulingana na wao alikuwa na wakati mzuri na wa kufurahisha. Mfalme aliangaziwa zaidi na kusifiwa na kufurahiwa miongoni mwa jamii ya juu ya ufalme wa Babeli.

### II. Chombo Cha Kulewa (Danieli 5:2-3)

Kwa upande wa Belshaza, alitumia nguvu zake za kiuchumi kuachilia hamu zake za mwili, na katika upendeleo wake wa maadili, alifika kiwango kingine katika kuanguka kwake kwa binafsi. Kwa sababu ya upumbavu na udhaifu wa Belshaza, Babeli iliyojivuna ilikuwa inaenda kuanguka. Kama kawaida, mfalme alikuwa tayari kuwa na muda wa sherehe pamoja na marafiki wake. Alijivunia nguvu zake, na moyo wake ukawa na kiburi juu ya Mungu wa mbinguni. Lakini katika ulevi na kufurahia kwa usiku huo, Mungu alikuwa anaenda kufungua milango ambayo ilikuwa imetabiriwa na nabii Isaya miaka nyingi kabla kwa maneno haya: *"Bwana asema hivi kwa mteuliwa wake, Koreshi, ambaye mkono wake wa kuume naushika ili ayashinde mataifa yaliyo mbele yake na kuzivunja nguvu za wafalme, kufungua malango ya mji mbele yake ambayo haitafungwa."* (Isaya 45:1)

Belshaza, katika vikombe vyake, alipoteza akili yake. Aliamuru vyombo vitakatifu vya Kiyahudi viletwe ili kila mtu avitumie kunywa ili wote waiabudu miungu yao ya kipagani. Ingawa Nebukadneza mara kwa mara kwa kiburi alipinga Mungu wa milele, hakuwahi kuthubutu kutumia vyombo vya hekalu ambavyo vilijulikana kuwa vitakatifu. Hata hivyo, mjukuu wake Belshaza alifanya hivyo. Mfalme alitaka kuthibitisha kwamba hakuna kitu kilikuwa kitakatifu kwa mikono yake. Kwa hivyo, watu walikunywa divai na kuisifu miungu ya wapagani ya dhahabu, fedha na shaba.

## III. Kukufuru Kukubwa (Danieli 5:4-31)

Je, unajua kukufuru ni nini? Kukufuru ni kukosa kumheshimu Mungu, kutumia vibaya chochote ambacho ni cha Mungu. Hivyo, Belshaza alikuwa akimcheka Mungu kwa kutumia vikombe vya hekalu la Yerusalemu kunywa na wakuu wake. Kwa hivyo, Mungu wa enzi papo hapo alimwondoa kutoka kwa ufalme na ikulu ya Babeli. Kwa hivyo, Mungu we enzi papo hapo alimwondoa kutoka kwa ufalme na Ikulu ya Babeli kama vile Danieli alivyotabiri. Mfalme Belshaza alikunywa akitumia vyombo hivyo takatifu kuonyesha chuki yake juu ya watu wa Israeli na juu ya Mungu wa Danieli.

Tunaona kile dhambi inafanya karibu nasi na kuhisi kujaribiwa kuuliza kwa nini Mungu asifanye jambo ya kuwazuia watu hawa? Lakini, Mungu ana muda mwingi; Hana haraka ya kutenda. Ataishughulikia hali kama vile alivyomshughulikia Mfalme Belshaza. Hatupaswi kusahau kwamba Mungu ni mwenye haki.

### A. Hukumu Kubwa (Danieli 5:5-28)

Danieli 5:5 anatueleza: *"Mara, vidole vya mkono wa mwanadamu vikatokea na kuandika kwenye ukuta, karibu na kinara cha taa katika nyumba ya mfalme. Mfalme alitazama mkono ukiandika."* Mungu alikuwa anaingilia kati. Hakuzungumza ingawa alikuwa na ndoto au maono kwa sababu huyu alikuwa mtu ambaye Mungu alikusudia kumuadhibu. Mungu hangevumilia matusi haya maovu kwa mbingu, kwa hivyo aliandika kwenye ukuta wa nyumba ya karamu. Tunaamini kwamba yule aliyeandika haya kwenye ukuta ndiye aliyeandika juu ya mchanga wakati walimleta mwanamke aliytenda dhambi (Yohana 8:1-11).

Yale aliyoona kwenye ukuta yalimwogopesha na alilemewa na uoga. Hatimaye, yafuatayo yalitokea: *"Mfalme Belshaza akapaza sauti waletwe wachawi, Wakaldayo wenye hekima na wanajimu. Kisha akawaambia watu hawa wa Babeli, "Yeyote atakayesoma maandishi haya na kunijulisha maana yake, atavishwa mavazi rasmi ya zambarau na mkufu wa dhahabu shingoni mwake, na kupewa nafasi ya tatu katika ufalme.."* (mstari wa 7)

Mara tu mkono ulipoanza kuandike, *"MENE, MENE, TEKELI, PARSINI"* (mstari wa 25), sherehe, muziki, kucheza, vicheko, kula tagrija, sifa na makofi kwa mfalme vilikoma. Kulikuwa na kimya cha ujauzito wakati Mungu alisaeneza ujumbe wake. Magoti ya Mfalme Belshaza yaligongana kwa hofu. Mfalme alisumbukana kwa mkono mmoja tu. Fikiria juu ya tukio hili kwa mwenye dhambi asiyeamini siku ile watatoa hesabu ya dhambi zao mbele ya hakimu mtukufu, Bwana wetu Yesu Kristo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa bwana.

### B. Adhabu Kubwa (Danieli 5:29-31)

Yale yaliyoandikwa kwenye ukuta yalisema *"MENE, MENE, TEKELI, PARSINI".* Sasa kwa suala la tafsiri, tutaona tofauti katika neno la mwisho. Peresi ni umoja wa PARSINI. Halisi, yanaweza kutafsiriwa kama, *"kuhesabiwa, kupimwa, na kugawanywa".* Tafsriri ya maandishi kwenye ukuta ni: *"MENE: Mungu amehesabu siku za ufalme wako na kuukomesha. TEKEIL: Wewe umepimwa katika mizani, nawe ukaonekana huna uzito wowote. PERESI: Ufalme wako umegawanywa katika ya Wamedi na Wapersi."* (mistari ya 26-38) Mfalme Belshaza alikufa usiku huo huo (mstari wa 30). Kifo chake kilikuwa cha mapema. Dhambi dhidi ya Mungu nyingi huongeza kasi ya kuondoka milele. Ufalme uliondolewa kwake; utukufu wake wote ulipotea kwa muda mchache, na alienda uzimani bila Mungu na bila tumaini lolote.

Tusiwe waasi juu ya Mungu, tusiwe na kiburi, kwa sababu maisha yetu yanaweza kupotea kwa wakati usiotarajiwa. Tuyatoe maisha yetu kwa Bwana Yesu Kristo ili atusamehe na kutubadilisha, na tunaweza kutazamia uzima wa milele na Yeye.

Katika hadithi ya Mfalme Belshaza, tunaweza kuona wazi kwamba mshahara wa dhambi ni mauti. Mfalme huyu alianguka katika dhambi kadhaa kama vile kiburi, ulevi, na kukufuru, na hizi zote zilihukumiwa na Mungu, na kuelekeza kwa kifo chake cha ghafla.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni matukio gani yaliyotokea wakati Belshaza alikuwa chini ya ushawishi wa divai?
- Je, ni taswira gani ambayo Danieli anaeleza katika siku ya mwishi ya utawala wa Belshaza?
- Je, dhambi yetu kubwa ni gani?

## HITIMISHO

Siku moja sisi sote tutaenda mbele za Mungu kuhukumiwa kulingana na kutembea kwetu hapa duniani. Je, kuna dhambi yoyote iliyojificha katika maisha yetu? Kama ni hivyo, tunapaswa kutubu kwa moyo wetu wote na kumuomba Bwana msamaha! Lakini kama tunahisi kwamba kila siku tunatembea na Mungu, basi tuombe kwamba tutaendelea kuongeza hatua imara kwenye njia ya utakatifu.

**Somo la 45:**

## MAANDISHI KWENYE UKUTA

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba dhambi husababisha maangamizo.


**Methali:** "Uovu huingia kama sindano, husambaa kama mti wa mfuu."

**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 5:1-31

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 5:20 - "Lakini Nebukadneza alikuwa na kiburi na roho ngumu. Aliondolewa katika kiti chake cha enzi. Akanyang'anywa utukufu wake."

**Maswali ya Kujadili:**
Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Tuachane na dhambi, tuombe msamaha kabla siku ya hukumu kuwadia.



| Somo la 46 | UJASIRI KATIKATI YA MAJARIBIO |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 6:1-28 |

| Lengo |
|---|
| Kujifunza kutumaini katika ahadi za Mungu na kuamua kutokata tamaa katikati ya majaribio. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Mungu wangu alileta malaika wake kuvifumba vinywa vya si simba hawa, nao hawakunidhuru, kwa sababu alijua mimi sina lawama yoyote kwake." **Danieli 6:22a** |

## UTANGULIZI

Katika maisha yake yote, Danieli alikutana na mabadiliko makubwa na pia alipata mizozo mbali mbali ya kisiasa. Matukio mbali mbali yalitendeka ambayo yamerekodiwa katika Danieli sura ya 1 hadi 5. Katika sura ya 6, Danieli, sasa mtu mzee kiasi, anaanza kuzoea ufamle mpya – Wamedi na Wapersi chini ya mfalme wao Koreshi. Ufalme huu mpya ulikuwa mpana kuliko ufalme wa Babeli. Ulienea kutoka Ghuba ya Persiani mashariki, kwenda Makedonia Magharibi, upande wa Kskazini mipaka yake ilifika Armenia, na upande wa Kusini kwenda Misri mpaka Mto Frati. Ufalme huu haukuwa tajiri kama Wababeli, ingawa jeshi lake lilikuwa na nguvu zaidi. Ufalme wa Wamedi na Wapersi ulidumu kwa miaka 208, kutoka 539 hadi 331 Kabla Kristo. Danieli alikuwa ameendelea kwa miaka, labda zaidi ya 80. Aliheshimiwa kwa vile alipata mafasi katika taswira mbali mbali za kisiasa za wakati wake. Katika darasa hili tutasoma juu ya siku ambazo alitupwa katika tundu la simba.

### I. Wakati Imani Inapingwa na Kujaribiwa (Danieli 6:1-13)

A. Nafasi ya Danieli Kwenye Jukwaa la Siasa (mistari ya 1-2)

Wakati mabadiliko ya utawala yalifanyika, Danieli alikuwa bado anaheshimiwa kama mtumishi mwaminifu wa umma kwa sababu ya sifa zake ambazo Mungu alikuwa amempa. Kwa hivyo, aliendelea kuhudumu chini ya utawala wa Dario, mfalme wa Medi, na Koreshi, mfalme wa Persi. Wakati wa utawala wa Dario, ufalme mkubwa uliimarishwa chini ya usimamizi wa ufanisi ukiongozwa na wakubwa na makazi.

Tunaona kwamba Mfalme Dario aliwateuwa wakuu 120 na wasimamizi watatu (watawala) ili wasimamie mfumo wa utawala (mistari ya 1-2). Wakuu walikuwa maafisa ambao waliwajibika kwa wasimamizi hawa watatu au maliwali, na watatu hawa hatimaye wangentoa hesabu za moja kwa moja kwa mfalme. Na Danieli alikuwa mmoja wa wasimamizi hao watatu wa utawala (mstari wa 2). Danieli alikuwa mmoja wa wale watu watatu waaminifu ambao mfalme alikuwa amewaweka kama maliwali. Cha kushangaza ni kwamba hakuwa Mpersi, lakini alikuwa Myahudi, bali ambaye sifa zake zilikuwa, bila shaka za uadilifu.

B. Uadilifu wa Mtu Mwaminifu (mistari ya 3-4)

*Danieli 6:3 inasema: "Muda si muda, Danieli akadhihirika kuwa bora kuliko wale wasimamizi wengine na wakuu wote kwa kuwa alikuwa na roho njema. Hivyo mfalme akanuia kumpa uongozi wa ufalme."* (mstari wa 3) Sababu ilikuwa wazi; mtu huyu Myahudi, msimamizi wa utawala, alikuwa mwaminifu na muazi kabisa. Ushuhuda wa kuvutia wa mtu wa uadilifu katika Nyanja au nafasi za mamlaka ni muhimu sana! Kwa hivyo, si jambo la kushangaza kwamba walijaribu kufanya lolote ili wamuondoe mamlakani na kumshtaki kwa mfalme. Biblia inatueleza kwamba maliwali wengine na wakuu walijaribu kumshtaki katika hali nyingi juu ya usimamizi mbaya wa kiutawala au kosa fulani la usimamizi katika kazi yake, lakini hawakupata kosa lolote (mstari wa 4).

C. Mtego Mbaya (mistari ya 5-9)

Wakikablia na kutowezekana kwa kumshtaki Danieli, maafisa waliamua kwamba njia pekee ya kumdhalilisha ingekuwa kupitia imani yake, inayohusianna na *"sheria ya Mungu wake."* Walikusanyika na kupanga kuanguka kwake (mstari wa 5). Basi, walimshauri mfalme kwamba atie saini hati ya kuamuru kwa kipndi cha siku thelathini, hakuna mtu angemuomba mungu mwingine mwingine au mwanadamu yeyote ili tu mfalme (mstari wa 7). Mpango ulikuwa ni kumshika Danieli akimwabudu Mungu.

Kujitolea Kwa Mungu Katikati ya Uhasama (mistari ya 10-13)

Wakati Danieli alijua juu ya ilani, kando na kutishwa au kuogopa, alienda kumuomba Mungu katika chumba chake (mstari wa 10-11). Hakufinya kujitolea kwake kwa Mungu. Mtu mwingine kwa nafasi yake pengine angekuwa mwangalifu na kuamua kujificha au kutii tu amri kwa kutofanya ibada zake tatu kwa siku. Mtu wa uadilifu hauonyeshi tu wakati yuko kazini, siku yote. Danieli alionyesha kujitolea kwake kwa Mungu, bila kujali maadui walikuwa wamemwekea mtego. Hii inatukumbusha yale mitume walijibu baraza *"Lazima tumtii Mungu, wala ni wanadamu!"* (Matendo ya Mitume 5:29). Mtazamo huu si uasi rahisi wa kiraia, bali uamuzi thabiti wa utiifu na kujitolea kwa Bwana.

## II. Mungu Hulinda na Kuambatana na Waaminifu Wake (Danieli 6:14-24)

A. Mfalme Ambaye Hangeweza Kumwokoa Mfungwa (mistari ya 14-20)

Danieli alishtakiwa na maadui wake kwa kukosa kutii amri ya mfalme. Ilikuwa dhairi kuwa mtego ambao walikuwa wameunda ulikuwa umefanikiwa (Danieli 6:13). Hata hivyo, Mfalme Dario alihisi vibaya baada ya kukubali ombi hili (mstari wa 14). Kuongezea kwa haya, ilikuwa ni kwa sheria kwamba mamlaka ya kifalme haikuweza kupingwa au kufutwa (mstari wa 15). Kama sheria ya nchi ingevunjwa rahisi, utawala wa kisiasa ungepotea.

Danieli alitupwa ndani ya tundu la simba. Dario, akiwa amehuzunika, alitaja tumaini la pekee la mkuu wake mpendwa Danieli: *"Mungu wako unayemtumikia daima, na akuokoe!"* (mstari wa 16).

Ni wazi kwamba mfalme huyu mwanadamu hangeweza kumuokoa Danieli, ingawa alitaka kufanya hivyo. Lakini Mungu, Mfalme wa wafalme, angemuokoa; Kwake hakuna jambo lisilowezekana (Luka 1:27), na hawaachi watumishi wake wanaomtumaini waahibike (Zaburi 22:5).

B. Uwepo Wa Mungu Kwa Wale Wanaomtumainia. (mstari wa 21-23)

Mshangao mkubwa hu! Hii ilisababisha furaha kubwa kwa mfalme, lakini zaidi ya yote, ushuhuda mkubwa kwa mfalme mpagani! Mungu alikuwa amemuokoa mtumishi wake mwaminifu! Danieli hakuwa na majeraha yoyote alipotolea katika tundu la sima (mstari wa 23). Maelezo ya kibiblia ya tukio hili ni rahisi: *". . . kwa sababu alimtegemea Mungu wake."* (mstari wa 23) Mungu alikuwepo katika tukio hili la kusikitisha. Zaburi 138:7 inasema: *"Hata nikikumbana na taabu, wewe wanilinda; waunyosha mkno wako dhidi ya hasira ya maadui zangu wakali; kwa kuwa nguvu yako kuu wanisalimisha."*

## III. Kuinuliwa Kwa Mungu Ni Matokeao ya Ujasiri Ulioonyeshwa (Danieli 6:25-28)

A. Wenye Nguvu Humtabua Mungu Anayeishi (mstari wa 25-27)

Matokeo ya mwisho ya ushuhuda huu ulio hai ulisababisha amri nyingine ya mfalme kwa wakazi wote wa ikulu yake ambapo aliamuru kila mtu kuheshimu na kutetemeka mbele ya uwepo wa Mungu wa Danieli (Danieli 6:22-27). Dario aliongezea kwamba Bwana alikuwa Mungu *"aliye hai"*; yaani Mungu wa kweli. Alikubali kwamba utawala wake hauishi kamwe (mstari wa 26). Katika hali hii, tunaweza kuona kwamba mfalme alielewa kuwa kosa halikuwa kweli dhidi ya Danieli; lakini juu ya Mungu wa kweli.

B. Kujitolea Huleta Utajiri (mstari wa 28)

Leo, Wakristo wengi wako na imani yao ikiwa inajaribiwa. Lakini, uhusiano wetu na Mungu hafuai kuchanganya. Watu wa uadilifu watafanikiwa. Tukumbuke kwamba Neno linasema: *"Basi, Danieli akapata fanaka wakati wa utawala wa mfalme Dario na wa mfalme Koreshi, Persi."* (mstari wa 26) Mungu huwaheshimu wale wanaoonyesha uadilifu katika hali zote na pia kuonyesha ujasiri wakati wote.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni matendo gani yaliyoonyesha uadilifu wa Danieli?
- Fikiria juu ya mfano ambao kujitolea kwako kwa Mungu kulijaribiwa?
- Je, unaweza kufanya nini ili fanaka isikutenge na kusudi la Mungu katika maisha yako?

## HITIMISHO

Mungu mara nyingi yuko katikati ya majaribu ambayo watoto wake wanapitia, na atatukuzwa na uadilifu na bidii ya watoto wake kuwa waaminifu kwake.

**Somo la** 46

## UJASIRI KATIKATI YA MAJARIBIO

**Lengo la Somo:** Kujifunza kwamba ahadi ya Mungu ni chanzo cha ujasiri wetu katikati ya majaribio.


**Methali:** "Haijalishi usiku mrefu, Asubuhi Yaja."

**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 6:1-28

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 6:22a "Mungu wangu alileta malaika wake kuvifumba vinywa vya simba hawa, nao hawakunidhuru, kwa sababu sina lawama yoyote kwake."

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Ahadi za Mungu ni ujasiri wangu.



| Somo la **47** | **FALME NA UFALME WA MUNGU** |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 7:1-28 |

| Lengo |
|---|
| Ili kuhamasisha uthabiti katika maisha ya Kikristo, ingawa wakati mwingine hatuoni matokeo yanayotarajiwao, hatupaswi kukata tamaa bali kusonga mbele katika mipango ya Mungu kwetu. |

| Mstari wa Kumbukumbu Memory Verse |
|---|
| Lakini watakatifu wa Mungu watapewa ufalme, nao wataumiliki ufalme huo milele na milele. **Danieli 7:18** |

## UTANGULIZI

Kitabu cha Danieli ni cha kundi la vitabu vya ambavyo vinawakilisha idadi kubwa eskatolojia picha, maumbo na maono. Kinatumia lugha za kinabii na kimejaa taipolojia. Kwa ajili ya haya, ni ngumu kidogo kufikia utafsiri mmoja ulio wazi.

Tunapowasilisha somo hili, tutakumbuka kwamba hatuna majibu kamili au tafsiri ya kipekee ya maneno. Katika maneno ya maono ya wanyama wanne, wengi wa watoa maoni wamepatana katika tafsiri zinazofanana sana.

### I. Maono ya Wanyama Wanne (Danieli7:1-14)

A. Maono ya Kihistoria nay a Ukalimani

Kabla ya kutafsiri maneno ya Danieli, ni lazima tuchambue maono. Danieli alikuwa na ndoto na akaona maono wakati wa utawala wa kwanza wa Belshaza katika Babeli (mstari wa 1). Maono haya hayako kwa mpangilio kufuatia tundu la simba, ambayo yalitokea wakati wa Utawala wa Wapersi. Maono ya sura ya 7 yametangulia sherehe ya Belshaza ya ulevi karibu kwa kiwango cha miaka 16 au 17. Sherehe hii ilifanyika mnamo mwaka wa 17 wa utawala wake. Kwa hivyo, mpangilio wa vifaa katika kitabu cha Danieli ni wa kithiolojia na wala si mpangilio.

Maono ya kwanza ya Danieli (Danieli 7:2-14) yana vitu kadhaa vya mfano:

i). Bahari, ikiashiria mataifa ya ulimwengu ya Mataifa (Isaya 17:12, Ufunuo wa Yohana 17:15). Inaweza pia kutaja shimo la kawaida, ambalo lilifafanuliwa kama makao ya wanyama wa barahini ambao walikuwa na uadui kwa Mungu (Ayubu 26:12, Zaburi 74:13-14);

ii). Dhoruba, ikiashiria vita vya ulimwengu (Isaya 17:12);

iii). Wanyama wakiashiria falme za nguvu za ulimwengu.

iv) Wanyama katika sura hii wanawakilisha chuma kama vile ilivyokuwa katika mfano wa Danieli 2. Hiyo ni kusema: Babeli, Mede-Persi, Ugiriki na Roma;

v) Siku za Uzeeni zinamaanisha Mungu (Danieli 7:13);

vi) Mwana wa Mungu aliyetajwa katika Danieli 7:13, akiwakilisha muundo wa Yesu.

vii) Danieli anamwonyesha Kristo kwa uungu/mwanadamu na kwa maana ya kimasihi. Moja kama vile *"... mwana wa adamu ..."* (mstari wa 13) alikuwa Mwana wa Adamu, Mwokozi wa ulimwengu. Kinyume chake kwa uwanja wa wanyama, amepewa ufalme wa ulimwengu na wa milele. Bila shaka, istilahi hii iliyotumiwa katika Danieli inazungumzia Yesu kinabii na kuanzishwa kwa Ufalme Wake.

B. Wanyama Wanne (mistari ya 4-8)

1. Mnyama wa Kwanza– Kama Simba (Danieli 7:4)

Mnyama wa kwanza amechukuliwa kuwakilisha taifa la Babeli. Mwisho huu ulifikiwa, kati ya zingine kwa sababu ya kufunuliwa kwa Daneili 2, his conclusion has been reached, among others, due to the revelation of Danieli 2, ambapo anatambua wazi kichwa cha dhahabu kama Nebukadneza, mfalme wa Babeli. Kuna ishara pia katika hii kwa vile Babeli alikuwa na sanamu ya simba walio na mabawa, na pia nabii Yeremia alizungumza juu ya Nebukadneza kama simba (Yeremia 50:17).

2. Mnyama wa Pili – Kama Dubu (Danieli 7:5)

Anawakilisha Ufalme wa Wamedi na Wapersi, mrithi wa Wababeli. Kihistoria, anatambuliwa hivi. Katika Palestina, ilikuwa kawaida kwa dubu kuchukuliwa wa pili kwa ukali, mara nyingi baada ya sima.

3. Mnyama wa Tatu – Kama Chui (Danieli 7:6) Wakati Babeli ilikuwa na mabawa mawili, ufalme huu ulikuwa mabawa nne. Hii ilimaanisha Ugiriki, taifa lenye nguvu la zamani ambalo, chini ya amri za Alexander Mkuu na jeshi lake, waliweza kushinda ulimwengu kwa muda mfupi. Pia, inawezekana kwamba "vichwa vinne vya chui" vinamaanisha migawo nne ya Ufalme wa Giriki uliongozwa na wakuu wanne baada ya kifo cha Alexander.

4. Mnyama wa Nne (Danieli 7:7-8)
Ingawa wanyama wa hapo awali walionyesha kufanana kwa wanyama, mnyama wan ne alikuwa tofauti. Alikuwa na nguvu zaidi. Mnyama huyu alirejelea Ufalme wa Kirumi. Roma katika historia alikuwa mrithi wa Ugiriki.

**II. Maelezo ya Maono Na Maelezo ya Eskatolojia (Danieli 7:15-28)**

A. Tafsiri ya Kibiblia-Kihistoria
Danieli 7:17 ni kielelezo cha kuelewa kifungu hiki. Mwandishi anatueleza wazi kwamba wanyama wanne wanawakilisha falme nne ambazo zitaibuka duniani. Hii inatuonyesha maendeleo ya kihistoria; mstari wa 18 hutuangazia katika tafsiri ya mwisho wa maono haya. Lakini Danieli alitaka kujua kwa maelezo maana ya mnyama wa nne, (Danieli 7:19). Sifa za mnyama wan ne (Roma) zinapatika katika mistari ya 23 hadi 25.

B. Tafsiri ya Eskatolojia ya Mnyama wa Nne Ni ya kushangaza katika maandishi ya kibiblia ambayo kuanzia na Danieli 7:19, mwandishi anaonyesha hoja kubwa katika mnyama wa nne, kwa vile alikuwa tofauti sana. Hiyo ndio sababu tunazingatia tafsiri zingine kama zifuatazo: Historia inaekeleza Rumi. Tafsiri hii inaonyesha mnyama kuwa Rumi, na pembe kumi zinawakilisha idadi isiyojulikana ya wafalme na utawala hadi kurudi kwa Kristo.

**III. Mafundiyo ya Leo**

A. Mungu Anaonyesha Maono Kwa Watoto Wake (Danieli 7)
Ufunuo zote za Danieli zilileta faraha kwa watu wa Israeli waliokuwa wakiteseka na kudhulumiwa. Kupitia maneno haya, Mungu alionyesha hawa wa Israeli kwamba alibaki upande wako, kama tu vile alivyokuwa na Danieli na wanzake. Hii ndio ilikuwa moja ya kusudi la maono.

B. Mungu Anatawala Falme Zote za Ulimwengu Huu (Danieli 7:10-11)
Ingawa falme za nguvu kama hizi nne zimekuwepo katika historia, na zingine ambazo tunazifahmu leo, Mungu anatawala na zote lazima ziwe chini ya mamlaka na nguvu yake. Falme hizi ni za muda tu. Siku moja, zinaibuka, zinafikia kilele, lakini mwishowe zinaanguka, na kudhoofishwwa. Falme zote za ulimwengu huu ziko chini ya hukumu ya uungu (mstari wa 10). Kila kitu kiko chini ya utawala wa Bwana mkuu.

C. Mungu Wakati Wote Huwapa Watu Wake Ushindi (Danieli 7:27)
Danieli anaonyesha kanuni inayoonekana kote katika Maandiko, Mungu wakati wote huwapa watu wake ushindi. Hata wakati wanyama, mataifa, ibilisi, n.k. zinainuka juu ya watu wa Mungu, huwapa ushindi. Tunamuona kila siku Mungu anayetusaidia kupata ushindi juu ya ushindi, lakini ushindi wa mwisho utaonekana wakati wa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo.

D. Mungu Anaahidi Ufalme Bila Usawa (Danieli 7:14, 18, 22, 27)
Neno linalotumiwa mara kwa mara katika kifungu cha Danieli 7 ni *'ufalme.'* Ingawa katika maono ya kwanza wanyama wanne wameonyeshwa kama falme nne kuu, Mungu anafunua ukuu na tabia ya Ufalme Wake. Kiunabii anatangaza ufalme wa Masihi, wa Kristo, ambapo Mfalme ni Mwana wa Adamu (mstari wa 13). Mamlaka yanatoka kwa Mungu (Siku za Uzeeni)

## MASWALI YA ZIADA

- Je, Mungu amekufundisha nini leo kwa mafunzo ya somo hili?

## HITIMISHO

Falme kadhaa zimefananishwa kama wanyama na kila mmoja alikuwa na sifaa za kipekee za mwili na ukali, maelezo ya wanadamu wasio na Mungu. Lakini ametangaza katika Neno lake ukuu wa Ufalme Wake, ambao haulinganishwi. Huu ni Ufalme uso na kifani ambao huleta tumani kwetu sote.

**Somo la** 47:

## FALME AND UFALME WA MUNGU

**Lengo la Somo:** Kuelewa kwamba falme za dunia ni za muda tu bali Ufalme wa Mungu ni wa milele.

**Methali:** Jeshi la kondoo liongozwalo na simba, hushinda jeshi la simba linaloongozwa na kondoo.

**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 7:1-28

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 7:18 "Lakini watakatifu wa Mungu Mkuu watapewa ufalme, nao wataumiliki ufalme huo milele na milele."

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kulitokea katika hadithi hii? Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Ni Ufalme wa Mungu peke yake unaodumu.



| Somo la 48 | MAONO YA DANIELI JUU YA KONDOO NA MBUZI |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 8:1-27 |

| Lengo |
|---|
| Kutafakari juu ya udhihirisho wa kuona maovu na nezi kuu ya uaminifu ya Mungu kwa niaba ya watu Wake. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Kisha akaniambia, 'Sikiliza, ninakufahamisha matokeo ya ghadhabu ya Mungu yatayavyokuwa. Maono hayo yanahusu wakati wa mwisho.'" **Danieli 8:19** |

## UTANGULIZI

Tunahitaji kuelewa baadhi ya historia ya Wayahudi ya kipindi cha karne mbili. Antiokias wa IV (175-164 KABLA KRISTO) alikuwa mtawala wa Giriki iliyo kati Kilikia. Alijipa jina la mwisho la 'Epifine' linalomaanisha 'Mungu anayeonekana.' Alikuwa na machungu juu ya Wayahudi, na alikuwa amejitahidi kuwaangamiza wao na dini yao. Aliumiza Yerusalemu katika mwaka wa 168 KABLA KRISTO, akachafua Hekalu, akatoa sadaka ya nguruwe kwenye madhabahu, alijenga madhabahu kwenye nyota ya Jupita, akapinga ibada ya Hekalu, akakataza tohara juu ya uchungu wa kifo, akawauza maelfu ya familia za Wayahudi katika utumwa, akaharibu nakala zote za Maandiko ambayo yangeweza kupatikana, na kuchinja kila mtu aliyepatikana na nakala kama hizo, na wakaamua kwa kila mateso yanayowezekana kuwalazimissha Wayahudi waachange na dini.

Sura hii inazungumzia kipindi, ambacho Danieli anaishi bado ikiwa ni wakati wa Wababeli wakati aliona maono. Danieli 8:14 anaahidi kwamba hekalu lililochafuliwa lingepatikana. "Aliniambia, - Kwa muda wa nyakati za jioni na asubuhi 2,300; kisha maskani ya Mungu itapata tena hali yake halisi." Wayahudi wanasherehekea siku ambayo waliweza kulitakasa tena hekalu katika karamu yao ya Hanukah leo. Picha zilizorekodiwa katika maono ya Danieli ni ngumu kufikiria. Mandhari ya kijiografia katika maono haya yote ni Mashariki ya Kati ya siku hizo.

### I. Maono Ya Kondoo na Mbuzi (Danieli 8:1-14)

Katika mwaka tatu wa utawala wa Belshaza, Danieli alikuwa na maono ambayo yalianza na maelezo ya kondoo na pembe mbili, iliyofuatwa na mbuzi ambayo ilikuwa na pembe moja (mistari 1-5). Kondoo alionekana kuwa na nguvu sana kwa vile ufalme wake ulienea hadi pembe za sehemu nne za dunia. Alikuwa na kiburi na alishambulia nchi zingine bila mtu yeyote kuwa uwezo wa kumzuia (mstari wa 4). Hata hivyo, haikuwa muda mrefu kabla nguvu za kondoo kudhoofishwa na kuonekana kwa mbuzi kutoka magharibi (mstari wa 5). Mbuzi huyu alimchinja kondoo kwa mafanikio makubwa, akumwumiza na kuharibu pembe zake. Zaidi, hata aliikanyaga, na hakuna mtu ambaye angeweza kuitete!

Kusudi la Kuibuka Kwa Mbuzi

Angalia uwakilish wa ile pembe ndogo, iliyotajwa katika Danieli 8:9. Pembe hii ambayo ilitokea ghafla kutoka kwa moja ya zile pembe nne iliyowakilishwa katika sura hii ni umbo mmoja na yule *'pembe mdogo'* wa Danieli 7. Kusudi la kuonekana kwake ni kuwa na ukuu kwa falme dunia, ikiwa ni pamoja na *'nchi tukufu'* (Danieli 8:9), labda Palestina. Sura hii inazungumzia mfalme wa dunia, alihimizwa na mwovu ambaye aliingilia historia yetu. Tunafahamu kwamba Mungu ametukomboa kwa utukuf kutoka kwa makucha ya nguvu zake. Tunamwabudu kwa yote ametutendea, akitupatia ushinding juu ya adui, Shetani.

A. Kusudi la Uwepo Wa Malaika

Danieli alishindwa na uwepo wa malaika, na alihitaji kufufuliwa na kufarijiwa na malaika (mstari wa 18). Baada ya maono haya, Danieli alichoka! Aligonjeka kwa siku kadhaa na alishangaa na kushtuka kwa yale aliona.

### II. Gabriel Aelezea Maono Kwa Danieli (Danieli 8:15-27)

A. Maana Ya Kondoo Na Mbuzi

Malaika Gabrieli alieleza kile wanyama hawa waliwakilisha. Mbuzi aliwakilisha nguvu za Wamedi na Wapersi ambao walitawala kutoka 539 hadi 331 Kabla Kristo (mstari wa 20 na mbuzi, aliwakilisha Ugiriki (mstari wa 21).

Hapa tunaona baadhi ya ikulu mbili zilizotawala ulimwengu kwa wakati huu. Wamedi na Wapersi chini ya Koreshi walishinda na kumiliki ikulu ya Babeli. Lakini baada ya muda tu, Alexander mkuu, shujaa hodari wa Ugiriki, aliwashinda Wamedi na Wapersi Alipokufa akiwa na miaka thelathini na tatu, majenerali wake wanne waligawanya ufalme kati yao (pembe nne). *"Wakati falme hizo zitakapofika kikomo chake na uovu wao kufikia kilele chake, patatokea mfalme mmoja shupavu na mwerevu."* Haya yalizungumiza mmoja wa watawala wa Ugiriki aliyewatawala wote (mstari wa 23). Hapa unabii unaguzia Antiokias wa IV, ambaye alitenga maeneo makubwa ya kijiografia akawateka umati wa wenyeji, na hata kuwatesa wengi wa watu wa Mungu (mistari ya 24-25).

### B. Utawala Usio Na Mwisho Na Nguvu Ya Pembe Ndogo

Ingawa mstari wa 14 unaeleza mwisho wa furaha, kile Mungu alikuwa akiwaonya watu wake kilikuwa kwamba walikuwa wanaenda kuteseka kupitia mlipuko wa pembe. Kwa muda, watu wa Mungu wangehangaika. Maono haya, kwa Danieli, yangewakilisha tukio la kutisha. Danieli alisukumwa sana na mateso haya yaliyotabiriwa na malaika na alitetemeka na kuzimia. Lakini wakati ulikuwa unakuja, bali Mungu alikuwa anawaahidi kwamba atafanya mwisho ulio mwema.

Je, ni mara ngapi kanisa, wanapopitia majaribu, hawakutaka kukubali kwa uvumilivu njia ya msalaba, na mateso! Hata hivyo, Bwana yuko tayari kutia nguvu roho zetu katikati ya mafadhaiko, kama tu vile malaika Gabrieli alitenda kabla ya tukio lisilotarajiwa la Danieli, mtumishi wa (Danieli 8:18).

## III. Ujumbe Kwetu Leo (Danieli 8:1-27)

Wengine wamesema kwamba Danieli sura ya 8 ni ndoto ya mhubiri. Hata wasomi waliojulikana wanasita kuwa wenye msimamo mkali katika tafsiri yao ya sura hii. Ingawa malaika Gabrieli anaeleza maana ya kihistoria kwa Danieli, tunapaswa kujiuliza kama kifungu hiki kina maelezo juu ya wakati mbele ya falme hizi zilizokuja na kwenda.

Hata hivyo kifungu kinazungumza juu ya wakati huo, kuna umuhimu kwa nyakati zote. Madhalimu wamekuja tena na tena. Tunaona haya katika kipindi cha mateso ya Warumi, ambacho ni dhana ya kitabu cha Ufunuo wa Yohana, kwa mfano. Biblia inaonekana kutabiri nguvu za uovu katika mwisho wa wakati. *"Pembe ndogo"* anaonekana kubadilika mbele ya macho yetu, kutoka kwa mwanadamu anayekufa hadi kufikia mwili wa Shetani mwenyewe. Lengo linaonekana kuhama kutoka kwa Waisraeli, Israeli, Yerusalemu, na hekalu, hadi kwa *"jeshi la mbinuni"* na *"nyota za mbinguni."* Picha hii pia inaweza kuwakilisha takwimu za nguvu za siku za usoni ambazo zinaweza kuleta mateso na dhiki kwa watu wa Mungu. Kwa vile Mungu alimpa Antiokiasi wa IV ushindi katika mgogoro wowote au mateso ya kisiasa ambayo huenda tukalazimika kupitia, tunajua kwamba Anaweza kutenda tena.

Historia imenonyesha kwamba yale Danieli aliona wakati wa kipindi cha Babeli katika maono ya baadaye yalitimia. Roho wa Mungu amewahimiza waandishi wa biblia kurekodi unabii huu kutukumbusha kuwa Mungu anatawala. Unabii nyingi za Agano la Kale zilitimia wazi katika Agano Jipya. Unabii unatuhakikishia utakatifu usio na mwisho wa Mungu, hekima, nguvu, na wema. Tunaweza kumtumainia.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, kondoo alifanaje na alifanya nini?
- Je, Danieli alhisije baada ya kuona maono na kupokea tafsiri? Je, unafikiri ni kwa nini alihisi hivyo?
- Taja baadhi ya unabii ambazo zimetimia?

## HITIMISHO

Kwa hivyo, tunapaswa kujiimarisha nguvu katika furaha na uingiliaji wa baadaye wa Bwana wetu Yesu Kristo. Tunaamini kwa uaminifu kwamba watu wote watashinda. Kwa wakatu huu, tupigane vita kwa ujasiri na tumaini kubwa katika Mungu. Tusiangalie hatua yoyote ya dira; bali tutazame juu, kwa Mungu wa kweli, na ushawishi mkuu, tutangaze kama vile Musa alifanya: *"Mungu akiwa upande wetu tutashinda, yeye atawaponda maadui zetu."* (Zaburi 60:12) Amina.

**Somo la** 48:

## MAONO YA DANIELI JUU YA KONDOO NA MBUZI

**Lengo la Somo:** Kuangazia uaminifu wa Mungu katikati ya maovu.


**Methali:** "Fahari wawili wakipigana, ziumiazo ni nyazi."

**Kifungu cha Kusoma** Danieli 8:1-27

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 8:19 "Akaniambia, Tazama nitakujulisha yatakayokuwa wakati wa mwisho na ghadhabu; maana, ni ya wakati wa mwisho ulioamriwa."

**Maswali ya Kujadili:**
Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Mungu huwaangamiza maadui zetu na tunapata ushindi



| Somo la 49 | MAOMBI: UWEZO WETU MKUBWA |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 9:1-27 |

| Lengo |
|---|
| Kuangazia baraka kuu na faida za maendeleo ya maisha ya maombi ya kudumu, prayer, kama ilikuwa na Danieli. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Kwa hiyo , ee Mungu, isikilize sala yangu na maombi yangu mimi mtumishi wako. Kwa hisani yako, uifadhili tena maskani yako iliyoharibiwa." **Danieli 9:17** |

## UTANGULIZI

Nabii Danieli alilazimika kutumia huduma yake akiwa uhamishoni. Alichukuliwa Babeli katika kuhamishwa kwa kwanza kwa Wayahudi na Mfalme Nebukadneza (605 KABLA KRISTO). Sehemu ya unabii za nabii Yeremia, ambaye zamani alikuwa ametangaza uharibifu wa hekalu la Mungu na Yerusalemu, ulitimia (Yeremia 25:11).

Danieli alitumia taaluma yake ya unabii kwa miaka kadhaa, na wakati alikuwa amezeeka, alisoma unabii wa Yeremia na kuona kwamba wafungwa walikuwa wakikaribia miaka 70 ambayo Yeremia alikuwa ametabiri. Hii ilimchochea aende kwa Mungu katika sala, akimuuliza atomize utabiri wake (Yeremia 25:11-13).

## I. Maombi ya Danieli Kwa Watu Wake (Daniel 9:1-19)

### A. Ombi Lake

Katika hali ile ambayo Mungu alimhimiza Danieli amtafute kupitia Maandikos na maombi, Mungu anatuita kutafuta uso wake sasa. Anatamani kwaba nasi pia tuwe a mioyo iliyo na hamu kubwa ya kutafuta uwepo wake kupitia maombi (Zaburi 105:4, Amosi 5:4).

Danieli hakuomba tu, bali **alimtafuta** Bwana kwa maombi (Danieli 9:3). Alimsihi Bwana kwa ajili ya watu wake. Neno kusihi linaashiria mtazamo wake wa kujisalimisha kwa unyenyekevu na kusujudu, akitafuta kwa moyo wake wote huruma ya Bwana. Kuomba au kumsihi Bwana kunaashiria utegemeze wetu kwa rehema ya Mungu. Tunaelewa kwamba Yeye pekee ndiye aliye na usukani na mamlaka. Mungu ni wa kipekee na halinganishwi.

### B. Danieli Alifunga

Danieli hakumtafuta Bwana tu kwa maombi, alifunga (mstari wa 3). Hii ni moja wapo ya silaha zenye nguvu zaidi ambazo Mungu ametupa kwa faida yetu. Ili kutumia silaha hii, ni lazima tuielewe na kujua jinsi ya kuitumia. Kufunga bila utiifu kwa Neno ni kujiepusha tu na chakula. Kwa hivyo, kufunga kwa utiifu wa dhati kwa Neno huendelea kuwa sehemu muhimu ya kumtafuta Mungu. Ni wakati wa kujitenga na kila kitu ili kujitolea kukutana na Yesu Kristo.

### C. Gunia na Majivu

Nguo ya gunia ilikuwa nguo mbaya ambayo ilitumika kama ishara ya kuomboleza au huzuni kubwa. Haikuwa na starehe. Wakati mwingine walilala pia kwa majivu (Esta 4:3, Yona 3:6). Labda inayofanana nayo ingekuwa kupata mahali pa kupiga magoti kwenye sakafu ngumu, badala ya kuomba tukiwa vitandani. Kusujudu kwa majivu ilikuwa dhihirisho la fedheha kubwa na maumivu kwa waumini wa zamani. Katika maombi yake, Danieli alikiri kwa Mungu kwa ajili ya dhambi zake na dhambi za watu (Danieli 9:4-6). Ingawa alibaki mwaminifu kwa Mungu katika Babeli, na Mungu alikuwa amemfunulia mambo makuu, Danieli alikuwa na unyenyekevu wa kutambua kwamba hakuwa mkubwa kuliko wengine. Maombi yake yaliguza moyo wa Mungu, na bila kusubiri hadi mwisho, Mungu alimtuma malaika Gabrieli kusema naye (Danieli 9:20-21).

## II. Mungu Ajifuonyesha Kwa Danieli (Danieli 9:20-23)

### A. Mungu Ni Wa Kweli

Danieli 9:20-21 inasema kwamba ni lazima tuwe na uhakika kabisa kwamba wakati tunamtafuta Mungu, tutampata. Yeye hujionyesha kwetu wakati imani yetu iko sawa. Tunahitaji kuamini katika Bwana wetu aliye hai, wa kweli na ambaye yupo. Kutokea kwa malaika Gabrieli (si katika maono tend, bali kwa hali ya mtu) ilikuwa kuonekana kusiokuwa kwa kawaida kwa

sehemu ya Mungu (mstari wa 21). Tunapoomba to Mungu, tunapaswa kumwendea kwa imani na hakikisho kamili kwamba tutapata jibu kutoka kwa Mungu. Katika hali hii, Biblia inatuhimiza kwa njia ifuatayo: *"…basi pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana kila mtu anayemwendea Mungu ni lazima aamini kwamba Mungu yuko, na kwamba huwatuza wale wanaomtafuta."* (Waebrania 11:6) Bila imani hii, haiwezekani kumpendeza Mungu. Je, tutapataje jibu kutoka kwa mtu kama hatumwamini!

### B. Mungu Ajionyesha Mwenyewe

Katika hafla hiyo, Mungu aliendelea zaidi. Alimruhusu malaika Gabrieli kujionyesha katika njia inayoonekana na ya kweli (mstari wa 21). Hili lilikuwa tukio la kushangaza kwa nabii, kwa vile ilikuwa zaidi ya yale alitarajia kama jibu la Mungu la maombi yake. Hii inatusaidia kuangazia ni mara ngapi tunamuomba Mungu na hakika tutarajie majibu ya imani yetu.

Mungu hutumia njia nyingi za kujibu maombi yetu. Kwa hivyo wakati huo, wakati Danieli alilia, Mungu alimtuma malaika, ingawa Mungu angetumia pia aina ingine ya kujionyesha. Wacha tuombe sio tu kwa imani kwa kupata jibu, bali kwa ujasiri kamili kwamba Mungu mwenye Enzi atatukuzwa katikati ya kumtafuta kwa haki na imani kwake.

### C. Mungu Alimpa Danieli Ufahamu na Hekima

Maneno ya ajabu kiasi gani kwa moyo wa Danieli! Mungu alijibu maombi ya Danieli kwa sababu Alimpenda sana. Bila shaka tunaweza kujifunza mengi kutoka kwa mistari hii. Jibu la Mungu lilikuja kwa hali isiyo ya kawaida kwa sababu Danieli alikuwa na ushirikiano na Mungu kwa sababu ushirikiano wa Danieli na Mungu ulikuwa wa ndani na wa msingi. Ni Mungu ndiye aliyemsaidia Danieli kuelewa maono. Kiwanadamu, Danieli hangeweza kuyaelewa. Mungu alifungua mawazo na moyo wa Danieli ili kumsaidia aelewe. Katika hali hiyo, Mungu hutenda nasi. Tukimuomba, Atatupa hekima na ufahamu ili kuelewa jambo analotupa (Mithali 2:6).

## III. Jibu la Mungu (Danieli 9:24-27)

### A. Urejesho wa Israeli

Kumbuka kwamba Danieli alikuwa akitafuta jibu kutoka kwa Mungu katika mwisho wa kipindi cha uhamishoni wa Wababeli ambacho yeye na wenzake waliteseka. Danieli alijua kulikuwa na sehemu ya unabii wa kibiblia ambayo ilihakikisha kwamba Mungu alikuwa anaenda kuleta urejesho, na hivyo kukomesha utumwa wa watu wa Israeli katika Babeli.

Hivyo, kile malaika Gabrieli alikuwa akimwonyesha Danieli kilikuwa hakika wakati ambao haya yote yatatendeka; lakini pia wakati huo, ingempelekea zaidi ya hapo (Danieli 9:24). Alielewa kwamba uhuru wa kweli wa Israeli haungekuja tu na urejesho, bali pamoja na dhabihu kamili ambayo ingewafanya wawe huru kutoka kwa utumwa wote wa kiroho.

### B. Kusulubiwa

Katika Danieli 9:26-27, tunasoma juu ya ufunuo mkuu. Mistari hii inazungumza juu ya kusulubiwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo, Mteule wa Mungu. Zaidi ya kuelewa unabii, kile tunapaswa kufahamu ni kwamba jibu la Mungu kwa maombi ya Danieli lilikuwa wazi na fupi. Tunapomtafuta Mungu katika njia iliyo sawa, tutapokea majibu ya mara moja.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni aina gani ya neema ambayo tunao kwa faida yetu leo ili kusonge karibu na Mungu?
- Je, unaamini kwamba utiifu kamili ni muhimu ili kupokea majibu ya Mungu? Kwa nini?
- Je, maisha yako ya maombi yako aje?

## HITIMISHO

Maombi ni raslimali kubwa zaidi ambayo Mkristo anaweza kuwa nayo, lakini wakati huo, ni moja ya changamoto kubwa kwa sababu yanahitaji mambo mengi kutoka kwetu kama tunataka utufuku wa Mungu ukidhihirishwa. Tunahitaji kuishi katika utiifu na kusubiri kwa imani jibu la maombi yetu. Tusiache maombi Prayer and intercession are important aspects of our Christian life if we want to live for the glory of Mungu!

**<u>Somo la</u>** <u>49:</u>

## MAOMBI: UWEZO WETU MKUBWA

**Lengo la Somo:** Kutafakari kuhusu Maisha ya maombi na faida zake


**Methali:** Utunzaji wa mama, humpa usalama mtoto asiye na meno.

**Kichwa cha Somo:** Danieli 9:1-27

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 9:17 "Basi sasa Ee Mungu wetu, yasikilize maombi ya mtumishi wako, na dua zake, ukaangazishe uso wako juu ya patakatifu pako paliko ukiwa, kwa ajili ya Bwana."

**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Tunapoomba kwa Imani Mungu anasikia maombi yetu, anatujibu na anatukuzwa!



| Somo la 50 | KUTAFUTA BWANA WAKATI WA MIZOZO |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 10:2-21 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuwahimiza wanafunzi kuamua kumtafuta Bwana, hasa katika wakati mgumu. | "…Ndipo yeye akaniambia, 'Danieli, usiogope. Mungu alilisikia ombi lako tangu siku ile ya kwaza ulipoamua kujinyenyekeza mbele yake ili upate ufahamu, na mimi nimekuja kwa ajili ya ombi lako hilo.'" **Danieli 10:12** |

## UTANGULIZI

Sura tatu za mwisho za kitabu cha Danieli zinapaswa kuchukuliwa kama kitengo kimoja, ambapo tendo la wakuu wa ulimwengu na dhiki ya watu wa Mungu zinafunuliwa mpaka ukamilifu wa ufalme Wake. Ufunuo huu, ambao una sifa tofauti kwa ufunuo wa awali uliofanywa kwa Danieli, ulimruhusu kujua zaidi utukufu wa Mungu na thihirisho la nguvu Zake wakati wa migogoro ya watu wake. Ujumbe wa sura hii ni muhimu kwa wakati wote. Danieli 10 hasa inatusaidia kutambua umuhimu wa kufunga, kuabudu na kuthamini Neno Lake..

### I. Kufunga, Sila Ya Nguvu (Danieli 10:1-3)

Baada ya miaka nne kupita tangu maono ya wiki sabini, wakati wa mizozo ya kisiasa na kabla ya siku za uson ambazo zilionekana kutokuwa na uhakika kwa watu wa Mungu, Danieli, sasa akiwa amezeeka, aliamua kuanza kampeni ya maombi ya kufunga. Alitenga kando wakati maalumu ambao alichagua kutafuta kwa bidii uongozi wa Mungu na uwepo wake mtakatifu. Alijinyima chakula na kinywaji na pia mafuta na marashi (mstari wa 3). Katika njia hii, alikuwa anatenda wakati fulani, raha halali za kila siku, kutafuta wema zaidi: Uwepo wa Mungu na uongozi wake wa kufanya mapenzi Yake. Haya yalileta matokeo ya mara moja kwa Danieli na wakati wake, na kuangazia njia muhimu ya neema iliyo na thamani ya milele.

Tunapokumbana na mizozo maishani, nyingi ya mizozi isiyotarajiwa, je, tunakumbanaje nayo? Tunaweza kujaribiwa kujizamisha katika dhiki na maumivu. Wakati kama huu, nidhamu za kiroho kama kufunga, kuomba au kusoma prayingorreadingthe Maandiko itaelekeza akili na moyo wetu kwa Mungu. Hizi zote zitatusaidia kuimarisha ushirika wetu Naye, kutia nguvu imani yetu na kukua kiroho kwa kuangazia juu ya kusudi lake la milele kwa mapamgano yetu ya kila siku. Kwa hivyo, tunapaswa kufikiria juu ya kufunga kama silaha yenye nguvu, hasa wakati wa mzozo.

Kama kufunga hakujaelekezwa kwa Mungu, basi ni zoezi la mwanadamu tu ambalo matokeo yake hayatujengi au kutufanya tukue kiroho, bali, kinyume chake, yanatuweka mbali na Mungu kwa kuangazia jitihada zetu, akili na moyo juu yetu na ukweli wetu. Kinyume chake, kwa kuelekeza kufunga kwa Mungu, tunajiondoa kwa masilahi yetu wenyewe na kujisalimisha kwa mwelekeo na mapenzi Yake.

Hatari ingine ni kutumaini kwamba kupitia kufunga, tunaweza kupata kibali cha Mungu. Yesu anatufundisha juu ya haya katika hadithi yake kuhusu Mfarisayo na mtoza ushuru ambapo Mfarisayo alijivunia kufunga mara mbili kwa wiki (Luka 19:12), akiamini haki yake na kuwadharau wengine, akipuuza hata yule mtoza ushuru aliyekuwa karibu naye, akitubu dhambi zake, ambaye Yesu alisemba angehesabiwa haki mbele zake (Luka 18:9-14).

Mwishowe, hatari ingine ni kutumia kufunga kuonyesha udini au kuonyesha mbele ya macho yaw engine kiwango cha juu kinachodhaniwa cha kiroho. Yesu alituonya juu ya hatari hii katika Mathayo 6:16, ambapo tunasoma: *"Mnapofunga, msiwe na huzuni kama wanafiki. Wao hukunja nyuso zao wapate kuonekana na wamekwisha pata tuzo lao.."*

### II. Bwana Aonyesha Utukufu Wake Kwa Danieli (Danieli 10:5-9)

Danieli 10:5-9 inatueleza vile mtu Myahudi alikutana na kiumbe kitukufu, akitukumbusha juu ya maono ambayo Mtume Yohana alikuwa nayo kwenye kisiwa cha Patmo (Ufunuo wa Yohana 1:9-20). Kuna ulinganifu kati ya maelezo haya mawili ya kiumbe huyu mtukufu. Tunaona

kwamba katika hali zote, kiumbe hiki kilikuwa kimefunga dhahabu, kiliangaza kutoka kwa kichwa hadi mguu kwa nuru iliyoinuliwa, macho yake yalikuwa kama mienge ya moto, na alikuwa na sauti kama ya umati wa watu.

Tunapopitia hali za mzozo ambazo zinatusumbua, tunaweza kuamua kutumbukia katika kukata tamaa na maumivu, au kumtafuta Bwana kwa bidii zaidi. Wakati huo, nidhamu za kiroho kama kufunga zitatusaidia kuzingatia utaftaji huu mkali wa mwongozo wa uwepo Wake. Uzoefu wa Danieli unatukumbushwa kwamba hakuna jambo linalotendeka kwetu litabadilisha uzur na utukufu wa Bwana wetu. Hata wakati wa giza kubwa la maisha, waumini wanaweza kukaribia uwepo Wake mtukufu ili kupata uwazi kukabiliana na mahitaji yetu. Katika kufanya hivyo, tunaweza kurejesha uwezo wa kuona yale yanatendeka kwetu kutoka kwa kiwango cha kiroho, badala ya kuona tu magumu ya kweli yanayotupiga. Imani yetu itaimarishwa tunapangazia utukufu na mng’ao wa Bwana wetu.

Tunapokabiliwa na mizozo ya maisha, na hasa wakati wa mateso, tunaweza kuamua kumtafuta Bwana kwa undani zaidi, na kufahamu uwepo wane wa uongozi katika maisha yetu. Hadi hapa, kufunga ni moja wapo ya silaha kali ambayo Mungu wetu ametupatia, lakini tunapaswa kuepuka kuanguka katika hatari fulani ambazo zinatishia maana ya kweli ya nidhamu hii inayoinua.

### III. Bwana Asema Na Danieli (Danieli 10:11-21)

Danieli 10:11-12 inatueleza kwa upana yale Bwana alimwambia Danieli. Bwana alimgusa na kumpa maneno ya faraja na usalama (mstari wa 11-19). Wakati wa mizozo ya kisiasa na mateso ndani ya moyo wake, Danieli alikuwa akiomba kwa wiki tatu. Bwana alimwambia kwamba alikuwa amesikia hata tangu siku ya kwanza ya maombi yake (mstari wa 12).

Tunapokuwa tayari kujitolea kwa uaminifu kwa mapenzi ya Bwana, na kumtafuta na kumwabudu na utu wetu wote, ni lazima tujiepushe na majaribu ya kuamini kwamba Bwana hasikii maombi yeut, hasa kama tunapitia hali ya mzozo au kama kuna mateso moyoni mwetu. Lakini tunapaswa tuendele kuvumilia katika maombi, *“tukiwa waangalifu na kushukuru”* (Wakolosai 4:2), kwa uhkaika wa kujua kwamba Bwana anasikia maombi yetu. Kama vile mwandishi wa Waebrania anavyosema: *“Basi bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana kila mtu anayemwendea ni lazima aamini kwamba Mungu yuko, na kwamba huwatuza wale wanaomtafuta”* (Waebrania 11:6).

Imani inachukua nafasi kuu katikamaisha ya mtu anayeomba, ikifungua moyo wake kwa Bwana na ujasiri wa kujua kwamba anasikia maneno yake. Mchanganyiko wa nidhamu za kiroho kama vila kufunga na kuomba zitatusaidia kupata katika Bwana kile tunachohitaji ili kushinda hali ngumu zaidi na zisizotarajiwa za maisha. Bwana hufanza watu wake kuibuka washinid hata katika hali ambazo zinaonekana kuwa nguvu kushinda sisi wenyewe. Tunapojitoa kwa mapenzi Yake, tunaweza kupokea faida zinazopatikana kupitia ushindi wa enzi pale msalabani.

Kwa wakati huu, ambapo waumini wengi wanavutiwa na kishawishi cha kusikiliza mafundisho ya ziada ya kibiblia, ujumbe ulifunuliwa kwa Danieli unatukumbusha umuhimu wa Neno la Mungu wa kuchambua ukweli wa mafundisho yoyote au matendo yake. Leo, tunapaswa kuangazia Biblia, ambayo tulipewa kupitia himizo la jumla, kama sheria ya imani na mamlaka ya mwisho katika maisha ya kanisa. Maandiko ni ufunuo dhahiri kwa waumini, na hayawezi kubadilishwa na mawazo ya Kikristo. Ingawa mafundisho mapya na kanuni zinaonekana kuvutia kama njia ya kufanya kanisa upya, lazima tuchunguze kwa uangalifu kulingana na Maandiko.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, ni baadhi ya hatari gani ambazo mwumini anayejitayarisha kufunga anaweza kuanguka ndani?
- Je, ni nini hutendeka wakati tunamtafuta Bwana kwa moyo ulio wazi?
- Je, Neno la Mungu linapaswa kuwa wapi katika maisha ya muumini?

## HITIMISHO

Tunapmtafuta Bwana zaidi, Atatuimaimarisha na kutongoza katika kuchukua hatua sawa. Ibada ya kweli itatuekeleza katika kujitoa kwa mapenzi yake na kumtukuza. Pia, tunahitaji kutambua kwamba Bwana atatuongoza kwa Neno Lake, ambalo haliwezi kubadilishwa na mafundisho ingine yoyote au kanuni za wanadamu. Bwana anawatafuta waumini wanaomtafuta kwa wazi, kwa kutumia njia ya neema kama kufunga, maombi na kuwa na shauku ya Neno Lake.

**Lengo la** 50:

## KUTAFUTA BWANA WAKATI WA MIGOGORO AU MAPAMBANO

**Lengo la Somo:** Kuhimiza wanafunzi kutafuta Bwana haswa kwa wakati mgumu.


**Methali:** Ukweli huruka moto bila kuteketezwa.

**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 10:2-21

**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 10:12 - "Ndipo akaniambia, usiogope, Danieli, kwa maana tangu siku ile ya kwanza ilipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa, nami nimekuja kwa ajili ya ombi yako."

**Maswali ya Kujadili**: Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Kukua katika Ukristo unahitaji kusoma Biblia, kuomba na kuabudu kila siku.



| Somo la 51 | DANIELI NA UNABII WA MWISHO |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 11:2-39 |

| Lengo | Mstari wa Kumbukumbu |
|---|---|
| Kuelewa kusudi la matendo ya unabii wa kibiblia ili tuweze kuimarisha uhusiano wetu na Mungu. | "Kumbukeni mambo niliyotenda hapo kale; Mimi ndimi Mungu, na hakuna mwingine; naam, mimi ni Mungu, wala hakuna mwingine kama mimi. Natangaza mambo ya mwisho tangu mwanzo, tangu kale nilitangaza mambo yatakayotukia. Lengo langu litatimia.'" **Isaya 46:9-10** |

## UTANGULIZI

Unabii wa Kibiblia wakati wote umekuwa moja ya vichwa vinavyovutia sana kwa waumini, na hakai moja ya vichwa vilivyo na changamoto kwa wasomi wa kibiblia. Kwa bahati mbaya, mchanganyiko huu wa kuvutia na tamaa ya kuelewa unabii inawaongoza wengu kugeuza umakini wao kutoka kwa matumizi ya vitendo ya maisha ya kila siku ya Kikristo. Kwa thibitisho hili, hatukusudii kuondoa sifa au umuhimu kutoka kwa mada za unabii wa kibiblia, lakini tunapokutana na mambo 'magumu' ya thiolojia, hatupaswi kupoteza ukweli kwamba, kwanza, baadhi ya masuala haya yanawakilisha maajabu ya kiungu ambayo hatuwezi kuyafikia hapa duniani. Kwa upande mwingine, baadhi ya unabii za kibiblia tayari zimetimia, ili kwamba maarifa yao na thibitisho tayri ni sehemu ya ukweli ambao unaelezea thiolojia yetu.

### I. Kabla ya Kuzingatiwa Kwa Kihistoria na Kwa Kinabii (Danieli 11:2-4)

Unabii wa Danieli 11 unayo maelezo fulani juu ya ufalme mkuu na nguvu za kisiasa ambazo zingewaathiri watu wa Kiyahudi wakati wa mwisho. Kumbuka kwamba kutoka kwa ndoto ya Nebukadneza (Danieli 2), na maono ya wanyama wanne (Danieli 7), Mungu tayari alikuwa amemwonyesha Danieli juu ya falme nne za ulimwengu ingatangulia ufalme wa Mungu. Maono ya Danieli 11 yana utangulizi waka katika sura iliyopita. Danieli 10:1 inasema: *"Mnamo mwaka wa tatu wa utawala wa mfalme Belteshaza, alipewa ufunuo. Ufunuo huo ulikuwa wa kweli, lakini ulikuwa mgumu sana, haukueleweka. Hata hivyo alielewa ufunuo huo maana pia alifahamu maono."*

#### A. Vipengele Vya Kinabii Vimetimizwa

Vipengele vya kwanza vya unabii wa Danieli 11 tayari vimetimizwa. Hivyo, mfalme wa nne aliyezungumziwa ni Mfalme Ahasuero (mstari wa 2). Mfalme alivamia Ugiriki na kutawala miaka ya 485-464 KABLA KRISTO. Kisha, 'mfalme mjasiri' aliyetajwa katika Danieli 11:3 alikuwa, bila shaka, Alexander Mkuu, ambaye kwa muda karibu miaka minane alipata ushindi wa kijali ulio wa ajambo katika historia. Danieli 11:4 inatueleza kwamba utawala *"utavunjwa na kugawanyika katika sehemu nne kuelekea pepo nne za mbingu."* Haya yalitimia wakati akiwa kwenye kitanda chake, Alexander Mkuu aligawa ufalme kati ya wakuu wake wanne: Cassander alitawala Makedonia na Ugiriki, Ptolemy alitawala sehemu ya chini ya Syria, Palestina na Misri, Lesymachus alitawala Asia ndogo, na Seleuco Nicator Siria ya juu. Sehemu ya Ptolemy na sehemu ya Seleucian iliwakilisha falme za Giriki zilizoathiri Yuda, Misri– *"mfalme wa kusini"* na Siria *"mfalme wa kaskazini".*

#### B. Vipengele Vya Unabii Kutimizwa

Danieli 11 haifunui majina ya wafalme wa kaskazini na kusini; hata hivyo, vipengele vya kihistoria vya utimizo wa unabii vinaonyesha majina haya kwetu kupitia historia yenyewe. Hakika, inatosha kurejelea matukioa ya kihistoria ya kupata majina ya wafalme wa falme hizi zinazopingana, bali yasiyoweza kuelezwa kwa upana katika somo hili kwa sababu ya nafasi. Pia, ni bora kutaja kwamba maelezo *'mfalme wa kaskazini'* na *'mfalme wa kusini'* yametajwa kijamii kwa kila ufalme kwa wakati fulani katika historia. Hapa unabii haumaanishi wafalme fulani bali usimamizi wao juu ya Yuda. Kwa upande mwingine, utambulisho wa wafalme wa wakati wa mwisho haujafafanuliwa.

### II. Wafalme wa Kaskazini na Kusini (Danieli 11:5-39)

Acha tuanze kwa kusema kwamba ufalme ulio kaskazini mwa Yerusalemu ulikuwa wa Ufalme wa Syria, na ufalme

uliokaa kusini mwa Yerusalemu ulikuwa wa Misri. Historia inarekodi uvamizi wa Antiokia kutoka Syria hadi Yerusalemu, na vita dhidi ya Wamakabayo, familia ya Wayahudi ambayo ilipinga majaribu ya kushinda Ufalme wa Syria (Danieli 11:7). Baadaye, kati ya miaka ya 65-30 KABLA KRISTO, wote Syria na Misri walianguka katika Ufalme wa Wwarumi.

1. Majina ya wafalme inayowezekana ya kaskazini na kusini wakati wa kipindi kirefu yajatambuliwa, ingawa mabishano ya mara kwa mara kati ya milki zote mbilie yamethibitishwa.

2. Pengine sababu kuu ni kwamba muda huo wote mrefu hakukuwa na taifa la Israeli. Kuundwa kwa Taifa la Israeli katika mwaka wa 1948 kuliashiria utimilifu wa ajabu wa unabii. Tangu wakatu huo, Falme za kaskazini na kusii (Syria na Misri) tena zilikuwa muhimu wakati wa unabii wa watu Wayahudi, kama tunavyoona katika vita vya Siku 6 za Vita katika mwaka wa 1967.

3. Watu Wakristo ambao wamekuwa wasikilivu kwa matukio haya ya kihistoria na unabii wanapaswa kuzingatia, sasa kuliko hapo awali, kwamba utimizo wa unabii ulikuwa na utaendelea kuzunguka Israeli. Kwa hivyo, tunapaswa kutazama kwa makini saa ya Mungu katika Mashariki ya Kati. Israeli inabaki kuwa watu wa Mungu.

### III. Athari za Kiutendaji (Danieli 11:5-39)

1. Unabii za Kibiblia zinaunganishwa katika nyakati tofauti za kibiblia na kihistoria. Unabii hizo za Danieli 2 na Danieli 9 zinaonekana kuwa na uhusiano na kima moja, na ambazo zimetimia. Pia, unabii wa wiki 70 unahusiana na ule wa Yeremia 25:1-11. Unabii mwingine uliorekodiwa katika Ufunuo wa Yohana 17 pia unahusiana na Danieli 11 lakini bado haujatimia.

2. Kutimizwa kwa unabii ni thihirisho na thibitisho la kuwepo kwa Mungu. Kutoka kwa nabii za Isaya, hadi za Danieli, tunaona kuashiriwa kwa Mungu wa kweli juu ya miungu ingine ya mataifa ya kipagani, miungu ambayo watu wa Israeli hawakuwa waaminifu kwa Mungu katika hali nyingi. Sasa katika wakati wetu, uchunguzi wa nabii za kibiblia unathibitisha tena uwepo na kukaa kwa Mungu wetu katika matukio yote ya kihistoria ya wanadamu.

3. Unabii zilizotimia ni hakikisho kwamba unabii wa wakati wa mwisho pia utatimizwa. Kwa vile hadithi hiyo hiyo inathibitisha ukweli wa unabii wa Mungu na uwepo halisi wa Mungu wa unabii, hatupaswi kuwa na shaka kwamba Mungu ni wa kweli, na kwamba Neno Lake litatimizwa kwa uaminifu.

Ni muhimu kusisitiza kwamba matukio ya kinabii na maelezo ya giza hayapaswi kupunguza lengo ambalo limewekwa katika Kristo. Kuna hatari kubwa katika kuvutiwa na mambo yajayo, na *'wanabii wengi wa uongo,* huchukua faida ya kiunganishi hiki cha kithiolojia kuwadanaga na kuwageuza watakatifu. Unabii za Danieli zinathibitisha kwetu maneno ya Yesu Yohana 14:3 ambapo tunasoma: *"...Nitarudi kuwachukeni kwangu, ili nanyi muwe pale nilipo mimi"* Mkombozi wetu atarudi kwa ajili yetu. Unabii zilizotimizwa zinatuhakikishia ukweli huu. Tusubiri kurudi Kwake. Huu ni unabii wa kwelii wa Mungu.

## MASWALI YA ZIADA

- Je, Wakristo wanapaswa kuwa waanglifu na nini kuhusiana na unabii na watu wa Kiyahudi?
- Je, ni mafundisho gani ambayo tunaweza kupata kutoka kwa unabii za Danieli kwa maisha yetu ya Kikristo?

## HITIMISHO


Unabii za Danieli ziliwakilisha faraha na ushahidi kwa watu wa Kiyahudi kwamba Mungu hakuwa amewaacha, licha ya mateka waliyokuwa ndani yake. Leo, tunaweza kuthibitisha tena ukweli wa kiungu kati yetu. Tunaweza kutumaini kwamba Mungu atatimiza yale ameahidi katika Neno Lake, na kwamba licha ya ishara za wakati wa mwisho, watu wa Mungu watapokea tuzo. Unabii za Mungu zinahakikisha uaminifu wake. Unabii zilizopewa Danieli zinaonyesha wakati mgumu kwetu. Hata hivyo, zinatuhakikishia pia ushindi juu ya nguvu za uovu.

<u>**Somo la 51:**</u>

## DANIELI NA UNABII WA MWISHO

**Lengo la Somo:** Kuelewa nia ya utendaji wa unabii wa Biblia
**Methali:** Ukweli mchungu ni bora kuliko uongo mtamu.
**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 11:2-39
**Mstari wa Kumbukumbu:** Daniel 11:4 "Naye atakaposimama ufalme wake utavunjika na kugawanyika katika pepo nne za mbinguni, lakini hautakuwa wa uzao wake, wala hautakuwa kama mamlaka yake ambayo alitawala kwayo, kwa maana ufalme wake utangolewa hata kwa ajili yao engine Zaidi ya hao."
**Maswali ya Kujadili:** Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii? Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

**Himizo la Hadithi:** Kumtegemea Mungu kikamlifu inatusaidia katika nyakati mgumu.



| Somo la 52 | DANIELI NA TUMAINI LETU LA BAADAYE |
|---|---|
| | **Maandiko:** Danieli 12:1-13 |

| Lengo |
|---|
| Kuelewa unabii za wawakati wa mwisho kama tumaini la Mungu la baadaye la ukombozi na wokovu, ukituhimiza kuanzisha uhusiano wa karibu na Mungu. |

| Mstari wa Kumbukumbu |
|---|
| "Ila sasa, Danieli, weka siri mambo hayo; kifunge kitbu na kukitia mhuri mpaka wakati wa mwisho utakapofika. Wengi watakimilia huko na huko, nna maarifa yataongezeka.'" **Danieli 12:4** |

**UTANGULIZI**

Unabii zilizorekodiwa katika kitabu cha Danielizinatuonya juu ya wakati mgumu wa baadaye kwa ulimwengu wote. Danieli 12 inaonekana kutuweka kihistoria katika wakati wa sasa wa urejesho wa taifa la Israeli katika mwaka wa 1948, tukio la kihistoria lililo na uzito mkubwa wa kinabii kwa nyakati za mwisho. Hakika, mstari wa 1 unaanza kwa kufanya rejeleo kwa dhana ya kifungu kilichopita (Danieli 11:36-45), ambayo inamaanisha kwamba unabii wa Danieli 12 inakadiriwa kwa nyakati zetu.

## I. Ahadi ya Wokovu na Ufufuo (Danieli 12:1-2)

### A. Ugani wa Upenyo

Kwa mara ya kwanza katika Agano la kale, ufufuo unachukuliwa kama tuzo kwa waaminifu. Ufufuo wa nyakati za mwisho ni sehemu ya uhuru ulioahidiwa kwa watu wa Mungu. Hakika, na kama vile Danieli 12:2 inapendekeza na vile Yesu mwenywe alisema baadaye katika Yohana 5:29, kutakuwa na ufufuo mwingine ulihifadhiwa 'kwa wale waliotenda maovu, *"ufufuo wa lawama"*.

Ufufuo wa kwanza umetabiriwa kama tukio tofauti la wokovu wa watu wa Mungu, waumini waaminifu katika Kristo, ambao watapokea tuzo lao la uzima wa milele. (1 Wathesalonike 4:16). Unabii wa Danieli 12 una makadirio ya kihistoria kwa watu wa Mungu, Israeli, wakati kabla na baada ya Danieli, ambayo inatujumuisha leo, na waumini wote katika karne yote.

### B. Mikaeli, Mkuu

Sura ya Mikaeli katika unabii huu chombo muhimu cha kuangazia kwa sababu ya kuhusika katika matukio ya wakati wa mwisho. Wengine humchua Mikaeli kama mkuu kati ya malaika (malaika mkuu) kama malaika mkuu Gabrieli, mjumbe wa Mungu. Mikaeli anawakilishwa katika Maandiko kama malaika shujaa ambaye alimsaidia malaika wa mjumbe (labda Gabrieli), ili apeane ujumbe wa unabii wa Danieli (Danieli 10:13). Pia, malaika huyu shujaa anaonekana kama kiongozi wa jeshi la Mungu katika vita vikuu juu ya nyoka na malaika wake (Ufunuo wa Yohana 12:7). Katika unabii huu wa Danieli 12, anajulikana kama *"mmoja wa wakuu"* ambaye alitenda kwa niaba ya watoto wa Mungu.

Kwa sababu ya kuhusika huku kwa kipekee kwa Mikaeli, wengine wanamchukua kama sura ya Kristo, na Gabrieli kama sura ya Roho Mtakatifu. Walakini tunavyotafsiri kifungi hiki, yeye mwenyewe anasema kwamba unabii wake utatimizwa, Hata hivyo, tunatafsiri kifungu hiki, ukithibitisha kuwepo kwa Mungu kusikoweza kukataliwa.

## II. Nyakati Za Mwisho (Danieli 12:3-9)

### A. Kazi ya Watu Wa Mungu

Mstari wa 3 una tuzo kwa wale ambao tunapeleka ujumbe wa injili kwa ulimwengu mzima, na kwa wale tunaobaki waaminifu na imara hadi mwisho. Kwa hivyo, kanisa la Mungu linapaswa kubaki hai katika agizo kuu.

Kanisa lina jukumu la kueneza ujumbe wa Mungu, likionya kuhusu nyakati za mwisho. Unabii wa Danieli, kwa kiwango kikubwa, ni uthibitisho tena wa haki ya Mungu kwetu wote ambao tumempokea Yesu. Kanisa la leo lina misheni ya kuunda kanisa hadi mwisho wa wakati, na lina limekuwa na misheni hii tangu Yesu mwenyewe alilikabithi kwa wanafunzi

wake (Mathayo 28:18- 20).

B. “Kufunga Kitabu”

Katika mstari wa 4, Danieli alipokea amri ya kufunga maneno na kufunga kitabu, ambayo ilimaanisha mchanganyiko kwa wengi. Kama tutahubiri injili, na mahubiri ya injili yahusishe unabii wa matukio ya mwisho, kwa nini ufunge pazia kwa ghafla? Je, ni kwa nini mambo zingine za unabii zinakatazwa kwetu kama unabii wenyewe ni sehemu ya ujumbe?

C. Hii inamaanisha mambo kadhaa.

Mwanzo, inapendekeza kwamba siri zingine za unabii hazitafunuliwa kwa kanisa la nyakati za mwisho, ikithibitisha tena kwamba ujumbe wa kanisa ni lazima uwe wokovu kwa imani. Kwa upande mwingine, na kulingana na ufafanuzi wa Ryrie, siri zilizofichwa na kufungwa katika umabii zitakuwa kwa matumizi tu ya wale wataelewa dokozi kwa Mpinga Kristo, na watakaowaongoza wengine kwa ukweli wakati kipindi cha dhiki kuu. Hii ni muhimu kwa sababu bila kuzingatia tafsiri hii kuwa sahihi, hii itaruhusu watu wa Israeli kurudi kwa misheni ambayo sasa imeanguka kwa kanisa, na kuendeleza matukio ya unabii wa the Apocalipso katika Nchi Takatifu.

Hii ndio sababu inaweza kuwa hatari kwenda kando na misheni yetu ya kutaka kujua na kuamua vipengele vya unabii ambavyo havifahi kufunuliwa hadi iwe muhimu.

## III. Swali La Danieli: Swali La Kila Mtu (Danieli 12:10-13)

A. Maelezo Kuhusu Wakati Wa Mwisho

Mistari ya 10 hadi 12 ina vifaa vya kupendeza sana ambavyo vimechukuliwa ndani ya eskatolojia yote inayowezekana na kujulikana. Inasemekana kwamba ufahamu wa unabii huu unahitaji mawazo ya kiroho na maada wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu.

Maelezo mengine muhimu kuhusu nyakati za mwisho ni kwamba wasiomcha Mungu, wale ambao licha ya ufunuo na ujumbe wa Mungu kupitia kanisa, wataendelea kutenda bila makosa; yaani, hawataelewa au waweze kufahamu mwisho wa nyakati (mstari wa 10). Kwa bahati nzuri, na kwa neema ya Mungu, nafasi ya kufahamu wakati, kupokea ujumbe na kuachana na maovu bado ni kweli. Kwa hivyo, misheni yetu inabaki muhimu kwa ajili ya wokovu wa roho. Tuendelee kusisitiza kazi yetu. Bado wengi wanaweza kuokolewa.

B. Faraja ya Mungu

Mwishowe, Danieli alipokea kutoka kwa Mungu ahadi ya faraja ambayo kila muumini katika Kristo hupokea. Bwana alithibitishwa kuptia unabii huu kwamba tuzo ni la uaminifu. Siku za baadaye za wenye haki ni hakika katika Yesu na ni utimizo wa unabii.

Faraja hii na hakikisho hili havitapota na mwisho wa kifo chetu, bali ufufuo wa wafu katika Kristo utakuwa wa wokovu wa milele. Ufufuo wa Yesu ni tunda letu la kwanza lenye haki (1 Wakorintho 15:20). Kwa hivyo, tunaweza kutulia na kuwa na ujasiri wa hakikisho la unabii, na hakikisho la ahadi za Mungu. Danieli anatulia na matarajio hayo hayo kama tutaeneza uzima kabla ya kuja kwa Bwana wetu

## MASWALI YA ZIADA

- Je, kwa nni misheni ya kanisa ingali muhimu wakati wetu? Kwa ufupi eleza jinsi umeathiriwa na yalie yaliyozungumizwa katika somo la leo.
- • Je, kazi ya kanisa ndai ya muundo wa kinabii wa Danieli ni gani?

## HITIMISHO


Unabii zilizotimizwa zinatueleza kwamba Mungu ni wa kweli. Ahadi za Mungu zitatimia. Tuendelee kuwa imara na wa kudumu katika utume wetu. Leo, ni sisi ndio tunapaswa kung’aa kwa sababu sisi ni nuru ya ulimwengu. Ikiwa tutabaki thabiti katika Bwana na kutimiza utume wetu, tuzo yetu itakuwa kubam mbinguni. Kazi katika Mungu si ya bure (1 Wakorintho 15:58).

**Somo la 52:**

# DANIELI NA TUMAINI LETU LA BAADAYE

**Lengo la Somo:** Kuelewa ya kwamba msingi wa tumaini letu la baadaye in ukombozi na wokuvu.
**Methali:** Usifanye haraka usiku, jua litaamka kila wakati kwa ajili yake mwenyewe.
**Kifungu cha Kusoma:** Danieli 12:1-13
**Mstari wa Kumbukumbu:** Danieli 12:4 "Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya ukatie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka"
**Maswali ya Kujadili:**
Swali la 1. Je, ni nini kilitokea katika hadithi hii?
Swali la 2. Je, mambo haya yalitokea kwa nini?
Swali la 3. Je, ni wapi tunaona utiifu na kutotii katika hadithi hii?
Swali la 4. Je, tunajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?
Swali la 5. Je, utaielezaje hii hadithi kwa mtu mwingine katika wiki hii?

Himizo la Hadithi: Kutimia kwa unabii inatuonyesha ya kwamba Mungu ni halisi.



Africa Nazarene Publications

ISBN: 978-0-7977-1538-7
P O Box 1288
Florida 1710
Republic of South Africa

MAKING CHRISTLIKE DISCIPLES IN THE NATIONS • SUNDAY SCHOOL & DISCIPLESHIP MINISTRIES INTERNATIONAL